Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

### Kikao cha Arobaini – Tarehe 3 Agosti, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### DUA

*Naibu Spika, (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA (K.n.y. MHE. EDWARD N. LOWASSA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka 2011/2012 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS (K.n.y. MHE. EZEKIA D. WENJE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 315

### Malipo ya Malimbikizo ya Wafanyakazi – Geita

**MHE. DONALD K. MAX** aliuliza:-

Wafanyakazi wa Wilayani wananyanyaswa sana na hawalipwi malimbikizo yao na wakati mwingine fedha zao zinapoletwa wanalipwa kidogo kidogo:-

Je, ni lini wafanyakazi Wilayani Geita watalipwa mafao yao? Kwani malimbikizo hadi sasa yanafikia Sh. 484,000,000/=.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Donald Max - Mbunge wa Geita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wafanyakazi wa kada mbalimbali ambao sio Walimu katika Halmashauri ya Geita wana malimbikizo ya madai mbalimbali yanayofikia kiasi cha Sh. 484,000,000/=. Madai haya yanatokana na likizo, matibabu, masomo, uhamisho, posho ya kujikimu na mapunjo ya mishahara. Jumla ya watumishi wanaodai madai haya ni 456 na madeni haya tayari yamehakikiwa. Kwa mishahara pekee, tayari Serikali imelipa jumla ya Sh. 178,921,409/= kuanzia Septemba, 2011 hadi Machi, 2012.

Aidha, madeni mengine yasiyotokana na mapunjo yamewasilishwa Hazina kupitia barua yenye Kumb. Na. GDC/DC.80/3/46 ya tarehe 16 Aprili, 2012 baada ya kufanyiwa uhakiki ili yalipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa Idara ya Afya pekee katika Halmashauri hiyo ya Geita, walikuwa na madai ambayo yanafikia kiasi cha Sh. 115,151,381/=. Halmashauri kwa kuzingatia umuhimu wa kada hii, iliazimia kwamba deni hilo litalipwa kupitia

fedha za matumizi mengineyo *(OC)* ambapo hadi sasa zimelipwa Sh. 77,082,779/= katika mwaka wa fedha 2011/2012. Katika robo ya kwanza ya mwaka 2012/2013 (Julai - Septemba), Halmashauri imepanga kulipa jumla ya Sh. 64,000,000/= kwa kutumia utaratibu huo. Madai haya yamekuwa yakilipwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhibiti malimbikizo ya madeni ya watumishi, Serikali imetoa maelekezo kupitia Waraka wa Katibu Mkuu Kiongozi ambao ulianza kutumika tarehe 1 Mei, 2009 kwa waajiri wote kuhusu udhibiti wa ongezeko la madeni ya Serikali kwa Watumishi wa Umma. Msisistizo uliotolewa ni kwamba, kwa waajiri wasiwahamishe watumishi kama hakuna fedha.

Kwa ajili hiyo, kutowapandisha vyeo watumishi bila kuwepo kwa Ikama na Bajeti ya mishahara na kuacha utaratibu wa kuwataka watumishi kujigharamia huduma mbalimbali kwa ahadi za kurejeshea fedha zao. Bajeti ya Serikali ni *Cash Budget*, hivyo fedha zinazotengwa zitumike kwa ajili ya malengo yaliyokusudiwa ili kuepuka kuzalisha madeni kwa Watumishi wa Umma.

**MHE. DONALD K. MAX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi tena. Namshukuru kaka yangu Naibu Waziri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Lakini kinachonishangaza, nafikiri tunaelewa kitu gani kinachofanyika. Kwa sababu kama mishahara hewa ipo, sielewi kwa nini haya madeni yatokee na hii mishahara hewa sijui inatokea wapi!

(a) *Scales* za mishahara zinaeleweka. Sasa kama *scales* za mishahara zinaeleweka, kwa nini haya mapunjo ya mishahara yawepo? Mtu asipate hela yake ya likizo na matibabu kwa sababu ndiyo vya msingi! Je, haya madeni kwa sababu yameanzia mbali, hao watu wanaolipa mishahara hewa wamechukuliwa hatua?

(b) Matatizo haya haya yanajitokeza kwa wastaafu: Je, pana uwezekano wa kuifuta kabisa *PSPF* kwa sababu wastaafu wanahangaika mno huko? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hii mishahara hewa inatoka wapi, mishahara hewa inatokana na kutokuwepo kwa uaminifu. Wewe unao watumishi 350, unasema mimi ninao watumishi 600. Ni hicho! Katika Halmashauri zetu, sisi tunachoambiwa hapa ni kwamba, tunatakiwa tuwe waangalifu na tuhakikishe kwamba tunadhibiti hali hiyo isijitokeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukishakuwa na watu ambao sio waaminifu wakakaa pale, kikundi cha watu kikakaa pale, kitakutengenezea tu orodha ya ajabu ajabu na ndiyo maana sasa tulichofanya ni kuhakikisha kwamba tunapitisha Halmashauri zetu, wote tumepitia kote, tukakaa pale tukasema; tena wakati fulani tulitaka hapa kutoa maelekezo kwamba tupitie dirishani kwanza ili tujue ni nani ambao hawatatokea

pale dirishani. Ziko jitihada zinazofanyika kuhakikisha kwamba tunaondokana na tatizo hili.

Waheshimiwa Wabunge, tunaomba tushirikiane wote kwa pamoja. Hela hizi ni walipa kodi wa Tanzania, wanalipa na haziwezi kulipwa tu hivi hivi. Zoezi hili linafanyika na wale watu wote ambao tumegundua kwamba wamefanya udanganyifu kule, wamechukuliwa hatua.

Sasa kwa nini mapunjo haya yanajitokeza? Mapunjo haya yanayozungumzwa hapa yametokea toka mwaka 2009 mpaka sasa hivi tunavyozungumza hapa. Nataka nimwambie Mheshimiwa Max kwamba, Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Hawa Ghasia alikwenda mpaka Geita na akafika pale na akaona kwamba kweli kulikuwa na haya madeni na ni *genuine* na ameagiza Serikali, kwa maana ya sisi Wizara hapa, kwamba tufuatilie kupitia Hazina.

Mapunjo haya yametokea kwa sababu mtu anafanya *reallocation*. Unakuta wakati mwingine amepangiwa hapa, kwamba lipa hapa; hakulipa, amekwenda kulipa kitu kingine. Matokeo yake, yanayotokea ni haya. Ndiyo maana tunasema hapa, Mheshimiwa Rais mwenyewe wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania alishasema, kama huna hela za kumhamisha mtumishi, usimhamishe. Sasa akishasema Mheshimiwa Rais pale na Serikali imesema hivyo, ni nani mwingine anaweza akafanya hivyo? Wewe unahamisha watu, unajua kwamba mimi sina hela za kuwahamisha, matokeo yake utapata hiki unachokiona hapa. Unawapandisha watu madaraja,

huna hela za kuwapandisha madaraja, na ndiyo maana tumeisema hapa.

La mwisho kuhusu hawa wastaafu, tatizo ambalo limejitokeza hapa ni kwamba hatuendi kwa ule utaratibu tunaoufahamu wote. Wakati mwingine wanalipwa katika kipindi cha miezi mitatu, miezi sita ndivyo tulivyosema. Lakini nasema kwamba kufuta jambo hili itakuwa ni *unfair* kwa sababu hawa watu ni watu ambao wametumikia Taifa kwa muda mrefu. Ukisema tuiondoe hii, sasa maana yake ni nini? Lazima tuendelee, kama kuna upungufu huu, tutaendelea kuondokana na huu upungufu ili waweze kusaidiwa.

Na. 316

**Ulipaji wa Karo za Shule Kupitia Benki**

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA** aliuliza:-

Jimbo la Mwibara ni miongoni mwa Majimbo nchini ambayo hayana Benki yoyote:-

Je, ni sababu gani zinaifanya Serikali kuagiza ada zote za wanafunzi wa Sekondari zilipwe kupitia Benki wakati maeneo mengine yanafahamika kabisa kwamba hayana Benki?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola - Mbunge wa Mwibara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto zilizokuwepo katika ukusanyaji na matumizi ya ada za wanafunzi wa Shule za Sekondari, Serikali kupitia Waraka Na. 3 wa mwaka 2008 kuhusu utaratibu wa kulipa ada katika Shule na Vyuo vya Serikali ilitoa maelekezo kuwa malipo yote ya ada na michango iliyoidhinishwa yafanyike Benki katika akaunti za Shule au Chuo husika. Lengo lilikuwa kuhakikisha kuwa ada zinakusanywa, kutunzwa na kutumika kwa kuzingatia kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za Umma. Changamoto zilizokuwepo ni pamoja na baadhi ya wanafunzi kutolipa ada ingawa wamepewa na wazazi na shule kutumia fedha za ada kabla ya kuziweka Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ugatuaji wa uendeshaji na usimamizi wa Shule za Sekondari kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na kwa kuzingatia hali halisi ya uendeshaji, Shule za Sekondari za Kata katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali ilitoa miongozo mbalimbali ikiwemo inayohusu utaratibu wa kukusanya maduhuli na kusimamia matumizi yake katika Shule za Sekondari ndani ya Halmashauri. Katika utaratibu huu, ulipaji wa ada unafanyika kama ifuatavyo:-

- Wazazi walio karibu na huduma ya Benki watalipa ada Benki katika akaunti ya Shule na kuwasilisha Shuleni hati za malipo *(pay in slip);*

- Wazazi walio mbali na huduma ya Benki watalipa ada Shuleni na kukatiwa Stakabadhi ya Halmashauri husika;

- Uongozi wa Shule unawajibika kuandaa utaratibu wa kuziwasilisha Benki fedha zote zilizokatiwa Stakabadhi Shuleni kabla hazijatumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na udhibiti wa makusanyo, Mkuu wa Shule anatakiwa kuwasilisha nakala ya *pay in slip* ya Benki na *Revenue Collectors Cash Book Summary* - *RCCB* na makusanyo ya kila mwezi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri yake. Matumizi ya fedha zilizokusanywa yatafanywa kulingana na kasma iliyoidhinishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri kupitia kwa Afisa Elimu wa Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaamini kuwa kwa utaratibu uliopo, wazazi wanaweza kupata huduma Benki na Shuleni pasipo usumbufu wowote ule. Napenda kutumia fursa hii kuwahimiza Wakuu wa Shule nchini kuhakikisha maelezo ya kujiunga na Shule (*joining instruction)* yanajitosheleza vya kutosha kuhusu utaratibu wa malipo ya ada ili wazazi wakiwemo wa Jimbo la Mwibara wasipate usumbufu. *(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wana-Mwibara haturidhiki kabisa na majibu haya ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wana-Mwibara tulitaka kujua, pamoja na changamoto hizi ambazo zilikuwa zinapelekea Serikali ituletee Benki kwa kutatua changamoto hizo, lakini matokeo yake wakijua Mwana-Mwibara kutoka Kisolya kwenda Benki Bunda ni kilomita 85, Kutona Nafuba Kisiwani ni kilomita 95: Swali letu ni kwamba, tulitaka kujua, kwa nini Serikali wakati ikijua hatuna Benki, wakatoa Waraka wa namna hii? Ndiyo nilitaka kujua sababu.

(b) Katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema baada ya kuona changamoto hizi, wakatoa Waraka Na. 3 wa mwaka 2008 ili Wana-Mwibara tuweze kulipia Benki, lakini huku mbele anasema kwamba kutokana na ugatuaji, uendeshaji na usimamizi wa Sekondari ulipelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lakini mpaka sasa hakutuambia ni Waraka Na. 3 ngapi katika majibu yake uliokuwa unafuta waraka Na. 3 wa mwaka 2008 kwamba sasa wazazi walipie kwenye Benki. Je, Naibu Waziri haoni kwamba kutotuambia ni Waraka gani, bado Wakuu wa Shule wanaendelea kutambua Waraka Na. 3 wa mwaka 2008? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpe pongezi sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini jibu langu kwa swali hili ni kwamba, Waraka ambao ulikuwa umetolewa kulipia ada Benki, Waraka ule pia ulitoa *exception* kwa maeneo yale ambayo hayana huduma ya Benki kuweza kulipa moja kwa moja kule Shuleni.

Kwa hiyo, maeneo yale ambayo Mwibara, na maeneo mengine katika Wilaya ya Bunda ambayo yako mbali sana na Benki, *exception* hii ipo ya kuweza kulipa moja kwa moja Shuleni na Waraka huu umetolewa kwa sababu kubwa za kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama atakumbuka, mwezi Agosti, 2007, Chuo cha Ualimu Morogoro kilivamiwa siku hiyo ambapo ada zililipwa pale na hela zikaibiwa; lakini pia Pugu kulikuwa na tukio kama hilo siku wanafunzi walilipa ada majambazi waliingia ili waibe ada ile na katika purukushani zile, mwanafunzi mmoja aliuawa.

Sasa matukio haya lazima tuyalinde, hatuwezi tukaacha tu itokee watu wafe, tusiwalinde walimu, wanafunzi, Wahasibu katika mashule yetu. Lazima Serikali ichukue hatua ambazo zinahakikisha kwamba kuna usalama. Pale ambapo hakuna Benki karibu, Waraka huu unatoa *exception* kwamba wanafunzi ama wazazi wao walipe moja kwa moja pale shuleni. *(Makofi)*

Na. 317

**Kujenga Barabara ya Lami Wilayani Kasulu**

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA** aliuliza:-

Ni muda mrefu tangu wananchi wa Wilaya ya Kasulu waombe kujengewa barabara ya lami na ahadi nyingi zimetolewa juu ya kutekeleza ombi hilo:-

(a) Je, Serikali itakubali kuwa huu ni wakati muafaka wa kujenga barabara ya Nyakanazi - Kigoma kwa kiwango cha lami?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kupandisha hadhi barabara ya Makere - Itanga ili itengenezwe haraka kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa Kilimo Kwanza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera - Mbunge wa Kasulu Vijijini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa barabara ya Nyakanazi - Kigoma (km 335.7) kwa kiwango cha lami na hatua mbalimbali zimeshachukuliwa ikiwemo kukamilisha usanifu wa kina wa barabara sehemu ya Kidahwe - Nyakanazi (km 300) kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.4 na kukamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya barabara ya Kigoma - Kidahwe (km35.7) kwa gharama ya Shilingi bilioni 32.543 fedha za ndani.

Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali mwaka 2012/2013 zimetengwa Shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kujenga sehemu ya barabara ya Kidahwe - Nyakanazi (km300) kwa kiwango cha lami.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupandishwa hadhi barabara ya Makere - Itanga, tunamshauri Mheshimiwa

Mbunge afuate utaratibu ulioainishwa kwenye Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007 kwa kupitisha maombi haya kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Kigoma na ndipo yawasilishwe Wizarani ili yafanyiwe kazi.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake. Lakini nina swali moja dogo kwamba: Je, kwa kuwa ujenzi wa barabara hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, na tumekuwa tukiipigia kelele kwa muda mrefu, Wizara iko tayari kutoa kipaumbele, fedha hizi zilizopangwa ihakikishe zinafika Mkoa wa Kigoma mapema iwezekanavyo?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nimtaarifu tu Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba mimi ni Mjumbe wa Bodi ya Barabara Mkoa wa Kigoma.

Kwa hiyo, naomba nimtaarifu kwamba, taratibu zote zimeshapitiwa na tunachokisubiri ni utekelezaji. Hatua ya ziada, mimi mwenyewe nimeshaandika barua ya maombi maalum kwa ajili ya umuhimu wa barabara hii. Kubwa zaidi, mkizingatia kwamba Kasulu tumepokea dhamana, heshima ya Taifa letu kwa kupokea Wakimbizi ambao kule kuna Makambi ya Wakimbizi wanaoathiri kwenye barabara hii; naomba Mheshimiwa Naibu Waziri apitie kwenye Taarifa zake za

Kiofisi, ili aweze kupitia maombi yetu rasmi na ayafanyie kazi haraka iwezekanavyo, kwa umuhimu wa barabara hii. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tunapokea shukrani na pia tunakupongeza kwa namna unavyofuatilia ahadi za Serikali na za Mheshimiwa Rais kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. Naomba nikuhakikishie kwamba, kwa sababu tumeshaziweka fedha hizo kwenye bajeti, kazi yetu ya kwanza itakuwa ni kumtafuta Mkandarasi mwenye uwezo ili aweze kuanza kujenga barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la kupandisha hadhi barabara, kama nilivyosema ni kwamba, ukishapitisha kwenye Bodi ya Mkoa, inakuja kwetu Wizarani, na kuna Kamati Maalum ambayo itakwenda kule Kigoma kuhakiki, kuona vigezo vile vimefuatwa na vinakidhi ili barabara hiyo iweze kupandishwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda leo, tutakubaliana kwamba, twende kwa utaratibu huu ninaoenda nao. Kwa hiyo, mnikubalie hivyo.

Bado tuko Kigoma. Swali, litaulizwa na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Na. 318

**Ruzuku ya Pembejeo, Bei na Wataalam wa Kilimo**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA** aliuliza:-

Wakulima wa Manyovu, Wilaya ya Kasulu ni wakulima wazuri wa zao la Kahawa, lakini wanakabiliwa na tatizo la bei ndogo, ukosefu wa ruzuku za pembejeo na Wataalamu wa Kilimo:-

(a) Je, ni lini Serikali itaweka ruzuku ya pembejeo za kilimo ili zao hilo lizalishwe kwa wingi zaidi?

(b) Je, ni lini bei ya Kahawa itapanda ili kumpatia Mkulima pato kubwa la kutosha?

(c) Je, ni lini kutakuwa na Wataalamu wa Kilimo wa kutosha, ili kuzungukia mashamba ya wakulima kwa lengo la kuboresha zao hilo kwenye Jimbo la Manyovu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba - Mbunge wa Manyovu, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya zao la Kahawa kuanzia mwaka 2007/2008, ambayo huhusisha uzalishaji na upatikanaji wa miche bora ya Kahawa inayouzwa kwa wakulima kwa bei nafuu. Ili kuhakikisha miche hiyo inawafikia

wakulima wa Wilaya ya Kasulu, hususan Jimbo la Manyovu, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa zao la Kahawa *(TACRI)* inatumia Kituo kidogo cha Mwayaya ambacho kinazalisha miche bora na kutoa huduma kwa wakulima wa Wilaya za Kigoma Vijijini, Kasulu, Kibondo na Ngara.

Vilevile mwaka 2011 wadau wa zao la kahawa nchini wameanzisha mfuko wa kuendeleza zao *(Coffee Development Trust Fund)* ambao wadau na Serikali itachangia fedha kwa ajili ya kusaidia kuendeleza zao na hasa wakulima wadogo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya Kahawa kwa wakulima inategemeana na hali ya Soko la Dunia. Hivi sasa bei katika Soko la Minada ipo kwenye wastani wa Sh. 5,500/= kwa kilo ya Kahawa aina ya arabika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei hiyo ni ya juu ikilinganishwa na gharama za uzalishaji wa kilo moja ya Kahawa ya arabika ya wastani wa Sh. 1,900/= kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Kituo cha Utafiti wa zao la Kahawa *(TACRI)* mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima watapata kipato kikubwa zaidi kutokana na bei hizo pale watakapoongeza tija kwa kupanda aina mpya ya miche bora inayotolewa na *TACRI* na kuuza Kahawa yenye ubora katika madaraja kwenye Soko la Mnada *(Green Beans),* badala ya kuuza Kahawa ghafi *(Maganda)* kwa wachuuzi *(Middlemen)* Vijijini.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, inatambua kuwa, lipo tatizo la upungufu wa Maafisa Ugani hapa nchini. Hadi kufikia mwezi Juni, 2012, Wilaya ya Kasulu ilikuwa na jumla ya Maafisa Ugani 89, wakiwemo 17 katika Makao Makuu ya Wilaya ya Kasulu na 72 katika ngazi za Kata na Vijiji. Upungufu uliopo ni wa Maafisa Ugani 72.

Hivyo kwa kutambua upungufu huo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya nchini inaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuimarisha Huduma za Ugani, kupitia Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* ambao unalenga kutoa mafunzo kwa vijana tarajali na kuwaajiri. Lengo ni kupata Maafisa Ugani wa kutosha ambao baadhi yao watapelekwa kwenye Jimbo la Manyovu kwa lengo la kuboresha kilimo cha kahawa.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza, namshukuru Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa majibu mazuri kabisa. Ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo vikundi kule kwetu ambavyo ni *KACOFA (Kalinzi Coffee Farmers Group)* na tunacho kikundi kingine cha *Kalinzi Organic Coffe Farmers Group* na *Mkabogo.* Hawa walinunua Kahawa za Wakulima kwa ahadi ya kuwapa fedha nyingi, wengine walilipwa na wengine hawakulipwa. Je, Serikali, itasaidiaje wakulima hawa waweze kulipwa na hivi vikundi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa bei ya Kahawa inachangiwa vilevile na Kahawa hiyo kuwa imehifadhiwa vizuri, na moja ya tatizo walilonalo Vyama vya Ushirika vya Kanyovu, ni ukosefu wa maghala: Je, Serikali itatusaidiaje watu waweze kupata maghala bora kwa kuhifadhi Kahawa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili tatizo la *KACOFA,* kwa maana ya *Kalinzi Coffee Farmers* na hii *organisation,* hii Taasisi ya *Kalinzi Organic* kwa bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge ameshakuja kwangu na tumelizungumzia hili jambo. Hapa inaonekana kuna makubaliano yaliyofikiwa baina ya hawa wawili na wakulima, ambayo yamekosa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimtaarifu tu kwamba, tunaandaa taratibu za kuwasiliana na uongozi wa Wilaya yake kupitia Halmashauri ili tupate Mkataba ule wa makubaliano ambao wakulima walitoa Kahawa yao kwa hawa mabwana na hawakupata hela yao. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba naomba tushirikiane kwa karibu ili tupate ufumbuzi wa haraka wa tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili, ni kweli kwamba, ukipata maghala bora na mnada ukafanyika pale pale, usisafirishe ile Kahawa kwa umbali mkubwa, Kahawa inabaki na ubora wake. Kwa hiyo, katika hili, tunaiomba Halmashauri ya Manyovu na Mheshimiwa Mbunge tushirikiane tuone ni namna gani ambavyo tutaongeza pesa kidogo kwa upande wa Serikali Kuu,

lakini na wao Halmshauri waweke kidogo, kwa kutambua kwamba, inaongeza ubora wa kahawa yao na mapato kwa wakulima.

Na. 319

**Tatizo la Maafisa Ugani Mkoa wa Dodoma**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Serikali, iliwahamasisha wananchi wa Mkoa wa Dodoma kulima zao la Korosho, Alizeti na Ufuta, kama mazao ya biashara; na wananchi wameitikia wito huo kwa kulima zao la alizeti kwa wingi, lakini tatizo ni Maafisa Ugani:-

Je, ni lini Serikali, italeta Maafisa Ugani wa kutosha kwa Mkoa wa Dodoma ili kuwaelimisha wananchi zaidi juu ya Kilimo cha mazao tajwa hapo juu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister A. Bura - Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Felister A. Bura, kwamba, upo upungufu wa Maafisa Ugani kwa Mkoa wa Dodoma na siyo tu hapa, bali hata kwa Mikoa mingine nchini. Kufuatia upungufu huo, Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Kuimarisha Huduma za Ugani Nchini ulioanza mwaka 2007/2008 ambao unatoa mafunzo kwa vijana

tarajali na kuwaajiri kuwa Maafisa Ugani. Mpango huo umewezesha idadi ya Maafisa Ugani katika ngazi ya Kata na Vijiji nchini kufikia 7,974 ukilinganisha na Idadi ya 3,379 iliyokuwepo mwaka 2007. Hili ni sawa na ongezeko la wastani wa Maafisa Ugani 918 kila mwaka.

Aidha, wapo jumla ya wahitimu 1,500 wenye Stashahada ambao hawakupata nafasi ya ajira kwa mwaka 2011/2012 na vijana tarajali 1,000 waliohitimu mafunzo ya kilimo mwezi Juni, 2012 wameombewa Kibali cha Ajira na watatarajiwa kupata ajira hiyo mwaka 2012/2013. Lengo la Wizara ni kuwa, kila Kijiji na Kata, awepo Mtaalamu mmoja wa Kilimo, kwa jumla ya Kata na Vijiji 15,082 vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dodoma, una jumla ya Maafisa Ugani 263 katika ngazi ya Kata na Vijiji, kati ya 742 wanaohitajika kwenye Kata na Vijiji vya Mkoa huu. Kwa hali hiyo, Mkoa una upungufu wa Maafisa Ugani wapatao 479. Katika hatua za kuziba pengo hilo, Mkoa wa Dodoma kupitia Halmashauri zake, umeajiri Maafisa Ugani 75 na hivyo kuchangia kupunguza pengo lililopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuajiri kadiri uwezo utakavyoruhusu hadi kukidhi lengo la kuwa na Maafisa Ugani mmoja kwa kila Kijiji na kila Kata kwa nchi nzima. Vilevile Wizara yangu inazishauri Halmashauri zinazozalisha mazao ya korosho, alizeti na ufuta, kupitia Mipango ya *DADPs,* zitenge fedha kwa ajili ya kuwapatia Wataalamu wake mafunzo rejea, yanayolenga mazao hayo ili kuimarisha uwezo wa

Maafisa ugani waliopo katika kuhudumia wakulima. *(Makofi)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Maafisa Ugani tulionao hawatoshelezi, na waliopo hawawashauri vizuri wakulima kuhusu zao geni la Korosho tulilonalo na matokeo yake wakulima wanadhani kwamba bibo ndiyo zao lenyewe la korosho: Je, Serikali, ina mkakati gani mahususi kuhusu zao la korosho Mkoani Dodoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, Maafisa Ugani tulionao hawana vitendea kazi, na Dodoma hakuna zao ambalo halistawi; tatizo letu ni ushauri kuhusu mazao tunayolima au mazao mageni? Je, Serikali iko tayari kuwasaidia Wagani hawa vitendea kazi ili wafanye kazi yao ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruksa yako, hapa kwenye zao la korosho kwa upande wa Mkoa wa Dodoma, ni kweli kwamba Dodoma kama unavyofahamu wewe mwenyewe, zao la Korosho limeonekana kweli linakubalika. Sasa kwa swali alilouliza la mkakati gani, mkakati uliopo sasa hivi, na jana tumekaa na Bodi ya Korosho tumewaagiza, uzalishaji wa Korosho sasa hivi ni tani 160,000, lakini

Tanzania, ina *potential* ya uzalishaji na ina *potential* ya soko kwa zaidi ya tani 400,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi tani 400,000 hazitatoka Mkoa wa Pwani tu na Mkoa wa Mtwara na Lindi, kwa sababu, tumebaini kwamba, Dodoma korosho inakubali sana; Tanga, Morogoro mpaka kule Mbinga na Ludewa kwa akina Mheshimiwa Kapteni Komba na Mheshimiwa Filikunjombe, inaonekana korosho inakubali. Sasa ili tufikie zile tani 400,000 lazima Bodi ya Korosho, kwa maagizo tuliyowapa jana kwamba watengeneze mkakati wa kuwa na miche bora milioni 10 ndani ya miaka mitatu ijayo. Tunalenga maeneo kama haya ya Dodoma ili liweze kuwa moja ya maeneo ambao yatapanua uzalishaji wa korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili la bibo, ni kweli, kwa sababu, mara nyingi kama kule Pwani, bibo lina matumizi mengi. Hata kwa kupata kilaji, kutengenezea kilaji na *juice.* Kwa hiyo, inawezekana ndugu zangu wa hapa Kongwa, Mpwawa na wapi, wameona kwamba, bibo ndiyo zao lenyewe, kumbe utajiri uko kwenye ile Korosho. Kwa hiyo, hilo nalo tutatoa elimu hiyo kwa ajili ya kuwapatia ndugu zetu elimu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la ushauri, naomba niwasihi Waheshimiwa Wabunge kwamba, ni kweli, kwa utaalamu uliobaini *soil fertility,* Mkoa wa Dodoma ni katika Mikoa ambayo ina rutuba kuliko Mikoa yote Tanzania. Nawasihi Waheshimiwa Wabunge, waende Nane Nane na wapite kwenye mabanda, hasa yale ya Halmashauri za Dodoma kwa maana ya Singida, Kondoa, Kongwa, Mpwapwa,

wataona kwamba pale pana kilimo ambacho kinatokana na Wilaya hizo, ambacho kimezidi viwango vya kila aina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tatizo tulilokuwanalo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, ni namna ya kuhamisha ushauri huu na utaalamu kutoka nadharia ambayo imeonekana inafaa kuipeleka kwa wakulima, ili kuongeza tija na uzalishaji. Jana tumekubaliana na Mkuu wa Mkoa kwamba, Wizara yangu tunataka tukae na Wakuu wa Wilaya na Wabunge, ili tupate Mkakati Maalum wa kuhamisha taaluma hii ambayo inaonekana pale Nane Nane, inawezekana kuipeleka kwa wakulima wa Dodoma. *(Makofi)*

Na. 320

**Uhitaji wa Madaktari wa *I.C.U.* Hospitali ya Wilaya ya Bunda**

**MHE. ESTER A. BULAYA** aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Bunda *(BDDH)* ina chumba cha wagonjwa mahututi *(ICU),* lakini huduma hiyo, haitolewi kwa sababu, hakuna Wataalamu/Madaktari wa kutoa huduma kwenye eneo hilo muhimu sana.

Je, ni lini Serikali itapeleka Wataalamu wa *ICU* kwenye Hospitali hiyo ili kuhudumia wagonjwa wanaokuwa katika hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya – Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Bunda, inamilikiwa na Kanisa la *KKKT* Dayosisi ya Mara. Hospitali hiyo inatumika kama Hospitali Teule ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda. Katika makubaliano yaliyofanywa kati ya Halmashauri ya Bunda na Kanisa ni kwamba, mwenye jukumu la kutafuta Watumishi ni mmiliki wa Hospitali. Serikali, ina jukumu la kutoa fedha za mishahara, dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, huduma za *ICU (Intensive Care Unit)* zinatolewa na Wataalamu waliopata mafunzo ya uzamili katika fani ya *Critical Care.* Kwa sasa katika Hospitali hiyo, huduma hizi zinatolewa kwa kiwango cha awali kwa kutumia manesi wawili waliopata mafunzo ya *ICU* katika Hospitali ya Bugando, na Daktari mmoja atapelekwa kupata mafunzo hayo kwa wiki sita ili aweze kutoa huduma na kutumia vifaa vya *ICU* vilivyopo hapo. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza nasikitika kwamba napata majibu mawili tofauti katika Wizara moja. Mwaka 2011 wakati tunapitisha bajeti ya Wizara ya Afya, Waziri

aliyekuwepo aliji-*commit* kupeleka Wataalam kutokana na hali halisi iliyokuwepo pale. Hospitali ime-*fight* kupitia Wafadhili mbalimbali, imepata vifaa vya kisasa kutoka Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mpaka sasa hivi ninapoongea, huu ni mwaka wa nane, chumba hicho hakitumiki, wananchi wa Bunda wanapata matatizo, wengine wanafia njiani kwenda kupata huduma hiyo Hospitali ya Bugando. Sasa je, mbali na jitihada ambazo zinaoneshwa na Hospitali ya *DDH,* Serikali bado haioni kama kuna umuhimu wa kupeleka Wataalamu wao kwa sababu ni zaidi ya miaka mitatu mfululizo Viongozi wa pale wamekuwa wakiomba Wataalamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ni kwamba, Hospitali ambazo ziko barabarani zinapata changamoto kubwa sana, hasa inapotokea ajali na majanga mbalimbali. Sasa matokeo yake wamekuwa wakitumia dawa za ziada na kumaliza dawa hizo kabla ya muda muafaka ambao wamepangiwa. Sasa je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kupeleka dawa na vifaa vya ziada katika Hospitali zote ambazo ziko barabarani ili kukabiliana na changamoto mbalimbali hasa za ajali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona umuhimu wa kupeleka Wataalamu pale ambapo tayari kuna vifaa na kuna vyumba na kuna mahitaji. Lakini kutokana na ukweli kwamba, taaluma hii ya *Intensive Care Unit* bado imo katika ngazi ya Hospitali zile za Rufaa, na

kwamba itatuchukua muda kidogo ili kuweza kufikisha Wataalamu hao katika ngazi ile ya Wilaya. Kwa sasa kwenye eneo ambalo tayari kwa juhudi ambazo zimefanyika kwenye Hospitali hiyo kuwa na hicho chumba na kuwa na hivyo vifaa, manesi ambao wapo, tayari wamepata mafunzo pale Bugando na huyo Daktari ambaye atakuwa amepelekwa na kupata mafunzo ya wiki sita, naamini wataweza kutumia vile vifaa vilivyopo na kuweza kutoa huduma hiyo ambayo itaweza kuokoa maisha ya Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, ni muhimu kwamba hospitali zilizopo katika maeneo ya barabara ambako kwa hakika wanapokea wagonjwa mahututi, hasa wale wa ajali za barabarani wanakuwa na mahitaji zaidi ya matumizi ya madawa pamoja na vitendanishi, lakini vilevile hata utaalam na kwa namna fulani yale mahitaji ambayo wanapokea kwa kawaida, huwa yanakwisha haraka. Hili tunalifahamu. Lakini tunachokiomba, takwimu sahihi zinapowasilishwa za matumizi ya vifaa na madawa waliyopewa yanaweza yakajenga hoja ya kupata nyongeza ya mahitaji haya. *(Makofi)*

Na. 321

**Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini vya Jimbo la Hai**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Tangu mwaka 2005 Serikali imekuwa na ahadi wa kupeleka umeme katika Jimbo la Hai Kata za Hai Mjini,

Kitongoji cha Kingereka na Kata ya Machame Kusini, Kijiji cha Shirima Mguma na mpaka sasa hakuna kilichofanyika:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza miradi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa jibu hilo, naomba nifanye masahihisho katika jibu tulilolета kwako na jibu tulilompatia Mheshimiwa Mbunge la maandishi. Tumesema mradi aliouliza umekamilika kwa asilimia 100 sasa. Napenda nitoe taarifa na nifanye marekebisho kwamba mradi huu haujakamilika kwa asilimia hizo. Baada ya masahihisho hayo, naomba kujibu swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Serikali kupitia Shirika la Umeme la *TANESCO* limetekeleza miradi katika vijiji vya Kingereka na Shirima Mguma. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hii ni pamoja na mradi wa njia ya umeme wa Msongo wa Kv 33 na kusimamisha nguzo zote za njia za umeme wa msongo wa Voti 400 lakini mradi huu bado haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unakadiriwa kugharimu kiasi Shilingi milioni 81. Aidha, *REA* kupitia

mpango kabambe wa awamu ya pili wa mwaka wa fedha 2012/2013 itatekeleza kazi ya upelekaji na usambazaji umeme katika Wilaya ya Hai kwenye vijiji vya Mtakuja, Mungushi, Ukambani, Tindigani, Palestina, Sokoni na Darajani. Mradi huu unakadiriwa kugharimu Shilingi bilioni 1.85. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mradi huu wa umeme kule katika Jimbo la Hai umechukua muda mrefu sana, sasa hivi ni miaka saba na kilichofanyika wamesimamisha nguzo tu na wananchi wanapita wakiangalia nguzo tu. Sasa ningependa kupata majibu kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, atupe *time frame*, ni lini sasa *TANESCO* wataweka nyaya pamoja na *transforma* ili wananchi wale waweze kupata umeme?

Swali la pili, kwa sababu inaelekea watu wa *TANESCO* walimtumia tu Mheshimiwa majibu na yeye hakwenda kwenye *site*, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari baada ya kikao hiki cha Bunge au wakati muda utakapomruhusu twende naye tukatembelee Jimbo la Hai ili aone hali halisi?

**NAIBU SPIKA:** Itabidi mwombe kibali cha Naibu Spika. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na nimwombe radhi kwa kumjibu swali la maandishi kama nilivyosema, lakini niliongea na Meneja wa *TANESCO* wa Kilimanjaro Bwana Zakayo Temu, akaniambia hali

ilivyo na mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Lucy Owenya kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi haina hiyana, tutajitahidi sana kuhakikisha kwamba tunawapelekea Hai umeme na kwa hatua ambayo tumefikia na sehemu iliyobakia ni kidogo sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha tutahakikisha utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo ilisimama kidogo pale Hai, kwamba tutaitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kama nikipata fursa, basi twende wote. Ila ningependa tu anihakikishie usalama kama mambo yote kule yatakuwa sawa sawa, mimi niko tayari kwenda naye. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 322

**Kukomesha Vitendo vya Watendaji Kuweka Vizuizini Wananchi**

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA** aliuliza:-

Imefahamika kuwa, baadhi ya Watendaji wa Vijiji na Kata Wilayani Meatu wamekuwa na tabia ya kuwakamata watuhumiwa wa makosa mbalimbali na kuwaingiza kwenye maghala ya chakula na Pamba kama sehemu ya adhabu bila kuwapeleka Mahakamani.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupiga marufuku tabia hiyo kwa vile inapingana na utawala bora na haki za binadamu?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa - Mbunge wa Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria za Mahakama za Mahakimu sura ya 11 imetamka na kutoa madaraka kwa baadhi ya Watendaji kuwa walinzi wa amani, na kwa mujibu wa sheria hiyo, Maafisa Watendaji wa vijiji hawakutajwa kuwa walinzi wa amani. Kwa hiyo hatua yoyote Afisa mtendaji wa Kijiji kumkamata na kumweka mtu mahabusu ni kosa kwa mujibu wa sheria za nchi na kuzuia uhuru wa mtu bila kuwa mamlaka, ni uvunjwaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu, kwa upande wa Maafisa Watendaji wa Kata, Maafisa hawa wao wamepewa mamlaka, kwani wanalo jukumu la ulinzi wa amani kisheria na wanayo madaraka ya kumkamata mtu aliyefanya kosa au kumweka mahabusu, yaani *lock-up* kwa mujibu wa kifungu 53 cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu sura ya 11 ili kusiwepo na uvunjifu wa amani katika sehemu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kifungu cha 70 cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu kinampatia Waziri wa Mambo ya Ndani mamlaka ya

kuanzisha na kuzitembelea mahabusu zilizo katika maeneo yaliyokubalika. Sheria hii inamruhusu Waziri wa Mambo ya Ndani kukasimu madaraka hayo kwa Watendaji wa Halmashauri walioteuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingia taratibu na Sheria ya Mahakama za Mahakimu, naomba kutoa wito kwa Watendaji wa Halmashauri hasa ngazi za vijiji kuwa makini wanapotekeleza ili kulinda hali ya utulivu katika maeneo yao. *(Makofi)*

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa na kutokana na swali langu jinsi lilivyo, nilikuwa naulizia kwamba kumekuwa na tabia ya Watendaji wa Vijiji na Kata kuwafungia watuhumiwa kwenye magodauni au maghala ya chakula, sikusema kwamba kwa ajili ya kuwapeleka kwenye mahabusu. Sasa nilitaka kujua au kumwuliza Mheshimiwa Waziri kama ni sahihi kwa Watendaji hawa wa vijiji na Kata kuwafungia watuhumiwa wa makosa mbalimbali hasa kwenye maghala ya chakula pamoja na maghala ya pamba kama sasa inaruhusiwa.

Swali la pili, katika majibu ambayo ametoa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema sheria inamruhusu Waziri kukasimu madaraka hayo kwa Watendaji wa Halmashauri walioteuliwa. Sasa ningependa kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Watendaji walioteuliwa ni akina nani? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza, sheria inatambua mahabusu. Kwa hiyo, suala la kumpeleka mtu katika ghala haliruhusiwi. Lakini ukiangalia katika sehemu nyingine, unatakiwa kisheria haraka iwezekanavyo unapomkamata umpeleke Polisi na ndani ya masaa 24 mtu huyu basi aweze kupelekwa Mahakamani. Lakini wote tunatambua miundombinu mbalimbali na changamoto zilizopo vijijini kwetu, unakuta sehemu nyingine ni umbali mkubwa kufika Polisi.

Wakati mwingine Afisa Mtendaji wa Kata anapoitisha gari la Polisi la kumchukua mhalifu yule inachuku muda mrefu na hawezi kumweka nyumbani kwake, anaweza akaambiwa amembaka au amepewa rushwa, ndiyo maana unakuta sehemu nyingine wahawahifadhi katika sehemu ambazo ni nzuri, lakini kumweka katika ghala la pamba na chakula kwa kweli siyo haki.

Katika swali la pili, ametaka kujua watendaji waliokasimiwa madaraka ni akina nani? Kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 189 la mwaka 1975 pamoja na Sheria za Mahakama, za Mahakimu zinawatambua walinzi wa amani ambapo wapo pia Watendaji wa Kata kama ambavyo nimeeleza awali katika jibu la msingi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Swali linalofuata ni la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Miss Bunge. *(Kicheko)*

Na. 323

## Ujenzi wa Reli Mpya ya Dar es Salaam - Tabora - Mpanda na Tabora - Mwanza

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Serikali ina mpango kabambe wa ujenzi reli mpya toka Dar es Salaam mpaka Tabora – Mpanda na Tabora hadi Mwanza:-

Je, ni lini mpango huo utaanza na kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa - Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali ina mpango wa ujenzi wa reli mpya ya kutoka Dar es Salaam hadi Isaka mpaka Kigali kupitia Keza na kutoka Isaka kupitia Keza – Gitega hadi Msongati nchini Burundi kwa kiwango cha *Standard Gauge*. Kwa sasa Serikali za Burundi, Rwanda na Tanzania zinaendelea na mradi huo na tayari mshauri mwelekezi ameanza upembuzi wa kina, yaani *detailed study* kuanzia Februari mwaka huu na anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo mwezi Februari, 2013. Mara baada ya kukamilisha kwa upembuzi huo, taratibu za kupata fedha na hatimaye ujenzi utafanyika.

Mheshimiwea Naibu Spika, Serikali inaendelea na uimarishaji wa Reli ya Kati ya Tabora – Mpanda, Tabora

– Kigoma na Tabora – Mwanza. Mshauri Mwelekezi *M/S COWI Consult* tayari amekwishapatikana. Mpango uliopo hivi sasa ni Serikali kuendelea kukarabati njia hizo za reli pamoja na matawi yake hadi ujenzi wa reli mpya utakapoanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu jana, Wizara imetenga fedha Shilingi bilioni 30 fedha za ndani kwa ajili ya ukarabati wa reli nchini kama ifuatavyo:-

Ubadilishaji wa reli kuwa na uzito mkubwa kufufua, mradi wa kokoto Tura, Ujenzi wa madaraja kati ya Bahi na Kintinku, upembuzi wa kina reli ya Dar es Salaam – Isaka – Keza - Gitega Msongati na Ujenzi wa vituo vya makasha.

Aidha, katika mwaka 2012/2013, Wizara imetenga Shilingi bilioni 104 kwa ajili ya kuzijenga upya yaani *remanufacture* na kununua injini mpya za treni, ununuzi na ukarabati wa mabehewea mapya ya abiria na mizigo na ukarabati wa karakana za Tabora na Dar es Salaam.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni jana tu bajeti ya Wizara ya Uchukuzi imepita, kwa lugha nyingine fedha zipo kuanzia sasa na kwamba katika kupitisha bajeti hiyo, Wizara imekubali kukarabati treni kutoka Dar es Salaam, Tabora hadi Mwanza na mwisho kwamba kutakuwa na treni sasa kwa ahadi ya Wizara kwamba Septemba treni itaanza kutoka Dar es Salaam - Tabora hadi Mwanza na wana Mwanza wananisikia kwa ahadi ya

Wizara, kwa majibu hayo ambayo naamini ni sahihi na kwa majibu ya leo ambayo naamini ni sahihi, basi nakubaliana na Naibu Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hapa ni lazima nimshukuru sana mama yangu Mheshimiwa Maria Hewa kwa kuona ukweli na nimhakikishie tu kwamba ahadi za Wizara na Serikali kwa ujumla tutajitahidi kuzitekeleza kadri zilivyotolewa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuruni sana kwa ushirikiano mlionipa. Leo imekuwa taabu kidogo kwa sababu ratiba yetu hapa Mezani iko ngumu kidogo. Kwa hiyo, nawashukuruni sana na naomba mwendelee kunipa ushirikiano kwa sababu namna ya ku-*manage* mambo hapa itahitaji sana ushirikiano wenu siku ya leo. Nafikiri umeona *Order Paper,* kidogo inahitaji twende kwa muda uliopangwa. Sasa kabla ya Wageni, nianze na matangazo ya vikao kwa sababu wageni ni wengi kuliko kawaida.

Mheshimiwa Abbas Mtemvu - Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam anawaomba Wabunge wa Mkoa huo wakutane Chumba Na. 227 jengo la utawala baadaye saa 7.30 hivi.

Tangazo lingine linatoka kwa Spika - Mheshimiwa Anne Makinda, anaomba kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kuhusu ujio wa Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro - Naibu Katibu Mkuu Mstaafu wa Umoja wa Mataifa kwamba atakuja hapa Dodoma Jumamosi

Tarehe 4, kesho na atakuwa na mazungumzo na Waheshimiwa Wabunge wanawake wote katika Ukumbi wa Pius Msekwa saa 10.00 jioni na baadaye futari itaandaliwa kwa Wajumbe wote. Hivyo Waheshimiwa Wabunge wote wanawake mnaombwa kushiriki katika mazungumzo hayo na baadaye katika futari itakayotolewa katika Ukumbi wa *basement*. Kwa hiyo, kesho saa 10.00 jioni mnaomba mkutane pale Pius Msekwa, atakuwepo Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro na baada ya hapo itakuwepo futari.

Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu kwamba maonyesho ya Nane Nane yanaendelea, tunaomba hasa keshokutwa tusikose kufika katika viwanja vile.

Waheshimiwa Wabunge, sasa baada ya matangazo haya ya kazi, nitangaze haraka haraka wageni ambao kama nilivyokiri kwamba ni wengi kwa siku ya leo.

Kwanza wageni wa Spika - Mheshimiwa Anne Makinda, yupo mgeni wake kutoka Malaysia Dkt. Idris Jala - Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu kutoka nchi ya Malaysia na ni Mtendaji Mkuu wa Taasisi inayoitwa Penandu, wapo Dodoma hawa ndugu zetu kutoka Malaysia kwa ajili ya kuendesha warsha kwa Mawaziri na Makatibu Wakuu kesho siku ya Jumamosi na Jumapili kuhusu mfumo wa kusimamia utekelezaji wa mipango na program za maendeleo na ameambatana na ujumbe wa watu tisa kutoka nchini Malaysia pamoja na Dkt. Fili Mipango - Katibu Mkuu Tume ya Mipango. Naomba wageni wote wasimame.

Ahsante sana na tunawakaribisheni Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni hawa wafuatao, Katibu Mkuu wa Wizara - Bwana Mbarak M. Abdulwakil; Inspekta Jenerali wa Polisi – Bwana Said Mwema, karibu sana; yupo Naibu wa Kamishina wa Magereza – Bwana John C. Minja, karibu sana; yuko Kamshina Mkuu wa Uhamiaji – Bwana Magnus Ulungi, karibu; yuko Kaimu Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji – Bwana Pius Nyambacha, karibu sana; yuko Kamishna wa Polisi wa Utawala Rasilimali - Bwana Clodwig Mtweve, yuko Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wilaya - Bi Agnela Nyoni, karibu sana. Vilevile yuko Kamanda mahiri sana wa Polisi Mkoa wa Dodoma – Bwana Zellote Steven, karibu sana kamanda wangu. *(Makofi)*

Wengine ni Mkuu wa Magereza Mkoa wa Dodoma – Bwana Kibwana Kamtande; Afisa Uhamiaji Mkoa wa Dodoma – Bi Norah Massawe; Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Dodoma – Bwana Nestory Kisenya wa Dodoma na Bwana Joseph Makani – Kaimu Mkurugenzi Idara ya Uzalishaji wa Vitambulisho vya Taifa. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Mheshimiwa Abdallah J. Saadalla Abdallah - Naibu Waziri wa Afrika Mashariki. Ni familia yake, wakiongozwa na Dkt. Badriya Gurnah ambaye ni mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri. Karibuni sana Bungeni. Mheshimiwa Naibu Waziri anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Sikuwaona wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki, lakini naomba nimtambue Mheshimiwa Mama Margareth Sitta. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wetu wa Afrika Mashariki ambao tuliwapigia kura sisi wenyewe naomba niwatambulishe. Kwanza ni Mheshimiwa Angela Charles Kizigha, Mheshimiwa Nderukindo Perpetua Kessy, Mheshimiwa Makongoro Nyerere, Mheshimiwa Shyrose Banji na Mheshimiwa Bernard Murunya. Karibuni sana. Lakini pia ningependa kumtambulisha Mwenyekiti wa Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki Mheshimiwa Adam Kimbisa. Karibuni sana Waheshimiwa Wabunge na kila mnapokuja tunafarijika sana kuwa pamoja nanyi miongoni mwetu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni kutoka Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni Dkt. Julius Rotich ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni kutoka Zanzibar ambao ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar - Bwana Said Natepe, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna Mkurugenzi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Zanzibar - Bwana Khamis Ali Khamis. Karibu sana. *(Makofi)*

Watumishi wa Wizara ni Katibu Mkuu - Dkt. Stergomena L. Tax. Karibu. Pia yupo Katibu Mkuu Dkt.

Abdullah J. Abdullah na Naibu Katibu Mkuu Bwana Uledi A. Mussa. Karibuni sana pamoja na Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo kutoka Wizarani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wengine ni Washirika wa Maendeleo wakiongozwa na Mkurugenzi Mkazi - *Trademark East Africa* -Bi. Paulina Elago, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna Washirika kutoka Sekta Binafsi wakiongozwa na Bwana Faustine Mwakalinga, ambaye ni Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji, Chamba ya Biashara, Viwanda na Kilimo au *TCCIA*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo ni kama wafuatao:-

Kwanza ni wanafunzi 100 pamoja na Walimu wao kutoka Shule ya Sekondari ya *Lord Barden Power Memorial* iliyopo Bagamoyo. Wanafunzi wote kutoka Bagamoyo, tunawakaribisha sana Bungeni Dodoma. Tunafurahi sana kwa kututembelea ninyi pamoja na Walimu wenu. Lakini miongoni mwa wanafunzi hawa yupo Mwenyekiti wa Taifa wa Jumuiya ya Chipukizi ya Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi. Naomba asimame popote alipo na anaitwa Gabriel Makalla. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, wanafunzi 45 pamoja na Walimu wao kutoka Shule ya Mtakatifu Joseph *Millenium*. Karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 50 pamoja na Walimu wao kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri. Karibuni sana.

Vile vile kuna wanakwaya 34 pamoja na viongozi wao wa kwaya ya Moravian kutoka Nyakato Mwanza wakiongozwa na Mchungaji Ezekiel Yonah. Karibuni sana na Baba Mchungaji Ezekiel Yonah Karibu sana Bungeni. Tunaomba utuombee na usiondoke bila kutuombea. *(Kicheko/Makofi)*

Pia tuna wageni 10 ambao ni viongozi wa *UWT* ngazi ya Kata mbalimbali kutoka Jimboni Same Mashariki, ambao ni wageni wa Mheshimiwa Anne K. Malecela. Naomba wasimame popote walipo. Mheshimiwa Kilango anafanya kazi nzuri hapa Bungeni na tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

Samahani, katika orodha yangu nilimruka Kamishna wa Polisi Zanzibar, naomba popote alipo asimame. Ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni mgeni wa Mheshimiwa Ezekia Wenje ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambaye ni Ndugu Daudi Ezekiel Mjumbe wa Baraza la Vijana *CHADEMA* kutoka Nyamagana. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Opulukwa kutoka Meatu wakiongozwa na Ndugu

Shilinde Ngalula kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Esther Matiko ambao ni wadogo wake mmoja anaitwa Nyangi na mwingine anaitwa Bange Matiko na wote ni kutoka Tarime, hawa wanatoka Tarime kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Naomba kuwatambulisha wageni wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, ambao ni Madiwani 13 kutoka Iramba Mashariki, Jimbo la Mheshimiwa Salome Mwambu, lakini wako hapa vilevile kama wageni wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Martha Mlata pia. *(Makofi)*

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba nimtambulishe mgeni wa Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Chonanga anatoka Jimbo la Iringa Mjini, yeye ni Mheshimiwa Diwani. Ahsante sana na tukakukaribisha sana, huyu ni Diwani wa Kata maarufu inayoitwa Kata ya Nduli, Iringa. Karibu sana Bungeni! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, sasa tunaendelea, Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013
### Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, leo nawaomba sana kama inawezekana kila mmoja isizidi dakika moja, tafadhali.

Tuanze na Mheshimiwa Salim!

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Leo kwa mujibu wa *Order paper* tuna Wizara muhimu sana, yaani Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Natambua kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tunamalizia, lakini Wizara ya Afrika Mashariki ndiyo tunaanza. Tuna wasiwasi na ndiyo hali halisi ilivyo kwamba hatutakuwa na muda wa kutosha kujadili Wizara ya Afrika Mashariki na hiyo ina maana kwamba hatutawatendea haki Watanzania katika hili, yaani Wizara ambayo ni muhimu sana.

Kwa hiyo, naomba kwamba Wizara hii tuanze leo na tuendelee hadi kesho kwa sababu kesho kwa mujibu wa ratiba, hakuna shughuli zozote za Kibunge ili tuweze kuchangia vizuri na kuwawakilisha vizuri Watanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie kanuni za Bunge lako tukufu, kanuni

ya 68 (7) pamoja na kanuni ya (5) na kuokoa muda, ni kusisitiza tu umuhimu wa Wizara hii ili tuitendee haki Wizara ya Afrika Mashariki, kazi ifanyike leo na kesho kwa umuhimu wa Wizara hii. *(Makofi)*

Naomba kutoa hoja!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tumekabidhiwa ratiba mpya ya Bunge ambayo inaonyesha Mkutano unakwisha tarehe 16, na tofauti na ratiba ya awali…

**NAIBU SPIKA:** Samahani, anza tena!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 68 (7) tumekabidhiwa ratiba mpya ya Bunge inayoonyesha kwamba Bunge linakwisha tarehe 16 na kwa mujibu wa ratiba mpya, hoja binafsi au hoja za Wabunge zimeondolewa kwenye ratiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba kulitolewa ahadi ya kuwepo kwa hoja binafsi inayohusu suala la marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iliyoondoa fao la kujitoa. Sasa kuondolewa kwa hoja binafsi kwenye ratiba kunafanya kwamba suala hili lisishughulikiwe kwenye Mkutano huu wa Bunge.

Sasa kutokana na unyeti wa jambo lenyewe, kwa kuwa tarehe 16 kuna nafasi ya Miswada ya Sheria na vilevile kuna nafasi ya shughuli za Serikali. Naomba mwongozo wako ili ama Serikali itakiwe kutoa kauli ya kubatilisha uamuzi uliofanywa na *ACCRA* wa

kusimamisha kutolewa kwa mafao haya na kujitoa kwa wafanyakazi au Kiti chako kiruhusu, ili tarehe 16 pamoja na Miswada hii mingine iliyopo tulete Muswada binafsi wa Hati ya Dharura wa marekebisho ya hii sheria ili kuweza kufanya marekebisho ya jambo hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge wote watatu. Nianze na mwongozo wa Mheshimiwa Mnyika.

Naomba niseme kwamba yote mawili mliyoyaleta, yapo kwenye *domain* ya Kamati ya Uongozi ya Bunge ambayo ndiyo inapanga ratiba na iliona kwamba ni busara ipange ratiba kutokana na maoni mengi ambayo yalitolewa pamoja na humu Bungeni kuhusu umuhimu wa kuweza kumaliza mapema ratiba yetu ya Bunge kwa ajili ya kuweza kuwahi shughuli za Eid! Lakini pandekezo hilo basi, kwa sababu Kamati ya Uongozi bado ipo, tutalitazama na kwa wakati muafaka itatoa taarifa yake endapo itakubaliana ku-*incorporate* hilo ombi ambalo limetolewa au vinginevyo, lakini kwa sasa ratiba inabaki kama hiyo ambayo ipo tayari Mezani.

Kuhusu ombi la mwanzo la Afrika Mashariki, naomba tuendelee, kwani ninalifanyia kazi, lakini kabla sijamwita Waziri wa Afrika Mashariki, nitalitolea mwongozo wake baadaye kidogo, lakini naomba ushirikiano wenu. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi moja kwa moja. Mheshimiwa Waziri una nusu saa, na sasa ni saa 8.15. Karibu sana!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa ya kufanya marekebisho mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi na kwa kuzungumza kwa michango yao yote mizuri ambayo yote ilionyesha kutuombea fedha zaidi ili tuweze kutimiza majukumu yetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo aliyatoa wakati akichangia hoja ya Wizara yangu. Lakini nitumie nafasi hii vilevile kuwashukuru sana Watendaji, Maafisa, Watumishi na Askari wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikiano mkubwa ambao wameutoa katika kufanya kazi na katika kujibu hoja zinazohusu Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wa hoja hii kwa ujumla wao walikuwa 201 na kati yao waliochangia kwa kuzungumza ni 39 na 162 wamechangia kwa maandishi. Ni wazi kwamba hata ukiamua kujibu kwa dakika moja moja tutatumia dakika 200 mara nne ya muda ulionipa. Kwa vyovyote vile tunalazimika kwenda kwenye baadhi ya hoja na kuzijibu na nyingine mtazipata katika majibu kwa njia ya Bangokitita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwatambue Wabunge waliochangia hoja hii kwa

kuanzia na waliochangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Fatuma A. Mikidadi, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Silvestry F. Koka, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Saidi M. Mtanda, Mheshimiwa Amos G. Makalla, Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mheshimiwa George H. Mkuchika, Mheshimiwa Livingstone J. Lusinde, Mheshimiwa Joshua S. Nassari, Mheshimiwa Dkt. Fenella E. Mukangara, Mheshimiwa Charles M. Kitwanga, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Jerome D. Bwanausi, Mheshimiwa Juma S. Nkamia, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes na Mheshimiwa David E. Silinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengine ni Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lucy P. Owenya, Mheshimiwa Modestus D. Kilufi, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mheshimiwa Asha M. Jecha, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Brig. Gen. Mstaafu Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Abia M. Nyabakari, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mheshimiwa Janet Z. Mbene, Mheshimiwa Ally K. Mohamed, Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Athumani R. Mfutakamba, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo na Mheshimiwa Clara D. Mwatuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Amina N. Makilagi, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Christine M. Lissu, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Angellah J. Kairuki, Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mheshimiwa Anna Marystella J. Mallac, Mheshimiwa Mwanamrisho T. Abama, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mheshimiwa Chiku A. Abwao, Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Majaliwa K. Majaliwa, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Kapt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Deo H. Filikunjombe, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa Sylvester M. Kasulumbayi, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Moza A. Saidy, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Goodluck J. Ole-Medeye, Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mheshimiwa Ritta E. Kabati na Mheshimiwa Mendrad L. Kigola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Mussa Z. Azzan, Mheshimiwa Sarah A. Msafiri, Mheshimiwa Eng. Gerson H. Lwenge, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Abdul R. Mteketa, Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Mahamoud H. Mgimwa, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba, Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa, Mheshimiwa Dkt. Titus M. Kamani, Mheshimiwa Iddi M. Azzan, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Dkt. Augustine L. Mrema, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere na Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mheshimiwa Dkt. Dalally P. Kafumu, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa Abdullah Juma Abdullah, Mheshimiwa Subira H. Mgalu, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Mch. Israel Y. Natse, Mheshimiwa Omary A. Badwel, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Naomi M. Kaihula, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mheshimiwa Katherine V. Magige, Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos Nyimbo, Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mheshimiwa Jadi Simai Jadi, Mheshimiwa Abdulsalaam S. Amer, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Omari R. Nundu, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mheshimiwa Diana

M. Chilolo, Mheshimiwa Magreth A. Mkanga, Mheshimiwa Faith M. Mitambo na Mheshimiwa Suzan A. Kimwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Cecilia D. Paresso, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mheshimiwa Joyce J. Mukya, Mheshimiwa Mansoor S. Hiran, Mheshimiwa Moses J. Machali, Mheshimiwa Esther L. Midimu, Mheshimiwa Maulida A. Komu na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Salvatory N. Machemli, Mheshimiwa Neema M. Hamid, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, Mheshimiwa Dkt. David M. Mallole, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mheshimiwa Juma S. Nkumba, Mheshimiwa Deo K. Sanga, Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Shawana Bukheti Hassan, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na Mheshimiwa John S. Magalle. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kuzungunza hapa Bungeni jumla yao ni 39 ambao ni kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mheshimiwa Juma

Othman Ali, Mheshimiwa Deo H. Filikunjombe, Mheshimiwa Alphaxard K. N. Lugola, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Zaynab M. Vullu, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mheshimiwa Iddi M. Azzan, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Sabreen H. Sungura, Mheshimiwa Joseph R. Selasini, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo na Mheshimiwa Naomi A. M. Kaihula. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Salvatory N. Machemli, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa Sylvester M. Kasulumbayi, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mheshimiwa Chiku A. Abwao, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Mch. Israel Y. Natse, Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Philipa G. Mturano, Mheshimiwa Pereira Ame Silima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwatambua Wabunge waliochangia kuhusu Wizara yangu wakati wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Rajab Mbarouk

Mohammed, Mheshimiwa Assumpter N. Mshama, Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Eng. Gerison H. Lwenge, Mheshimiwa Fatuma A. Mikidadi, Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba na Mheshimiwa Antony G. Mbassa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba yangu, sasa naomba nijielekeze katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na kujibu hoja zilizotolewa na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Nianze na kuongelea hoja kuhusu umuhimu wa kukamilika kwa Sera ya Taifa ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako kwamba, kwa kuwa jambo hili ni la Muungano, limeshajadiliwa katika Kamati ya Makatibu Wakuu na sasa limepelekwa katika Baraza la Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kupata maoni yake kabla ya kumalizia mchakato huo. Nikuhakikishie tu kwamba tutajitahidi kuwasiliana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kwamba tuweze kulimaliza jambo hili mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa ruhusa yako pia nitambue uchangiaji wa Mheshimiwa Ignus A. Malocha ambaye naye amechangia katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine ya Kamati ya Mambo ya Nje kuhusu uhamiaji, wametupa

maelekezo ya kuimarisha vituo vya mipakani, kuimarisha vitendea kazi kwa uhamiaji na kuziimarisha zaidi huduma za uhamiaji kwa kuzifanya kuwa za kisasa zaidi. Naomba kuliarifu Bunge lako kwamba tumepokwa maelekezo haya na tutayatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika eneo la Uhamiaji ilihoji kwamba iliwezekanaje wahamiaji haramu wakaweza kusafiri kutoka Kilimanjaro mpaka Dodoma bila kutambulika na kusababisha vifo vyao?

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba, kwanza tatizo la uhamiaji halitukabili peke yetu, hata nchi kubwa zinakabiliwa na tatizo hilo. Lakini sisi tuna tatizo kubwa zaidi kutokana na uwezo wetu katika kuviwezesha vyombo vyetu kufanya kazi kwa umakini zaidi. Hii inatokana na ukubwa wa mipaka yetu, lakini vilevile inasababishwa na kutokuwa na vitambulisho vya Taifa, jambo ambalo linafanya iwe vigumu sana kwa Askari wetu kutimiza wajibu wao vizuri. Tuna tatizo la Watanzania wenyewe kujishughulisha uwakala wa biashara hizi za kusafirisha watu, jambo ambalo ni baya zaidi, lakini pia tuna njia zisizo rasmi nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua uzito wa tatizo hili, Serikali imeamua kuunda kikosi kazi maalum kwa ajili ya kushughulikia jambo hili ambacho kitafanya kazi kwa karibu sana na nchi nyingine za jirani. Hivi karibuni tumeanza mazungumzo na nchi jirani, nchi ambazo wahamiaji wanatoka na zile ambazo wanakwenda. Ni kama siku tano tu zilizopita nilikuwa na mazungumza na Waziri wa Afrika Kusini anayehusika

na jambo hili na amekubali kutoa ushirikiano kwetu. Pia kikao cha *organ* ya usalama ya nchi za *SADC* ambacho kimekutana siku tatu zilizopita na Naibu Waziri alikuwa huko wamekubaliana pia kushirikiana katika jambo hili. Kwa hiyo, naomba tu Watanzania tuichukue hii kama ni vita ya pamoja na tushirikiane kulimaliza tatizo hili.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia ilisema inaona kwamba, Uhamiaji inatumika sana na Chama Tawala na mifano iliyotolewa ni ya Waheshimiwa Keissy na Wenje kusema kwamba sio raia. Kwa mujibu wa sheria, wajibu wa kwanza wa kuthibitisha wewe ni raia au sio raia ni wa kwako mwenyewe.

Kwa hiyo, pia ukiulizwa wewe ni raia au sio raia, ni fursa ambayo ni adimu ambayo Mheshimiwa Wenje na Mheshimiwa Keissy waliipata na baada ya kuthibitisha kwamba ni raia, hakuna anayeweza kuwauliza tena suala hilo. Wako pia viongozi wa CCM ambao wamewahi kuthibitika kuwa sio raia, wakaulizwa wakashindwa kuthibitisha na wakatakiwa waombe uraia, wakaomba na wakapewa. Kwa hiyo, siyo suala la Siasa za Vyama, ni suala la sheria tu, kwamba inasema nini. Wenzako wakihisi wewe sio raia, kazi yako wewe ni kuthibitisha tu. Siyo kazi kubwa, na hii inaonesha nchi yetu ina utawala wa sheria, ndiyo maana watu wamethibitisha na leo wamo humu Bungeni wanatamba kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ambazo zimetolewa na wachangiaji mbalimbali kwa maneno na maandishi yanayohusu eneo la Uhamiaji, kuna hoja

ya wageni kufanya kazi zinazoweza kufanywa na Watanzania. Nataka tu niliambie Bunge lako kwamba, tutajitahidi, tumeshakubaliana na Waziri wa Kazi na Ajira kushirikiana katika eneo hili kuona kwamba, kwa kadri inavyowezekana kazi zinazoweza kufanywa na Watanzania zifanywe na Watanzania. Lakini vilevile tutoe wito kwa Watanzania wenzetu, waajiri wengi wanapata taabu sana ya kuwaajiri Watanzania, na sababu kubwa ni mbili; kwanza, kuna utamaduni wa kutopenda kufanya kazi, jambo ambalo tusipolisemea tunapokwenda huko mbele ya safari nchi yetu itapata matatizo makubwa katika uwekezaji. Watanzania hatupendi kufanya kazi.

Leo hii mkipita kwenye korido za ofisi mbalimbali za Serikali na binafsi mtakuta mazungumzo yanayoendelea hapo mengi hayahusiana na kazi inayohusika kwenye shughuli hiyo. Watu wanaongea mambo yasiyohusika na kazi wanayoifanya, wanatumia muda mwingi kufanya mawasiliano yasiyohusika na kazi wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumeanza kuwa maarufu kwa kukosa uaminifu kuanzia ngazi ya chini mpaka juu katika uongozi wetu. Kila mahali Mtanzania anapoaminiwa, akipelekwa mahali akajenge mtaro ataiba sementi. Kwa hiyo, hata wasimamizi wa shughuli lazima kila mtu asimamie mifuko ya sementi; imeingia mingapi? Hata kama ujenzi huo unahusisha mifuko mitano ya sementi, Mtanzania lazima atafute namna ya kupiga. Sasa hamwezi kuwa na Taifa la hivyo. Lazima tufike mahali tuseme maadili yetu yamepotoka

kupita kiasi na watu wanapoteza hamu ya kutuajiri. Watanzania lazima tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya watu kutozwa fedha kwa maana ya kuwa na *Visa* za kukaa nchini na kulipishwa Sh. 100,000/= bila kupewa risiti. Ziko *Visa* ambazo zinaitwa *Peasant Visa*, hizi zinalipiwa Sh. 10,000/= na ni kwa ajili ya watu waliokaa nchini kwa muda mrefu sana. Wengine wamezaliwa hapa wamekaa miaka 60, miaka 70, lakini wanafanya shughuli zao hapa na ni wale wakulima wadogo wadogo. Sasa uko utaratibu huu, lakini zina risiti. Usipopewa risiti maana yake ni kwamba, umeibiwa wewe na Serikali pia imeibiwa. Tunaomba wanaohusika katika kutafuta *Visa* hizi wajue kwamba kutopewa risiti ni kuibiwa wewe na kuibiwa Serikali. Watusaidie kuhakikisha wao hawaibiwi na Serikali haiibiwi. Lakini vilevile yakitokea mazingira ya aina hiyo wasisite kutoa taarifa kwenye ngazi za juu ili hatua iweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuimarisha usalama kwenye Ziwa Tanganyika tumelipokea na tutalifanyia kazi. Suala la Uhamiaji kuimarisha operesheni kabla ya zoezi la sensa kwenye Mkoa wa Kigoma, tumeshaanza kulitekeleza. Nadhani mtakuwa mnasikia huko Kigoma kumetikisika kidogo, kwani unapita msako wa kutosha tu na siku za karibu hapa kule Uvinza watu 97 wamerudishwa makwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja nyingine iliyosema kwamba Idara ya Uhamiaji Wilaya ya Karagwe inatoa uraia bila kuzingatia sheria na

taratibu. Naomba tu kuliarifu Bunge lako, kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Uraia ya nchi yetu, mwenye mamlaka ya kutoa uraia ni Waziri wa Mambo ya Ndani peke yake. Kwa hiyo, madai kwamba Karagwe wanatoa uraia bila kuzingatia sheria na kanuni, kwa kweli huo siyo uraia, watakuwa wanapeana kitu kingine kwa sababu uraia anatoa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa hiyo, kama kuna taarifa za watu kupeana kitu wanachoita uraia, naomba tu tuletewe taarifa hizo ili tuzifanyie kazi kwa sababu hicho wanachopeana ni kitu tofauti kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine ambalo lilitolewa ni la kuweka Kituo cha Uhamiaji huko Kigomasha Pemba ili kukuza utalii. Naomba kuliarifu Bunge lako kwamba, kwa sasa tunategemea zaidi kituo kilichopo Wete na tungeomba Waheshimiwa Wabunge katika mazingira ya sasa watuache tu tuendelee kutumia kituo hicho.

Suala la *Passport* ni haki ya kila raia, wapewe bila kubuguziwa, na lenyewe tumelizingatia lakini tutaendelea kuzingatia vigezo muhimu ambavyo vinatuhakikishia kwamba raia wetu wanaokwenda huko nje wanakwenda kufanya shughuli halali ambazo zitawasaidia wao na Taifa, lakini pia hawaendi kuleta madhara katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Wahamiaji haramu Wilayani Ngara ambao wanaingia na mifugo yao, tunaendelea kulifanyia kazi na naomba nikiri mbele ya Bunge lako kwamba hili ni tatizo kubwa sana, la wahamiaji kuvamia katika

maeneo mbalimbali ya mipaka ya nchi yetu, kuchukua maeneo ya ardhi, kuwasukuma wenyeji pembeni na wakati mwingine kuwaletea madhara makubwa. Serikali tunalifanyia kazi jambo hili na muda siyo mrefu tutachukua hatua za kutosha za kuliondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tuhuma za mtu mmoja mmoja ambazo zilitolewa katika eneo hili la uhamiaji naomba tu kusema kwamba, tunazifanyia kazi na zile zitakazothibitika kwamba ni kweli, tutachukua hatua zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wakimbizi wa Katumba na Mishamo waliopewa uraia siku za nyuma ambao wanazidi 160,000, naomba kuliarifu Bunge lako kwamba baada ya malalamiko ya kutosha kutoka kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wabunge kuhusu utaratibu wa kuwasambaza sehemu mbalimbali katika nchi yetu wale watu waliokuwa wapewe uraia, zoezi la kuwapa uraia lilisitishwa kwa muda ili Serikali itafakari upya maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Wakuu wa Mikoa ili tufuate uamuzi ambao una tija kwa nchi yetu. Kwa hiyo, muda muafaka wa kutoa taarifa ya jambo hilo utakapofika tutatoa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipokuwa ikichambua masuala ya Jeshi la Polisi iliitaka Wizara kuangalia mkakati wa kujenga nyumba za kuishi kwa wingi za Askari Polisi. Kwa sasa mahitaji yetu ya nyumba za Jeshi la Polisi ni karibu 38,000 ili ziweze kutosha Askari wetu wote. Kwa vyovyote vile, jambo hili haliwezi kumalizika kwa siku

moja au mbili. Upo utaratibu ambao tunashirikiana na vyombo vya fedha ambavyo viko nchini, lakini siyo utaratibu ambao utatufikisha kwenye kuondoa tatizo hili. Nataka tu nitumie nafasi hii kuwahakikishia Askari wetu wote wa Polisi, Magereza na Uhamiaji kwamba kwanza nayajua vizuri maisha wanayoishi kwa sababu rafiki yangu Mheshimiwa Kangi Lugola atakuwa ni shahidi kwamba mie pia nimekulia *Line Police* wakati Kangi akiwa Askari, tulikuwa tunakaa wote huko kwenye *quarters* za *Line Police.* Kwa hiyo, na sisi ni watoto wa *line,* hivyo nayajua mazingira yanayoongelewa na Waheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachofikiria na tunalala tukiwaza, tunapataje mikopo ya masharti nafuu ya muda mrefu ya kulimaliza tatizo hili? Naamini kwa dhati kwamba muda sio mrefu tutapata majibu. Ninachoomba tu Waheshimiwa Wabunge, maana tunalo tatizo hapa, tukisema tunawaambia Waheshimiwa Wabunge jambo hili tunalifanyia kazi mwakani, tukirudi hapa watu wata-*quote* maneno yake halafu anasema Mheshimiwa Waziri uliahidi kwamba tatizo hili litakwisha. Nasema tutalifanyia kazi. Tunatafakari namna sahihi ya kulimaliza tatizo hili. Tatizo ni zito, Askari wetu wanaishi kwa shida na wanashindwa kufanya kazi katika mazingira mazuri. Lakini tunalichukua kama tatizo kubwa na la msingi ambalo linapaswa kufanyiwa kazi kwa haraka. Tutajitahidi kufanya hivyo na tutakuwa tukitoa taarifa ya mara kwa mara kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, lakini pia kwa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuzagaa kwa silaha katika nchi yetu; Jeshi la Polisi limekuwa likiendelea na misako katika maeneo mbalimbali, lakini pia limekuwa likiwaomba Watanzania kusalimisha silaha zao katika maeneo mbalimbali. Pia tumeanza zoezi la kuweka alama katika silaha zote ili tuweze kuzitambua mapema linapotokea tatizo. Nilihakikishie Bunge lako kwamba, tutajitahidi kufanya kazi kwa juhudi ili uzagaaji huu wa silaha uendelee kupunguzwa na ikiwezekana kuondoka kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kulipatia Jeshi la Polisi vitendea kazi bora zaidi, haya ni maelekezo tumeyachukua na tutayatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo swali tumeulizwa na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwamba tufanye utafiti ili kujua ni sababu gani zinazopelekea Watanzania kupenda kujichukulia sheria mikononi ikiwemo kuvamia Vituo vya Polisi, na watu wanaoitwa wenye hasira kali? Hili ni tatizo kubwa kwa sababu kwanza kwenye hili eneo linaloitwa la hasira kali ambalo nilikuwa nawaomba wenzangu wa vyombo vya habari, nadhani siku hizi tumeanza kuelewana kidogo kwamba badala ya kusema watu wenye hasira kali, wamemuua mtu, waseme watu wasiopenda kufuata sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu za mwaka 2011 peke yake watu 600 waliuawa na watu wanaojiita wenye hasira kali. Hili ni jambo ambalo kwa utawala wa sheria halikubaliki hata kidogo. Kwa mujibu wa Katiba yetu, mtu hana hatia mpaka Mahakama

itakavyosema hivyo. Mara nyingi wanaouawa wanakuwa wameonewa tu. Unakuta mwizi anakimbizwa, amekatiza Mtaa, kaingia nyumba fulani, mtu mwingine hajajua yule anakimbia kwa sababu gani, anaanza kukimbia anadakwa yeye. Hapewi nafasi ya kujitetea, anapigwa mawe mbaka anauawa. Kwa hiyo, niseme tu kwamba ni lazima tufanye kila linalowezekana ili kuwaelimisha wananchi kila mtu mahali alipo kwamba kuchukua sheria mkononi ni kunyima haki ya mwenzako na kuvunja sheria katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuvamia Vituo vya Polisi, hili nalo limeanza kukua kwanza kwa wananchi wenyewe kutojua kwamba Polisi ni wa kwao. Maana Polisi yupo, na kazi yake kuu ni ulinzi wa raia na mali zake. Sasa mtu anayelinda mali zako na kukulinda wewe mwenyewe unavamia Kituo cha Polisi, wakati mwingine unakichoma moto! Hiyo inaonyesha kwamba wewe mwenyewe una mtindio wa akili. Unashindwa kujua kwamba Polisi ni wako na zile mali za Polisi ni zako wewe katika kodi zako ndiyo umejenga Kituo kile na ndiyo unayewalipa mishahara halafu unawavamia. Jambo hili kila Mbunge, kila Kiongozi na kila mwananchi amwelimishe mwenzake kwamba hili ni tatizo kubwa, likiachwa liendelee litakuja kuleta matatizo makubwa sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niwaombe wanasiasa kwamba, pale zamani na mpaka siku za karibuni mwanasiasa ili awe maarufu, ni lazima aonyeshe kwamba yeye haogopi kitu na watu walikuwa wanaogopa Polisi. Kwa hiyo, watu wakikaa

kwenye Mkutano wa hadhara wanasema aah, nyie Polisi mko wapi? Angalieni hivyo viatu vyenu ni vibovu, angalia hili. Sasa yeye anadhani anajipa umaarufu kwa wale watu wanaomsikiliza, kumbe anadhalilisha kazi ya Polisi, anawafanya watu wawaone Polisi kwamba hawana maana bila kujitambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunasema au aliyekuwa pale Mkuu wa Wilaya anataka wajue kwamba yeye ni Mkuu wa Wilaya pale anasema *OCD* yupo wapi? Anainuka, anapiga saluti, anasema naam. Anarudia mara ya pili, *OCD* yupo wapi, anainuka tena anapiga saluti, halafu anasema mmeona, mimi ndio *OCD* hapa! Ule ni utoto, unataka kuonyesha *power* kwa namna ya kumdhalilisha mwenzako! Kwa hiyo, nasema wanasiasa lazima watumbue kwamba vyombo hivi ni vyetu, tunahitaji kuvisaidia vifanye kazi. Tuwatie moyo Polisi wafanye kazi yao vizuri, tuwasaidie wafanye kazi yao vizuri. Polisi wakitiwa moyo na kuonyeshwa kwamba wanapendwa na wanaowaongoza watafanya kazi vizuri na uhalifu utapungua au utakwisha kabisa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kulipa madeni ya Polisi tumelipokea kama maelekezo, tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye posho za Polisi. Imekuwepo dukuduku hapa kwamba Serikali iliahidi tangu mwaka 2011 kwamba posho ya Polisi ingeongezwa kutoka Sh. 100,000/= hadi Sh. 150,000/= kwa mwezi posho ya chakula na wamesema na Serikali ilifanya *commitment*. Mimi nataka niseme tu,

suala la *commitment* ya Serikali ni suala la utaratibu kwamba kwa utaratibu, posho ya Jeshi la Polisi ya Chakula inaongezwa na Kamati ya Pamoja ya Polisi na Magereza ambayo ipo chini ya Mheshimiwa Waziri. Lakini Sheria inataka mabadiliko yoyote yanayohusu fedha, Wizara ya Fedha itoe kibali. Lakini pia kibali hicho pia kipitie Ofisi ya Rais, Utumishi ndiyo iandike taarifa ya kupandishwa kwa posho hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa maana ya Wizara ikimaliza kazi yake, inaweza kusema tumefanya kazi, tunaongeza. Lakini mwisho, mwenye fedha akisema zipo, ndiyo waraka unaandikwa inakuwa shughuli ni rasmi. Kwa hiyo, wakati wa Kamati ya Pamoja ya Polisi na Magereza ilipopandisha posho zile kisheria, maana yake zilikuwa halali, lakini baada ya kupitishwa na Hazina. Mwaka 2011 Hazina hawakuwa na fedha, hivyo hawakupitisha, na mwaka huu hali kadhalika kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo siku ile nilipokutana na Viongozi wetu wa Vyuo vya Ulinzi na Usalama, nikazungumza nao. Nilizungumza na *IGP*, Mkuu wa Magereza, Mkuu wa Uhamiaji nikawaambia bajeti yetu imepungua sana. Lakini hatuwezi kudai kila kitu. Tukidai kila kitu, tutakosa. Hali ya bajeti ni mbaya, niambieni kitu kimoja tu ambacho tunaweza tukaenda tukaomba kwa Mheshimiwa Rais, tukasema Mheshimiwa Rais sisi mengine yote tunakubali, lakini tusaidie hiki kimoja, *IGP* akasema Mheshimiwa Waziri ukinisaidia Polisi wangu wakaongezewa ile posho ya chakula utakuwa umewasaidia sana na Mkuu wa Magereza akasema hivyo hivyo, na wa Uhamiaji

akasema hivyo hivyo. Nikawaambia basi niandikieni barua, wote wakaandika na mimi nikaongeza barua moja juu nikapeleka barua kwa Mheshimiwa Rais, barua nne zikaingia kwa Mheshimiwa Rais siku moja.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais akaniita nikamweleza uzito wa tatizo na kwamba tumeambiwa fedha hakuna. Mheshimiwa Rais akaita Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa likazingatia barua zile likashauri kwa Baraza la Mawaziri kwamba fedha hiyo itafutwe popote. Baraza la Mawaziri likakaa likakubaliana na hoja ya Baraza la Usalama kuwa fedha hiyo itafutwe, ndiyo matokeo ya kuipata Shilingi bilioni 28. Ndiyo uamuzi huu sasa utaanza kutekelezwa mwaka huu wa Fedha. Sasa baada ya hapo ndiyo mchakato umekamilika. Kwa hiyo, mtu akisema ilianza mwaka 2011, mchakato haukwisha. Ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge mnajua kwamba katika fedha mlizopitisha mwaka 2011, hela hizi hazikuwepo. Kwa hiyo, mkituuliza kwa kweli mnatuonea tu, hauwezi kuuliza hii hela kwa nini haukupewa wakati unajua Bungeni hukuipitisha na haikuwepo kwenye kifungu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwahakikishie tu Polisi kwamba tunatambua umuhimu wa kuendelea kuiongeza posho yao na kila tutakavyoweza tutafanya hivyo. Lakini kwa namna ya pekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kulisimamia jambo hili yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makato ya Mfuko wa Kufa na Kuzikana, ili kutunza muda, niseme

kwamba Mfuko huu ni wa hiari. Askari ambaye anadhani hataki kushirikiana katika Mfuko huu anaweza kujitoa. Ni utamaduni tu, hata Mitaani upo. Wanaanzisha Mifuko ya Kufa na Kuzikana ndiyo utamaduni wetu wa Kiafrika. Lakini jukumu la msingi la mazishi kwa maana ya sanda, usafiri na jeneza linafanywa na Jeshi la Polisi. Fedha hizo ambazo wanapeana huwa ni rambirambi tu kwa ajili ya kufarijiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la bajeti finyu ya magari ya Polisi, ni kweli bajeti ni finyu kwa sasa wastani wa lita tano kwa siku katika magari yetu na kimsingi zinatakiwa ziwe lita 15, lakini uwezo wetu wa kifedha umeishia hapo, hatuna namna ya kutoka zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuimarisha ulinzi shirikishi ni suala la msingi ambalo lazima tushirikiane kulifanyia kazi na hasa kuwahamasisha raia. Kwa sababu utafiti uliofanyika karibuni umeonyesha kwamba Watanzania asilimia 89 wanaamini kwamba ulinzi ni kazi ya Serikali. Ni asilimia 11 tu wanaamini ulinzi ni kazi ya watu wote.

Kwa hiyo, ni suala la kuendelea kuhamasisha wananchi wajue kwamba wa kwanza kabisa ni yeye mwenyewe. Halafu baada ya hapo ndiyo inafuata Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niongelee hoja ya kuwa na Jeshi dogo la kisasa kuliko kuwa na Jeshi kubwa. Niseme tu kwamba, katika majeshi madogo ya

Polisi tuliyonayo, la kwetu ni dogo sana, ukilipunguza zaidi ya hapo utaleta kiama. Maana *ration* ya Kimataifa ni Askari mmoja kuhudumia watu 450, *ration* yetu sisi kwa sasa Askari mmoja anahudumia zaidi ya watu 1,300 badala ya watu 450. Kwa hiyo, bado tupo nyuma sana katika idadi ya Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la madawa ya kulevya tutaendelea kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya. Lakini tunaomba na raia kila wanapopata fursa ya kugundua, watoe taarifa haraka inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Askari kuwabambikizia wananchi kesi za uongo ni suala baya, tutaendelea kulichukulia hatua kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ucheleweshaji wa upelelezi wa kesi na lenyewe ni jambo lisilokubalika na ndiyo maana sasa tumewaondoa Polisi katika kuendesha mashtaka ili wafanye kazi ya upelelezi. Wale wote waliokuwa waendesha mashtaka wamehamishiwa kufanya shughuli za upelelezi ili kazi iende vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwachukulia hatua Askari wanaojihusisha na rushwa tunakubaliana. Naomba niseme tu kwamba katika jambo ambalo linakera sana ni mtu kununua haki yake. Hili napenda Askari wetu wote na vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama ambavyo vipo chini ya Wizara yangu watambue kwamba katika jambo linalokera ni hilo.

Nami kama Waziri ningependa vyombo vyangu vipendwe na raia, haviwezi kupendwa na raia wakati vinakula rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema tu, wale Askari tumekubaliana na viongozi wa vyombo vyangu vya Ulinzi na Usalama kwamba wale ambao wanakula rushwa wakipatikana na hatia katika mchakato wa Kijeshi, basi watangazwe ili kwamba wenzao wajue kwamba wenzetu wameshughulikiwa kwa sababu gani? Haki ya mtu haiwezi kununuliwa. Jambo hili ni baya kuliko mambo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutumia teknolojia kudhibiti makosa ya uhalifu tunakubaliana nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira za Polisi kwamba zitangazwe kwa uwazi, tutaendelea kufanya hivyo kama tunavyofanya sasa. Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutoa gari Nungwi imekwisha kamilika karibu watapelekewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu magenge ya wavamizi wa ardhi, tutaendelea kuwachukulia hatua na tumeanza kuchukua hatua kwa waliovamia shamba la masista. *(Makofi)*

*(Hapa Kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nikiangalia saa,

nilikuwa bado nina dakika tatu. Naomba uridhie nizimalizie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimya chako kinaashiria umeridhia. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna malalamiko ya Waheshimiwa Highness Kiwia na Mheshimiwa Salvatory Machemli ya kwamba hawakupata nafasi ya kuhojiwa baada ya tukio waliloshambuliwa. Kwanza, tunawapa pole kwa yaliyowapata. Lakini pili, niseme tu kwamba shambulio lenyewe lilikuwa kubwa kidogo liliwasumbua na linaweza kusababisha kusahau rekodi zinaonyesha wote wawili walihojiwa tarehe 3 Aprili, 2012 na waliandika maelezo na kusaini. Kwa hiyo, tunawapa pole kwa yaliyowapata. Ni mazingira ya kawaida, hata mimi ningevamiwa vile vile, unaweza kusahau tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu suala la Askari wa Pemba kumshawishi msichana, naomba tu aliyeuliza swali hili anione baadaye, naomba majibu yake nisije nikaharibu saumu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu viongozi wa dini waliodhalilishwa na Polisi pale Bagamoyo kama ambavyo tulisema awali, Mkuu wa Mkoa aliombea radhi jambo hili, nami kwa niaba ya Serikali naliombea radhi sana. Ni kutokana tu na taarifa ambazo walipata Polisi wakidhani kwamba ni watu wasio na nia njema kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa muda ulionipa na baada ya maneno hayo. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Tunashukuru sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Katibu!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt.* … … … … Shs. 1,556,063,100/=

**MWENYEKITI:** Mshahara wa Waziri. Mheshimiwa Shekifu tuanze.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote* 51 *programme* 10, *Sub-vote* 1001.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge endelea moja kwa moja, mshahara wa Waziri.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nia kabisa ya kushika mshahara wa Waziri. Lakini katika mchango wangu nilizungumzia, najua Waziri amejieleza kidogo kuhusu matatizo ya nyumba za watumishi pamoja na Ofisi za Watumishi katika Jeshi la

Polisi na Magereza. Sasa Lushoto kwa kweli hali ni mbaya sana kwa sababu wanatumia magofu ya Wajerumani, Ofisi ya *OCD* ukienda kwenye eneo la Magereza kwa kweli inatisha sana. Sasa naomba angalau Mheshimiwa Waziri atoe kauli, najua ana wagonjwa wengi, lakini Lushoto ipo *intensive care*. Hebu atamke kidogo kuhusu Jeshi la Polisi Lushoto pamoja na Magereza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Shekifu kama ifuatavyo:-

Katika mazingira haya, jibu pekee la maana sana ninaloweza kulitoa ni kumhakikishia Mheshimiwa Shekifu kwamba tutalitembelea Jimbo lake tuangalie hali ya Ofisi hiyo.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza angalizo sijui kama tunatimia *quorum* humu ndani.

**MWENYEKITI:** Umeanza fujo tena. Endelea Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kupata maelezo ya Wizara kuhusu suala la Kitengo cha Kupambana na Majanga. Inaonekana kuna dhana kwamba Kitengo hiki kipo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, wakati kiuhalisia kila Mtanzania anatakiwa

afahamu jinsi ya kupambana na majanga. Lakini kitengo hiki kinaonekana kana kwamba hakipo kwa sababu hakuna Kitengo kilicho imara chenye vitendea kazi vya kutosha, na ndiyo maana tunapata ajali mbalimbali za meli na za barabarani, za moto na nyinginezo.

Sasa nataka tu kupata maelezo kutoka Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni dhana pana, wamejipanga namna gani kuhusu kuimarisha Kitengo cha Kupambana na Majanga na kuondoa ile dhana ya kwamba masuala ya majanga ni masuala ya maafa ambayo yapo Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa sababu tunadhani kwamba maafa ni kupambana na kugawa vyandarua na mablanketi tu.

Sasa kitengo hiki cha majanga tunakiimarisha namna gani na kuwaeleza Watanzania kwamba majanga siyo masuala ya Polisi tu? Ni dhana ambayo ni pana na Serikali ina mkakati gani, hata kama bajeti hii haitoshi, zitatafutwa fedha hata kama ni za kukopa ili kuimarisha kitengo hiki ili Jeshi la Polisi liweze likafanye kazi yake vizuri? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Mbatia kwa swali lake. Niseme moja ya hatua ambazo Serikali imechukua pamoja na kuchukua shughuli zote za Zimamoto kutoka kwenye Halmashauri, kuziweka chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Katika kuchukua hatua hizo, tumechukua pia hatua ya kuhakikisha kwamba mapato yote ambayo yatapatikana kutokana na tozo

au tuzo za Kikosi cha Uokoaji na Zimamoto yatachukuliwa kama *retention* na Idara ya Zimamoto ili kuijengea uwezo wa kifedha. Tukimaliza kuijengea uwezo wa kifedha, tutakuwa na nafasi ya kukiimarisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda kutumia nafasi hiyo kutoa elimu kubwa zaidi kwa umma, maana tatizo letu kubwa ni kuwa kuna mambo mengine ya uokoaji hayahitaji hata fedha yanahitaji mtu awe anajua anachotakiwa kukifanya. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbatia kwamba Mkuu wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji alimsikiliza kwa makini sana alipokuwa akielezea namna ya mambo ya uokoaji kwenye televisheni na akanihakikishia kwamba anamtafuta wakae ampe yale mambo kwa undani zaidi.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilimwandikia Mheshimiwa Waziri kuhusiana na watu ambao wanaishi nchini kinyume na sheria na tukizingatia juzi tu wameokotwa miili ya watu zaidi ya 40 wakiwa wamekufa ambao waliokuwa ni wahamiaji haramu. Sasa nilimwandikia Mheshimiwa Waziri kwa majina, watu ambao wamekuwa wakifanya kazi nchini bila ya kufuata taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya kuisaidia Wizara nilimwandikia idadi ya watu watatu, raia wa India ambao wanafanya kazi kwenye Hoteli za Kitalii kule Arusha kwenye Kampuni moja ya *Hotels and Lodges Tanzania Limited* inayomiliki Hoteli za Kitalii

ambazo zilikuwa chini ya Serikali. Hawa watu wao wanafanya kazi za kawaida tu, kazi za Ufundi na Uhasibu ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie kwa sababu tumemsaidia wale watu wanaishi nchini kwa kutumia *CTA,* hawana *permit* za kufanya kazi kwa muda ambao wamekuwepo nchini kwa zaidi ya miaka mitano. Sasa kwa maana ya kulinda uhamiaji haramu, lakini pia kwa maana ya kulinda ajira kwa ajili ya watu wetu ningeomba kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Nassari kwa hoja yake, lakini pia namshukuru kwa kusaidia kazi ya uhamiaji katika mkoa wake. Labda kwa faida tu ya Bunge lako ni kwamba taarifa alizozitoa za wale watu aliowataja ilithibitika kwamba wote walikuwa na vibali halali vya kufanya kazi nchini na mmoja kibali chake kilikuwa kimekwisha muda wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa maana ya kuhakikisha kwamba Mheshimiwa Nassari anapata *data* za maana zaidi zinazoweza kusaidia na kwa kuwa ana nia ya kusaidia kupitia kikao chako namwelekeza Mkuu wa Uhamiaji, Mkoa wa Arusha ampe ushirikiano Mheshimiwa Nassari katika kumwelimisha kuhusu namna ya kuzijua hizo *documents.*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi niliomba Serikali iangalie uwezekano wa kutupa gari la doria, Kituo cha Polisi cha Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Itigi kwenda Tabora kuna kituo kidogo cha Polisi Igalula ni karibu zaidi ya kilomita 200. Halafu ukitoka Itigi kwenda mpakani na Chunya kule kituo kingine kipo pale Mgando, Mitundu, lakini hakuna gari lolote la doria, gari la doria labda gari la Polisi, liko Manyoni. Kama unavyofahamu Wilaya ya Manyoni ni kubwa zaidi ya kilomita za mraba 18,000, unaweza ukahitaji gari kutoka Manyoni lakini gari liko Sanza. Nimeandika sana juu ya suala hili halafu Serikali inajua matukio ya ujambazi, watu wetu wamekuwa wakivuliwa nguo, mabasi yanasimamishwa wanaporwa na hakuna doria yoyote, wanasubiri mpaka tukio litokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hayo magari 30 na kitu yaliyotengwa kununuliwa mwaka huu je, itapatikana gari moja kwa ajili ya Kituo cha Itigi?

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri na nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge maswali ya sera.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Lwanji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapata taabu sana kuanza kugawa magari ndani ya ukumbi huu. Kwa

kuwa urafiki wangu na Mheshimiwa Lwanji haujakwisha anaweza kunitafuta baada ya kikao tuzungumze zaidi.

**MWENYEKITI:** Ungepata taabu maana yake hata Kongwa gari hakuna.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilisema kwamba majengo ya Polisi yaliyoko katika kituo cha Konde ni mabovu na yamefikia hatua baadhi ya maeneo kuanguka. Lakini vile vile Chuo cha Mafunzo kilichopo Wete kimefikia hatua ambapo hakistahili tena kuwapeleka watu katika sehemu ile, hata kama ni wahalifu, basi hawastahili kupelekwa katika sehemu kama ile. Lakini vile vile mnaingizwa watu kwa tuhuma ambao si wahalifu. Sasa je, Mheshimiwa Waziri atatoa maelezo gani juu ya Chuo cha Mafunzo Wete pamoja na Kituo cha Polisi Konde?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo kama ifuatavyo:-

Kuhusu swali la *infrastructure* kwa maana ya majengo ya watendaji wa Polisi. Nafikiri maelezo yaliyotolewa ni kwamba, tunakiri kuna udhaifu na kuna ubovu mkubwa na kuna mahitaji hata majengo mapya. Masuala haya tunayafanyia kazi kwa kupitia bajeti, lakini pia tumesema tunatazama uwezekano wa kupata mipango zaidi nje ya bajeti ili tuyatekeleze. Namhakikishia Mheshimiwa Kombo kama nilivyomwahidi wakati najibu swali linalofanana na hili kwamba tutakwenda kuyatembelea na ikiwezekana

tutayaweka kwenye mipango ambayo Jeshi la Polisi linayo.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri nchi yetu ni ya Mfumo wa Vyama Vingi na mojawapo ya shughuli za Mfumo wa Vyama Vingi ni Vyama vya Siasa kufanya shughuli zake za uenezi wa kivyama. Lakini kwa kipindi cha hivi karibuni kuna watu ambao ni walevi wa kiitikadi, walevi wa madaraka na kwa sababu ya ulevi wa kiitikadi na madaraja wanajikuta wanafanya vitu ambavyo ni kinyume na taratibu na kanuni zetu za uendeshaji wa shughuli za kisiasa. Hivi karibuni Jeshi la Polisi yakitokea matukio fulani wamekuwa na tabia ya kuzuia mikutano na shughuli za uenezi wa Vyama vya Kisiasa.

Kwa mfano, hivi karibuni Chama cha CHADEMA kimekuwa kikiandaa mikutano huko Morogoro, Jeshi la Polisi limezuia, ni kwa nini Jeshi la Polisi linafanya kama hivi na haya mazuio yanadumu kwa muda gani katika hii sera ya Vyama vya Siasa nchini Tanzania?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mchungaji Msigwa kama ifuatavyo:-

Kwanza Polisi madaraka yao yanatokana na sheria na kama yanatokana na sheria maana yake wanayo kila siku. Kitu kinacholevya ni unachokipata mara chache, sio wakati unacho kila siku. Kwa hiyo, kanuni tu ya kawaida kimaumbile inakataa kulewa kitu ambacho unacho muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitumie nafasi hii kusema kila mahali ambapo Jeshi la Polisi katika jukumu lake la msingi la ulinzi wa raia na mali zao itakapoona uwezekano wa kuvunjika amani linawajibika kuchukua hatua za kulinda amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo haya pamoja na kuwa yana nguvu ya kisheria nitumie kikao chako Mheshimiwa Mwenyekiti, kuliagiza Jeshi la Polisi kwamba sio tu kwa Vyama vya Upinzani hata kwa Chama cha Mapinduzi kama kuna dalili ya kuvunjika amani wasisite kuchukua hatua ya kuzuia.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Waziri maana yake badala ya mikutano inakuwa ni kusambaza matusi na kashfa.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kwa maandishi nilielezea suala zima la Kituo cha Polisi Kibiti ambacho kipo ndani ya hifadhi ya barabara na nilielezea ni namna gani wenzetu wa *TANROAD* walivyoweka vipimo vyao na wakaelekeza kwamba lile jengo libomolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kuelekeza kwamba jengo lote la Kituo cha Polisi, Kibiti libomolewe wakatoa na notisi ya miezi mitatu kwamba naomba na hawa watu wahame na jengo lile liwe limevunjwa. Lakini toka notisi hiyo ilivyotolewa na wananchi waliokuwa kwenye hifadhi ya barabara wamebomoa nyumba zao jengo hili la Kituo cha Polisi,

Kibiti *still* linaendelea kusimama pale pale, sasa wananchi wanajiuliza hivi sheria hii inamhusu nani, inawahusu raia tu Jeshi la Polisi haiwahusu au inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba maelekezo au Mheshimiwa Waziri aniambie ana mkakati gani wa kukiondoa kile Kituo cha Polisi, Kibiti wakati tayari maeneo yapo makubwa katika Kijiji cha Kibiti A na Kibiti B muweze kuchagua kujenga majengo yenu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru.

**MWENYEKITI:** Hili ni swali la siku hii?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Marombwa kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kweli kwamba kituo hicho kiko katika hifadhi ya barabara. Lakini tunaendelea kutengeneza mkakati wa kupata eneo jipya kwa ajili ya kujenga kituo kingine. Lakini nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana kwa mchango wake wa shilingi milioni mbili ili kufanikisha ujenzi wa kituo kipya katika eneo lile. Lakini kwa muda huu katika mazingira ambayo tunayo sasa ya kutokuwa na fedha za haraka za kujenga kituo kile, kituo kile kitaendelea kuwepo pale kikisaidia pia kulinda hifadhi hiyo ya barabara.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi

nataka Serikali kutoa msimamo kuhusiana na kauli ambayo imepata kutolewa na Wizara hii wakati Mheshimiwa Mapuri kwamba asilimia 70 ya wakazi wa Mkoa wa Kigoma ni Wakimbizi. Kauli ambayo ni ya kibaguzi, kauli ambayo imepelekea watu wa Mkoa wa Kigoma kujitoa kwenye makucha ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba msimamo wa Serikali kuhusu kauli hii kwa sababu mpaka sasa watu wa Uhamiaji wamekuwa wakitumia kauli hiyo kuwasumbua sana raia wa Mkoa wa Kigoma. Akiwa na mjomba Burundi anaitwa Mrundi. Akiwa na mjomba Congo anaitwa Mkongomani. Naomba *position* ya Serikali kwa sababu suala hili ni *very serious* na watu wanaumizwa sana pasipo sababu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa David Kafulila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza utakumbuka kwamba katika nchi yetu idadi ya Wakimbizi imewahi kufikia zaidi ya 1,300,000 kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, ni vizuri kuzingatia kauli ya Waziri ilipotoka ilikuwa wakati gani. Kwa sababu ni wazi kwamba imeshakuwa ni hadidu kubwa katika kijiji hicho cha Wakimbizi unaweza ukajikuta una Wakimbizi wengi zaidi kuliko raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala la wakimbizi, la wahamiaji haramu katika mikoa hii hasa Mkoa wa Kigoma limekuwa tatizo kubwa sana kwa

Serikali. Sisi kama Serikali tusingependa raia wanyanyaswe kwa namna yoyote. Lakini tuombe Serikali za Mitaa zitoe ushirikiano wa kutosha kuhakikisha kwamba, wahamiaji haramu hawajichanganyi na raia na hasa kwenye mazingira ya sasa ambapo Waziri wa Mambo ya Ndani ameshasaini hati ya kufuta hadhi ya ukimbizi kwa wakimbizi 38,000 wa Burundi ambao wamekaa tangu mwaka 1994. Watajaribu sana wengine kutoka na kujichanganya na wananchi. Tunaomba wananchi kule watusaidie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa wale Watanzania ambao kwa kweli ni Watanzania Serikali haifurahishwi hata kidogo na wao kunyanyaswa. Lakini mazingira ya Kigoma viongozi wote, Wabunge, Madiwani, Viongozi wa Vijiji watusaidie kuhakikisha eneo linakuwa salama. Hawa Wakimbizi na wahamiaji haramu wana nchi zao kwa nini wanang'ang'ania kwetu na sisi nchi yetu tunahitaji tukae sisi wenyewe tuone raha ya kupewa kipande hiki tulichopewa na Mungu.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa kuwa na Magereza nyingi nchini haipunguzi uhalifu wala haisaidii kukomesha uhalifu nchini. Kwa kuwa vile vile kuwa na askari wengi nchini haipunguzi wala haisaidii kukomesha uhalifu. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu kuanzisha *Crime Prevention Programme*, programu ambazo zimeonesha mafanikio makubwa katika nchi zingine zilizoendelea ikiwemo Marekani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Leticia Nyerere kwamba matumizi ya nguvu peke yake kama kupeleka watu Magerezani hayasaidii kupunguza uhalifu. Ndiyo maana mazingira ya sasa yanaonesha kwamba, asilimia zaidi ya 30 ya wafungwa wetu wakitoka katika Magereza wanarudia kufanya tena makosa yale yale. Kwa hiyo wazo lake ni la msingi sana. Tunalo tatizo la kuamini vifungo virefu vinasaidia ambayo kwa kweli vinaweza visisaidie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuna tatizo la kutozungumza na wakosaji. Kwa mfano, kwenye nchi hiyo anayoongelea ya Marekani wana utaratibu wa *bargain* kwamba wale mahabusu mnazungumza nao, wengine wanakuwa tayari kueleza ni kweli nilifanya na wakifanya hivyo vifungo vinapungua. Kwa hiyo, kwa namna hiyo wanapunguza wimbi kubwa la wahalifu katika nchi. Kwa hiyo, niseme tu mpango wako au maoni yako ya kuwa na *Crime Prevention Programme* tunayakubali na tutaona namna ya kuyafanyia kazi.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilipenda Serikali inifafanulie ni kwa nini kuna tofauti kubwa ya maslahi kati ya askari wa Wizara ya Ulinzi na wale askari wa Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa mfano, kwenye maslahi yao Wizara ya Ulinzi askari wanapata asilimia 42 na Mambo ya Ndani wanapata asilimia 15. Ukiingia kwenye posho ya kujikimu Wizara ya Ulinzi wanapata shilingi 300,000 kwa mwezi, wenzao wanapata shilingi 150,000 kwa mwezi, hata mishahara yao pia ipo juu na mingine iko chini. Ukiangalia

mambo yote kwa ujumla, hawa wa Mambo ya Ndani wanaonekana...

**MWENYEKITI:** Kwa *rank* ile ile au *rank* tofauti au vipi?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Wakatki CV zao ni zile zile. Kwa *rank* zile zile, lakini hawa upande mmoja wanapata kikubwa na wengine wanapata kidogo. Ni kwa nini kuna utofauti hiyo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Magdalena Sakaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza vyombo vyetu hivi vina sheria tofauti zinazoziongoza na sheria zake zinaeleza pamoja na mambo haya ya maslahi mbalimbali. Katika hizi asilimia ambazo Mheshimiwa ameziongelea nyingi katika hizo alisimamia nyongeza ile Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi alipokuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na mimi nilikuwa Naibu wake. Kwa hiyo, dhamira ya sisi sio kushindanisha, maana tatizo lingine hili naogopa sana Bunge hili likitumika kama sehemu ya kuchonganisha askari wetu. Tunataka Polisi wapate mishahara mikubwa kwa nini tuwalinganishe na Wanajeshi, hatuna sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Waziri wa Mambo ya Ndani ambacho ningependa kukiona ni kwamba, katika vyombo vyote vya ulinzi na usalama, vyombo vilivyo chini ya Wizara yangu vinapata

mishahara mikubwa zaidi na ningependa Polisi wapate mishahara mikubwa zaidi. Tutaendelea kufanya jitihada ili waweze kukidhi hali ya maisha. Maana yake tunachotaka sisi ni askari wetu kuishi maisha mazuri kutokana na kipato halali wanachopata, sio wanashindana na nani. Mashindano ni kosa kubwa sana tunaloweza kufanya na hasa tukilikubali ndani ya Bunge hili.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua dhana nzima ya kutii sheria bila shuruti, kwa sababu tumekuwa tukishuhudia Polisi wanawakamata watuhumiwa, lakini wanawapiga, wengine wanakuwa vilema, tumeshuhudia baba zetu, kaka zetu wanavunjwa mpaka korodani, wengine wanakufa. Kwa hiyo nilitaka nijue ni nini dhana ya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko inatakiwa lugha ya Kibunge. Endelea Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Hiyo lugha nimepewa na Profesa Kahigi, sasa nyingine ni mbaya zaidi. Unakuta na mwisho wa siku yaani hawa Polisi wanatumika kama ndio Mahakama, kwa hiyo, nataka nijue nini dhana nzima ya kutii sheria bila shuruti wakati watu wanaumizwa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo:-

Kwanza dhana ya utii wa sheria bila shuruti na suala la wanaotuhumiwa kwa uhalifu kuteswa havina uhusiano. Kwa sababu utii wa sheria bila shuruti maana yake kwanza wewe uzijue kwamba sheria zile zipo, ujue zipo kwa ajili yako, kwa ajili ya kukulinda wewe na mwenzako, uzitii zile Sheria na kuzifuata. Lakini suala la kwamba mtu anakamatwa na Polisi kwanza si sera ya Polisi na si sera ya Serikali na si Sheria ya Polisi kutesa watu. Kwa hiyo, mtu akiteswa na Polisi katika mazingira ya kawaida maana kuna mazingira mengine tunaita mateso ambayo Sheria inasema *defense* ya mtu yeyote yule si Polisi tu inaweza kutumika nguvu ya ziada kidogo kama unadhani unawekwa wewe hatarini.

Sasa hata Mbunge akiwa anawekwa hatarini, mmeona kule Wabunge wenzetu, mtu akishambuliwa amewekwa hatarini na chupa naye anapambana kidogo, Hapa hakukusudia kupigana lakini mwenzake kaja vibaya na mtu yeyote hata wewe Mheshimiwa Esther Matiko, mtu akija vibaya mtamwona atakavyojitetea kiufundi. Ni utaratibu wa kawaida. Kwa hiyo, nasema, hivi vitu havihusiani. Lakini kauli ya Serikali ni nini, kutesa raia si sahihi. Hii ndiyo kauli ya Serikali na utii wa Sheria bila shuruti ndiyo Sera yetu kwa sasa.

**MWENYEKITI:** Wa mwisho Mheshimiwa Alphaxard K. Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia suala la hii posho ya chakula kupewa jina la posho ya

chakula ilihali inatakiwa iitwe posho ya lishe. Pia sikubaliani na Mheshimiwa Waziri kusema kwamba hatuwezi kulinganisha majeshi haya JW pamoja na Polisi au Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya posho hizi za lishe ni ubaguzi ambao uko dhahiri na namwomba Mheshimiwa Waziri anisikilize kwa makini. Ule ukakamavu pamoja na nguvu ambazo askari hawa wanatumia wakati wa sherehe za Muungano au Uhuru gwaride lao linakuwa ni moja. Kamanda anawaamrisha wote wakiwa wamoja watoe salamu wote wanapiga nguvu sawa, viatu vinachanika kofia zinadondoka sawa, hawa hawa wanapotoa heshima ya utii kwa Amiri Jeshi Mkuu, Paredi Kamanda anasema *hima! Hima!* Wote wanaitikia Tanzania! Kwa nguvu zile zile na ni lishe ile ile. Wote wanapoambiwa wasonge mbele na kutoa heshima kwa maana ya hatua 15, wote pamoja wanakwenda hatua sawa na kupiga mguu sawa kwa nguvu zile zile. Anaposema hawa hawako sawa katika posho ya lishe, mimi simuelewi. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, naomba mazingira yao nilisema ya kuuliwa, ya kuumizwa ni yale yale. Watofautiane kwenye mishahara kwa maana ya uzoefu, *rank*, usomi. Lakini inapokuja suala la lishe ya kumtengeneza askari awe mkakamavu na afya lazima Majeshi haya yaweze kuoanishwa ili wasiwe na sera ya ubaguzi. Naomba maelezo kwa nini anawatenganisha wakati hii ni lishe?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa

kumtaja kwa jina la Afande Lugola maana alisahau ku-*declare interest*. Lakini pili, napenda kumkumbusha kwamba yeye ni askari wa akiba wa Jeshi la Polisi. Kutofautiana na mimi ni utovu wa nidhamu. (*Kicheko*)

Tatu, ni nia ya Wizara yangu kwamba, Polisi wetu wawe na mapato zaidi kuliko wengine wote na waweze kukidhi maisha yao. Kwa hiyo, nia yetu iko pale pale na naomba Polisi wajue kwamba tunawapenda sana na tuna nia ya kuona maisha yao yanabadilika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kwa sababu ya muda sasa tunaingia kwenye *guillotine*. Wabunge 11 wamepata nafasi na 23 hawajapata nafasi. Katibu.

Kif. 1002 - *Finance and Account* … Sh. 247,628,300/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … Sh. 296,355,500/=
Kif. 1004 - *Probation &Comm Serv, Div*. … … … … … Sh. 1,303,485,200/=
Kif. 1005 - *Government Comm. Unit* … … … … … … Sh. 157,117,500/=
Kif. 1006 - *Management Info System Unit* … … … … … … Sh. 114,692,600/=
Kif. 1007 - *Internal Audit Unit* … ... Sh. 136,045,900/=
Kif. 1008 - *Procurement Mngnt Unit* Sh. 205,252,300/=
Kif. 1009 - *Complaints Div.* … … ... Sh. 247,629,000/=
Kif. 1010 - *Legal Services Div* … ... Sh. 257,186,500/=
Kif. 4001 - *Refugees Unit* … … … … Sh. 488,353,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 14 –JESHI LA ZIMAMOTO

Kif. 3001 - *Fire and Rescue Service* Sh.12,867,960,000/=
Kif. 3002 - *Fire and Rescue Service Training Institution* … … … ... ... ...Sh.511,135,000/=
Kif. 3003 - *Fire Safety* … … … … Sh. 266,278,400/=
Kif. 3004 - *Operation* … … … … … Sh. 358,000,000/=
Kif. 3005 - *Dar es Salaam Regional Office* … … … … … … Sh. 163,441,000/=
Kif. 3006 - *Arusha Regional Office* … Sh. 150,250,000/=
Kif. 3007 - *Dodoma Regional Office* …Sh. 95,350,000/=
Kif. 3008 - *Mwanza Regional Office* … Sh. 129,250,000/=
Kif. 3009 - *Mbeya Regional Office* … Sh.131,400,000/=
Kif. 3010 - *Kinondoni Regional Office* Sh. 140,450,000/=
Kif. 3011 - *Mara Regional Office* … Sh. 137,650,000/=
Kif. 3012 - *Kigoma Regional Office* … Sh. 122,914,600/=
Kif. 3013 - *Pwani Regional Office* … … Sh. 97,100,000/=
Kif. 3014 - *Manyara Regional Office* …Sh. 98,520,000/=
Kif. 3015 - Geita Regional Office … Sh. 36,950,000/=
Kif. 3016 - *Temeke Regional Office* … Sh.143,600,000/=
Kif. 3017 - *Singida Regional Office* … Sh. 106,100,000/=
Kif. 3018 - *Tabora Regional Office* … Sh. 101,150,000/=
Kif. 3019 - *Iringa Regional Office* … … Sh. 113,400,000/=
Kif. 3020 - *Rukwa Regional Office* … Sh. 135,900,000/=
Kif. 3021 - *Ruvuma Regional Office* … Sh. 141,800,000/=
Kif. 3022 - *Kagera Regional Office* … Sh.132,600,000/=
Kif. 3023 - *Mtwara Regional Office* … Sh. 96,775,000/=
Kif. 3024 - *Lindi Regional Office* … … Sh.100,250,000/=
Kif. 3025 - *Njombe Regional Office* … Sh. 71,610,000/=
Kif. 3026 - *Shinyanga Regional Office* Sh. 108,850,000/=
Kif. 3027 - *Ilala Regional Office* … … Sh. 151,750,000/=
Kif. 3028 - *Kilimanjaro Regional Office* Sh. 106,450,000/=

Kif. 3029 - *Morogoro Regional Office* Sh. 110,850,000/=
Kif. 3030 - *Katavi Regional Office* … …Sh. 40,100,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 28 - JESHI LA POLISI**

Kif. 1002 - *Finance and Accounting* Sh. 1,509,775,000/=
Kif. 2001 - *Police Main force* … … Sh.105,312,577,800/=
Kif. 2002 - *Police Marine* ... … … … Sh. 1,713,896,000/=
Kif. 2003 - *Railway Police Div*. … Sh. 994,599,000/=
Kif. 2004 - *Police Signals Branch* … Sh. 4,406,855,000/=
Kif. 2005 - *Police Zanzibar* … Sh. 11,460,990,500/=
Kif. 2006 - *Police Air wing* … … Sh. 2,277,711,000/=
Kif. 2007 - *TAZARA Police* … … Sh. 1,051,015,000/=
Kif. 2008 - *Field Force Unit* … Sh. 10,401,215,200/=
Kif. 2009 - *Traffic Police* … … … Sh. 3,206,136,000/=
Kif. 2010 - *Police Airport* … … … Sh. 1,152,000,000/=
Kif. 2011 - *Police Dog and Horses* Sh. 1,300,624,000/=
Kif. 2012 - *DSM Special Zone* … Sh. 4,228,227,500/=
Kif. 2013 - *Police Ilala* … … … … Sh. 4,814,193,000/=
Kif. 2014 - *Police Kinondoni* … … Sh. 5,909,550,000/=
Kif. 2015 - *Police Temeke* … Sh. 3,756,488,000/=
Kif. 2016 - *Police Arusha* … Sh. 6,176,350,000/=
Kif. 2017 - *Police Iringa*… … … Sh.4,813,100,000/=
Kif. 2018 - *Police Kilimanjaro* … Sh. 5,779,260,000/=
Kif. 2019 - *Police Kigoma* … Sh. 4,550,012,500/=
Kif. 2020 - *Police Kagera* Sh. 5,053,362,500/=
Kif. 2021 - *Police Lindi* … … Sh. 3,511,790,000/=
Kif. 2022 - *Police Mwanza* … Sh. 6,794,612,500/=
Kif. 2023 - *Police Mara* Sh. 3,900,032,500/=

Kif. 2024 - *Police Tarime Rorya* Sh. 2,921,162,500/=
Kif. 2025 - *Police Mbeya …* Sh. 5,431,762,500/=
Kif. 2026 - *Police Mtwara …* Sh. 3,788,682,500/=
Kif. 2027 - *Police Morogoro …* Sh. 6,402,170,000/=
Kif. 2028 - *Police Manyara …* Sh. 3,700,262,500/=
Kif. 2029 - *Police Singida …* Sh. 3,935,612,500/=
Kif. 2030 - *Police Pwani … …* Sh. 4,845,362,500/=
Kif. 2031 - *Police Ruvuma …* Sh. 3,750,425,000/=
Kif. 2032 - *Police Rukwa …* Sh.3,932,512,500/=
Kif. 2033 - *Police Shinyanga … …* Sh.5,259,862,500/=
Kif. 2034 - *Police Tabora … … …* Sh. 4,119,362,500/=
Kif. 2035 - *Police Tanga … …* Sh. 5,119,062,500/=
Kif. 2036 - *Police Mjini Magharibi* Sh. 7,994,200,000/=
Kif. 2037 - *Police Kusini Unguja …* Sh. 2,447,500,000/=
Kif. 2038 - *Police Kaskazini Unguja* Sh. 2,102,150,000/=
Kif. 2039 - *Police Kusini Pemba* Sh. 2,092,600,000/=
Kif. 2040 - *Police Kaskazini Pemba* Sh. 2,346,800,000/=
Kif. 2041 - *Police Dodoma* Sh. 6,001,352,500/=
Kif. 3001 - *Police College Moshi* Sh.16,054,500,000/=
Kif. 3002 - *Police College* Sh. 1,967,650,000/=
Kif. 4001 - *Police Vehicles Maintenance Unit…* Sh. 2,942,108,000/=
Kif. 5001 - *Police Medical Unit*... Sh. 2,103,805,000/=
Kif. 6001 - *Police Building Brigade* Sh. 4,933,600,000/=
Kif. 7001 - *Criminal Investigatio Div* Sh. 22,899,937,500/=
Kif.7002 - *Stock Theft Prevention Unit* Sh. 1,106,500,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 93 – UHAMIAJI**

Kif. 2001 - Immigration Zanzibar … Sh. 4,926,210/=

Kif. 2002 - Immigration Mainland ... Sh. 51,369,467,000/=
Kif. 2003 - Regional Immigration
Office ... ... ... ... ... ... Sh. 12,641,406,000/=
Kif. 2004 - TZ Regional Imgrt Training
Acd ... ... ... ... ... ... ... Sh. 2,456,250,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 14 – JESHI LA ZIMAMOTO**

Kif. 3001 - Fire and Rescue Service ... Sh. 0/=

**FUNGU 28 – JESHI LA POLISI**

Kif. 2001 - Police Main force ... ... Sh. 3,332,250,000/=
Kif. 2002 - Police Marine ... ... ... Sh. 0/=
Kif. 2004 - Police Signals Branch ... Sh. 0/=
Kif. 2005 - Police Zanzibar ... ... Sh. 0/=
Kif. 2006 - Police Airwing ... ... ... Sh. 0/=
Kif. 2017 - Police Iringa ... ... ... ... Sh. 0/=
Kif. 2020 - Police Kagera ... ... ... Sh. 0/=
Kif. 2004 - Police Mwanza ... ... ... Sh. 0/=
Kif. 2023 - Police Mara ... ... ... ... Sh.0/=
Kif. 2041 - Police Dodoma ... ... ... Sh. 0/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 29 – JESHI LA MAGEREZA**

Kif. 1001 - *Prisons Head Quarters* … …Sh.300,000,000/=
Kif. 2002 - *Prisons Welfare and Rehabilitation*
… … … … … … … … .. .Sh. 241,000,000/=
Kif. 4001 - *Prisons Building Brigade* Sh. 400,000,000/=
Kif. 4002 - *Prisons Industries* … … Sh. 300,000,000/=
Kif. 4003 - *Prisons Farms* ... Sh. 314,500,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 51 – WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … .. Sh. 0/=
Kif. 4001 - *Refugees Unit* … Sh. 650,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 93 – UHAMIAJI**

Kif. 2002 - Immigration Mainland Sh. 10,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mheshimiwa Mtoa hoja, taarifa!

## TAARIFA

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia makadirio ya matumizi ya fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hatimaye Bajeti ya Wizara hii sasa imepitishwa rasmi na Bunge hili, tunawatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Katibu Mkuu, ndugu zetu wote viongozi wa vyombo vyote vya ulinzi na usalama ndani ya Wizara hii na askari wetu wote, tunajua kazi mnayoifanya ni kazi ngumu, ni kazi nzito na tunajua kabisa bajeti tuliyowapa ni ndogo lakini

tunaamini kabisa mtafanya kazi nzuri sana na tukikutana mwakani tutakuwa na nafasi ya kuwapongeza tena. Baada ya maelezo hayo naomba niwashukuru sana, nimwombe Katibu sasa tuendelee na kinachofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2012/2013
### Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki nitoe mwongozo kuhusiana na maombi niliyokuwa nimepata asubuhi ya leo kutoka kwa Mheshimiwa Salim na Mheshimiwa James Mbatia kwamba Wizara hii ni Wizara muhimu sana na kwa muda uliotengewa na Kamati ya Uongozi ya Bunge ni muda mdogo. Ili kuitendea haki walitoa maoni na ushauri kwamba, ni vizuri tukaangalia namna ya kuongeza muda kidogo kwa ajili ya kuiangalia vizuri zaidi Wizara hii.

Jambo hili ni jema, nimewasiliana na Mheshimiwa Spika, Anne Makinda na kama mtaafiki kwamba tuendelee leo tuimalizie kesho asubuhi. Lakini kama mnavyojua tutaanza saa tatu moja kwa moja hakuna maswali na ndani ya masaa mawili tuwe tumemaliza mambo yote yanayohusu Wizara hiyo. *(Makofi)*

Ahsanteni sana na makofi haya yanaashiria kwamba mnaafiki na kwa jinsi hiyo sitarajii tena mtu atasimama aseme habari ya *column*. Nitawaomba

Waheshimiwa Wabunge kesho saa tatu tujitahidi, tufike mara moja tuweze kuimalizia Wizara hii ili tuweze kuitendea haki.

Sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Samwel Sitta.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaisoma hotuba yangu naomba uniruhusu nitoe matangazo machache ya utendaji. Kila Mheshimiwa Mbunge kwa hotuba hii atapata vijitabu vitano, kwa hiyo msishangae. Hotuba kwa Kiswahili, Hotuba kwa Kingereza, maswali yanayoulizwa kuhusu Jumuiya na majibu yake, Mtengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mifumo, Taratibu na Misingi na hatua za mtengamano hadi sasa na mwisho taarifa muhimu kuhusu Mtengamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mtapewa vitabu vitano na naomba wahudumu wasisahau kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Afrika Mashariki wapo pale kwenye *Gallery* wawafikishie kama wanavyowafikishia humu ukumbini pamoja na Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya Ndugu Rodrich ambaye yupo juu pale. Mwisho ni kwamba, kwa sababu nitakayoisoma ni Hotuba kwa muhtasari naomba *Hansard* watambue kwamba hotuba yenyewe kwa ukamilifu ni kile kitabu ambacho nitaomba yote yaingie katika *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama,

iliyowasilishwa hapa Bungeni kuhusu Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Taifa limekumbwa na simanzi kubwa kufuatia ajali ya kuzama kwa meli ya *MV. Skagit* iliyotokea karibu na Kisiwa cha Chumbe, Visiwani Zanzibar. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wote kwa ujumla kutoa salamu za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa abiria wote waliopoteza maisha kufuatia ajali hiyo. Aidha, tunamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki majeruhi wa ajali hiyo ili wapone haraka. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012 Bunge lako Tukufu limefanya uchaguzi wa Wabunge wanaoiwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Napenda kuchukua fursa hii kulipongeza Bunge lako Tukufu kwa kuendesha uchaguzi huo kwa mafanikio makubwa. Aidha, nawapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wabunge hao wapya wa *EALA* ambao ni Mheshimiwa Abdulah Alli Hassan Mwinyi; Mheshimiwa Alhaji Adam Kimbisa; Mheshimiwa Angela Charles Kizigha; Mheshimiwa Bernard Musomi Murunya; Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere; Mheshimiwa Nderkindo Perpetua Kessy; Mheshimiwa Maryam Ussi Yahaya; Mheshimiwa Shy-Rose Banji na Mheshimiwa Dkt. Twaha Issa Taslima. Sisi Wabunge tunaamini kuwa

wataiwakilisha nchi ipasavyo katika Bunge la Afrika Mashariki huku wakizingatia na kusimamia maslahi ya Taifa letu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi na ofisi yako kwa ushirikiano mkubwa katika maandalizi ya mfumo na Hadidu za Rejea za Utendaji na Uwajibikaji wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa Bunge la Tanzania. Mfumo huo utawezesha Bunge letu kupata taarifa za mara kwa mara kuhusu uendelezaji wa Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na utendaji wa Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Aidha, nakushukuru kwa kuwezesha na kushiriki katika Semina Elekezi ya Wabunge wapya wa Bunge la Afrika Mashariki iliyofanyika Kunduchi, Dar es Salaam tarehe 23 – 24 Mei, 2012. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushiriki na michango yao muhimu kwenye semina hiyo. Nawashukuru pia Wataalam toka Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Dkt. Stergomena L. Tax na Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah kwa maandalizi yenye kiwango ya semina. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki waliomaliza muda wao nawapongeza kwa kazi kubwa waliyofanya katika Bunge la Pili la Afrika Mashariki. Nawatakia kila la kheri katika majukumu yao mapya. Nampongeza Mheshimiwa Margaret N. Zziwa, Mbunge kutoka Uganda, ambaye

amechaguliwa kuwa Spika mpya wa Bunge la Afrika Mashariki na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza kuliongoza Bunge la Afrika Mashariki. Aidha, kupitia Bunge lako Tukufu namshukuru na kumtakia mafanikio na maisha ya ustaafu aliyekuwa Naibu Spika, Mheshimiwa Abdi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kupokea, kuchambua na kutoa ushauri muhimu katika maandalizi ya Makadirio ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2012/2013. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu imezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandalizi ya hotuba hii, Wizara imezingatia maudhui ya Hotuba kwa mwaka 2012/2013 aliyoitoa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Bunge lako Tukufu. Aidha, Hotuba hii imezingatia Taarifa ya Hali ya Uchumi iliyotolewa na Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, na Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2012/2013 iliyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Waziri wa Fedha. Nawashukuru viongozi hao kwa hotuba zao nzuri zilizoweka mwelekeo wa shughuli za Serikali na Dira ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, sina budi kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Abdullah J. Abdullah, Naibu Waziri; Dkt.

Stergomena L. Tax, Katibu Mkuu; Ndugu Uledi A. Mussa, Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na Watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaonipa. Nawapongeza sana kwa kuitikia kwa vitendo wito wangu wa kazi kwa viwango, kasi, uadilifu na kwa uzalendo wao katika kutekeleza kazi za umma. Wizara yangu ina umoja na ina watu wanaojituma isivyo kawaida. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho katika utangulizi, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha Hotuba hii kwa umakini na ndani ya muda. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo na mipango 2011/2012, majukumu yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 ni pamoja na:-

(a) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano;

(b) Kukamilisha Mkakati wa Kitaifa na Mpango wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja;

(c) Kuongoza na kuratibu majadiliano ya Uanzishwaji wa Umoja wa Fedha;

(d) Kuratibu na kukamilisha zoezi la kuwianisha sheria, kanuni na taratibu zilizopo nchini ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja;

(e) Kuratibu Uendelezaji wa Miundombinu ya Kiuchumi na Kijamii katika Afrika Mashariki;

(f) Kuratibu utekelezaji wa Programu za kisekta za kiuchumi, kijamii na za kiuzalishaji;

(g) Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya Itifaki na Sheria mbalimbali za Jumuiya;

(h) Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya Ubia wa Kiuchumi baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya;

(i) Kuratibu na kuongoza majadiliano ya Utatu wa Jumuiya za *COMESA-EAC-SADC*;

(j) Kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu mtangamano wa Afrika Mashariki;

(k) Kukamilisha uchambuzi wa changamoto za uanzishwaji wa Shirikisho la Kisiasa;

(l) Kuratibu na kushiriki katika masuala ya siasa na utawala bora;

(m) Kuratibu utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Amani na Usalama; na

(n) Kujenga uwezo wa Wizara kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2011/12 ulizingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011 – 2015), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini

Tanzania (MKUKUTA II), Kilimo Kwanza, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (2010 – 2015), Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake, Mpango wa Maendeleo wa Jumuiya, na Maamuzi ya Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama na ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Dira, Sera na Mipango ya Kitaifa niliyoainisha hapa, kwa makusudi kabisa pia tumeweka Dira na Dhima ya Wizara katika Hotuba hii. Tumefanya hivyo kwa sababu tunaamini kuwa wananchi waliotutuma katika Bunge hili hawatatuamini iwapo tutakosa Dira na Dhima. Mwandishi na Mwanazuoni mashuhuri Barani Afrika, Marehemu Frantz Fannon, alibainisha kama ifuatavyo kuhusu hili:-

*“Each generation must, out of relative obscurity discover its mission and fufill it.”*

Yaani kila kizazi sharti kibainishe Dhima yake na kuitimiza. Tukiweza kutekeleza majukumu yetu, kwa viwango na kasi tutaweza kutimiza Dhima ya Taifa na ya Wizara hii.

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alituasa kuwa *“Play your Part it can be Done”.*

Hivyo sote tushirikiane katika kuijenga Jumuiya ya Afrika Mashariki yenye tija na manufaa kwa Watanzania, inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara ilitengewa jumla ya Sh. 17,447,397,654. Kati ya fedha hizo, Sh. 1,154,756,354 ilikuwa kwa ajili ya mishahara na kiasi cha Sh. 16,292,641,300 Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, mchango wa Tanzania katika Jumuiya ulikuwa Sh. 11,016,151,636. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012, Wizara ilikwishapokea kiasi cha sh. 17,446,428,648.00 (asilimia 99%).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sera na mkakati; maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano. Nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara imekamilisha Rasimu ya Sera ya Taifa ya Mtangamano *(National Policy on Regional Integration).* Wizara imewasilisha Sera hii Serikalini ili iweze kuidhinishwa. Aidha, katika mwaka 2011/2012 Wizara iliratibu na kushiriki katika kukamilisha Mkakati wa Nne wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(4th EAC Development Strategy 2011/12 – 2015/16).* Maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Mkakati huo ni utekelezaji wenye manufaa wa Itifaki ya Soko la Pamoja; Uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha; na ushirikishwaji stahiki wa sekta binafsi na asasi za kiraia katika mtangamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja ili kufanikisha utekelezaji wa Soko la Pamoja; katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja. Mkakati huo umeainisha fursa zitokanazo na Soko la

Pamoja, uwezo wa Tanzania katika kulitumia Soko la Pamoja na changamoto zinazoikabili Tanzania katika kunufaika na fursa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kunufaika na Soko la Pamoja, Mkakati umeainisha maeneo muhimu yatakayotiliwa mkazo katika ufunguaji wa masoko ya biashara ya bidhaa na huduma, ajira, mitaji na fursa nyinginezo zilizokubalika katika Itifaki ya Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyobainishwa katika mkakati ni pamoja na:-

(a) Soko Huru la Bidhaa; maeneo ya kimkakati ni uendelezaji wa Kilimo, Viwanda vya Kusindika Mazao ya Kilimo, upanuzi na Uboreshaji wa Miundombinu inayoiunganisha Tanzania na Nchi Wanachama na pia nchi za Afrika ya Kati na Kusini. Miundombinu hiyo ni pamoja na Barabara, Reli, Bandari na Umeme;

(b) Soko Huru la Huduma; mkazo umewekwa katika kuendeleza miundombinu ya TEHAMA, kukuza taaluma ya sekta ya utalii nchini na sheria za haki miliki;

(c) Soko Huru la Ajira; ili kuwezesha Watanzania kushindana katika Soko la Ajira, Mkakati unatilia mkazo katika kuinua ubora wa elimu, ujuzi, na weledi wa nguvu kazi, hususan katika maeneo yaliyofunguliwa, na kuweka mfumo wa kuzitangaza nafasi za ajira zilizopo Afrika Mashariki;

(d) Soko Huru la Mitaji; Soko la Mitaji la Tanzania bado ni changa. Hivyo, Mkakati unatilia mkazo urekebishaji wa sheria za mitaji kuruhusu wananchi kushiriki katika soko hilo kikamilifu, kukuza soko la mitaji na upatikanaji wa mikopo kutoka taasisi za fedha; na

(e) Haki ya Kuanzisha Shughuli za Kiuchumi: Katika eneo hili, Mkakati unatilia mkazo katika kurahisisha sheria na taratibu za kuanzisha biashara na kuvutia wawekezaji makini na kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati huu unalenga kuratibu na kuchochea programu na mipango ya kisekta itakayochangia katika upatikanaji wa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii kwa kuwawezesha Watanzania kuzitumia fursa za Soko la Pamoja na kunufaika na mtangamano wa Afrika Mashariki kwa jumla. Aidha, Mkakati umeainisha majukumu ya wadau katika utekelezaji wa Soko la Pamoja. Wizara ipo katika hatua za mwisho za kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini utakaotumika kupima utekelezaji wa Soko la Pamoja Kitaifa, ikiwa ni sehemu ya Mkakati wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na taratibu zilizowekwa Mkakati huu unatarajiwa kuidhinishwa na Serikali katika mwaka wa fedha 2012/13 ili kuanza utekelezaji. Natoa wito kwa Wizara za kisekta kuandaa mipango ya utekelezaji ya kisekta ili kuwezesha utekelezaji kamilifu wenye manufaa kwa Taifa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki maendeleo ya viwanda katika Jumuiya ni suala lililopewa kipaumbele katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ibara ya 80 (1) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, imeelekeza Nchi Wanachama kubuni Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa Jumuiya ili kukuza uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Mkakati wa kuendeleza Viwanda wa Jumuiya vimekamilika na kupitishwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya mwezi Novemba, 2011. Nchi Wanachama zinaendelea na utekelezaji wa Sera na Mkakati huo ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hadidu za Rejea kwa ajili ya kufanya uchambuzi na utafiti katika uendelezaji Viwanda, Teknolojia na Uvumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuendeleza viwanda, Jumuiya kwa kushirikiana na *UNIDO*, kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Viwanda katika Jumuiya *(EAC-UNIDO Industrial Upgrading and Modernization Programme)*, imeandaa mpango kazi wenye lengo la kuboresha viwanda ili viwe vya kisasa zaidi kuendana na mahitaji ya bidhaa na maendeleo ya teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Mikakati kuhusu Jinsia na Maendeleo ya Jamii katika mwaka 2011/2012, Wizara iliratibu na kushiriki katika kukamilisha

majadiliano ya Rasimu ya Sera ya Watu wenye Mahitaji Maalum ya Jumuiya *(EAC Policy on Persons with Disabilities)*. Lengo la Sera hiyo ni kuwawezesha watu wenye mahitaji maalum kushiriki katika masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano ya maandalizi ya Sera ya Vijana. Majadiliano hayo yanatarajiwa kukamilika katika mwaka 2012/2013. Vile vile, Wizara imeratibu na kushiriki katika maandalizi ya Sera ya Watoto, Sera ya Jinsia, na Sera ya Hifadhi na Ustawi wa Jamii *(EAC Social Protection and Social Welfare Policy)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la Sera hizi ni kuhakikisha kuwa makundi yote ya watu katika Jamii yananufaika na Jumuiya na hatimaye kuleta maendeleo ya Jamii. Aidha, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliratibu na kushiriki pia katika maandalizi ya Mwongozo wa Maendeleo ya Jamii katika Jumuiya *(EAC Social Development Framework)*. Mfumo huo utakapokamilika, utatoa mwongozo wa jinsi ya kuhuisha na kuboresha masuala ya Maendeleo ya Jamii katika Jumuiya. Shughuli hizi zinatarajiwa kukamilishwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Mikakati hii ni muhimu katika kutumia kikamilifu fursa za kiuchumi, kijamii na kisiasa na pia kukabiliana na changamoto zilizopo na zitakazojitokeza. Rais wa zamani wa Marekani, John F. Kennedy, katika muktadha huu alinema kama ifuatavyo na ninanukuu: *“Change is the*

*law of life. And those who look only to the past or the present are certain to miss the future."*

Mabadiliko ni sheria katika maisha. Wale wanaozingatia tu yaliyopita na yaliyopo kuna hatari wakashindwa kubaini yajayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Hatua za Mtangamano, katika karne ya sasa ambapo uchumi wa Dunia unaongozwa na ushindani kutokana na mfumo wa utandawazi unaoigeuza Dunia kuwa kama Kijiji, ushiriki kwenye Jumuiya za Kikanda ni hatua isiyoepukika katika kujenga uwezo wa kukabiliana na changamoto za uchumi, jamii, teknolojia na za siasa zitokanazo na utandawazi. Hivyo, Taifa lolote lile linalopuuza ushirikiano wa Kikanda linajiandaa kushindwa katika kujitafutia maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Umoja wa Forodha; Kifungu cha 49(c) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, kinaitaka Serikali kujenga mifumo imara ya viwanda, biashara na masoko yenye kuendeleza na kukuza mauzo nje. Katika kutekeleza Kifungu hiki, Wizara katika mwaka 2011/2012, imeendelea kuratibu utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao umeendelea kuwa na mafanikio makubwa katika kukuza mauzo ya bidhaa katika Nchi za Jumuiya, na hivyo kuongeza ajira, uwekezaji na uzalishaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauzo ya Tanzania katika soko la Jumuiya yameendelea kuongezeka

mwaka hadi mwaka. Katika kipindi cha mwaka 2010, mauzo yaliongezeka hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 462.7 kutoka Dola za Kimarekani milioni 285.0 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 62.3. Hata hivyo, takwimu za awali za mwaka 2011 zinaonesha kuwa mauzo ya Tanzania katika Jumuiya yameshuka kidogo na kufikia Dola za Kimarekani milioni 409.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa zilizouzwa kwa wingi katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni mbolea, saruji, mchele, chuma, samaki, ngano, sukari na nguo. Grafu Na. 1 hapa chini inaonesha mwenendo wa mauzo ya Nchi Wanachama.

**Grafu Na. 1: Mauzo Baina ya Nchi za Jumuiya Katika Milioni za Dola za Marekani**

Kimar Chanzo *EAC Trade Report* 2011

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya imeendelea kuwa soko kuu la bidhaa za Tanzania, ikiwa inachukua asilimia 60.17 ya mauzo yote ya bidhaa za Tanzania katika Jumuiya. Aidha Kenya imeendelea kuchukua sehemu kubwa ya soko la bidhaa toka Nchi Wanachama ikichukua asilimia 60 ya soko*(market share)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa zilizouzwa kwa wingi kutoka Tanzania kwenda Kenya ni pamoja na vyandarua, bidhaa za plastiki, chai, transfoma, karatasi na bidhaa za karatasi. Tufe Na. 1 hapa chini linaonesha uwiano wa mauzo baina ya Nchi Wanachama katika mwaka 2011.

**Tufe Na. 1: Uwiano wa Mauzo ya Nchi Wanachama Katika Soko la Jumuiya katika Mwaka 2011**

Chanzo EAC Trade Report 2011

Mheshimiwa Naibu Spika, thamani ya manunuzi ya Tanzania kwa bidhaa kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ilishuka kwa asilimia 7.1 mwaka 2010, kutoka Dola za Kimarekani Milioni 316.9 mwaka 2009 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 295.9 mwaka 2010. Takwimu za awali za mwaka 2011, zinaonesha kuwa manunuzi yatapanda tena kufikia Dola za Kimarekani milioni 378.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanda kwa manunuzi kunatokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa kutoka Nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo uagizaji wa bidhaa kutoka Uganda umeongezeka kwa zaidi ya mara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa ambazo Tanzania inaagiza kwa wingi kutoka Uganda ni pamoja na vifaa vya umeme, viatu na sabuni. Bidhaa nyingine zilizoagizwa kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ni pamoja na dawa, chuma na bidhaa za chuma, mafuta, magari ya mizigo na matela ya mizigo.

Grafu Na. 2 hapa chini inaonesha mwenendo wa mauzo ya Tanzania katika Nchi Wanachama. Aidha, Tufe Na. 2 hapa chini linaonesha uwiano wa manunuzi baina ya Nchi Wanachama katika mwaka 2011.

Grafu Na. 2: Manunuzi Baina ya Nchi za Jumuiya Katika Milioni za Dola za Kimarekani

Chanzo EAC Trade Report 2011

**Tufe Na. 2: Uwiano wa Manunuzi ya Nchi Wanachama Katika Soko la Jumuiya katika Mwaka 2011**

Chanzo *EAC Trade Report* 2011

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa thamani ya biashara miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mwaka 2010 thamani ya biashara ya bidhaa miongoni mwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliendelea kuongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 3,437.3 mwaka 2009 hadi kufikia Dola za Kimarekeani milioni 3,800.7 mwaka 2010, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za awali za mwaka 2011 pia zinaonesha kutakuwa na ongezeko zaidi la biashara ya bidhaa miongoni mwa Nchi Wanachama itakayofikia takribani Dola za Marekani millioni 4,485.9, ikiwa ni ongezeko la asilimia 18 ikilinganishwa na ongezeko la mwaka 2010. Katika kipindi hicho, Tanzania imeweza kuongeza biashara yake ya bidhaa katika Jumuiya kwa asilimia 26.0 mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya imeendelea kuongoza katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuchukua mgao wa soko (market share) mkubwa zaidi, ikifuatiwa na Tanzania, Uganda, Rwanda na

Burundi. Aidha kwa upande wa manunuzi, Nchi ya Uganda ndiyo inaongoza kwa kununua bidhaa zinazozalishwa ndani ya Jumuiya ikifuatiwa na Tanzania, Kenya, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Grafu Na. 3 na Tufe Na. 3 hapa chini, zinaonesha jinsi Nchi ya Kenya imeendelea kuongoza katika soko la Afrika Mashariki, ambapo mwaka 2011 Kenya imechukua wastani wa asilimia 41 ya biashara yote ndani ya Jumuiya, ikifuatiwa na Uganda asilimia 27, Tanzania asilimia 18, Rwanda asilimia 11 na Burundi asilimia 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, natoa wito kwa Watanzania kujipanga na kuzichangamkia fursa za kibiashara zilizopo katika Jumuiya ili kuongeza mgao wa soko *(market share)* wa Tanzania katika soko la Jumuiya.

**Grafu Na.3: Mgao wa Soko (Market Share) Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (Milioni za Dola za Kimarekani)**

*Chanzo EAC Trade Report 2011*

**Tufe Na.3: Mgao wa Soko (Market Share) Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki Katika Mwaka 2010**

Chanzo *EAC Trade Report* 2011

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mgao mdogo wa soko ilionao nchi yetu katika Jumuiya, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa urari wa

biashara yetu katika Jumuiya umeimarika kutoka nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 31.9, mwaka 2009 na kufikia urari chanya wa Dola za Kimarekani milioni 166.8 katika mwaka 2010. Hivyo, mbali na mwaka 2009 ambapo biashara ya Tanzania ilishuka kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani, biashara imeendelea kupanda kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo ikiwa na urari chanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa Uwekezaji; utekelezaji wa Umoja wa Forodha umeendelea kuchangia katika jitihada za Serikali za kuvutia na kukuza uwekezaji. Idadi na thamani ya miradi inayowekezwa Tanzania na wawekezaji toka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2011, miradi mipya 21 iliwekezwa ikiwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 58.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011, sekta zilizoongoza nchini katika uwekezaji toka Nchi Wanachama za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Viwanda, Ujenzi, Utalii, Usafirishaji na Kilimo. Hali hii inaonesha kuwa sekta za viwandani na huduma inaendelea kukua kwa kasi nzuri kutokana na utekelezaji wa Umoja wa Forodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko la uwekezaji baina ya Nchi Wanachama, nafasi za ajira zitokanazo na uwekezaji huo zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2011, ajira mpya zilikuwa 1,668, ikilinganishwa na ajira 1,575 kwa mwaka 2010 kama inavyoonekana katika Tufe Na. 4. Sekta

zilizoongoza katika kuongeza nafasi za ajira ni pamoja na uzalishaji viwandani, kilimo, usafirishaji, utalii na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uanzishwaji wa Himaya Moja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika Hotuba yangu ya mwaka 2011/2012, nilieleza kuhusu majadiliano ya kuimarisha Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki ili kuunda Himaya Moja ya Forodha (*Single Customs Territory*). Aidha, nilieleza kuwa Wakuu wa Nchi Wanachama waliliagiza Baraza la Mawaziri la Jumuiya kufanya uchambuzi wa kina kuhusu suala hili na kuwasilisha mapendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi huo umekamilika na mapendekezo kuwasilishwa katika Mkutano Maalum wa 11 wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya uliofanyika mwezi Aprili, 2012 mjini Arusha. Katika Mkutano huo, Viongozi Wakuu wa Jumuiya waliridhia mfumo wa kila Nchi Mwanachama kusimamia shughuli za kiforodha na kukusanya mapato yake *(destination model).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mfumo huu, imekubalika kuwa bidhaa zinazopitia nchi moja kuelekea nchi nyingine mwanachama *(transit goods)*, zitakaguliwa na kodi itakusanywa katika kituo cha forodha cha kwanza bidhaa inapoingia katika Jumuiya. Baada ya ukaguzi huo, mapato ya kodi hiyo yatapelekwa kwa nchi husika baada ya kuthibitisha kuwa mzigo umevuka mpaka. Baraza la Mawaziri la Jumuiya limeunda Kikosi Kazi kitakachoandaa utaratibu wa utekelezaji wa mfumo uliokubalika. Kazi hii

inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha. katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu imeendelea kuratibu na kushiriki katika utekelezaji wa Mpango Maalum wa Kikanda wa Kushughulikia Vikwazo Visivyo vya Kiforodha. Katika kipindi hicho kati ya vikwazo 50 vilivyobainishwa, 27 viliweza kuondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa vikwazo vilivyoondolewa ni: Tozo kwa magari yaingiapo nchi nyingine mwanachama, malipo ya zuio la kuuza nje chakula na mbegu, vikwazo vya uuzaji wa konyagi; ushuru kwenye madawa; upatikanaji wa cheti cha uasili wa bidhaa mipakani na kutambulika kwa vyeti vya viwango vya ubora vinavyotolewa na Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizi za kupunguza Vikwazo Visivyo vya Kiforodha, katika mwaka 2011/12 vikwazo vingine vipya 16 vimebainishwa. Vikwazo vipya ni pamoja na:-

Kupunguzwa kwa muda wa msamaha kwa bidhaa kukaa bandarini kabla ya kuanza kutozwa gharama za kuhifadhiwa bandarini, msongamano wa mizigo bandarini; kutofautiana kwa viwango vya tozo kwa watumiaji barabara wanapozidisha uzito miongoni mwa Nchi Wanachama; upimaji uzito wa malori yasiyo na mizigo na hivyo kuwapotezea muda wasafirishaji; mlolongo mrefu wa taratibu katika kupata dhamana

kwa mizigo inayopita kuelekea nchi nyingine; kuzuia maua yanayosafirishwa kwenda Ulaya kupitia nchini jirani na tozo kwa bidhaa za kilimo zinapouzwa ndani ya Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi, 2012, uliitishwa Mkutano Maalum wa Mawaziri Mjini Mombasa, Kenya, kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa Mpango Maalum wa Uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha katika Jumuiya. Katika Mkutano huo, Nchi Wanachama zilikubaliana kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha vilivyobainishwa na pia kukamilisha utafiti wa mfumo wa kisheria wa kusimamia uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha ili kuweza kupata suluhisho la kudumu. Napenda kuchukua fursa hii kuziomba mamlaka za kisekta zinazohusika katika mchakato huu kuchukua hatua za haraka kuondoa vikwazo vilivyobainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine iliyochukuliwa kupambana na vikwazo visivyo vya kiforodha ni uanzishaji wa Vituo vya Utoaji Huduma kwa Pamoja Mipakani (*One Stop Boader Posts - OSBPs).* Lengo la kuanzishwa vituo hivyo ni kuondoa urasimu usio wa lazima katika huduma za kiforodha; uhamiaji; udhibiti wa ubora, viwango na usalama wa bidhaa na usalama kwa jumla. Aidha, hatua hii itapunguza muda unaotumika kukamilisha taratibu za kuvuka katika vituo vya mpakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi Wanachama zinaendelea kujenga Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani katika mipaka ya Tanzania na Nchi

Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ifuatavyo:-

(a) Rusumo/Rusumo (Tanzania na Rwanda);

(b) Namanga/Namanga (Tanzania na Kenya);

(c) Sirari/Isebania (Tanzania na Kenya);

(d) Holili/Taveta (Tanzania na Kenya);

(e) Horohoro/Lungalunga (Tanzania na Kenya);

(f) Mutukula/Mutukula (Tanzania na Uganda); na

(g) Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi).

Ujenzi wa vituo hivyo umekwishaanza na upo katika hatua mbali mbali za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta zenye dhamana ya usimamizi wa masuala yatakayoshughulikiwa katika Vituo vya Pamoja vya Mipakani (ushuru wa forodha, uhamiaji, ubora na usalama wa bidhaa, usalama, usafirishaji wa bidhaa na usafiri) imeunda Kamati ya Kitaifa ya Wataalam ya Usimamizi wa Vituo vya Utoaji huduma kwa Pamoja Mipakani. Kamati hii imepewa jukumu la kufuatilia uanzishaji wa vituo hivi na utekelezaji wa majukumu husika katika vituo hivi na kutoa mapendekezo katika Kamati ya Makatibu Wakuu ili kuwezesha utekelezaji wa haraka na wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika kufuatilia suala la Karafuu na vikwazo vingine vya kibiashara kwa Zanzibar, ilifanya ziara nchini Kenya, hususan Mombasa na Shimoni, kuanzia tarehe 18 hadi 20 Oktoba, 2011. Madhumuni ya ziara hiyo yalikuwa ni kutimiza ahadi ya Waziri kushughulikia changamoto za biashara ya Karafuu na udhibiti wake; tuhuma kuhusu kunyanyaswa kwa wasafiri na wakaazi kutoka Zanzibar waingiapo Kenya kupitia kituo cha Shimoni; Uvuvi haramu katika Mkondo wa Pemba (Pemba *Channel*); na Gharama kubwa za Vibali vya Kufanya Kazi nchini Kenya *(Work Permits)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara hiyo, Viongozi wa Tanzania na Kenya walikubaliana kushughulikia changamoto hizi kwa pamoja kwa kufanya vikao vya mara kwa mara kati yao, kufanya utafiti ili kubaini utaratibu ambao kwao wafanyabiashara toka Kenya na wakulima wa Karafuu watakuwa na bei mahsusi ya kununulia Karafuu Zanzibar; Kituo cha Uhamiaji cha Shimoni kufanya kazi kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni na baada ya saa hizo wasafiri watumie simu namba +254722494948 kupata huduma za uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, pamoja na juhudi hizo za kikanda kumekuwa na juhudi za Kitaifa ambapo harakati zenye maudhui *WIPO/BRELA BRAND MISSION TO TANZANIA* imezinduliwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania, Serikali ya Marekani na Shirika la Kimataifa la Hati Miliki *World Intellectual Property Organization* - *(WIPO)*. Hatua hii itapelekea kusajiliwa

kwa zao la karafuu kwa kutumia sheria za "Hakimiliki za Maliubunifu" kwa kutumia *Geographical Indications* za zao hilo nyeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii itafanyika kwa mujibu wa kanuni zinazotambuliwa na Shirika la Maliubunifu Ulimwenguni *(World Intellectual Property Right Organization)* na itakuwa mwarubaini wa tatizo la magendo ya zao la Karafuu. Ni matumaini yangu kuwa juhudi hizi zitapunguza kwa kiwango kikubwa changamoto ambazo zimekuwepo kwa kipindi kirefu na zitaleta matunda ya kuitambulisha Karafuu kama *Zanzibar spice* na kuzingatia uhalisia na utamaduni wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha ujirani mwema na kukabiliana na changamoto za kibiashara mipakani mwa Nchi Wanachama, Wizara yangu imewasilisha ombi maalum katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kutaka kuwepo kwa Mikutano ya pande mbili ya majadiliano, hususan baina ya Tanzania na Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa masuala yaliyowasilishwa ili kupatiwa ufumbuzi kwa utaratibu huu ni pamoja na suala la biashara ya magendo ya Karafuu toka Zanzibar, pamoja na tozo ya ziada ya shilingi mbili za Kenya kwa kila kilo moja ya maua ya Tanzania yanayosafirishwa kwenda Ulaya kupitia Kenya. Ni matumaini yangu kuwa mikutano hii italeta suluhu ya kudumu katika kushughulikia changamoto hizi na zinazoendelea kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Soko la Pamoja la Afrika Mashariki; Kifungu cha 51(d) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, kinaitaka Serikali kuendelea kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Katika Mwaka 2011/2012, Wizara, kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi, imeendelea kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, imekamilisha mapitio ya baadhi ya Sheria za Tanzania ili ziweze kuendana na matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja. Mapitio hayo yamehusisha sheria zinazosimamia ajira, fedha, uwekezaji, usajili wa makampuni, ardhi, uhamiaji, biashara ya huduma kwenye sekta ya Utalii (Hoteli na Migahawa), bima na katika baadhi ya sekta za huduma za fedha. Maeneo yanayopendekezwa kufanyiwa marekebisho yamekamilishwa na kuwasilishwa katika Wizara husika za kisekta kwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013 Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta itaendelea kufanya mapitio ya sheria zinazosimamia maeneo yaliyosalia kwenye biashara ya huduma katika sekta za Benki na Fedha, Utalii, Elimu, Ugavi, Usafiri, Mawasiliano na Huduma za Utaalamu. Marekebisho ya sheria hizo yatawezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja katika maeneo ya uhuru wa kusafiri, uhuru wa kufanya kazi, uhuru wa kufanya biashara ya huduma, uhuru wa kuweka mitaji, haki ya ukaazi na haki ya kuanzisha na kuendesha shughuli za biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuratibu utekelezaji wa Soko la Pamoja, katika mwaka 2011/2012, Jumuiya imekamilisha maandalizi ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Mfumo huo unaainisha makubaliano yaliyopo katika Itifaki ya Soko la Pamoja, na viashiria vya kupima hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wake. Kulingana na mfumo huu, Nchi Wanachama zinatakiwa kutoa taarifa za utekelezaji zitakazojadiliwa katika vikao vya kila nusu mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mfumo huu uweze kuwa na tija, Nchi Wanachama hazina budi kukamilisha marekebisho ya sheria zao ili kusaidia utekelezaji wa Soko la Pamoja. Ni matumaini yangu kuwa wadau wote watakamilisha zoezi hilo muhimu la kurekebisha sheria husika katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kuwa utekelezaji wa Soko la Pamoja hauendi kwa kasi iliyotarajiwa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo Nchi Wanachama kutokamilisha mapitio ya sheria zao, Nchi Wanachama zilikubaliana kuanzisha Kamati za Kitaifa za Kusimamia Utekelezaji wa Soko la Pamoja. Tanzania imekwishaunda Kamati ya Kitaifa ya Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi kusimamia utekelezaji wa Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii itafuatilia na kusimamia utekelezaji wa Soko la Pamoja, na kubuni mikakati itakayoliwezesha Taifa letu na Watanzania kunufaika kutokana na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hususani Soko la Pamoja. Aidha, kama

ilivyokwishaelezwa katika hotuba hii, Wizara imekamilisha maandalizi ya Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja utakaoiwezesha Tanzania kujipanga, na hivyo Taifa na Wananchi kuzitumia fursa za Soko la Pamoja kwa manufaa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uanzishwaji wa Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; katika mwaka wa fedha 2011/12, Wizara imeendelea kuratibu na kuongoza majadiliano ya Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ili kujipanga Kitaifa, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango, na Benki Kuu ya Tanzania na wadau wengine wamefanya uchambuzi kuhusu utayari wa Tanzania kujiunga na Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi huo ulilenga kupima hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa hatua za awali za mtangamano, yaani Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja, kama msingi wa kuelekea katika Umoja wa Fedha; kupima utayari wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuanzisha Umoja wa Fedha; kupima utayari wa Tanzania kujiunga na Umoja wa Fedha na kujifunza kutokana na mtikisiko wa kifedha unaoukumba Umoja wa Ulaya hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi huo yamebainisha kuwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hazina budi kukamilisha masuala ya msingi ili kuweza kuingia katika Umoja wa Fedha. Kwa muhtasari, matokeo yameainisha kuwa Nchi Wanachama hazina budi kufanya yafuatayo:-

(a) Kutekeleza kwa ukamilifu hatua za awali za mtangamano kwa kuimarisha Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja;

(b) Kuimarisha misingi ya uzalishaji na miundombinu muhimu, ili kuweza kutumia fursa zitokanazo na hatua hizi za mwanzo za mtangamano wa Jumuiya kujenga uchumi imara na endelevu katika Nchi Wanachama;

(c) Kuhuisha chumi zao kwa kufikia vigezo vya kuoanisha uchumi mpana na hivyo, kuweka mazingira stahiki ya kuunda Umoja wa Fedha imara;

(d) Kuainisha mifumo yao ya uandaaji na utunzaji wa takwimu na hivyo, kuwa na mfumo wa pamoja wa ufuatiliaji na tathmini;

(e) Kuwa na mfumo wa fedha uliohuishwa *(Harmonized Accounting System);* na

(f) Kuwa na mfumo unaowezesha usimamizi wa pamoja wa sera za bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kuweka mazingira bora ya kuanzisha Umoja wa Fedha, Mwezi Januari, 2012 wajumbe wa Kikosi Kazi cha Majadiliano kutoka Nchi Wanachama walifanya ziara ya kujifunza katika Umoja wa Ulaya kwa lengo la kupata uzoefu kuhusu uanzishwaji wa Umoja wa Fedha na pia kufahamu chanzo cha mtikisiko wa kifedha unaokumba ukanda wa fedha wa Umoja huo pamoja

na hatua zinazochukuliwa kukabiliana na mtikisiko huo. Katika ziara hiyo, Jumuiya ya Afrika Mashariki imejifunza kuwa ili kuunda Umoja wa Fedha imara mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:-

(a) Nchi Wanachama sharti zifikie sifa stahiki ya kuwa katika ukanda mmoja wa fedha (*optimum currency area*). Sifa hizo ni pamoja na uhuru wa soko la mitaji na ajira na mtangamano wa sekta ya fedha;

(b) Nchi Wanachama zitekeleze kikamilifu hatua za awali za mtangamano (Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja) kwani hizi ndizo zitakazoandaa Nchi Wanachama kuwa na sifa stahiki za kufikia Umoja wa Fedha;

(c) Nchi Wanachama zinatakiwa kuwa makini katika kuruhusu nchi kujiunga na Umoja wa Fedha kwa kuhakikisha kuwa zinafikia vigezo vilivyokubalika vya kuoanisha uchumi mpana na kudhihirisha uwezo wa kuendelea kuzingatia vigezo hivyo ndani ya Umoja wa Fedha. Chimbuko la kuyumba kwa Umoja wa Fedha wa Ulaya ni kuziruhusu nchi kujiunga na Umoja wa Fedha wa Umoja wa Ulaya kwa sababu za Kiulinzi na Kiusalama bila kuzingatia vigezo stahiki vya kiuchumi;

(d) Nchi Wanachama zizingatie umuhimu wa kuwa na uratibu wa pamoja wa Sera za Bajeti. Kutokana na ugumu wa kuratibu kwa pamoja Sera za Nchi za Bajeti unaosababishwa na kuwa na mahitaji tofauti ya kiuchumi na maendeleo baina ya nchi na nchi, ni vema kuhakikisha uoanishaji wa uchumi halisi ili kupunguza tofauti za mahitaji ya kimaendeleo na

vipaumbele vya nchi mbalimbali ndani ya Umoja wa Fedha;

(e) Nchi Wanachama ziimarishe nidhamu ya bajeti kwa kuhakikisha kuwa matumizi ya Serikali yanaendana na uwezo wa mapato na hivyo kuepuka kulimbikiza madeni yasiyolipika; na

(f) Nchi Wanachama zizingatie umuhimu wa kuwa na mfumo sahihi wa utoaji takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia matokeo ya uchambuzi wa ndani, na ziara katika Jumuiya ya Ulaya, Tanzania itaendelea kusimamia umuhimu wa kujenga misingi ya uanzishwaji wa Umoja wa Fedha kabla ya kuanza kwa utekelezaji wake. Lengo ikiwa ni kuwa na Umoja wa Fedha Himilivu na Jumuiya endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki; katika hotuba yangu ya mwaka 2011/2012, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba timu ya Wataalam itaundwa kuchambua kero, hofu na changamoto zilizopo sasa katika utekelezaji wa hatua za mtangamano za Umoja wa Forodha, na Soko la Pamoja na zile zinazoweza kujitokeza endapo Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki litaanzishwa kwa pupa na bila kuzingatia misingi na malengo ya Jumuiya ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya timu ya Wataalam ilikamilishwa na kuwasilishwa katika Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya uliofanyika Mjini Bujumbura mwezi Novemba, 2011. Viongozi Wakuu wa Jumuiya waliiagiza Sekretarieti ya Jumuiya

kuandaa Modeli ya Muundo wa Shirikisho ili kuendeleza mjadala wa suala hili na kupanua uelewa wa wananchi wa Afrika Mashariki kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, timu ya Wataalam ilibainisha kuwa hadi sasa wananchi walio wengi hawajaona ama kupata manufaa yaliyo wazi katika utekelezaji wa hatua za mtangamano. Hivyo, timu ilizitanabaisha Nchi Wanachama kuzingatia utekelezaji wenye tija na manufaa wa hatua za msingi na za awali za mtangamano wa Afrika Mashariki kabla ya kuanza mchakato wa kuunda Shirikisho. Tahadhari hii itazingatiwa na Tanzania wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kuendeleza mtangamano hatua kwa hatua ulibainishwa pia na Rais mwaka 2010, wakati akikabidhi Uenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa maneno yafuatayo naomba kunukuu kwa kiingereza:-

*"But if to plan is to choose, to cite Mwalimu Nyerere's dictum, the EAC should henceforth be more focused and selective, with few key priorities that will result into visible and tangible results."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikiano na Jumuiya Nyingine za Kiuchumi; Utatu wa Jumuiya za *COMESA, EAC na SADC*; Kifungu cha 51(a) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, kinaielekeza Serikali kuhamasisha matumizi ya fursa za masoko ya ndani, kikanda na kimataifa. Katika kutekeleza azma hii, na kulingana na majukumu ya Wizara kwa mwaka 2011/2012, Wizara yangu

imeendelea kuratibu na kuongoza maandalizi ya majadiliano ya uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Jumuiya za Utatu wa *COMESA-EAC- SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa Kwanza wa Viongozi Wakuu wa Nchi za Jumuiya za *COMESA, EAC,* na *SADC* uliofanyika mwezi Oktoba 2008, Kampala-Uganda; Viongozi Wakuu walikubaliana kuanzisha Utatu wa *COMESA-EAC-SADC*. Ilikubalika kuwa ushirikiano huo ujumuishe mihimili mitatu ambayo ni mtangamano wa Masoko, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu wa *COMESA-EAC-SADC;* Uendelezaji wa Miundombinu; na Uendelezaji wa Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Mpango wa Utekelezaji (*Roadmap*) wa kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu wa *COMESA-EAC-SADC* na Muundo wa Kisheria na Kitaasisi utakaosimamia mchakato wa uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara umekamilika. Awamu ya Kwanza ya mpango itahusisha majadiliano ya Eneo Huru la Biashara ya Bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu ya Pili, itayofanyika baada ya kukamilika kwa majadiliano ya Awamu ya Kwanza, itajumuisha masuala ya biashara ikiwa ni Biashara ya Huduma; Hati Miliki na Hataza; Sera ya Ushindani na Maendeleo ya Biashara na Uwezo wa Kiushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Nchi Wanachama zimeandaa kanuni za uendeshaji

majadiliano, mpangokazi utakaoongoza majadiliano, pamoja na kuunda vikundi vya wataalam katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kurahisisha majadiliano. Majadiliano rasmi yanatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi Baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya; katika mwaka 2011/2012, majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi *(Economic Partnership Agreement - EPA)* baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya yaliendelea katika maeneo ambayo hayakufikiwa muafaka kwenye Mkataba wa Mpito *(Framework for Economic Partnership Agreement – FEPA)*. Maeneo hayo yanahusu masuala ya Kodi na Ushuru kwa Mauzo ya Nje; Upendeleo Maalum *(Most Favoured Nations- MFN)* na Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, majadiliano yameendelea pia katika maeneo mapya yanayojumuisha Uasili wa Bidhaa *(Rules of Origin)* na ushirikiano katika sekta ya kilimo. Aidha, pande zote zilikubaliana kuahirisha majadiliano katika masuala ya Biashara ya Huduma *(Trade in Services)* na Masuala Mengine yanayohusu Biashara *(Trade Releted Issues)*, hadi pande zote zitakapokuwa tayari kujadili maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa *EPA* unatoa fursa kwa bidhaa za kutoka Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuingia katika soko la Umoja wa Ulaya

bila ushuru wa forodha na vikwazo vingine visivyo vya kiforodha. Aidha, katika mkataba huu Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki hazina budi kufungua maeneo kadhaa ya soko lake kwa upendeleo kwa bidhaa kutoka Umoja wa Ulaya. Mkataba huu unatarajiwa pia kuendeleza ushirikiano wa kiuchumi na maendeleo ili kuzisaidia Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kupambana na changamoto za maendeleo, hasa za uzalishaji na miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa sekta zote zinazohusika katika majadiliano ya Mkataba wa *EPA* kuendelea kuwa makini na kuendesha majadiliano hayo kwa weledi ili hatimaye majadiliano yakamilike na tuweze kuingia kwenye mkataba wenye manufaa kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano katika sekta za uzalishaji; usalama wa chakula*;* kama hatua za kuimarisha usalama wa chakula, Wizara imeshiriki na kuratibu maandalizi ya Mfuko wa Kilimo wa Jumuiya; na Uanzishwaji wa Soko la Mauzo ya Bidhaa za Kilimo *(Regional Commodities Exchange)* kupitia Mradi wa Kikanda wa Uendelezaji wa Sekta ya Fedha *(EAC Financial Sector Development and Regionalization Project - FSDRP).* Shughuli hizi zinatarajiwa kukamilishwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka 2011/2012, Nchi Wanachama zimeanza majadiliano ya kuanzisha Mpango ujulikanao kama *“EAC Emergency Preparedness and response Plan for pastoralists in the dry lands of EAC”* utakaowawezesha

Wafugaji katika maeneo ya Nyandakame kujiandaa na majanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huu utahusisha ujenzi wa makazi imara ya wafugaji; kuimarisha huduma za kijamii katika maeneo ya wafugaji; kuepuka ajira za watoto na hivyo kuwawezesha kwenda shule na kuepukana na migogoro ya ardhi ya mara kwa mara baina ya wakulima na wafugaji. Majadiliano na maandalizi ya mpango huu yanatarajiwa kuendelea na kukamilishwa katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Makongamano ya Pamoja ya Uwekezaji; katika kuhamasisha uwekezaji, Nchi Wanachama zina utaratibu wa kuwa na Makongamano ya Pamoja ya Uwekezaji ndani ya Jumuiya. Lengo la utaratibu huu ni kukuza biashara na uwekezaji kwa kuwakutanisha wafanyabiashara na wawekezaji wa Afrika Mashariki, na wawekezaji toka sehemu mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makongamano haya ya pamoja ni matukio ya kila mwaka yanayofanyika ndani ya Nchi Wanachama kwa utaratibu wa mzunguko. Katika mwaka 2011/2012, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Kongamano la Uwekezaji katika Bonde la Ziwa Tanganyika lililofanyika mwezi Novemba 2011, Bujumbura, Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kongamano hilo lilikuwa ni kutangaza fursa mbali mbali za uwekezaji zilizopo katika bonde hilo na kukuza biashara kwa

kuhamasisha wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani na nje ya Jumuiya kuwekeza. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru waandaaji wa Kongamano hili muhimu na kuwaomba wadau wa Bonde la Ziwa Tanganyika kufuatilia na kutekeleza maazimio yote yaliyofikiwa kwa maslahi yao na kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maonesho ya Nguvu Kazi; katika mwaka 2011/2012 Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya 12 ya Jua Kali/Nguvu Kazi ya Jumuiya yaliyofanyika jijini Kampala, Uganda. Maonyesho haya hufanyika kila mwaka ikiwa ni kutoa fursa kwa wajasiriamali kutoka Nchi Wanachama kukutana na kubadilishana uzoefu juu ya kukuza na kuendeleza biashara, na kuweza kujifunza teknolojia mpya, na kuanzisha uhusiano wa kibiashara. Kama ilivyokuwa kwa maonesho yaliyopita, maonesho haya yalikuwa ya mafanikio makubwa kwa wajasiriamali wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze kwa dhati kabisa, wajasirimali walioshiriki katika maonesho haya na hususan, wale walioweza kuingia katika mikataba ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utalii na Wanyamapori; katika mwaka 2011/12, Wizara iliratibu mafunzo ya wataalam wa kutathmini hadhi na Viwango vya Hoteli na Migahawa katika Jumuiya ambapo jumla ya Wataalam 15 kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar walifuzu na kutunukiwa vyeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la zoezi hili lilikuwa ni kuwawezesha Wataalam hawa kuongeza kasi ya zoezi la kuzipanga Hoteli na Migahawa katika hadhi ya Nyota stahiki ili kuleta ushindani ulio sawa katika Sekta ya Utalii Afrika Mashariki. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Sekta husika itaendelea kuratibu utoaji wa Nyota katika Hoteli na Migahawa katika maeneo ya Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viza ya Pamoja ya Utalii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; katika kutekeleza maagizo ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki kuzitaka Nchi Wanachama kuchukua hatua za kuitangaza Afrika Mashariki kama Kituo Kimoja cha Utalii *(single tourist destination)*, katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi Wanachama zimeendelea kufanya uchambuzi wa kuangalia utayari wa Nchi Wanachama kuwa na Viza ya Pamoja kwa Watalii. Matokeo ya awali ya utafiti huu yanaonesha kuwa utekelezaji wa Viza ya Pamoja kwa Watalii una changamoto ambazo hazina budi kuzingatiwa kwa kujiwekea mikakati mahsusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizo ni pamoja na ukusanyaji na mgawanyo wa mapato, usalama, miundombinu ya kiuchumi na kiteknolojia. Ili kujipanga Kitaifa, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta inafanya utafiti wa ndani utakaowezesha Tanzania kufahamu mahitaji ya kuwa na Visa ya Pamoja na kuweza kujiandaa ipasavyo. Shughuli hii itaendelea katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa Miundombinu ya Kiuchumi; utekelezaji wa programu za uendelezaji miundombinu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki unazingatia Ibara ya 89 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inayozitaka Nchi Wanachama kushirikiana katika uendelezaji wa miundombinu. Aidha, utekelezaji wa programu za uendelezaji na uimarishaji miundombinu unazingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, inayoelekeza uimarishaji wa miundombinu ili kuziwezesha sekta nyingine za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kifungu cha 19 (e) cha Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010 kinachoielekeza Serikali kuweka msingi wa miundombinu ya uchumi wa kisasa kwa kuhakikisha nishati yenye uhakika na uboreshaji wa miundombinu na huduma za kiuchumi kwa jumla, na Kifungu cha 19(f) cha Ilani kinachoielekeza Serikali kutumia fursa za kijiografia kukuza uchumi wa kisasa wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa Tanzania ni nchi pekee inayopakana na nchi zote Wanachama wa Jumuiya, ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya uchukuzi, hususan uimarishaji wa bandari, mitandao ya reli, ujenzi wa viwanja vya ndege, usafiri wa majini, anga na barabara ni miongoni mwa vipaumbele vya Tanzania katika Jumuiya. Uendelezaji huu wa miundombinu utaiwezesha Tanzania kutumia nafasi yake ya kijiografia kunufaika kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Katika kutekeleza azma hii, Wizara imeendelea kuratibu

utekelezaji wa miradi ya miundombinu katika Jumuiya kama ifuatavyo:-

Kwanza, Mtandao wa Barabara; katika mwaka 2011/2012, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeendelea kutekeleza Mtandao wa Barabara katika Jumuiya *(The East African Road Network Project)*. Mtandao huo unajumuisha barabara za kitaifa zenye umuhimu wa kikanda ambazo zinaunganisha Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, kwa upande wa Tanzania, uendelezaji wa miundombinu ya barabara kwa kila kanda ni kama ifuatavyo:-

Kanda ya Kwanza, hii ni Kanda ya Uchukuzi ya Kaskazini inayoanzia Mombasa - Malaba - Katuna - Kigali - Kanyaru -Bujumbura – Gatumba, ikijumuisha Marangu -Tarakea, Chalinze – Segera, na Segera - Himo. Ukarabati kwa kiwango cha lami umeanza kwa barabara ya kutoka Korogwe - Mkumbara - Same yenye urefu wa Kilomita 172; na usanifu wa kina umeanza kwa upande wa barabara ya Same - Himo yenye urefu wa Kilomita 80. Ukarabati na usanifu wa barabara hizi unafadhiliwa na Benki ya Dunia na utaendelea katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Kanda ya Pili, hii ni Kanda ya Uchukuzi ya Kati inayounganisha Dar es Salaam na Kigoma na nchi ya Burundi na Rwanda. Barabara hizi zinaanzia Dar-es-salaam - Isaka - Lusahunga - Mutukula - Masaka na Lusahunga - Nyakasanza – Rusumo - Kigali - Gisenyi.

Katika mwaka 2011/2012, ujenzi na ukarabati wa barabara hizi kwa upande wa Tanzania umeendelea kufanyika chini ya ufadhili wa Serikali ya Tanzania na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2012/13. Aidha, usanifu wa kina wa sehemu ya Lusahunga-Rusumo na Kobero-Nyakasanza yenye urefu wa kilomita 150 umeanza chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia na utaendelea katika mwaka 2012/2013.

Kanda ya Tatu, Kanda hii inahusisha mtandao wa barabara za Biharamulo - Mwanza - Musoma - Sirari - Lodwar – Lokichogio. Ujenzi wa sehemu ya Uyovu - Bwanga – Biharamulo yenye urefu wa kilomita 112 kwa kiwango cha lami utaanza katika mwaka 2012/2013.

Kanda ya Nne, Kanda hii inaunganisha Nyanda za Juu Kusini na Magharibi mwa Tanzania, ikianzia Tunduma - Sumbawanga - Kigoma - Manyovu (Mugina) - Rumonge - Bujumbura - Ruhwa (Bugarama) - Karongi - Gisenyi. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara kutoka Tunduma – Sumbawanga – Kizi umeendelea kwa fedha za Serikali ya Tanzania na ufadhili wa *Millenium Challenge Corporation (MCC)* na utaendelea katika mwaka 2012/2013.

Kanda ya Tano, Kanda hii inaanzia Tunduma - Iringa – Dodoma - Arusha - Namanga – Moyale. Katika mwaka 2011/2012 ujenzi wa barabara ya Iringa – Dodoma kwa kiwango cha lami umeendelea chini ya ufadhili wa AfDB. Barabara ya Dodoma – Mayamaya – Bonga – Babati imeendelea kujengwa kwa kiwango

cha lami kwa fedha za Serikali ya Tanzania kwa sehemu ya Dodoma-Mayamaya yenye urefu wa kilomita 43.8 na sehemu ya Bonga-Babati yenye urefu wa kilomita 19.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ujenzi wa sehemu ya Mayamaya-Bonga yenye urefu wa km 188.15 utaanza katika mwaka 2012/13 chini ya ufadhili wa *ADfB* na Serikali ya Tanzania. Kwa upande wa barabara ya Babati – Arusha, ujenzi na ukarabati kwa kiwango cha lami unaendelea kwa fedha za *AfDB* na Benki ya Dunia. Ujenzi wa barabara hizi utaendelea katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti kwa mwaka 2011/2012, ujenzi wa barabara ya Arusha – Namanga – Athi *River* unajumuisha barabara yenye urefu wa kilomita 104.4 kwa upande wa Tanzania. Katika mwaka 2011/2012, uwekaji wa lami na ujenzi wa madaraja umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Jumuiya inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa maeneo ambayo maji yanatuama wakati wa mvua ili kujenga madaraja 12 yenye njia mpya 43 na kuweka kingamo za kuzuia maji kuharibu barabara umbali wa kilomita 40. Inatarajiwa kuwa kazi hizi zitakamilika ili barabara hii iweze kufunguliwa rasmi na Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama mwezi Novemba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Arusha – Holili/Taveta – Voi; Wizara imeendelea kuratibu upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya

Arusha – Holili/Taveta – Voi, yenye urefu wa kilometa 158.8 kwa upande wa Tanzania na kilometa 122.5 kwa upande wa Kenya. Kazi hii inatarajia kukamilika katika kipindi cha mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Malindi – Lunga Lunga - Tanga – Bagamoyo; katika kipindi cha mwaka 2011/12, Wizara imeendelea kuratibu upembuzi yakinifu wa barabara ya Malindi – Lunga Lunga - Tanga – Bagamoyo, yenye jumla ya urefu wa kilometa 400. Kwa upande wa Tanzania, barabara hii ina urefu wa kilometa 240, kutoka Tanga hadi Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ilianza mwezi Februari 2011 na inatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2012. Katika mwaka wa fedha 2012/13 Wizara yangu itaendelea kuratibu hatua inayofuata baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Tanga – Horohoro; katika kipindi cha mwaka 2011/2012, ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro, yenye urefu wa kilomita 66 kutoka Horohoro mpakani mwa Tanzania na Kenya hadi Tanga mjini umeendelea. Barabara hii inajengwa kwa msaada wa Serikali ya Marekani kupitia mfuko wa *Millenium Challenge Corporation (MCC)* kwa gharama ya shilingi bilioni 69.9. Ujenzi huu ulianza mwezi Januari, 2010 ambapo hadi mwezi Machi, 2012 ujenzi umefikia asilimia 86 ya kazi zote za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyokuwa kwa sekta nyingine, uendelezaji wa barabara hizi zilizopo

katika mtandao wa barabara wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unafanyika chini ya usimamizi wa Wizara ya Ujenzi, hivyo maelezo ya kina ni kama yalivyotolewa katika Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ujenzi.

Pili, Mkakati wa Uchukuzi na Programu ya Maendeleo katika Sekta ya Barabara; katika kuboresha Sekta ya Uchukuzi, katika mwaka 2011/2012, Nchi Wanachama zimekamilisha Mkakati wa Uchukuzi na Programu ya Maendeleo katika Sekta ya Barabara *(EAC Transport Strategy and Road Sector Development Programme)*. Mkakati huu umeainisha miradi ya kutekeleza katika kipindi cha miaka kumi (2011/12 – 2019/20).

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Uchukuzi iliyojumuishwa katika Mkakati huu ni ile ya barabara, reli, usafiri wa anga, usafiri wa majini na mabomba ya kusafirishia vimiminika kama mafuta na gesi. Hatua inayofuata ni kufanya uchanganuzi *(Projects Unpacking*) wa miradi hiyo kwa lengo la kuitafutia fedha za utekelezaji. Zoezi hili litafanyika katika mwaka 2012/2013.

Tatu, mtandao wa Reli; katika mwaka wa fedha 2011/12 Nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi zimeendelea kushirikiana katika kuendeleza reli ya Isaka - Kigali/Keza hadi Musongati ambapo kazi za usanifu wa kina unaojumuisha upembuzi wa athari kwa mazingira; faida za kiuchumi na tathmini ya kisheria na mfumo wa kitaasisi ikiwa ni pamoja na namna ya kushirikisha sekta binafsi zimeanza. Kazi ya usanifu wa kina inatarajiwa kukamilika mwaka 2012/2013.

Mtandao huu wa reli ni sehemu ya Mpango Kabambe wa Reli wa Afrika Mashariki.

Nne, Sekta ya Usafiri wa Majini na Uendelezaji wa Bandari; katika kuendeleza sekta ya Usafiri wa Majini na Uendelezaji wa Bandari, Nchi Wanachama katika mwaka 2011/2012 zimekamilisha Hadidu za Rejea za kuandaa Mkakati wa Usafiri Majini. Mkakati huo utaainisha vipaumbele vya miradi ya kuendeleza usafiri wa majini na bandari katika Jumuiya. Wizara yangu itaendelea kuratibu maandalizi ya Mkakati huo katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Tano, Sekta ya Usafiri wa Anga; uboreshaji wa usalama wa anga; Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano yenye lengo la kuimarisha usafiri wa anga kwa kupanua matumizi ya mfumo rahisi wa mawasiliano ya anga *(Cheaper Navigation System)* unaotumia mfumo wa Kimataifa wa Mawasiliano ya *Satellite (Global Navigation Satellite System – GNSS)*; utekelezaji wa *Yamousokro Declaration (YD)* kuwezesha huduma za usafiri wa anga kuwa huria katika Jumuiya; mfumo wa kikanda wa kusimamia uchunguzi wa ajali za ndege; Uwekaji wa Mfumo wa Ulinzi kwa Kutumia Mitambo yenye uwezo wa kuona eneo kubwa la kiulinzi badala ya mfumo wa rada *(Automatic Dependent Surveillance-Broadcast-ADS-B)*. Shughuli hizi zitaendelea katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uboreshaji wa Sekta Ndogo ya Hali ya Hewa; katika kuimarisha sekta ndogo ya Hali ya Hewa, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara iliratibu na kushiriki katika mapitio ya

Mpango wa Maendeleo na Mkakati wa uwekezaji wa miaka mitano katika sekta ndogo ya Hali ya Hewa. Kazi ya mapitio ya Mpango wa Maendeleo wa Mkakati huo imekamilika. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Nchi Wanachama zitaendelea kutafuta fedha ili kuwezesha utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara iliratibu na kushiriki katika maandalizi ya Mpango Kabambe wa Mabadiliko ya Tabianchi *(Climate change Master Plan).* Rasimu ya Mpango Kabambe huo imekamilika na kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri la Sekta la Mazingira na kuelekeza iwasilishwe katika Nchi Wanachama kwa ajili ya kuitolea maoni. Mpango huo unatarajiwa kukamilishwa katika mwaka 2012/2013.

Sita, Sekta ya Nishati; Ibara ya 101 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya, inabainisha kuwa Nchi Wanachama zitachukua hatua ili kuwa na Sera na Mfumo wa kuwezesha matumizi ya rasilimali mbalimbali za nishati kwa lengo la kuzalisha na kusambaza umeme kwa gharama nafuu katika Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kifungu cha 63(b) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, kinaainisha kuwa Serikali itachukua hatua zenye lengo la kuunganisha Gridi ya Tanzania na Gridi za nchi jirani ili kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini. Katika kutekeleza vifungu hivi, kwa mwaka 2011/2012, hatua zifuatazo zimechukuliwa ili kuimarisha miundombinu ya nishati:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Kuunganisha Gridi za Nchi Wanachama; chini ya mpango wa kikanda wa kuunganisha Gridi za Nchi Wanachama *(East African Community Power Pool),* Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano ya maandalizi ya Rasimu ya Hati za Makubaliano zitakazowezesha Nchi Wanachama kuuziana umeme ili kuondoa uhaba wa umeme. Hati hizo ni makubaliano baina ya Serikali za Nchi Wanachama na Makubaliano baina ya Watoa Huduma. Hati hizo zinatarajiwa kukamilishwa katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Nchi Mwanachama imewasilisha kampuni za kutoa huduma za umeme zitakazohusika katika makubaliano haya. Kwa upande wa Tanzania, kampuni zilizowasilishwa ni Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) na Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*); Kenya imewasilisha Kampuni mbili; Nchi za Rwanda, Uganda na Burundi zimewasilisha Kampuni moja toka kila Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 63(u) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, kinaiagiza Serikali kuanza utekelezaji wa njia Kuu ya Umeme ya Zambia, Tanzania na Kenya (ZTK) inayounganisha mitandao ya Umeme ya nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika, sanjari na mpango wa Nchi za *EAC* na *SADC* unaolenga kuunganisha mifumo ya Kitaifa ya umeme chini ya mfumo ujulikanao kwa jina la *Southern Africa Power Pool*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya

kuunganisha Gridi za Tanzania na Kenya kutokea Singida hadi Arusha na Nairobi imeendelea kwa ufadhili wa Serikali ya Norway na kuratibiwa na *Nile Equatorial Lakes Subsidiary Action programme (NELSAP).* Shughuli hii itaendelea katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Kuzalisha Umeme Katika Miji ya Murongo/Kikagati; katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara iliratibu na kushiriki katika kukamilisha majadiliano ya Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Murongo/Kikagati unaotarajiwa kuzalisha *16MW*. Hati ya Makubaliano kuhusu mradi huu baina ya Serikali za Tanzania na Uganda iliwekwa sahihi mwezi Septemba, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hii nchi za Tanzania na Uganda zinaendelea na majadiliano ya Mikataba mbalimbali ya utekelezaji wa Mradi huu. Mikataba hiyo ni pamoja na Mkataba wa Makubaliano *(Bilateral Agreement)* ambapo rasimu ya Mkataba huu upo katika hatua ya mwisho ya kusainiwa. Maandalizi ya mikataba hii yanatarajiwa kukamilishwa katika mwaka 2012/2013 ili kuwezesha utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa mradi huu, Serikali haina budi kuandaa miundombinu ya kusambaza umeme huo katika maeneo tarajiwa nchini Tanzania. Serikali kupitia wakala wa Nishati Vijijini imetenga fedha katika bajeti ya mwaka 2012/2013 itakayowezesha kuweka

miundombinu hiyo ya kusambaza umeme katika maeneo husika katika Wilaya ya Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miradi ya Kipaumbele ya Uzalishaji na Usambazaji Umeme; katika kukabiliana na upungufu wa nishati ya umeme, mwaka 2011/2012 Nchi Wanachama zimeainisha miradi ya kipaumbele ya uzalishaji na usambazaji umeme ili kutafutiwa fedha kupitia ushirikiano wa kikanda. Kwa upande wa Tanzania, miradi iliyopendekezwa ni ifuatayo:-

Singida-Arusha-Nairobi *400kV Interconnector*; Masaka-Mwanza *220kV Interconnector*; Rusumo-Nyakanazi *220kV Interconnector; Stieglers Gorge Hydro-Power Project 2100MW*; Kiwira *Coal 200MW* na Rusumo *Hydro Power Plant 90MW*. Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea na taratibu za kutafuta fedha za kuwezesha utekelezaji wa miradi hii. Shughuli hii itaendelea katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Jumuiya ya Afrika Mashariki imekamilisha Rasimu ya Sera ya Kuunganisha Umeme katika Maeneo ya Mipakani *(Cross-Border Electrification Policy).* Sera hii itatoa mwongozo wa namna Nchi Wanachama zitakavyoshirikiana katika kuiwezesha miji na vijiji katika maeneo ya mipakani ya Nchi Wanachama kupata huduma ya umeme. Sera hii inatarajiwa kukamilishwa katika mwaka 2012/2013.

Saba, Sekta ya Mawasiliano; katika mwaka 2011/2012, Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano

ya uunganishaji wa Mkongo wa Mawasiliano kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The East African Broadband Infrastructure Network)*. Lengo la hatua hii ni kurahisisha mawasiliano miongoni mwao na dunia kwa jumla. Tanzania imefikisha mkongo wa mawasiliano katika mipaka yote ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Zambia na Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, mkongo wa Tanzania umeunganishwa na Rwanda. Majadiliano yanaendelea ili Nchi nyingine Wanachama ziweze kuunganishwa na kuweza kuboresha mawasiliano baina ya Watanzania, Wanaafrika Mashariki, na sehemu nyingine duniani. Hatua hii itachangia katika kuendeleza shughuli za kiuchumi na kijamii miongoni mwa Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rasimu ya Itifaki ya Ushirikiano katika sekta ya TEHAMA imekamilika. Itifaki itaweka msingi wa ushirikiano kwenye mfumo mpana wa sekta ya TEHAMA ambao utaiwezesha Tanzania na Nchi nyingine Wanachama kunufaika kibiashara. Itifaki hii inatarajiwa kukamilishwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwianishaji wa uzito wa magari katika barabara; katika mwaka 2011/12, Jumuiya ilikamilisha utafiti wenye lengo la kuwianisha sera na taratibu za udhibiti wa uzito wa magari kwenye barabara za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Nchi Wanachama zimekamilisha Rasimu ya Sheria na Kanuni za Udhibiti wa Uzito wa

Magari. Sheria hii inatarajiwa kukamilishwa katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, sheria hii inakusudia kuweka utaratibu wa kuwa na vituo vichache vya mizani kupima uzito wa magari *(optimal weighbridges),* ili kupunguza muda unaotumiwa na magari katika vituo husika, lakini bila kuathiri miundombinu ya barabara kutokana na kuzidisha uzito au uzito kubadilika kutokana na mizigo kuhama wakati ikisafirishwa au udanganyifu unaoweza kujitokeza njiani.

Nane, Ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya; napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya, ulioanza mwezi Januari 2010 umekamilika. Kwa sasa Serikali ya Tanzania inaendelea kufanya matengenezo ya barabara *(EAC Close)* itakayotumiwa na Viongozi Wakuu kuingia na kutoka katika Makao Makuu ya Jumuiya yenye urefu wa mita 300. Uzinduzi rasmi wa jengo hili unatarajiwa kufanyika mwezi Novemba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta za Huduma za Jamii; kwanza, Sekta za Elimu, Utamaduni na Michezo, Afya na Sayansi; Ibara ya 5(1) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya, inaainisha malengo ya Jumuiya kuwa ni pamoja na kuanzisha sera na mipango yenye lengo la kukuza ushirikiano baina ya Nchi Wanachama katika nyanja za jamii na utamaduni. Mkataba huo unabainisha pia maeneo ya ushirikiano kuwa ni pamoja na masuala ya elimu,

utamaduni, michezo, sayansi na teknolojia, afya, ajira na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kifungu cha 85 cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, kinaiagiza Serikali kuchukua hatua za kuboresha, kuimarisha na kupanua elimu ya awali hadi ya Chuo Kikuu, na kuhakikisha kwamba elimu ya ngazi zote itakayotolewa nchini tangu sasa iwe ya ubora utakaowawezesha vijana wetu kuchukua nafasi zao stahiki ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwianishaji wa Mifumo ya Elimu na Mitaala; katika mwaka 2011/2012, Nchi Wanachama wa Jumuiya zimeendelea na majadiliano yenye lengo la kuwianisha Mifumo ya Elimu na Mitaala katika Jumuiya. Uhuishaji wa mifumo na mitaala kutawawezesha Wanaafrika Mashariki kupata elimu inayoshabihiana na kuwezesha ushindani unaotoa fursa sawa kwa Wanaafrika Mashariki kupata ajira katika soko la ajira la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Uwianishaji wa Mifumo ya Elimu imekamilika. Aidha, majadiliano ya kuandaa Mpango wa Utekelezaji yataendelea katika mwaka 2012/2013. Natoa wito kwa Watanzania kuyatambua maeneo ya ajira yaliyofunguliwa katika Soko la Pamoja na kujiandaa ipasavyo kitaaluma, ili kuweza kunufaika na fursa hizo za ajira zinazopatikana katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Taasisi za Elimu Zilizobobea; katika mwaka 2011/2012, Jumuiya ya Afrika Mashariki imekamilisha zoezi la udahili wa Taasisi za Elimu zilizobobea kwa lengo la kutumika na Nchi zote Wanachama kama chachu ya kuendeleza Sayansi na Teknolojia na fani nyingine muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa wananchi. Kwa upande wa Tanzania, Taasisi zilizofanyiwa udahili ni kama ifuatavyo:-

(a) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo cha Sayansi za Baharini -Zanzibar;

(b) Taasisi ya Mafunzo ya Ubaharia *(DMI)*-Mafunzo ya Usafiri wa Majini na Teknolojia ya Uhandisi Majini;

(c) Taasisi ya Sanaa Bagamoyo *(TASUBA)*;

(d) Chuo Kikuu cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi *(MUCCoBs)*; na

(e) Chuo cha Wanyamapori - Mweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mashindano ya Insha ya Jumuiya; katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kuratibu Mashindano ya Insha ya Jumuiya yanayoshirikisha wanafunzi wa shule za Sekondari za Afrika Mashariki. Lengo la mashindano haya ni kujenga uelewa wa wanafunzi juu ya masuala mbalimbali yanayohusu Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mada inayoshindaniwa kwa mwaka 2012 ni: ‘Jadili Nafasi ya

Elimu katika Kuimarisha Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki'.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa washindi wa mwaka 2011 walikabidhiwa zawadi zao wakati wa Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama uliofanyika Bujumbura, Burundi mwezi Novemba, 2011. Bi. Neema John, Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Jangwani, kutoka Tanzania, alikuwa mshindi wa tatu.

Pili, Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki; ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika kikao cha 24 kilichofanyika Bujumbura, Burundi mwezi Novemba, 2011 liliteua Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mwenyeji wa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (EAC Kiswahili Commission). Makao Makuu haya yatakuwa Zanzibar.

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wadau wote, hususan Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kufanikisha mchakato huu. Zoezi la kuanzisha Kamisheni hii linaendelea, na inatarajiwa kuwa Kamisheni hii itaanza kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Tatu, Hifadhi ya Mazingira; Mradi wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria *(LVEMP II*); kwa kuzingatia kuwa Ziwa Victoria ni mojawapo ya rasilimali muhimu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya imeendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Mradi wa Hifadhi na Usimamizi wa

Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria iliyoanza mwaka 2009 (*Lake* Victoria *Environmental Management Program – LVEMP* II).

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu hii ya mradi inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2013. Mradi huu unatekelezwa katika sehemu kuu mbili; miradi ya Kikanda na miradi ya Kitaifa. Katika mwaka 2011/2012, miradi ya kikanda iliyotekelezwa na kukamilishwa ilihusisha uchambuzi na maandalizi ya sera na mikakati ifuatayo:-

(a) Mkakati wa Matumizi Endelevu ya Ardhi wa Bonde la Ziwa Victoria;

(b) Mkakati wa ufuatiliaji, uchukuaji takwimu, na udhibiti wa magugu maji katika Bonde la Ziwa Victoria;

(c) Mfumo wa usimamizi na utunzaji wa mazingira;

(d) Mifumo ya mawasiliano na ubadilishanaji wa taarifa mbalimbali za mazingira; na

(e) Sera ya kusimamia uachiaji na utoaji maji kwenye Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili inahusisha miradi ya Kitaifa inayolenga kuhifadhi na kupunguza uharibifu wa mazingira, hususan katika eneo la Mto Simiyu (Simiyu *Catchment Area*) na kuboresha hali za maisha ya jamii inayoizunguka Ziwa Victoria. Miradi hii iko katika Wilaya za Bariadi, Kwimba,

Magu, Maswa, Mwanza na Meatu zilizopo katika Mikoa ya Mwanza, Mara na Simiyu. Utekelezaji wa miradi hii upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa miradi hiyo, miongozo kumi ya kufundishia kuhusu uendeshaji na usimamizi wa miradi ya Jamii iliandaliwa na imeanza kutumika katika mwaka wa fedha 2011/2012. Jumuiya kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, inaendelea kuibua miradi mingine itakayofadhiliwa na Mradi wa *LVEMP* II katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria; katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria *(Lake Victoria Water Supply and Sanitation - LVWASTAN).* Mradi huu unatekelezwa katika miji Mitatu ya Tanzania ambayo ni Geita, Nansio na Sengerema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mradi huu ni kupunguza uharibifu wa mazingira pamoja na kutekeleza malengo ya *Millenia* kwa upande wa Sekta ya Maji na Mazingira. Katika mwaka 2011/2012, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilisaini Mkataba wa Makubaliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya ufadhili wa Mradi huo. Utekelezaji wa mradi huu utaendelea katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Utunzaji wa Mazingira na Afya katika Bonde la Mto

Mara; katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Utunzaji wa Mazingira na Bioanuai na Afya ya Jamii katika Bonde la Mto Mara. Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (2009- 2012) katika Nchi za Tanzania na Kenya. Lengo kuu la mradi ni kuhuisha usimamizi wa maliasili na mazingira katika Bonde la Mto Mara. Katika mwaka 2011/2012, mradi huu umewezesha yafuatayo:-

(a) Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Kenya na Tanzania kupatiwa mafunzo ya Shahada ya Juu ya Uzamili katika masuala ya Utunzaji wa Mazingira, ambapo jumla ya wanafunzi wanane (8) kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi toka Tanzania wamenufaika;

(b) Kufanya tafiti mbalimbali katika Bonde la Mto Mara ikiwemo:

- Tathmini ya Mkakati wa Mazingira *(Strategic Environmental Assessment);*

- Mkakati wa Mawasiliano katika Bonde la Mto Mara; na

- Mkakati wa Usimamizi wa rasilimali za Bonde la Mto Mara.

Nne, Sekta ya Afya; katika Sekta ya Afya, Jumuiya ya Afrika Mashariki inatekeleza Miradi na Programu mbalimbali zenye manufaa kwa wananchi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Programu na Miradi ambayo imewezesha kupatikana kwa mafanikio yafuatayo:-

(a) Mafunzo yalitolewa kwa Taasisi za kiraia zinazoshughulikia masuala ya afya ya watoto na vijana. Miongoni mwa Taasisi hizo ni *WAMA Foundation (Wanawake na Maendeleo), Private Nurses and Midwives Association of Tanzania – PRINMAT), Young Connection Association – YCA)* na *Tanzania Young Positive Ambassador – TAYOPA);*

(b) Uzinduzi wa mradi wa *EAC Medicines Registration Harmonization Initiative* (*EAC-MRHI*) unaolenga kuwianisha Sera, Sheria na Taratibu za Usajili wa Madawa utakaowezesha upatikanaji wa dawa za msingi kwa binadamu kwa urahisi zaidi na pia uzingatiaji wa viwango vya ubora. Mradi huu ni wa aina yake katika Bara la Afrika na unafadhiliwa na Melinda *Gates Foundation*;

(c) Kutoa mafunzo kwa wadau katika jamii zenye kuhamahama na kuishi kwa makundi (madereva na wanafunzi) kuhusu vyanzo vikuu vya maambukizi ya UKIMWI. Mafunzo yalitolewa katika maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria;

(d) Mafunzo kuhusu udhibiti wa magonjwa ya maambukizi kwa binadamu na wanyama yalitolewa kwa wananchi wa mipakani katika maeneo ya Rusumo kati ya Tanzania na Rwanda; Namanga kati ya Tanzania na Kenya na Kabanga na Kobero mpaka wa Tanzania na Burundi; na

(e) Kukamilishwa kwa majadiliano ya nyaraka za Haki Miliki (HATAZA) za utengenezaji madawa na Itifaki ya Biashara ya Madawa ya Afya ya Jamii. Katika

mwaka wa fedha 2012/2013, Nyaraka hizi zinatarajiwa kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri la Jumuiya kwa ajili ya kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi Wanachama zimeona umuhimu wa kuwianisha masuala ya mitaala, mafunzo kwa vitendo na utoaji wa huduma kwa ujumla ili kuwa na ulinganifu wa huduma katika Jumuiya. Maeneo ya taaluma yanayohusishwa ni pamoja na fani ya Udaktari, Ufamasia, Uuguzi na Wakunga. Aidha, Nchi Wanachama zimeendelea kushirikiana katika kuimarisha maabara ili kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza kama *TB* na magonjwa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilifanya ukaguzi kwenye Vyuo vya Mafunzo ya Wataalamu wa Meno na Madawa ya Tiba katika vyuo vya tiba vilivyopo katika Jumuiya. Awamu ya pili ya zoezi hili itafanyika kuanzia Septemba, 2012. Lengo la ukaguzi huu ni kuwa na uelewa wa hali ya vyuo vya mafunzo katika tiba ya meno na magonjwa mengine katika Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba nitumie fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu na kuwahamasisha wadau kuhudhuria katika Kongamano la Nne (4) la Afya na Sayansi *(4th Annual East African Health and Scientific Conference)* mwezi Septemba, 2012 nchini Rwanda. Kongamano hili litawakutanisha pamoja wataalam na wadau mbalimbali wa afya ili kubadilishana uzoefu, kujadii changamoto zinazoikabili sekta ya afya na namna ya kukabiliana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama; Ibara za 123, 124 na 125 za Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya zinabainisha kuwa Nchi Wanachama zitashirikiana katika masuala ya Siasa, Ulinzi na Usalama. Utekelezaji wa masuala ya Amani na Usalama yanaongozwa na Mkakati wa Kikanda unaosimamia Amani na Usalama uliosainiwa na Nchi Wanachama mwaka 2006. Aidha, masuala ya ulinzi yanasimamiwa na Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika Ulinzi iliyosainiwa na Nchi Wanachama mwaka 2001.

Kwanza, Mkakati wa Kikanda wa Kusimamia Amani na Usalama; Ibara ya 124 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya, inabainisha kuwa Nchi Wanachama zitashirikiana katika masuala ya Amani na Usalama. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kikanda wa Kusimamia Amani na Usalama *(The EAC Strategy for Regional Peace and Security)*. Wizara iliratibu na kushiriki katika vikao vya Wakuu wa Upelelezi pamoja na Wasajili wa Magari kutoka Nchi Wanachama kwa lengo la kubadilishana taarifa za uhalifu na usalama ili kukabiliana na uhalifu katika Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Nchi Wanachama zimekubaliana kuwa na operesheni za pamoja za mara kwa mara katika kukabiliana na wizi wa magari. Nchi Wanachama zilikubaliana pia kuangalia uwezekano wa kuzihusisha nchi za Sudani, Ethiopia na Afrika Kusini katika kukabiliana na

changamoto mpya ya biashara haramu ya usafirishaji binadamu.

Pili, uwianishaji wa Shughuli za Kipolisi; katika mwaka 2011/2012, Wizara iliratibu majadiliano katika ushirikiano katika shughuli za kipolisi. Katika majadiliano hayo, Nchi Wanachama zimeendelea kuandaa miongozo itakayosimamia uwianishaji na uendeshaji wa shughuli za kipolisi katika Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka 2011/2012, Nchi Wanachama zimeanza udahili wa maabara za utambuzi wa vielelezo *(Forensic Centers)* zilizopo ili kutambua uwezo wa kila nchi kwa lengo la kuteua maabara ya Jumuiya. Zoezi hili litaboresha huduma, na pia kuzipunguzia gharama Nchi Wanachama. Zoezi hili litaendelea katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Tatu, kupambana na Madawa ya Kulevya; katika mwaka 2011/2012, Nchi Wanachama zimeendelea kushirikiana kupambana na madawa haramu ya kulevya. Katika eneo hili, Nchi Wanachama zimeweza kubadilishana taarifa kuhusu mbinu na njia wanazotumia wasafirishaji wa madawa hayo. Jumuiya imepitia sheria za Nchi Wanachama kwa madhumuni ya kushauriana namna ya kuzihuisha ili zitoe adhabu zinazoshabihiana katika nchi zote wanachama. Zoezi hili litaendelea katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Nne, mapambano dhidi ya Ugaidi; katika mwaka 2011/2012, Nchi Wanachama ziliendelea na majadiliano kuhusu uandaaji wa Hati ya Makubaliano

ya Ushirikiano Katika Kukabiliana na Ugaidi *(EAC Cooperation on Counter Terrorism)*. Uandaaji wa Hati hii ni hatua muhimu katika kuimarisha ushirikiano katika kupambana na ugaidi katika kanda ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Nchi Wanachama zimeendelea kushirikiana katika utekelezaji wa mradi wa kudhibiti kusambaa kwa silaha haramu ndogo ndogo na nyepesi. Ushirikiano katika maeneo haya utaendelezwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba yangu ya mwaka 2011/2012, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba zoezi la kuweka alama katika silaha litafanyika nchi nzima. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa zoezi hilo kwa kuanzia limeendelea katika Mikoa ya Singida, Manyara, Tabora, Kigoma na Kagera na litaendelea katika maeneo mengine katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Tano, Itifaki ya Amani na Usalama; Katika mwaka 2011/2012, Jumuiya imekamilisha rasimu ya Itifaki ya Amani na Usalama pamoja na Viambatanisho vyake ambavyo ni Mpango wa Kuzuia, Kusimamia na Kusuluhisha Migogoro kwa Njia ya Amani *(Conflict Prevention, Management and Resolution Framework)* na Mfumo wa Kupeana Habari za Tahadhari za Majanga *(Early Warning Mechanism)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi Wanachama zinaendelea na zoezi la kutambua sheria

zitakazotakiwa kufanyiwa mabadiliko ili kuwezesha utekelezaji wa mfumo huo. Zoezi hili linatarajiwa kukamilishwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Sita, Itifaki ya Ushirikiano katika Ulinzi; katika mwaka 2011/2012, Jumuiya imekamilisha Itifaki ya Ushirikiano katika Ulinzi ya Jumuiya. Itifaki hiyo ilisainiwa na Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama mwezi Aprili, 2012 Jijini Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sehemu ya Itifaki hii, Nchi Wanachama zimekubaliana kuanza majadiliano kuhusu Mkataba wa Kushirikiana Kiulinzi *(Mutual Defence Pact)*. Majadiliano haya yataanza mara baada ya Nchi Wanachama kuridhia Itifaki ya Ushirikiano katika Ulinzi. Mkataba huu unatarajiwa kukamilishwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Saba, Mazoezi ya Pamoja ya Kijeshi; katika mwaka 2011/2012, Jumuiya iliandaa mazoezi mawili ya pamoja ya kijeshi, ikiwa ni utekelezaji wa Makubaliano ya Ushirikiano katika masuala ya Ulinzi. Mazoezi hayo ni *Exercise Natural Fire* 11 na Ushirikiano Imara. Zoezi la *Exercise Natural Fire* 11 lilifanyika Chukwani, Zanzibar mwezi Septemba, 2011 baina ya majeshi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya na yale ya Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la zoezi hilo lilikuwa ni kujenga uwezo wa majeshi yetu kukabiliana na changamoto za ugaidi, majanga, kurejesha amani pamoja na kupambana na uharamia. Aidha, zoezi hilo lililenga kujenga na kuimarisha mfumo na uelewa wa pamoja wa utendaji katika operesheni kama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zoezi la Ushirikiano Imara lililohusisha Wakuu wa Vituo vya Uongozaji Operesheni *(Command Post Exercise)* lilifanyika Musanze, Rwanda mwezi Oktoba, 2011. Zoezi hili lilikuwa na dhima ya Kurejesha Amani *(Peace Support Operations),* Kukabiliana na Majanga (*Disaster Management*), Kupambana na Ugaidi *(Counter Terorism*) na Kupambana na Uharamia (*Counter Piracy*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa sasa inaendelea kuratibu ushiriki wa majeshi yetu katika zoezi la pamoja la medani (*Field Training Exercise*) lijulikanalo kama "Ushirikiano Imara" litakalofanyika katika mwaka wa fedha 2012/2013 nchini Rwanda. Lengo la zoezi hili ni kuyapa utayari majeshi yetu kukabiliana na changamoto zozote za kiulinzi, kiusalama na majanga.

Nane, Ushirikiano katika Siasa; Kifungu cha 6(d) cha Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, miongoni mwa masuala mengine, kinazitaka Nchi Wanachama kuzingatia utawala wa kidemokrasia. Katika mwaka 2011/2012, Nchi Wanachama zimeandaa mwongozo wenye kuainisha vigezo vya msingi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya katika kuendesha uchaguzi ulio huru, wazi na wa haki. Mwongozo huu ndio utakaotumika kuongoza waangalizi wa Uchaguzi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha Nchi Wanachama wa Jumuiya kupata nafasi za uwakilishi

katika Taasisi na Mashirika ya Kimataifa na pia wananchi kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kupata ajira katika Taasisi za Mashirika ya Kikanda na ya Kimataifa, Nchi Wanachama zinaendelea kushirikiana kuwaunga mkono wananchi kutoka Nchi Wanachama wanaowania nafasi za ajira katika Mashirika na Taasisi za Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, ushirikiano huo umeiwezesha Tanzania kupata nafasi katika uchaguzi uliofanyika mwezi Novemba, 2011 huko New York, Marekani, ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Tanzania Bwana Ludovick Utouh, alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Ukaguzi wa Mahesabu ya Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kumpongeza Bwana Utouh kwa uteuzi alioupata ambao umeiongezea sifa nchi yetu katika medani za kimataifa. Aidha, natoa tena rai kwa Watanzania wanaoomba nafasi za kazi kwenye Taasisi na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa zenye kuhitaji kupigiwa kura, kuwasilisha majina yao Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili tuweze kuzishawishi Nchi nyingine Wanachama kuunga mkono.

Tisa, maombi ya Kujiunga na Jumuiya; katika mwaka 2011/2012 nchi za Jamhuri ya Sudan na Jamhuri ya Sudan Kusini zimewasilisha maombi ya kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 3(3) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, imeainisha vigezo na sifa ambazo nchi inayowasilisha maombi inapaswa kuwa nazo ili iweze kukubaliwa kuwa Mwanachama wa Jumuiya. Sifa na vigezo hivyo ni kama vifuatavyo:-

(a) Kuikubali Jumuiya kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya;

(b) Kuzingatia misingi ya utawala bora, demokrasia, utawala wa sheria, kuheshimu haki za binadamu na haki za kiraia;

(c) Kuwa na mchango katika kuimarisha mtangamano wa Afrika Mashariki;

(d) Kupakana kijiografia na nchi mojawapo mwanachama;

(e) Kujenga na kuendeleza uchumi wa soko; na

(f) Kuwa na Sera za kiuchumi na kijamii zinazowiana na zile za Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ibara ya 11(9)(c) ya Mkataba, inabainisha kuwa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama ndiyo wenye maamuzi ya mwisho katika kuiingiza nchi yoyote katika Jumuiya. Maombi ya Jamhuri ya Sudan yaliwasilishwa katika Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Nchi uliofanyika mwezi Novemba, 2011 mjini Bujumbura, Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia maombi hayo na kwa kuzingatia sifa na vigezo vilivyobainishwa hapo juu, Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama walibaini kuwa Jamhuri ya Sudan kwa sasa haikidhi baadhi za sifa na vigezo vilivyoainishwa katika Ibara ya 3(3) ya Mkataba hususan kupakana kijiografia na Jumuiya. Aidha, maombi ya Jamhuri ya Sudan Kusini yanafanyiwa tathmini kwa kuzingatia sifa na vigezo vilivyoainishwa katika Ibara 3(3) ya Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Somalia pia iliwasilisha maombi ya kujiunga na Jumuiya mwezi Februari, 2012. Maombi hayo yanatarajiwa kuwasilishwa kwa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama kwa ajili ya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Mahakama ya Afrika Mashariki imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuweza kutoa maamuzi katika kesi kumi na moja (11) kama inavyooneshwa katika Kiambatanisho Na.10. Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inafanya kazi nzuri na inastahili pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bunge la Afrika Mashariki, Bunge hili lilipitisha jumla ya Miswada 11 ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na matakwa ya Mkataba wa Jumuiya, sheria hutungwa kwa kupitia Miswada inayowasilishwa katika Bunge la Afrika Mashariki na Baraza la Mawaziri la Jumuiya au

Miswada Binafsi inayowasilishwa na Wabunge. Wizara imebaini changamoto katika uwasilishaji na upitishaji wa Miswada Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizo ni pamoja na ushirikishaji wa wananchi usiotosheleza; kutokuwapo kwa mfumo unaotoa nafasi kwa Mabunge ya Nchi Wanachama kuchangia katika miswada hiyo na mfumo uliopo kutotoa uwiano kati ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya na Bunge la Afrika Mashariki katika kutunga sheria za Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua changamoto hizi, na kwa kuzingatia misingi ya Jumuiya inayohitaji ushirikishwaji wa wananchi katika uendelezaji wa mtangamano wa Afrika Mashariki na maamuzi ya pamoja, Serikali imewasilisha mapendekezo ya kurekebisha Mkataba ili kuwezesha utungaji wa sheria kupitia Miswada binafsi katika njia bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeandaa Mwongozo wa namna ya kuboresha uwakilishi, wajibu na utendaji wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Mwongozo huo pamoja na mambo mengine unabainisha matakwa ya kisheria na ya kitaasisi kuhusu namna Wabunge wa Afrika Mashariki wanavyopaswa kutoa taarifa na kuwajibika katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kuboresha mahusiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kuwa mwongozo huo utumike ipasavyo ili kutoa nafasi kwa Bunge kupokea taarifa na kupata uelewa wa kina kuhusu mambo yanayojiri katika Bunge la Afrika Mashariki na uendelezaji wa mtangamano kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ushiriki Wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika uendelezaji wa mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushirikiano huu umeendelea kwa kufanya chambuzi na tafiti mbalimbali kwa pamoja na kuandaa misimamo ya Taifa kwa pamoja; kufanya maandalizi kwa pamoja kupitia vikao na vikosi kazi mbalimbali vya kitaifa na kijumuiya; na kushiriki katika vikao mbalimbali vya Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano huo umewezesha maslahi ya pande zote mbili za Muungano kuzingatiwa katika shughuli mbalimbali za Jumuiya na pia katika maamuzi mbalimbali yanayofikiwa kikanda. Vile vile, pande hizi mbili zinashirikiana katika maandalizi ya sera, mikataba, miradi na Itifaki mbalimbali za Jumuiya.

Kwanza, Miradi ya Zanzibar; katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2011/2012, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi saba ya Zanzibar iliyowasilishwa na kujumuishwa katika Miradi ya Jumuiya ili kuombewa ufadhili. Hatua iliyofikiwa katika miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba ni miongoni mwa miradi iliyojadiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) mwezi Novemba, 2011 kwa lengo la kupatiwa ufadhili. Kufuatia majadiliano hayo, Benki ya Maendeleo ya Afrika imekubali kufadhili utafiti wa mwisho wa uwanja huo kwa ajili ya kuweza kutoa ufadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Mkakati wa Uchukuzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliidhinishwa. Katika Mkakati huo mradi wa ujenzi wa Bandari ya Maruhubi ni kati ya miradi ya Tanzania ya kipaumbele iliyojumuishwa katika Mkakati huo. Aidha, katika Mkakati huo, Mradi wa Ujenzi wa Chelezo *(Dry Dock Construction)* na Kivuko *(Roll on Roll Off – RORO)* kati ya Bandari za Zanzibar, Dar es Salaam na Mombasa pia imejumuishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, miradi hii imewasilishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika miradi ya kipaumbele katika Ushirikiano wa Utatu wa *COMESA-EAC-SADC* ili kutafutiwa fedha. Katika miradi hii inayohusu Zanzibar ufuatiliaji wa SMZ ni muhimu kama ilivyo kwa miradi ya kila nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Elimu kwa Umma; ili kuwawezesha Watanzania kunufaika na fursa zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa kutoa elimu kwa umma kuhusu mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara imetoa elimu kwa umma kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo warsha na semina, vipindi vya luninga, redio na mikutano ya wadau, machapisho na vipeperushi kama ifuatavyo:-

(a) Wizara imeandaa vipindi vya Luninga na redio. Jumla ya vipindi vitano kupitia luninga vilirushwa hewani mara mbili kila kipindi. Vipindi hivi vinaendelea kurushwa katika mwaka wa fedha 2012/2013;

(b) Kutoa elimu kwa pamoja *(Joint Sensitization*) na Nchi Wanachama wa Jumuiya katika maeneo ya mipakani. Tanzania kwa kushirikiana na Uganda zilitoa elimu kwa pamoja katika mpaka wa Mutukula; Tanzania na Kenya katika mpaka wa Namanga;

(c) Kuwa na vikao na vyombo vya habari kila mwezi kwa ajili ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa hatua za mtangamano na miradi mbalimbali ya kikanda na maamuzi yaliyofikiwa katika vikao mbalimbali vya Jumuiya;

(d) Kutoa elimu kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na katika Vyuo vya Elimu ya Juu;

(e) Kuchapisha na kushiriki kutoa Elimu kwa Umma katika maonyesho ya Nane Nane na Maadhimisho ya Miaka Hamsini ya Uhuru wa Tanzania; na

(f) Kuandaa na kusambaza machapisho mbalimbali. Machapisho hayo ni kama ifuatavyo: Mafanikio ya Miaka Hamsini ya Uhuru katika Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Utambue Umoja wa Forodha na Fursa zitokanazo na Umoja wa Forodha; Zitambue fursa zitokanazo na Soko la Pamoja; Kipeperushi cha maswali na majibu yanayoulizwa mara kwa mara na wananchi kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki toleo la pili; Jarida la Wizara; Kitini kuhusu Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, taratibu, misingi na hatua za mtangamano zilizofikiwa na mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea na zoezi la kukamilisha Mkakati wa Mawasiliano ambao utatoa mwongozo wa utoaji elimu kwa umma kwa makundi mbalimbali. Rasimu ya Mkakati huo imekamilika. Mkakati unatarajiwa kukamilika na kuanza kutumika katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Utawala na Maendeleo ya Rasilimali Watu; kwanza, Kuimarisha Uwezo wa Wizara Kiutendaji; ili kujiimarisha katika utekelezaji wa majukumu na utoaji wa huduma, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilifanikisha yafuatayo:-

(a) Kujaza nafasi sita (6) za uongozi kwa njia ya uteuzi na nafasi tatu (3) za ajira mpya katika masharti ya kawaida *(Operational Service)* kama inavyoonesha katika kiambatisho Na.12;

(b) Kuwapandisha vyeo Watumishi Thelathini (30);

(c) Kuwathibitisha kazini watumishi saba (7), kuwathibitisha katika Madaraka Watumishi watatu (3) wa ngazi za Uongozi na kuwathibitisha katika vyeo watumishi wanane (8).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara iliandaa mpango wa mafunzo wa miaka mitatu 2011/2012-2013/2014. Hadi kufikia mwezi Mei, 2012, Watumishi 16 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi na wengine 35 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi, ndani na nje ya nchi.

Pili, Masuala Mtambuka; katika 2011/2012, jumla ya watumishi themanini (80) walipatiwa mafunzo elekezi ya maadili katika utumishi wa umma. Mafunzo hayo yalilenga katika kutoa elimu kuhusu usalama wa Serikali na jinsi ya kutunza nyaraka za Serikali katika utendaji kazi wa kila siku wa mtumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapambano dhidi ya maambukizo ya VVU na UKIMWI; katika mwaka 2011/2012, Wizara iliandaa mafunzo ya uhamasishaji kwa watumishi namna ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na kuondoa unyanyapaa kwa wanaoishi na VVU, ambapo Watumishi themanini na saba (87) walihudhuria Mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia imeendelea kuwahudumia watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI kwa kuwapatia virutubisho pamoja na taarifa kuhusu huduma ya tiba. Aidha, Wizara iliendelea kuhimiza

kukwepa vitendo vya unyanyapaa na ubaguzi kwa watumishi wanaoishi na VVU.

Tatu, ushirikishwaji wa Watumishi; Kifungu cha 80(c) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010, kinaielekeza Serikali kusuluhisha na kuamua kwa wakati migogoro yote ya kikazi na kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi. Katika kutekeleza maagizo haya ya Ilani, na ili kuwezesha utendaji wenye tija na amani sehemu ya kazi, Wizara imeendelea kuwashirikisha wafanyakazi katika yafuatayo:-

(a) Vikao vya Uongozi wa Wizara na watumishi wote vya kila mwaka;

(b) Vikao vya Menejimenti vya kila mwezi;

(c) Vikao Elekezi vya Kimkakati (Retreat) vya Menejimenti vya kila robo mwaka;

(d) Kuzingatia Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004, kwa kufanya Mikutano ya Baraza la Wafanyakazi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilifanya vikao viwili (2) vya Baraza la Wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa mapato na matumizi; katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi wa Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma, Sheria ya Ununuzi ya Umma, na maagizo ya Serikali ya kuwa na vikao vya kila robo mwaka vya Kamati ya Udhibiti wa Mapato na Matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara iliandaa na kutekeleza Mpango wa Ununuzi wa mwaka 2011/2012. Naomba kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara imeweza kupata Hati Safi ya Ukaguzi wa Hesabu toka Ofisi ya Mdhitibi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilifanyiwa Tathmini na Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Ununuzi wa Umma *(Public Procurement Regulatory Authority-PPRA)* kwa lengo la kupima namna Wizara inavyozingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya Mwaka 2004 na Kanuni zake. Tathmini hiyo imeonesha kuwa Wizara inazingatia kwa kiwango cha juu (84%) matakwa ya sheria hiyo pamoja na kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mchango katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatarajiwa kukamilisha kulipa michango yao ifikapo mwezi Desemba ya kila mwaka. Katika mwaka 2011/2012, kila Nchi Mwanachama wa Jumuiya ilipaswa kulipa mchango wa Dola za Kimarekani 6,333,700, ambazo ni sawa na Tshs. 11,016,151,636. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imelipa mchango huo kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto inayojitokeza ni kutokamilisha malipo kwa wakati, na kiwango cha mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

kuendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kupanuka kwa majukumu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ongezeko hilo limekuwa haliendani na ongezeko la kiasi kinachotengwa katika bajeti ya Wizara. Wizara inaendelea kujadiliana na Wizara ya Fedha ili kuzipatia ufumbuzi changamoto hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wizara na kwa niaba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, napenda kuwashukuru kwa dhati Washirika wa Maendeleo wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza Program na Miradi mbalimbali katika Wizara na katika Jumuiya hususan, Serikali za Uingereza, Ufaransa, Kanada, Norway, Sweden, Ubelgiji, Denmark, Finland, Marekani, Japani na Ujerumani; Mashirika na Taasisi za Kimataifa za Jumuiya ya Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *DFID*, Benki ya Japani ya Maendeleo ya Kimataifa, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japani, Benki ya Dunia, *GIZ, Rockefeller Foundation, Kilimo Trust, The Investment Climate Facility for Africa (ICF), AWEPA, African Capacity Building Facility (ACBF), British American Tobacco (BAT); Trade Mark East Africa (TMEA), na International Planned Parenthood Federation Africa Region (IPPFAR).* (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kutoa pongeza kwa nchi zote ambazo zimewasilisha hati zao za utambulisho wa kidiplomasia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto na hatua zilizochukuliwa; pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya

Wizara katika mwaka wa fedha 2011/2012, bado zipo changamoto ambazo Wizara inakabiliana nazo. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(a) Wizara za kisekta kutotoa uzito stahiki kwa masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, na hivyo, kutohuisha masuala ya uendelezaji wa mtangamano katika mipango ya kitaifa na kisekta, na hivyo kutoshiriki kikamilifu katika uendelezaji wa mtangamano, hususan katika maeneo yanayowahusu;

(b) Kupanuka kwa haraka kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kusikowiana na ongezeko la rasimali watu na fedha katika Wizara;

(c) Ufinyu wa bajeti unaosababisha Wizara kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu;

(d) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu mtangamano, na hivyo kuwafanya Watanzania kutozitumia kikamilifu fursa zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(e) Baadhi ya vyombo vya habari kutoa taarifa au habari zenye kupotosha kwa kutokujua au kwa makusudi; na

(f) Baadhi ya wadau wa ndani na nje kutaka kuharakisha uendelezaji wa mtangamano bila kujali athari za kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto zilizobainishwa, Wizara imechukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuandaa Sera ya Taifa ya Mtangamano;

(b) Kuendelea kuhimiza na kuzishirikisha sekta mbalimbali, ili kuwezesha kutoa uzito stahiki utekelezaji wa mtangamano katika sekta husika;

(c) Kufanya tafiti na chambuzi ili kujipanga katika majadiliano mbalimbali na kuweza kubainisha fursa na changamoto za mtangamano; kuandaa mikakati ya kuwawezesha Watanzania kuzifahamu na kuzitumia fursa zilizopo na jinsi ya kukabiliana na changamoto zilizopo;

(d) Kuandaa vikao vya maandalizi vya wadau kabla na baada ya vikao vya Jumuiya ili kuweza kujipanga na kuhakikisha kuwa mtangamano unaendelezwa hatua kwa hatua ili kujenga mtangamano himilivu na endelevu na kuwa maslahi ya Taifa yanalindwa katika uendelezaji wa mtangamano na maamuzi yaliyofikiwa katika Jumuiya yanatekelezwa kwa wakati;

(e) Kutekeleza mpango wa Elimu kwa Umma kupitia mbinu na mikakati mbalimbali;

(f) Kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, ili Halmashauri ziweze kuhuisha na kukasimia masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Bajeti na Mipango yao na pia kutoa mafunzo kwa

maafisa walioteuliwa kutoa mafunzo toka katika kila Halmashauri ili waweze kutoa elimu kwa umma katika maeneo yao;

(g) Kuandaa mpango wa utekelezaji wa Soko la Pamoja kwa kuainisha mikakati ya kisekta, hatua za kuchukua, majukumu ya kila mdau katika utekelezaji wa Soko la Pamoja na kuwawezesha Watanzania kunufaika ipasavyo; na

(h) Kuandaa na kutekeleza mpango endelevu wa mafunzo ili kujenga uwezo wa watumishi na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara, kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na wadau mbalimbali, itaendelea na utekelezaji wa majukumu yake katika mwaka 2012/2013. Shughuli zitakazopewa kipaumbele katika mwaka wa fedha 2012/2013 ni pamoja na:-

(a) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake;

(b) Kukamilisha mchakato wa Serikali kuidhinisha Sera ya Taifa ya Mtangamano ili ianze kutekelezwa;

(c) Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara ili uendane na Mkakati Maendeleo na Mkakati wa Maendeleo wa Jumuiya;

(d) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja;

(e) Kutoa Elimu kwa Umma ili kuwawezesha wadau mbalimbali kuzifahamu na kuzitumia fursa zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(f) Kukamilisha zoezi la kuwianisha sheria, kanuni na taratibu ili sheria za Taifa ziendane na matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja;

(g) Kuratibu na kuongoza ushiriki wa Tanzania katika majadiliano ya ushirikiano katika Utatu wa *COMESA-EAC-SADC;*

(h) Kuratibu na kuongoza ushiriki wa Tanzania katika majadiliano ya kuandaa Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki;

(i) Kuratibu na kuongoza ushiriki wa Tanzania katika majadiliano ya kuandaa mfumo wa utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(j) Kushiriki na kuongoza ushiriki wa Tanzania katika uhakiki utayari wa Sudan Kusini kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(k) Kuratibu utekelezaji wa Mitandao ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Jumuiya (Barabara, Reli, Mkongo wa Taifa na Mpango wa Uzalishaji na Usambazaji wa Nishati);

(l) Kuratibu utekelezaji wa Programu za Kisekta, katika sekta za uzalishaji na huduma za jamii;

(m) Kuratibu maandalizi ya Itifaki na sheria mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Itifaki ya Amani na Usalama; Itifaki ya Utawala Bora; Itifaki ya Kupambana na Rushwa; Itifaki ya Kuongeza Mamlaka ya Mahakama; Majadiliano ya Mkataba wa Ushirikiano kiulinzi (*Mutual Defence Pact*); kukamilisha maandalizi ya Mkataba wa Mfuko wa Maendeleo wa Afrika Mashariki *(East African Development Fund);* Mfumo wa Sheria na Vituo vya Pamoja vya Mipakani; Sheria ya Kuwianisha na Kudhibiti Uzito wa Magari na Itifaki na sheria ya viwango na ubora;

(n) Kuratibu utekelezaji wa Sera na Mikakati mbalibali ya Jumuiya ikiwa ni pamoja na Sera ya Uendelezaji Viwanda, Sera ya Usalama wa Chakula na Mpangokazi wa kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi na mpango wa kuondoa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Vituo vya Utoaji Huduma kwa Pamoja Mipakani;

(o) Kufanya chambuzi ili kuandaa msimamo unaozingatia maoni ya Wananchi katika kuandaa Modeli na Mfumo wa Shirikisho la Kisiasa la Jumuiya;

(p) Kujenga uwezo wa Wizara kiutendaji ili kuwa kitovu cha mawazo *(Think Tank)* katika masuala ya mtangamano na kufanya tathmini na chambuzi za kina kwa kushirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali ili kuwezesha kujenga hoja na misimamo yenye

kuzingatia maslahi ya Taifa katika majadiliano na katika hatua mbalimbali za mtangamano na;

(q) Kulipa mchango wa Tanzania katika Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Urambo Mashariki kwa imani, ushauri na ushirikiano wanaonipa ambao umeniwezesha kufanya kazi yangu ya Ubunge kwa ufanisi na tija. Nawaahidi wote kuwa nitaendelea kushirikiana nao kuhakikisha kuwa maendeleo ya Wilaya ya Urambo yanakua kwa kasi na kuweza kufikia viwango vya kuridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si vema nimalize hotuba yangu bila kumshukuru mke wangu mwema na mpendwa, Mheshimiwa Margaret ambaye wakati wote amekuwa mshauri wangu wa karibu. Naishukuru pia familia yangu kwa jumla kwa upendo na ushirikiano wao kwangu ambao umeniwezesha nyakati zote kutekeleza majukumu yangu kwa weledi, ujasiri na kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya Fedha za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013; ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu na mipango iliyoainishwa hapo juu na kuweza kufikia malengo tarajiwa, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaomba kuidhinishiwa jumla ya sh. 16,643,667,000 kwa mchanganuo ufuatao: Mishahara *(PE)* Sh. 1,378,292,000; Matumizi Mengine *(OC)* Sh. 15,265,375,000; Jumla Sh. 16,643,667,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya *www.meac.go.tz.* Hotuba hii inapatikana pia katika lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Samuel Sitta, kwa kusoma hotuba yako kwa umahiri mkubwa na hoja uliyoitoa imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge kwa kuwakumbusha tu, Mheshimiwa Sitta bado anaendelea na viwango vyake vilevile maana katika hotuba hii ametuletea hotuba ya kiswahili na hotuba ya Kiingereza, wenzangu na mimi mmezoea kulalamika haya sasa leo mambo yako hapa. Lakini vile vile vipo viambatanisho vya kutosha, viambatanisho vitatu vya ziada vyenye taarifa muhimu sana kwa ajili yetu vinatufanya tuweze kuwa na mjadala ambao una uwezesho mkubwa sana.

Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki tunakushukuru sana na tunawashukuru mara nyingine Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa kuwepo.

Waheshimiwa Wabunge sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) na 114(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2012/2013 na kuliomba Bunge hili liipokee na kujadili na hatimaye kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina Fungu *(Supply vote)* moja ambalo ni Fungu 97 linalohusika na majukumu ya Wizara na michango ya Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamati ilifuatilia utekelezaji

wa Mpango wa Bajeti kwa Fungu hili kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa namna mbalimbali. Mojawapo ya njia iliyotumika ni kufuatilia kwa karibu hali ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na hatua zinazofikiwa katika kuelekea Shirikisho la kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine iliyotumika ni kupokea na kuchambua taarifa zilizowasilishwa na Wizara hii kila ilipobidi. Katika ufuatiliaji huo, jambo kubwa lililojitokeza ni changamoto ya kuongezeka kwa kiwango cha michango ya uanachama katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tanzania ongezeko la ada ya uanachama haliendani na kiasi kinachotengwa katika bajeti ya Wizara hii. Ni maoni ya Kamati kuwa hali hiyo inapaswa kurekebishwa kama zinavyofanya nchi nyingine wanachama wa Jumuiya hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa malengo na mapitio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012; pamoja na kufuatilia utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha Julai – Desemba, 2011, tarehe 08 Juni, 2012, Kamati ilipitia na kujadili Taarifa ya Wizara hii kuhusu utekelezaji wa malengo ya Bajeti kwa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mapitio hayo, Kamati ilielezwa kuhusu utekelezaji wa malengo ya Bajeti sambamba na taarifa kuhusu mtiririko wa bajeti. Vile vile Taarifa iliyowasilishwa ilieleza kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati Bungeni

wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2011/2012, yalikuwa kumi na nne (14) likiwemo lile la kukamilisha sera ya Taifa ya mtangamano wa Afrika Mashariki ambayo hadi sasa haijakamilika. Maelezo ya Wizara yalionesha kuwa hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa Rasimu ya Sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile lengo lingine miongoni mwa malengo hayo lilihusu kukamilisha uchambuzi wa changamoto za uanzishwaji wa shirikisho la kisiasa. Katika lengo hili pamoja na maelezo ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kamati ilibaini kuwa bado kuna kazi kubwa ya kufanya kuelekea Shirikisho la Kisiasa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majadiliano ya *EPA* Kamati ilibaini kuwepo kwa masuala yenye mvutano baina ya Umoja wa Ulaya na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hali ilivyo, inaonekana Jumuiya ya Ulaya inaendelea na msimamo wake ambao unaathiri vibaya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ili nchi za Afrika Mashariki zijiweke nafasi nzuri katika majadiliano ya *EPA* jukumu la Sekretarieti ya Afrika Mashariki litekelezwe kwa umakini mkubwa katika kutetea maslahi ya kiuchumi kwa kanda yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mambo ya msingi yaliyozingatiwa na Kamati wakati wa kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya

Wizara hii ni mapitio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kama yalivyoripotiwa kwenye kikao cha Kamati. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara hii haikuweza kukusanya mapato kutokana na kutokuwa na chanzo cha mapato nje ya fedha zinazopokelewa kutoka Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa fedha taarifa ilionesha kuwa hadi tarehe 28 Mei, 2012 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya sh. 16,997,735,608/=, kati ya sh. 17,423,276,164/= zilizoidhinishwa na Bunge. Kiasi hiki ni karibu sawa na aslimia 97.6 ya bajeti iliyoidhinishwa. Uchambuzi ulionesha kuwa asilimia 68 ya kiasi cha matumizi mengineyo *(OC)* ilitumika kulipa mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kuwa shughuli za uratibu zinazopaswa kutekelezwa na Wizara hii zilitumia kiasi kidogo cha bajeti iliyotengwa kwa ajili ya uendeshaji. Ili uanachama wetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki uwe na tija Serikali iangalie kwa kina uwiano huu wa kibajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Kamati ilikuwa na Maoni na Ushauri katika masuala matano. Miongoni mwa ushauri huo ni kuhusu kasi ya kukamilisha Sera ya Taifa ya Mtangamano wa Afrika Mashariki. Ili kujiridhisha na namna Serikali ilivyozingatia ushauri wake, Kamati ilitaka kujua kuhusu utekelezaji wa ushauri huo kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa sehemu kubwa ya ushauri imezingatiwa. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuongezwa kwa kasi ya maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano. Katika kikao cha tarehe 8 Juni, 2012, Kamati ilielezwa kuwa Rasimu ya Sera hiyo imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ushauri kuhusu fedha kwa ajili ya michango na ada ya Jumuiya, Kamati ilishauri kuwa michango na ada hiyo iondolewe katika Fungu 97 sambamba na kuongeza msisitizo katika masuala ya mtangamano. Taarifa ilionesha kuwa ushauri huu unaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo yaliyotolewa, Serikali imezingatia ushauri kwa kuihamisha Wizara hii kutoka katika nguzo ya tatu ya utawala bora na kuiwekwa katika nguzo ya kwanza ambayo ni ya uchumi na kuongeza pato la Taifa. Kundi hilo kwa taarifa zilizotolewa, ni kundi la kipaumbele katika Mpango wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya ushauri uliozingatiwa vile vile Kamati ilijulishwa kuhusu ushauri unaoendelea kufanyiwa kazi. Kwa mfano, Kamati ilishauri kianzishwe Kitengo mahususi cha utafiti kitakachowezeshwa na kupewa rasilimali za kutosha kufanya tafiti mbalimbali. Taarifa ya Wizara ilionesha kuwa pendekezo lililopelekwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu uundaji wa kitengo hicho halikuidhinishwa. Kamati inasisitiza kuwa kwa vyovyote iwavyo, ili uanachama wa Tanzania katika

Mtangamano wa Afrika Mashariki uwe na tija, suala la utafiti ni jambo la Msingi. Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ijenge hoja na kuanzisha kitengo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine wa utekelezaji hafifu wa ushauri wa Kamati ni kuhusu elimu kwa umma. Kamati iliishauri Serikali kuongeza juhudi ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mtangamano wa Afrika Mashariki na hatua zake. Taarifa zilionesha kuwa Wizara imeendelea kuzingatia ushauri huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati ilielezwa kwamba utoaji wa elimu kwa umma umeendelea kwa kasi ndogo kuliko mahitaji na matarajio ya wananchi kutokana na ufinyu wa bajeti. Ni vema Serikali ilipe uzito stahiki suala la elimu kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo ya Serikali kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, bado kuna umuhimu mkubwa wa kufanyia kazi ipasavyo ushauri ambao haujazingatiwa kikamilifu. Kufanya hivyo kutawezesha upatikanaji wa manufaa ya mtangamano wa Afrika Mashariki sambamba na kuongeza tija ya ushirikiano huu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha tarehe 08 Juni, 2012, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu malengo ya bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na kuyachambua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo yanayopangwa kutekelezwa ni jambo la msingi katika uchambuzi wa bajeti. Kwa kuzingatia uhusiano baina ya majukumu yanayopangwa kutekelezwa na kiasi cha fedha kinachokadiriwa kutumika, Kamati ilipitia na kuchambua majukumu ishirini yanayolengwa na Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2012/2013. Majukumu hayo ni pamoja na kukamilisha zoezi la kuwianisha sheria, kanuni na taratibu ili sheria za Taifa ziendane na matakwa ya itifaki ya Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa jukumu hili lilipangwa kukamilishwa katika mwaka wa fedha 2011/2012, lakini linapangwa tena katika mwaka wa fedha 2012/2013. Hii ni ishara kuwa jukumu hilo halikutekelezwa ipasavyo katika mwaka wa fedha uliopita na kwamba lengo hili la bajeti halikufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu lingine lilikuwa ni kufanya uchambuzi ili kutayarisha msimamo wa Tanzania unaozingatia maoni ya wananchi katika kuandaa modeli na mfumo wa shirikisho la kisiasa la Jumuiya. Kamati inatambua kuwa ingawa shirikisho la kisiasa ni hatua inayotarajiwa katika Mtangamano wa Afrika Mashariki, lakini shirikisho hilo litakuwa na tija kwa Mataifa yote iwapo kila Nchi Mwanachama itachukua hadhari kubwa ya wasiwasi unaooneshwa na wananchi wake. Kwa upande wa Tanzania, bado wananchi wengi wanaendelea kuwa na wasiwasi kuhusu hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii yalilenga pia kuiwezesha

Wizara kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya itifaki na sheria mbalimbali za Jumuiya. Hata hivyo, taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati inaonesha kuwa moja ya changamoto katika utekelezaji jukumu hilo ni Wizara za Kisekta na Wadau wengine kutotoa uzito stahiki kwa masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kuwa hali hiyo inaweza kusababisha kutofanikiwa kwa jukumu linalopangwa kutekelezwa. Ni vema Serikali ilifanyie kazi jambo hilo kwa kuzielekeza Wizara zote kuzingatia masuala ya mtangamano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2012/2013, Kamati ilielezwa kuwa Wizara hii inaomba kuidhinishiwa jumla ya sh. 16,643,667,000/- ambazo zote ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Ni dhahiri kuwa Wizara hii haijapangiwa miradi ya Maendeleo licha ya kuwa inahitaji Ofisi badala ya kupanga. Mtoa hoja alifafanua madhumuni ya maombi ya fedha kwa kila Kasma na kifungu.

Kamati ilichambua kwa kina Makadirio hayo na kubaini kuwa kiasi hiki kimepungua kwa asilimia 4.5 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka uliopita lakini majukumu ya Wizara yanaendelea kuongezeka kutokana na hatua inayofikiwa katika mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la bajeti lililoathirika zaidi ni Kasma ya matumizi mengineyo (*OC*)

ambayo imepungua kwa asilimia 6.3 huku matumizi ya pango yakichukua asilimia tano ya Kasma hii. Eneo pekee lililoongezeka ni Kasma ya Mishahara iliyoongezeka kwa asilimia 2.2. Maelezo ya Wizara yameonesha kuwa ongezeko hili pamoja na sababu nyingine linatokana na kuongezeka kwa idadi ya Watumishi na nyongeza ya Mishahara kwa mujibu wa muundo wa utumishi wa umma. Aidha, katika kuchambua zaidi ongezeko la Mishahara, Kamati ilibaini kuwa wakati mwaka wa fedha 2011/2012 bajeti ya mishahara ilikuwa asilimia saba ya matumizi mengineyo (*OC*), Makadirio ya mwaka 2012/2013 yanaonesha kuwa mishahara ni asilimia tisa ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia uwiano huo tunaweza kusema kwamba msisitizo wa bajeti hii umeongezeka katika masuala ya Watumishi ili kuzingatia stahili zao kuliko shughuli za uendeshaji kwa ujumla. Kamati ina maoni kuwa ni jambo jema kutopuuzia stahili za watumishi, lakini ni vizuri kuzingatia matumizi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Kamati ilibaini kuwa mwenendo wa bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa miaka minne iliyopita hauwiani na hali ya ongezeko la uzito wa jukumu la msingi la Wizara hii. Kwa maelezo hayo, ni dhahiri kwamba tija itakayopatikana kwa ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwa kidogo ikilinganishwa na inavyopaswa kuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati pamoja na ufuatiliaji uliofanyika, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(1) Kuna umuhimu mkubwa kwa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa na utaratibu mzuri zaidi wa kuwajulisha Mawaziri na Wakuu wa Nchi katika jumuiya hiyo kuhusu majadiliano yote ya Kikanda kama vile suala la ubia wa maendeleo ya kichumi;

(2) Serikali iongeze kasi ya kushughulikia rasimu ya Sera ya Taifa ya Mtangamano ili kuongeza ufanisi katika fursa zinazotokana na ushirikiano wa Afrika Mashariki;

(3) Pamoja na maelezo ya Wizara kuhusu kutopata idhini ya kuanzisha kitengo cha utafiti, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa bado kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na kitengo hiki kwa madhumuni ya kuwawezesha Watanzania kubaini na kuzitumia fursa za kiuchumi, kisiasa na kijamii ndani ya ushirikiano wa Afrika Mashariki;

(4) Ushauri wa Kamati kuhusu utaratibu wa kulipa michango yote ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki moja kwa moja kutoka Hazina, uzingatiwe ili kuiwezesha nchi yetu kuwa na Sauti katika Jumuiya hiyo. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa jukumu la kulipa madeni ya Jumuiya ya Afrika Mashariki linatekelezwa kwa wakati;

(5) Ili kuwawezesha Watanzania na Taifa kwa ujumla kunufaika ipasavyo na mtangamano wa Afrika

Mashariki, Wizara hii ipatiwe fedha za kutosha kuratibu shughuli za ushirikiano wa Afrika Mashariki sambamba na kupewa rasilimali nyingine muhimu kwa utekelezaji wa majukumu yake yaliyoorodheshwa kwenye Hati ya Serikali *(Government instrument);*

(6) Kwa kuzingatia umuhimu wa maoni ya wadau ni vema kuwashirikisha Wataalam wa Sekta mbalimbali katika majadiliano ya kiuchumi chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki sambamba na kuzingatia ushauri wao kwa kadiri inavyowezekana;

(7) Pamoja na manufaa yanayoweza kupatikana katika itifaki ya kushirikiana kiulinzi, bado kuna umuhimu kwa Serikali kuongeza umakini ili kuepuka uhasama wa vikundi vya kigaidi kama vile Al-Shabab;

(8) Kwa kuwa Kiswahili katika ulimwengu wa leo ni bidhaa na kwamba Kiswahili sahihi na sanifu kinatoka Tanzania na kwa kuwa Wataalam wa lugha hii tunao wa kutosha, Serikali itumie fursa zilizopo katika soko ndani ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kukiuza kama bidhaa kutoka Tanzania. Ili kufanikisha azma hiyo, Wizara hii ishirikiane na Wadau wengine wa lugha hii kujipanga na kuuza bidhaa hii;

(9) Serikali ihakikishe kuwa barabara zinazojengwa chini ya miradi ya ushirikiano wa Afrika Mashariki zinajengwa kwa kiwango kinachotakiwa na kumalizika kwa wakati; na

(10) Ili kuzingatia maslahi ya Taifa na wananchi ipasavyo utaratibu wa

kukataa au kukubali mambo mbalimbali katika uendeshaji wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki uzingatie maoni ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii pamoja na maoni ya Kamati. Nawashukuru Mheshimiwa Samwel S. Sitta, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mheshimiwa Dkt. Abdullah J. Saadalla, Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ufafanuzi walioutoa kwa Kamati kila tulipokutana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru Dkt. Stergomena Tax, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Watumishi wengine wa Wizara hiyo kwa juhudi zao katika uratibu wa masuala ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukurani za pekee nazitoa kwa Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao wakati wa kupitia na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kwa kuthamini mchango wao, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mwenyekiti; Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Z. Chiligati, Mjumbe; Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mjumbe; Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mjumbe; Mheshimiwa Sadifa Juma

Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Muhamed Seif Khatib, Mjumbe; Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mjumbe; Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mjumbe na Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Mchungaji Israel Y. Natse, Mjumbe; Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mjumbe; Mheshimiwa Brig. Jenerali Mstaafu Hassan A. Ngwilizi, Mjumbe; Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mjumbe; Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mjumbe; Mheshimiwa Mohamed I. Sanya, Mjumbe; Mheshimiwa John M. Shibuda, Mjumbe; Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mjumbe; Mheshimiwa Annastazia J. Wambura, Mjumbe na Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa ambaye ndio mimi hapa Mjumbe. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu nawashukuru Ndugu Athuman Hussein na Ramadhani Issa, Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kufanikisha taarifa hii kwa wakati. Nawashukuru pia watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashilila, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuijadili pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Wizara hii kama alivyowasilisha mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaunga mkono hoja hii, naomba nichukue nafasi hii na fursa hii kushukuru sana familia yangu ambayo inaniunga mkono na kushikiriana nami hasa wakati ninaposhiriki kufanya na kutekeleza majukumu yangu ya kazi za Kibunge. Naomba nimtaje mke wangu mpenzi Siasi Vuai Sumai kwa kuniunga mkono, hali kadhalika familia yangu. Mwisho, kabisa wananchi na wapiga kura wa Jimbo la Amani. (*Makofi*)

Mheshmiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi)*

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS - (K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA USHIRIKIANO NA AFRIKA MASHARIKI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kwa kunijalia uhai na kuniwezesha kuwepo hapa leo kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 kanuni ndogo ya (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee natoa shukrani za dhati kwa wazazi wangu wapenzi Baba na Mama yangu kwa malezi bora wanayoendelea kunipa hadi sasa. Aidha, naishukuru familia yote kwa ushirikiano wanaonipa ambao unaniwezesha kutimiza majukumu yangu ya Kibunge na Kichama. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima namshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe kwa kutuamini na kutupa dhamana mimi na Waziri Kivuli Mheshimiwa Ezekeah Wenje kusimamia Wizara hii ya Afrika Mashariki. Tunapenda kumhakikishia kuwa tutatekeleza wajibu wetu kwa uwezo na nguvu zetu zote ili kukidhi matarajio ya Watanzania kunufaika na Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, nawapongeza sana viongozi na makamanda wote wa CHADEMA kwa kazi kubwa wanayoifanya bila kuchoka ya kuwahamashisha Watanzania kushiriki kikamilifu katika michakato ya kisiasa kupitia operesheni za *M4C* ambayo imefanikiwa kwa kiwango kikubwa sana. Aidha, natoa wito kwa wananchi wote kuendelea kukiunga mkono Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ili kiweze kuunda Serikali ifikapo mwaka 2015 na hivyo kukidhi matarajio na kiu ya Watanzania ya kuleta mabadilko ya kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenendo wa uchumi wa dunia na athari zake kwa shirikisho la Afrika Mashariki. Tunaposoma hotuba hii ni wakati ambao Ulimwengu unashuhudia kuporomoka kwa uchumi na uwekezaji kwa kipindi cha mwaka 2011 na hata baadhi ya nchi kufilisika kama vile Ugiriki na nyingine kuhitaji msaada wa haraka ili kuziepusha na tishio la kufilisika kama ilivyo sasa katika nchi ya Hispania na nchi nyingine za Jumuiya ya Ulaya. Aidha, ni wakati ambao tunashuhudia Mataifa ya Asia kama China na

India uchumi wake ukiendelea kuimarika na kukua kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa uchumi wa dunia ulitazamiwa kuporomoka kutoka asilimia nne za mwaka 2011 na kufikia kiwango cha asilimia 3.5 kwa mwaka 2012 kutokana na shughuli hafifu za kiuchumi kwa kipindi cha pili cha  mwaka 2011 na mwanzo wa mwaka 2012 na inategemewa kuwa ukuaji wa uchumi utaendelea kuwa dhoofu na hasa nchi za Ulaya ambao wanategemewa kuwa kwenye kipindi cha kati cha mdororo wa kiuchumi kutokana na kiwango cha madeni na kutokuimarika kwa uchumi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Ulaya. Nchi ya Japan uchumi wake uliporomoka kutokana na mafuriko yaliyoikumba nchi ya Thailand na hivyo kuharibu miundombinu na bandari za nchi hiyo na hivyo biashara kuwa ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* na Tathmini ya Uchumi wa Dunia ya Aprili, 2012,  inategemewa kuwa ukuaji wa pato la Taifa *(GDP)* kwa nchi zenye uchumi wa kati na zile zinazoendelea utapungua kwa  kiwango cha kutoka asilimia 6.2 ya mwaka 2011 hadi kufikia kiwango cha asilimia 5.7 mwaka 2012. Aidha, kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki pato la Taifa *(GDP)* linakadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 6.0 kwa mwaka huu wa fedha na hii inatokana na kuongezeka kwa kiwango cha biashara baina ya nchi wanachama kutokana na uwepo wa Itifaki ya Soko la Pamoja na Nchi Wanachama kuendesha biashara na nchi za Asia ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uzalishaji inachangia kwa kiwango cha asilimia 8.9 kwenye pato la Taifa *(GDP)* kwa nchi za Jumuiya ya Afrika mashariki *(EAC)*. Kiwango hiki ni cha chini kwa kuwa sekta ya uzalishaji inapaswa kuchangia wastani wa asilimia 25, kiwango ambacho Nchi Wanachama walikubaliana kukifikia ifikapo mwaka 2032.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wakati ambao uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki unakadiriwa kukua kwa wastani kwa Nchi Wanachama kama ifuatavyo:-

Kenya 5.2% mwaka 2012 na 5.7% mwaka 2013; Uganda 4.2% mwaka 2012, Tanzania kutoka ukuaji wa 6.7% mwaka 2011 na kuwa 6.4 % mwaka 2012 , Rwanda kiwango cha ukuaji kitashuka kutoka kiwango cha ukuaji wa 8.8% mwaka 2011 na kuwa 7.6 % mwaka 2012 na kuwa chini zaidi kwa 7% mwaka 2013, Burundi kiwango kitakuwa kutoka 4.2% mwaka 2011 hadi 4.8% na 5% mwaka 2012 na 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki kutokana na kuwa na Ushuru wa Pamoja wa Forodha (*Customs Union*) inaonesha kuwa ukuaji wa biashara baina ya Nchi Wanachama imeongezeka kwa kiwango kikubwa kutoka dola bilioni mbili mwaka 2005 na kufikia dola bilioni nne kwa mwaka 2011. Vile vile Jumuiya imeshuhudia kuwa nchi zilizokuwa zinaagiza tu bidhaa sasa nazo zinauza kwenye Jumuiya na kuwa na faida. Miongoni mwa nchi hizo ni pamoja na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na takwimu hizo ni dhahiri kuwa kuna nuru mbeleni, Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu ni kwa jinsi gani kama Taifa tunajiandaa katika kuzitumia fursa hizi za kiuchumi kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maamuzi na maazimio mbalimbali ya Jumuiya ya Afrika mashariki; yamefanyika maamuzi mengi sana katika kufikia malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ingawa maamuzi na maazimio hayo ni mazito na yana madhara ya moja kwa moja kwa nchi yetu bado taarifa zake hazifahamiki kwa Bunge letu na kwa wananchi kwa jumla. Hapa ni baadhi ya maamuzi na maazimio yaliyofikiwa hadi sasa:-

(a) Jumuiya ilishiriki kwenye majadiliano ya kibiashara yaliyofanyika mwezi Disemba, 2011 na kuingia mkataba na Jumuiya ya wafanyabiashara wa Uturuki chini ya umoja unaojulikana kama *Africa-Turkey Partinership,* mkataba ambao utaingiza zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni 350 kutokana na biashara mbalimbali. Hili litafanywa na sekta binafsi zaidi;

(b) Uandaaji wa Sheria ya Kudhibiti Uhalifu wa Kimtandao “Cyber Laws” hatua ya kwanza imemalizika na sasa ipo hatua ya pili ( Phase II );

(c) Uandaaji wa itifaki ya pamoja kuhusiana na kuwa na kituo kimoja cha utalii *Single Tourist Destination Protocol* na uwepo wa hati ya kusafiria na *visa* moja ya utalii *Single Tourist Visas* kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya;

(d) Kuandaa mfumo mmoja wa mitaala ya elimu ili kuweza kukidhi haja ya Soko la Pamoja la ajira la Jumuiya;

(e) Kusaini makubaliano ya pamoja *(MOU)* juu ya ushirikiano wa masuala ya kiulinzi mwaka 1998 na sasa unafikia hatua ya kuwa Itifaki *(Protocol)* na itakubaliwa/itaridhiwa ifikapo 30 Novemba, 2012;

(f) Zipo sheria mbalimbali zilizoandaliwa na kupitishwa kama vile:-

*The East African Community Human and Peoples' Rights Bill, 2012; The East African Legislative Assembly Elections Bill, 2011; The East African Customs Management (Amendment) Bill, 2012; The East African Community Trans-Boundary Ecosystems Management Bill, 2010; The EAC Polythene Materials Control Bill, 2011; The East African Community Elections Bill, 2012; The Administration of the East African Legislative Assembly Bill, 2011 and the East African Parliamentary Institute Bill, 2011;* na

(g) Kuanzishwa kwa Umoja wa Wafanyabiashara wa Samaki Ukanda wa Ziwa Victoria "*The Lake Victoria Fisheries Organization (LVFO)* ambacho ni chombo chenye mamlaka juu ya usimamizi wa shughuli zote za uvuvi katika Ziwa Viktoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika maamuzi na sheria kama hizi na mengineyo mengi yanayoamuliwa ni mambo makubwa sana kwa mustakabali wa nchi

yetu na ustawi wa Taifa letu kwa ujumla wake kwani zipo itifaki na sheria ambazo sasa zinakwenda kusimamia chaguzi zetu, Majeshi yetu, Rasilimali zetu kama samaki wa Ziwa Victoria, utalii, elimu yetu na maisha yetu kwa jumla .Kambi ya Upinzani inashauri ifuatavyo ili Bunge hili liweze kuwa na taarifa za kina kuhusiana na kila hatua ambayo tunapiga kuelekea shirikisho la kisiasa la Jumuiya ya Afrika Mashariki:-

(i) Iundwe Kamati mpya ya kudumu ya Bunge ambayo itakuwa inapokea na kujadili Miswada, Itifaki na mwenendo mzima wa Jumuiya na iwe na wajibu wa kutoa taarifa yake kwenye vikao vya Bunge mara kwa mara ili tuweze kuzijadili na kuishauri Serikali kikamilifu. Aidha, Kamati hii iwe na jukumu la kushughulikia nidhamu ya Wabunge wa Afrika Mashariki.

(ii) Pawepo na vikao vya pamoja baina ya Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wanaotoka Tanzania na Kamati hii ya Bunge ili kuweza kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusiana na utendaji wao wa kazi na masuala mbalimbali ya Jumuiya.

(iii) Tuwe na utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na kila hatua ambayo imefikiwa ili kuepusha kuwa na Jumuiya ya viongozi na badala yake iwe ni Jumuiya ya wananchi kwani watakuwa na taarifa za kina kuhusiana na kila hatua iliyofikiwa.

(iv) Kabla ya itifaki mbalimbali kuridhiwa ni vema Serikali ikaziwasilisha kwenye Bunge ili ziweze kujadiliwa

na kupitishwa au kukataliwa na Bunge kama ambavyo tumekuwa tukifanya kwa zile za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapendekezo ya jumla kuhusiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kuhakikisha kuwa Jumuiya ya Afrika mashariki inafanya kazi kwa ufanisi zaidi na kuhakikisha kuwa nchi yetu inakuwa sio kikwazo katika kufanikisha biashara kwenye Jumuiya, Kambi ya Upinzani tunapendekeza hatua zifuatazo ziweze kuchukuliwa:-

(a) Ukaguzi wa mizigo mbalimbali unaofanywa na vyombo vya dola kama vile Polisi na Mamlaka ya Mapato uwe unafanyika kwenye kituo kimoja na sio kufanyika kila eneo kama ilivyo sasa.

(b) Wataalam wa masuala mbalimbali kama vile afya, ubora wa mazao, mifugo, samaki na bidhaa nyingine mbalimbali wawe wanakaa kwenye vituo husika vya mipakani na sio kukaa maeneo ya Makao Makuu ya Mikoa kama ilivyo sasa. Hili litapunguza usumbufu na kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingia ndani ya mipaka zina ubora unaotakiwa.

(c) Vibali vya kuuza mazao mbalimbali viwe vinatolewa kwa wakati na urasimu uondolewe ili kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wetu wanaweza kusafirisha mazao yao kwa wakati na hasa yale ya ndizi, matunda na mbogamboga ambazo huharibika haraka kama yakicheleweshwa.

(d) Tozo ya dola za Marekani 200 kwa kila gari ya mizigo ambayo inaingia nchini kutoka miongoni mwa nchi za Jumuiya iondolewe kwani huku ni kwenda

kinyume na mkataba wa Afrika Mashariki kuhusu Soko la Pamoja na hali hii imekuwa ikilalamikiwa mara kwa mara kwenye vikao na kuifanya nchi yetu ionekane kama inakubali ila haitekelezi kama inavyopasa kuwa.

(e) Serikali iandae mazingira mazuri kwa wafanyakazi wa vituo vya mipakani kama vile kuwapatia nyumba, vifaa vya kazi, mahitaji muhimu kama vile upatikanaji wa maji safi na salama, chanjo dhidi ya magonjwa kama *Ebola* na mengineyo ili kuwafanya waweze kuwa na ufanisi katika utendaji wao wa kazi.

(f) Serikali iandae miundombinu mizuri na mazingira bora ya kibiashara ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaweza kufanya biashara kwa urahisi zaidi kwenye maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majadiliano ya Ubia wa Kiuchumi *(EPA)* na Jumuiya ya Ulaya *(EU)*. Kuhusu mwelekeo, hali na athari za Mkataba wa Ubia wa Uchumi kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Tanzania kwa upande mmoja na Jumuiya ya Ulaya *(EU)* kwa upande mwingine, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuendelea kukumbuka kuwa sera yoyote ya uchumi ikiwa pamoja na Sera za Uchumi za Kimataifa, lazima zizingatie maendeleo endelevu, ukuaji ulio sawia (*equitable growth*) na unaoleta faida kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hatua ya Serikali kuacha kuridhia Mkataba wa Ubia wa Uchumi mpaka hivi sasa, Kambi Rasmi ya

Upinzani inaitaka Serikali kuboresha ushiriki wa wananchi wa Tanzania kwa ujumla katika Mchakato wa Majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Uchumi ikiwemo kuandaa mkakati wa uelimishaji umma na kulihusisha Bunge kuwasilisha taarifa rasmi Bungeni kuhusu hatua ya majadiliano iliyofikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali iongeze uwazi katika mchakato mzima wa majadiliano na kuwa na uwakilishi mpana wa makundi mbalimbali nchini na kuhakikisha maslahi ya Taifa yanaendelea kulindwa kwa kutetea ustawi wa wananchi wakiwemo wakulima wadogo wadogo, wavuvi na wajasiriamali wengine hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba ikiwa Serikali itakimbilia kuridhia mkataba huo wa ubia wa kiuchumi nchi na wananchi watapata athari kubwa ikiwemo uzalishaji wa ndani kuathiriwa na ushindani wa bidhaa za vyakula vya kilimo zinazoingizwa kutoka Jumuiya ya Ulaya na kupungua kwa mapato kutokana na kodi ndogo za mapato ambako kutapunguza kiasi cha fedha ambazo zingeweza kutumika kugharimia huduma nyingine za kijamii na miradi ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zina matatizo ya upungufu wa chakula, hivyo basi kujiunga kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Ubia huu wa Kiuchumi kutaongeza matatizo mengine ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuendelea na msimamo wa kutosaini makubaliano ya *EPA* mpaka masuala yenye utata katika Mkataba wa Mpito *(FEPA)* yatakapotatuliwa na pia marekebisho makubwa yatakapofanywa katika mkataba unaojadiliwa hivi sasa ikiwemo ushirikiano wa maendeleo kuwa sehemu muhimu ya Mkataba na fedha za nyongeza kutengwa kugharimia upungufu wa bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nafasi ya Tanzania katika soko la ajira la Afrika Mashariki. Moja ya changamoto zinazowakabili wananchi wetu na hususan vijana ni tatizo la ukosefu wa ajira. Bila shaka matarajio ya wananchi wetu ni kwamba, shirikisho la Afrika Mashariki litatanua wigo wa ajira kwa wananchi wa Tanzania katika Ukanda huu wa Afrika Mashariki na hivyo kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Profesa Regina Mwatha Karega (2009) juu ya Faida zinazowagusa wananchi wa kawaida wa Shirikisho la Afrika Mashariki ni kwamba Tanzania iko nyuma ya nchi wanachama katika kufurahia matunda ya shirikisho. Kwa mfano, katika watu waliohojiwa juu ya fursa za kibiashara katika shirikisho ni asilimia 21 tu ya Watanzania dhidi ya asilimia 31 ya Wakenya na asilimia 45 ya Waganda waliohojiwa waliosema kuna ongezeko la fursa za kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuhusu uwezo wa kununua bidhaa kwa urahisi kutoka nchi nyingine ya shirikisho, asilimia 53 ya Wakenya wakifuatiwa na

asilimia 26 ya Waganda walisema walikubaliana na hoja ya uwezo na urahisi wa kununua bidhaa kutoka nchi nyingine. Katika suala hili ni asilimia nne tu ya Watanzania waliohojiwa waliokubaliana na hoja hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika ajira rasmi za wataalam bado Tanzania iko nyuma katika kupata ajira kwenye nchi nyingine za Jumuiya. Takwimu zinaonesha kwamba Wakenya wengi wanaokuja Tanzania wanapata ajira kirahisi zaidi na katika ngazi za uongozi tofauti na Watanzania wanaokwenda Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili linazidi kuwa kubwa hasa kwa imani hasi inayojengeka kuwa Wakenya na Waganda ni wachapakazi na wanafahamu lugha ya Kiingereza kwa ufasaha kuliko Watanzania. Kwa sababu hiyo mashule mengi ya binafsi hapa Tanzania ambayo yanatumia mitaala ya Kiingereza wameajiri Wakenya kuanzia ngazi ya Utawala, walimu na hata wahudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Utalii na hasa katika mahoteli ya kitalii, wageni wamepewa kipaumbele zaidi kuliko Watanzania ambao wana sifa vile vile. Wakati sisi Watanzania tunawakumbatia wageni katika ajira muhimu hapa nchini, hali ni tofauti kwa wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wananyanyapaliwa katika ajira katika shirikisho kutokana na kasumba na imani potofu iliyojengeka kwamba Watanzania ni wavivu na ni watu wenye *blaa*

*blaa* nyingi (kwa maana ya maneno mengi na utendaji mdogo).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze itatatua vipi mgogoro huu wa ajira kwa Watanzania katika Ukanda huu wa Afrika Mashariki ambao umejificha katika sera za utandawazi na uchumi wa soko huria. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kukubaliana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki juu ya uwiano wa ajira katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumo wa elimu na changamoto zake katika ajira. Bado hatujakuwa na mfumo mmoja wa elimu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mfano, Kenya wanatumia mfumo wa miaka 8-4-4 wakati Tanzania na Uganda zinatumia mfumo wa miaka 7-4-2-3/4, huku Rwanda ikiwa na mfumo wa 6-3-3-3 na Burundi ikiwa na mfumo tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, utofauti huu wa mfumo wa elimu unasababisha kuwa na wahitimu wenye uwezo na ujuzi tofauti na hivyo kuwafanya wengine waonekane kuwa hawana uwezo wa kutosha. Jambo hili hatimaye litasababisha nchi moja au nchi chache ndani ya Jumuiya kuwa na uwezo wa kunufaika zaidi katika soko la ajira kuliko nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia Wizara hii kuwaelekeza Wabunge wa Afrika Mashariki wanaoiwakilisha Tanzania kutoa hoja katika Bunge la Afrika Mashariki ya kuanzisha mfumo mmoja wa elimu katika nchi wanachama ili wanafunzi katika Jumuiya wawe na

vigezo sawa vya kielimu na hivyo kuwa na fursa sawa katika soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali vile vile kupitia Wizara hii kushawishi nchi wanachama ili kuwe na mfumo wa pamoja wa udahili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Mwanafunzi mwenye sifa ya kujiunga na chuo kikuu awe na uhuru wa kuchagua chuo chochote ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na adhaminiwe na Bodi ya Mikopo kutoka nchini mwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uharamia na hatma ya usalama katika Afrika ya Mashariki. Hivi karibuni kumekuwa na matukio ya uharamia katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki. Mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yamepata madhara mbalimbali kutokana na mashambulizi yanayofanywa na maharamia wa Kisomali kutokana na meli mbalimbali za mizigo kushambuliwa na kutekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ni kwa nini hakuna nguvu ya pamoja katika kukabiliana na tishio la maharamia hawa wakati tayari nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walishaweka saini makubaliano katika mambo ya Ulinzi na Usalama?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahofu kuwa ushirikiano huu unaweza kuwa ni wa kufaana wakati wa furaha na kuachana wakati wa dhiki na misukosuko kwa kuwa kuna dalili za wazi kabisa kuwa ushirikiano wetu katika ulinzi na usalama ni

dhaifu. Hii ni kwa sababu hadi sasa Kenya inapambana na Kikundi cha *Al-Shaabab* peke yake, Uganda inapambana na waasi peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la Pamoja na changamoto zake. Kuna malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara wengi wa Tanzania wanaofanya biashara zao kati ya Mwanza na Kenya, Dar es Salaam na Kenya kwamba wanapata usumbufu mkubwa sana kutoka kwa Polisi nchini Kenya wanapokuwa huko kwa shughuli zao za kibiashara. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzungumza na Serikali ya Kenya ili kuwaondolea wafanyabiashara hawa usumbufu usio wa lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haiungi mkono utaratibu uliopo sasa wa kuwa na viwango tofauti vya Kodi ya Ongezeko la Thamani katika nchi wanachama. Hiii ni kwa sababu wawekezaji watawekeza zaidi katika nchi ambayo viwango vya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ni ndogo na hivyo nchi ambazo viwango vyake ni vikubwa hazitapata wawekezaji na hivyo haziwezi kunufaika katika Soko la Pamoja. Kwa mfano kwa sasa viwango vya *VAT* Tanzania ni 18% wakati Kenya ni 16%. Kwa vyovyote vile Kenya itawavutia wawekezaji zaidi kuliko Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Umoja wa Sarafu na utekelezaji wake. Wakati Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Kikwete, akihutubia kwenye uzinduzi wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 18 Novemba, 2010, alisema:-

*“Kama mjuavyo tarehe 1 Julai, 2010 Soko la Pamoja limeanza baada ya kukamilika kwa mafanikio ujenzi wa Umoja wa Forodha. Hivi sasa mchakato wa kuanzisha Umoja wa Sarafu unaendelea kwa kasi na unategemewa kukamilika mwaka 2012. Lazima tuhakikishe kuwa tunashiriki kwa ukamilifu katika vikao vyote vinavyozungumzia masuala ya utangamano wa Afrika Mashariki ili kutetea na kulinda maslahi yetu”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua mchakato huu wa kuwa na Sarafu Moja ya Afrika Mashariki umefikia wapi ukizingatia kwamba mwaka 2012 ndio huu unamalizika?

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunataka kujua kama umefanyika utafiti wa kina juu ya ni kwa nini nchi za Jumuiya ya Ulaya pamoja na kuwa na Sarafu Moja bado kuna nchi wanachama ambao bado wanaendelea kutumia sarafu yao? Kuna utaratibu gani unaofanyika endapo nchi mwanachama wa Afrika Mashariki itataka kuendelea kutumia sarafu yake tofauti na ile ya shirikisho?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushindani katika sekta ya utalii. Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwamba Kenya inautangaza Mlima Kilimanjaro kuwa ni wa Kenya. Majibu ya Serikali katika hili ni kwamba mlima uko Tanzania. Ila ukweli ni kwamba watalii wengi wanaokuja kupanda Mlima Kilimanjaro wanapitia Kenya na fedha nyingi za kigeni kwa maana ya kupata huduma mbalimbali za mahoteli na manunuzi ya vitu mbalimbali vya kitalii zinabaki Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Kenya inajenga uwanja wa ndege wa kimataifa karibu kabisa na Mlima Kilimanjaro eneo la Taveta ambalo liko mpakani mwa Tanzania na Kenya. Ujenzi wa Uwanja huu una lengo la kuwavutia watalii zaidi kwa kuwa Mlima Kilimajaro utakuwa unaonekana vizuri kabisa kutoka kwenye uwanja wa ndege ambao upo upande wa Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaihoji Serikali kuwa ilikuwa wapi muda wote tangu Kenya inaanza mchakato wa kujenga uwanja wa ndege bila kufanya mazungumzo ili kuepuka kuhujumiwa kiuchumi? Kama kweli Kenya ni rafiki wa kweli na Kenya na Tanzania wanakaa pamoja katika Shirikisho la Afrika Mashariki, ni kwa nini inajenga miradi ambayo matokeo yake yatahujumu uchumi wa Tanzania na Serikali yetu inaendelea kukaa kimya?

Mheshimiwa Naibu Spika, utambulisho wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kama ilivyo kwa mataifa na tawala nyingine, kati ya vitu vinavyoitambulisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ni pamoja na Bendera ya Jumuiya na Wimbo wa Jumuiya. Hali ilivyo kwa sasa ni kwamba Bendera hiyo ya Jumuiya sanasana ipo Makao Makuu ya Jumuiya na Wizara ya Afrika Mashariki. Kuhusu wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki nao pia unaimbwa wakati wa vikao vya aidha Bunge au Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitu hivi (Bendera na Wimbo wa Jumuiya) ambavyo ni alama ya Umoja na

Mshikamano havijasambazwa vya kutosha miongoni mwa wananchi wa nchi wanachama, jambo ambalo linaashiria kwamba Jumuiya hii ya Afrika Mashariki ni kwa ajili ya viongozi na sio wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba, popote pale kwenye Bendera ya Taifa letu, pawepo pia na Bendera ya Afrika Mashariki. Aidha, popote pale Wimbo wa Taifa letu utakapoimbwa basi na Wimbo wa Afrika Mashariki uimbwe pia. Hii itasaidia sana kuwajengea wananchi umuhimu wa umoja wa Afrika Mashariki na kwa kufanya hivyo Umoja huo utaendelea kuwa na nguvu kwa kuwa wananchi wote wa nchi wanachama wanauelewa. Utaratibu huu ufanyike kwa nchi zote wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ahadi za Serikali kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwaka jana, Serikali ilitoa ahadi mbalimbali ya kutekeleza ili kuboresha zaidi Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miongoni mwa ahadi hizo ilikuwa ni pamoja na upanuzi wa kiwanja cha Ndege cha Zanzibar na Kiwanja cha Ndege cha Karume kule Pemba. Aidha, Serikali iliahidi kupitia Wizara hii ya Afrika Mashariki kuboresha usafiri wa majini kati ya Dar es Salaam – Zanzibar na Mombasa kwa kukarabati na kutengeneza upya bandari ya Maruhubi na kununua kivuko cha kisasa ambapo mfanyabiashara anaweza kuweka bidhaa zake kwenye gari kubwa anaingia kwenye *ferry* anakwenda hadi Mombasa, kivuko kinafunguka, anaendesha gari lake anakwenda kuuza bidhaa zake.

Kambi ya Upinzani inataka kujua ni hatua gani imefikiwa katika utekelezaji wa ahadi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi nyingine ya Serikali ilikuwa ni kutoa elimu kwa wananchi ili wauelewe barabara Umoja huu wa Afrika Mashariki pamoja na fursa mbalimbali zinazoweza kupatikana. Katika kuhakikisha hili linafanyika, Serikali iliahidi itanunua magari mawili maalumu ambayo yatawezesha kuitangaza Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni kama utaratibu wa kuitangaza Afrika Mashariki kwa kutumia magari mawili unaweza kufanikiwa kwa kiwango cha kuridhisha. Aidha, nyenzo zilizokuwa zikitumika kama vipeperushi, redio na televisheni havingeweza kuitangaza Afrika Mashariki kwa kiwango cha juu kwa kuwa bado kuna asilimia kubwa ya wananchi waishio vijijini ambao hawana televisheni na pia hawapati vipeperushi hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tafiti zinaonesha kuwa Tanzania iko nyuma katika uelewa wa mchakato wa utangamano wa Afrika Mashariki, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba, sambamba na kutilia mkazo usambazaji wa Bendera ya Afrika Mashariki na kusisitiza kuimbwa kwa Wimbo wa Afrika Mashariki, Serikali ianzishe mtaala elimu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mfumo wetu wa elimu katika somo la Uraia katika ngazi ya shule za Msingi, Sekondari na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa viwango vya ubora wa bidhaa. Msukumo wa kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki ni kuwa na Soko la Pamoja. Ili kulinda Soko hili la Pamoja, ni lazima ubora wa bidhaa udhibitiwe ili kuepuka uchakachuaji wa bidhaa na hivyo kuharibu heshima ya soko.

Mheshima Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzishawishi nchi wanachama wa Jumuiya ya Afirka Mashariki kuanzisha viwango sawa vya ubora wa bidhaa ili kudhibiti bidhaa kutoka nje ya Afrika Mashariki zilizo chini ya viwango na hivyo kuepusha Afrika Mashariki kuwa dampo la bidhaa zisizokidhi viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa miundombinu ya kiuchumi. Katika hotuba ya bajeti ya 2010/2011, aliyekuwa Waziri wa Wizara hii alisema kwamba nchi wanachama zilikuwa zikitekeleza Mpango Kabambe wa Kuendeleza Mtandao wa Barabara katika Jumuiya *(The East African Road Network Project)* ambao ulijumuisha kanda tano. Kanda ya kwanza ni barabara ya Mombasa – Malaba – Katuna- Kigali – Kinyaru Haut – Bujumbura Gatumba ikijumuisha Marangu -Tarakea, Chalinze - Segera na Segera – Himo. Kanda ya Pili ni Dar es Salaam – Isaka - Lusahunga – Mutukula - Masaka na Lusahunga – Nyakasanza – Rusumo – Kigali - Gisenyi. Kanda ya tatu ni barabara ya Biharamulo – Mwanza – Musoma – Sirari – Lodwar – Lokichogio ambayo pia ni sehemu ya mtandao wa barabara katika ukanda wa Ziwa Viktoria (*Lake Victoria Road Circuit).* Kanda ya nne ni barabara ya Tunduma – Sumbawanga – Kigoma – Manyovu

(Mugina) – Rumonge – Bujumbura- Ruhwa (Bugarama), Kigori – Gisenyi, Sumbawanga – Tunduma. Kanda ya tano ni Tunduma – Iringa - Dodoma – Arusha – Namanga – Moyale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ni mkubwa na muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi ya kanda husika. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tathmini ya maendeleo ya mradi huo wa barabara hasa kwa zile barabara zilizopo katika nchi yetu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua pia ni mafanikio kiasi gani yamefikiwa katika kutekeleza Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Reli Afrika Mashariki *(The East African Railway Development Master Plan).*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2012/2013. Wizara hii ya Afrika Mashariki inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 16,643,667,000, ikiwa shilingi 15,265,375,000 ni matumizi ya kawaida *(OC)* na shilingi 1,378,292,000 ikiwa ni mishahara *(PE).*

Mheshimiwa Naibu Spika, licha fedha hii kuonekana ni ndogo kulinganisha na majukumu makubwa ya Wizara lakini pia mchanganuo wake haupo wazi kwa kiasi cha kuridhisha. Hii ni kwa sababu bajeti hii haioneshi fedha za miradi ya maendeleo wala haioneshi ni fedha ngapi za ndani au ni ngapi za nje kama bajeti nyingine zinavyoonesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge hili kwa nini Wizara hii haina fedha za maendeleo? Kama Wizara hii

haina fedha za maendeleo, je, haina mpango wowote wa kutekeleza maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Afrika Mashariki 2012/2013. Bajeti ya Jumuiya kwa mwaka huu wa fedha kama ilivyopitishwa tarehe 24/5/2012, zimetengwa jumla ya USD 125,007,796 kama fedha za maendeleo kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatayo kwa mwaka wa fedha 2012/2013:-

(a) Dola 8,501,450 (6.8%) kwa ajili ya kushughulikia masuala yote yanayohusiana na Umoja wa Forodha *(Consolidating the Customs Union)*.

(b) Dola 23,503,612 (18.8%) kwa ajili ya Itifaki ya Soko la Pamoja na hasa katika kuwezesha Soko la Pamoja la ajira, kuwianisha masoko ya fedha ili kuhakikisha kuwa mitaji inaweza kusambaa.

(c) Dola 9,592,730 (7.7%) kwa ajili ya kumalizia mazungumzo ya Itifaki ya Umoja wa Sarafu Moja.

(d) Dola 12,531,382 (10%) kwa ajili ya miradi ya pamoja ya miundombinu ambayo ni:-

· Kuanza ujenzi wa barabara ya Arusha-Holili/Taveta-Voi na kukamilisha pembuzi yakinifu wa barabara ya Malindi-Lunga Lunga-Holili-Bagamoyo.

· Ujenzi wa Kituo Kimoja cha Mpakani *(One Stop Border Posts)* Namanga, Rusumo, Holili-Taveta, Lunga Lunga-Horohoro, Kabanga-Kombero na Kagitumba.

· Kumalizia upembuzi yakinifu wa reli ya Dar-Isaka-Kigali/ Keza-Msongati.

· Kuunganisha reli za Kenya-Uganda, Uganda-Tanzania.

· Kukamilisha mkakati wa pamoja wa nishati na kuunganisha vituo vitatu ambavyo tayari vimeainishwa.

· Kutafuta rasilimali *(Resource mobilization)* kwa ajili ya miradi ya ukarabati wa Bandari za Bujumbura, Mombasa na Dar es Salaam.

· Kufanya biashara ya usafiri wa anga kuwa wa soko huria *(Liberalization of air transport*).

(e) Dola 2,874,848 (2.3%) kwa ajili ya kuandaa mkakati wa pamoja wa usalama wa chakula na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi *(Food Security and Climate Change Master Plan).*

(f) Dola 38,144,605 (30.5%) kwa ajili ya *Lake Victoria Basin Commission* na kuhifadhi mfumo wa ekolojia za Mlima Elgon.

(g) Dola 29,859,169 (23.9%) ni kwa ajili gharama nyingine mbalimbali kwa ajili ya rasilimali watu *(Personnel emoluments*).

(h) Dola 10,105,618 kwa ajili ya baraza la Vyuo Vikuu la Afrika Mashariki *(Inter-University Council for the East Africa*).

(i) Dola 3,203,041 kwa ajili ya *Lake Victoria Fisheries Organization*.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Jumuiya zilikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Fedha kwa ajili ya Sekretarieti USD 68,339,098.
(ii) Bunge la Afrika Mashariki USD 12,511,772.
(iii) Mahakama ya Afrika Mashariki USD 4,117,210.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya mapato:-

(i) Michango ya Nchi Wanachama wa Jumuiya kupitia Wizara husika USD 35,375,722.
(ii) Nchi wanachama kupitia mashirika (*Agencies*): USD 4,825,709.
(iii) Michango ya wahisani na wafadhili USD 97,079,329.
(iv) Vyanzo vingine USD 1,035,695.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa umakini utaona kuwa Jumuiya hii inategemea wahisani kwa zaidi ya asilimia 80 kama chanzo cha mapato kwa ajili ya kuendesha shughuli za Jumuiya na wakati huohuo hata fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida bado tunategemea wahisani na wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani haikubaliani na utaratibu huu wa kutegemea wahisani hata kulipa mishahara watumishi wa Jumuiya na hivyo tunaitaka Serikali iwasilishe hoja kwenye vikao kuwa

Jumuiya iwe inategemea wanachama wake katika kujiendesha na sio kama hali ilivyo hivi sasa, kwani Jumuiya itakosa nguvu za kujadiliana mikataba na itifaki mbalimbali za kibiashara ambazo tutakuwa tunaingia na wahisani hao. Aidha, tungependa kujua kuna utaratibu gani kwa nchi wanachama katika kupendekeza miradi ya maendeleo na vipaumbele kwa nchi husika inayotekelezwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Raya kwa kusoma hotuba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tunakushukuru sana ingawaje ulipoanza pale kidogo hukutaka kujielekeza kwenye Afrika Mashariki, ulianza na Upinzani kwanza. Sasa wakanikumbusha Waheshimiwa Wabunge, nimewahi kusoma wakati fulani hivi, upinzani ulipoanza kwenye Bunge la Uingereza, nadhani kwenye miaka ya 1884 au *around* hapo, sasa yule aliyekuwa Kiongozi Mkuu wa Upinzani kwa mara ya kwanza akaulizwa, bwana mzee sasa wewe ndio Kiongozi wa Upinzani, hivi upinzani huu kazi yake nini? Akasema kazi yake rahisi sana, ziko kazi kama tatu, sijui kama nitazikumbuka, lakini moja kupinga kila kitu, ya pili kutopendekeza chochote na ya tatu, kuondoa Serikali iliyoko madarakani. Sasa naona bado mambo haya yanaendelea mpaka leo. *(Kicheko)*

Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Naomba tu kuwataarifu kwamba, walioomba kuchangia mpaka

sasa ni Wabunge sita tu ambao watachukua saa moja na kwa maana hiyo hotuba yetu inaweza kabisa ikakamilika leoleo kwa uendeshaji mahiri, kukawa hakuna sababu tena ya kesho kuweza kukutana. Kwa jinsi hiyo, kwa vile sasa nafunga orodha hii, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote jioni tuhudhurie ili tuweze kuitendea haki Wizara hii ya Afrika Mashariki, nina hakika kabisa tunaweza tukamaliza shughuli zake kwa leo.

Baada ya maelezo hayo, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 kamili leo jioni.

*(Saa 7.12 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, naomba nimwite mchangiaji wa kwanza Mheshimiwa Leticia Nyerere.

**MHE. LETICIA M. NYERERE**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia nikiwa mchangiaji wa kwanza, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni muhimu sana kwetu Watanzania. Nasema hivyo kwa nini? Tukitaka kuuendeleza usafiri wetu wa reli, ni lazima tukubaliane kushirikiana na wenzetu wa nchi za Afrika Mashariki. Tukitaka kuendeleza usafiri wa majini, ni lazima tukubali kwamba kuna haja ya kushirikiana na

wenzetu wa nchi za Afrika Mashariki. Tukitaka kuendeleza usafiri wa anga, hatuna budi kushirikiana na nchi zingine ikiwemo Burundi, Rwanda, Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia suala la fursa ya ajira kwa Wanaafrika Mashariki. Watu wengi wamekuwa wakilalamikia ushindani kwenye suala hili la ajira. Ninachopenda kusema, hatuwezi kukwepa ushindani kwenye eneo hili la ajira. Ili tuweze kushinda au ku-*penetrate* kwenye hili soko la ajira, Watanzania tutalazimika kupata elimu bora. Inabidi tuboreshe elimu zetu ili tuweze kuingia kwenye ushindani wa soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni lazima tukubali kwamba huwezi ukaingia kwenye ushindani wa soko la ajira kama huna juhudi ya kufanya kazi. Hata kama tutaendelea kulalamikia ushindani, endapo tutashindwa kuonyesha juhudi za kuchapa kazi, hakika tutakuwa tunajisumbua na hakika tutabaki nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira si suala la kuwa na elimu bora tu wala si suala la kuwa na juhudi ya kufanya kazi tu, tunatakiwa tuwe waadilifu. Tutaendelea kulalamika lakini endapo tutashindwa kutimiza hayo niliyoyasema, endapo sisi Watanzania tutayapuuza, hakika tutabaki tumeshikilia mkia tukilalamika sana. Ni bora niweke wazi kwamba uvivu si jambo jema, uvivu huzaa umaskini na umaskini huzaa wivu na vilevile wivu huzaa chuki. Hatutaki huyu mdudu chuki aendelee kulitafuna Taifa letu. Inabidi tutambue kwamba kama tunataka kujiendeleza kwenye utalii, ni

lazima tuwapende watalii. Kama tunataka kuelimika ni lazima tuwapende wasomi na kama tunataka kutajirika ni lazima tuwapende matajiri. Tukitaka kupata *international exposure,* ni lazima tuwapende wageni. Vilevile Taifa letu limekuwa likipigania uwekezaji lakini hatuwezi kuendelea kwenye uwekezaji kama tunawachukia wawekezaji. Ni lazima sasa Watanzania tujitambue, ni lazima sasa Watanzania tukubali *competition,* hakuna jambo ambalo halina *competition,* ni lazima tukubali kushindana na wenzetu wa Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi vinginevyo tutaendelea kulalamika na kubaki nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie jambo muhimu sana ambalo tukilizingatia Watanzania tutasonga mbele na tutanufaika na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ombi langu kwa Watanzania wote, tuache kulalamika, tuache wivu, tufanye kazi kwa bidii kama ilivyo kwa wenzetu Kenya. Hivi tunategemea nini, unafikiri *competition* ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki itatusamehe tu kwa sababu sisi tunalalamika? Hakuna! *We have to work hard*, hakuna jinsi tuingie kwenye ushindani. Kipimo cha uwezo wa mtu yeyote au kundi lolote au nchi yoyote ni ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ombi langu kwenu Watanzania wenzangu badala ya kuingia kwenye ushindani wa kushushana chini maana tumekuwa na *tendency* ya ajabu Watanzania, ukiona mwenzio anajua kitu na ana uwezo fulani badala ya kupigania ushindani umfikie au umpite wewe unaanza kutafuta *strategy* za kumshusha chini ili akukute kule uliko. Hii ni

mbaya, inabidi tabia zetu sasa tuzibadilishe, tuko kwenye utandawazi, dunia haiwezi kutusubiri sisi kwani sisi ni nani? Sisi ni binadamu kama binadamu wenzetu duniani kote. Sisi tunapaswa kuingia kwenye ushindani kama nchi zingine zote, mbona wenzetu Kenya, Burundi, Uganda wanaweza?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote tu mashahidi, kuna baadhi ya Watanzania wanaleta mpaka ma-*house girl* kutoka Kenya wakati tuna Watanzania. Sasa tujisikilize, tuna tatizo gani, kwa nini Watanzania wenzetu wanaajiri mpaka ma-*house girl* kutoka Kenya? Ni wito wangu kwa Watanzania tukitaka kufanikiwa kwenye ushirikiano wetu wa Afrika Mashariki tufanye kazi kwa bidii, tujiendeleze, tuachane na chuki, vinginevyo tutashindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Leticia Nyerere kwa hotuba yako nzuri sana. Unajua sisi Waswahili sijui kama tunasikilizana vizuri, Mheshimiwa Leticia amenigusa sana amesema tuache kulalamika, tuache wivu, tupende wageni, tupende matajiri, tuache ushindani wa kuporomoshana, pointi muhimu kweli.

Mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa heshima hii na ni mara yangu kwa kwanza kuzungumza tangu bajeti ianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Uzini. Pia kuwapa pole kwa maafa yaliyotokea ya ajali ya meli ambayo pia watu wengi katika Jimbo langu wamefariki. Natoa rambirambi nyingi sana kwao, Mungu awajalie, aweke roho zao peponi, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia jambo la lugha ya Kiswahili kwa sababu mwaka jana nilizungumza hapa kwamba Kiswahili kinafaa kiwe bidhaa ambayo Tanzania wanauza nje ya mipaka yao ili kupata fedha. Sina hakika kama Serikali imesikia. Napenda niwakumbushe kwamba Kiswahili kinaweza kuwa bidhaa kwanza kwa watu wetu kutunga vitabu vikasomwa nje, kuuza utaalamu wetu kwa kuwapeleka Wakalimani na Wafasiri nje, kuwapeleka Walimu nje na pia kuwapeleka Watangazaji wa redio na televisheni. Naamini kabisa hii ni fursa kubwa sana na hasa kwa sababu pia katika ushirikiano huu wa Afrika Mashariki ziko nchi ambazo zinahitaji sana wataalam wa Kiswahili kama Uganda, Rwanda, Burundi, Congo, Sudan na kadhalika. Kwa hivyo, tuache kudharau mali yetu, kilicho chetu. Tunaamini kwamba kusema Kiingereza sana ndio una akili nyingi sana, sidhani kama ni kweli. Lugha na akili ni kitu tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kwamba Mheshimiwa Waziri alizungumzia Kituo cha Utamaduni cha Lugha pale Zanzibar. Ni kweli kinafaa kiwepo lakini

mpaka leo sijui lini kazi itaanza. Tunaomba ianze haraka, hii ni fursa kubwa pia. Kamisheni hii ikiwepo Zanzibar ni fursa kubwa sana kwa Watanzania ambayo itajenga heshima ya nchi yetu na watu wetu. Naomba kazi ianze mara moja, Kamisheni hiyo ianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka nizungumzie Bunge la Afrika ya Mashariki na lugha ya Kiswahili. Sielewi kwa nini hawazungumzi Kiswahili kwenye Bunge la Afrika Mashariki, sijui kwa nini? Kama *OAU* wanazungumza Kiswahili, naomba sasa na ninyi pia muanze kuzungumza Kiswahili na Kiingereza kwa sababu ndiyo lugha nyingine lakini lazima sisi wenyewe Watanzania tuwe chachu ya kuanzisha jambo hili. Kwa hiyo, namwomba Waziri aanze kuweka agenda maalum katika vikao vyao ili tuanze kutumia lugha ya Kiswahili katika Bunge la Afrika Mashariki. Sisi lugha yetu ni maarufu sana duniani lakini hatuithamini, hatuijui. Lugha pekee katika Afrika yenye kuzungumzwa na watu wengi zaidi ni lugha ya Kiswahili katika lugha za Kiafrika hakuna nyingine. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kuwashawishi Mawaziri wenzake ili Kiswahili kiwe sehemu ya lugha ya kuzungumzwa katika Bunge la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, nizungumzie juu ya *Pan-Africanism*. Mtu mmoja ameniambia tafsiri yake ni Umajumui wa Afrika sijui kama ni kweli au si kweli lakini *Pan-Africanism* tafsiri yake ni vuguvugu la Uafrika katika Mshikamano wa Kudai Uhuru, Haki na Kujenga Umoja Thabiti. Jambo hili limeanza toka karne ya 18 kule Marekani na Caribbean si jambo jipya kabisa na baadaye likaja Afrika. Kama

mnakumbuka kulikuwa na mikutano mingi Afrika na watu ambao wamekuwa mstari wa mbele kupiga debe juu ya dhana hii ya *Pan-Africanism* ni pamoja na marehemu Gamal Bin Nasser, Sekou Toure, Modibo Keita, Nkrumah, Nyerere na Karume. Karume kwa sababu yeye ndio ametekeleza hasa kwa vitendo lile jambo ambalo lilikuwa likizungumzwa kwa muda mrefu kuwa na umoja, haki na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nasema kwamba kuna haja kuelezea kwamba vuguvugu hili ndilo lililozaa kitu kinaitwa *PAFMECA (Pan African Freedom Movement of East and Central Africa)* mwaka 1958 na kulikuwa na mikutano mingi sana inafanyika ya *PAFMECA* kwa vyama mbalimbali vya Afrika ili kutaka kuwapa nafasi ya kudai uhuru lakini mwisho wake kuleta Umoja wa Afrika. Kwa hiyo, *PAFMECA* imekuwa inafanya mkutano Zanzibar, ukafanyika Kampala, Uganda, nadhani suala hili la *PAFMECA* na Wizara ya Mheshimiwa Waziri ni matokeo ya dhana hizo za *Pan-Africanism,* ni matokeo ya *PAFMECA* na *PAFMESICA*, bila hivyo tusingekuwepo hapa. Kwa hiyo, nafikiri kuna haja ya kuthamini jambo hili na hasa mchango mkubwa wa wazee wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nizungumzie hata vyama vyetu vya Tanzania kwa maana ya *ASP* na TANU, vilikuwa wanachama wa *PAFMECA* na *PAFMESICA* na wao pia wamekuwa na ushindani mkubwa sana kati ya *ASP* na TANU. Ndio maana mkutano mmoja wa *PAFMECA* ulifanyika pale Zanzibar lakini ushirikiano wao pia ulikuwa wa kusaidiana. Nazungumza juu ya *PAFMECA*, *PAFMESICA*

nazungumza kuwepo kwa Umoja wa Taifa letu hili. Kwa hivyo kulikuwa na ushindani mkubwa sana kati ya *ASP* na TANU na nakumbuka kwamba TANU ilitoa nafasi kuwapa *ASP* magari, baiskeli za kampeni pamoja na kiongozi mmoja marehemu Bibi Titi kwenda Zanzibar na kuhutubia mkutano wa siasa kule baadaye akaambiwa wewe sio raia wa Sultani ondoka hapa, akafukuzwa. Kwa sababu gani, kila mtu kule alikuwa raia wa Sultani. Kwa hivyo kwamba hii *PAFMECA* ilijitoa kwa vitendo na vyama vyetu vya *ASP* na TANU.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Zanzibar kwa mfano kulikuwa na Chama cha *ASP* (*Afro Shiraz Party)*, Chama cha Waafrika wa Zanzibar na Waafrika wa Asili ya Bara, walianza kwa vitendo kuonyesha mfano huo. Lakini pia kulikuwa na kuundwa chama hiki, ni makundi mawili hayo. Lakini pia mwaka 1954 walishiriki katika kuleta Mapinduzi, kuwapa Waafrika haki sawa kwa wote maneno ya *CUF*. Kwa hivyo, nasema kwamba lazima kwanza tuwe na Taifa halafu tuwe na kundi la watu wa nchi fulani. Kwa mfano, huwezi kuwa na Afrika Mashariki kama huna Zanzibar, Kenya na Uganda. Kwa hivyo hawa viongozi wetu wa *ASP* na TANU walifanya kazi hiyo kulenga huko kwamba la kwanza lazima waikomboe nchi yao halafu ndio wajiunge na umoja mkubwa zaidi. Kwa hivyo, nasema kwamba Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 yalikuwa ni sehemu ya mchakato wa kufanikisha dhana nzima ya *Pan-Africanism* na *PAFMECA* na *PAFMESICA* kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba hata washiriki wa Mapinduzi Zanzibar walikuwa watu kutoka

Bara na Visiwani. Kwa hivyo ushirikiano huu wa nchi mbili hizi haukuanza jana wala juzi, zamani sana. Nitataja baadhi ya majina hapa watu 14 ambao waliandaa Mapinduzi haya kule Zanzibar kutoka Bara na Visiwani kwa mfano Mohamed Mfaranyaji, kutoka Songea huyo, Bwana Saidi Natepe, Khamis Daruwesh, Seif Bakari, Mohamed Kajole na kadhalika. Hili ni kundi la watu ambao asili yao sio Zanzibar lakini wametoa damu yao kwa ajili ya Taifa la Zanzibar, huwezi sasa hivi kuwatukana watu wa Bara kwa sababu wao walikuwa sehemu ya ukombozi wa Zanzibar, walishirikiana na ndugu zao wa Zanzibar akina Yussuph Hemed, Hamid Ameir, Said Bavuai na Ramadhani Fhaki. Ninachozungumza hapa ni kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa!

**MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB:** Tayari?

**NAIBU SPIKA:** Mzee tayari!

**MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB:** Duh! Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tungefaidika kwelikweli na historia hii lakini muda haupo upande wetu. Mheshimiwa Hamad Rashid atafuatiwa na Mheshimiwa Sanya.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na niwapongeze Waziri na timu yake yote kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakwenda kwenye kiambatanisho cha kwanza ambacho Mheshimiwa Waziri alitueleza juu ya mwenendo wa mauzo ya nchi wanachama katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki ikionyesha kwamba wenzetu Kenya wameweza kuuza dola 1544 milioni sisi tupo 409 na kadhalika. Sasa ukichukua ile ya Kenya tu peke yao ukijumlisha na nchi tatu zilizotajwa hapa lakini sijui kwa nini Rwanda haipo, bado unakuta kuna tofauti ya kama 603, kwa hiyo, hawa wako juu zaidi. Sasa hii inaashiria nini? Inaashiria kwamba katika Jumuiya hii pamoja na mazingira mazuri tuliyonayo Tanzania na hali yetu tuliyonayo bado kama Watanzania hatujalitumia vizuri soko la Afrika Mashariki. Sasa hii ni kasoro na inahitaji iwe mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kama tulifuatilia, tuliona kwamba wafanyabiashara wengi wa Tanzania wanalalamika juu ya vikwazo vingi vya kufanya biashara Tanzania. Sekta ya Utalii ina kodi na vikwazo vingi kiasi kwamba hatuwezi kuvipanua lakini leo wenzetu kwa sababu sekta ya utalii ya Tanzania imedumaa wanathubutu kujenga *airport* karibu na sisi ili waweze kutumia fursa ambazo sisi hatuzitumii. Suala la kwanza ambalo mimi naiomba sana Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla, yale maeneo ambayo tunaweza kuharakisha kupata maamuzi tukaondoka hapa, tuyafanye haraka, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni suala la Sarafu ya Pamoja, nafurahi kwamba tumekuwa waangalifu katika jambo hili na ni vema tukajifunza kwa wenzetu wa *EU,* nina sababu mbili kubwa. *EU* leo nchi wanachama wanazitegemea nchi mbili yaani Ufaransa na Ujerumani ndiyo wenye *strong economy*. Kwa hiyo, mnapokuwa na *currency* ya aina moja halafu wenzenu wana nguvu za kiuchumi *currency* ile kwa umoja haina maana yoyote kwenu ninyi ni kwamba kila wakati mnangoja hawa wawa-*bailout* tu ninyi, mkipatwa na tatizo mnakuwa watumwa tu. Mimi naomba hili tuwe *very careful,* tujenge *our strong economy*, tujenge *our strong financial institutions* kabla hatujafikia maamuzi ya kusema tuna *currency* moja katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu napenda vilevile sasa tufike mahali sisi Tanzania tuseme bidhaa tunazouza nje ni zipi au tunazouza katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni zipi? Tumezi-*identify* kama ni *cement* na kadhalika lakini katika hizi *item* ni ipi ambayo ndiyo inayotupa *value* zaidi? Katika kitabu hiki, karafuu sikuiona na mimi najua karafuu zinauzwa sana Kenya kwa magendo, kwa maana ya tafsiri ya Serikali lakini katika soko huria na hili nalisema wazi kila siku kwamba tumeamua kufanya soko huria kwa kila kitu lakini bidhaa za mkulima kila siku zinawekewa vizingiti lakini anayeuza *cement* au bati yake hawekewi kizingiti lakini bidhaa ya mkulima iwe ya pamba, karafuu, korosho na kadhalika kila siku ina vizingiti. Tuondoe hivi vikwazo na waacheni watu wauze bidhaa zao, tumekubali soko huria basi tuwe soko huria kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tunasema kwamba kutakuwa na njaa na kadhalika waacheni watu wauze wawe na hela, matokeo yake tunaleta mchele, tunawapa na mchele bure kwa sababu yale mazao yameharibika, hawakuuza na fedha ya kununua mazao mengine hawana, kwa hiyo, ninyi mnakula hasara tu. Waacheni wauze, wawe na fedha, mkiagiza mchele watanunua, *they have the money* lakini utaratibu wa kuwazuia wakulima wasiuze bidhaa zao *it is a wrong concept.* Mimi nasema kabisa, tukatae au tukubali mkulima atakuwa *disappointed* akiona mazao yake hakuyauza mwaka huu na mwakani hatalima. Hiyo ikataeni lakini ndiyo *theory* yenyewe, sisi tuna *experience* ya karafuu. Tulipoingiza nguvu sana za kuagiza karafuu isiondoke, watu waliacha mikarafuu inadondoka na hakuna mtu aliyeshughulika, lakini walipopata mwanya wa kupeleka Kenya, watu walishughulikia mikarafuu yao, Serikal mara hii ilipopandisha bei watu walichuma karafuu. Kwa hiyo, mimi nafikiri hii *monopoly* ya biashara ya kilimo kui-*control too much it is not fair* kwa wakulima, tunawaendeleza wawe maskini kila siku na hatuwezi kuwaondoa walipo. Hilo naomba nalo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne, nimekuta bidhaa kama cement na kadhalika, nimefurahi sana lakini hebu tufanye hesabu ni tani ngapi za *cement* zimekwenda Kenya? Ni tani ngapi za *cement* zimekwenda Uganda? Ili tujue mahitaji ya Afrika Mashariki ni kiasi gani halafu tutazame katika *production* ya Afrika Mashariki, je, sisi wenyewe tumejitosheleza? Nalisema hilo kwa sababu ukiangalia

*exports* za Afrika Mashariki kwa ujumla ni kubwa, urari wa biashara baina yetu sisi Afrika Mashariki na nje bado ni mkubwa kwa sababu hatuja-*take stock inside* kuangalia sisi ndani ni kiasi gani tunajitosheleza wenyewe na kwa kiasi gani tunaweza kupunguza *export* au *import* zetu kutoka nje. Mimi nafikiri hiyo haijafanyika na ningeomba ifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tano ni *harmonisation*. Tumekuta Mabunge ya wenzetu Kenya, Uganda wamekwenda Mahakamani na sisi Tanzania tulikwenda Mahakamani kwa sababu bado hatuja–*harmonise* taratibu zetu za kiuchaguzi. Tunatakiwa kama Afrika Mashariki tuna– *unified system* za uchaguzi wa Bunge la Afrika Mashariki. Sasa hivi tunategemea Kanuni zetu za Bunge la Tanzania na sheria zetu na Kenya hivyohivyo lakini kama kweli tunayo Mahakama ya Afrika Mashariki basi mambo yote ya uchaguzi ya Bunge la Afrika Mashariki yaende kule. Sasa ili yaende kwenye Bunge la Afrika Mashariki lazima tu-*harmonise* hizo sheria ziwe za aina moja na taratibu zetu ziwe za aina moja. Mimi nafikiri hili lifanyiwe kazi ndiyo tutaanza ile *process* ya kuonekana kwamba kweli tunakusudia yale ya Afrika Mashariki kweli ni ya Afrika Mashariki na yale ya nchi yabaki kuwa ya nchi. Mimi nafikiri hiyo itakuwa ni hatua nyingine ya kuendelea mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la sita ni kwamba sasa hivi tunazungumzia sana na atakapokuja Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje atalizungumzia ni kuhusu *dual citizenship,* sina hakika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki tumeanza kulizungumza. Hivi sasa tuna makampuni karibuni mia mbili na zaidi ya Kenya na

wakati mwingine hata hizi *product* unazoziona zinatoka Tanzania zinakwenda kule ni makampuni ya Kenya yanayozalisha Tanzania wakati mwingine wanapeleka *unfinished product* wanazi-*process* Kenya na kuzipeleka nje, hilo linatokea na tulifahamu. Wame-*abandon* baadhi ya viwanda walivyonunua hapa wanazalisha hapa *raw* wanapeleka kule wana-*process* wanasafirisha nje. Hili linatakiwa lifanyiwe kazi na tulifanyie kazi ili tujue kwamba kweli hizi bidhaa zinazotoka kweli zimezalishwa na Watanzania na kama zimezalishwa Tanzania *fine*, je, zinakwenda kama *finished product au semi finished products?* Nafikiri hiyo nayo itatusaidia vilevile lakini si tuache tu holela tuone kama bidhaa zimekwenda lakini kumbe kuna mambo mengi ndani yake, kuna siri ndani yake hatujaielewa. Leo magogo ya umeme tunanunua kutoka Kenya, yanatoka wapi? Iringa! Pengine hatuna habari na mambo mengine mengi ya aina hii. Mimi nafikiri hilo lingefanyiwa kazi na nina hakika tutafika hatua nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho, kabla ya kuvunjika kwa *East African Community* ya zamani tulikuwa na *membership* ya Zanzibar, Bara, Kenya na Uganda lakini leo tumeshaongezeka tupo na Rwanda na Burundi. Wenzetu kila wakati wanaangalia ni jinsi gani watapata *benefit* upande mwingine. Mimi nilikuwa najiuliza, wakati ule tulikuwa na uwakilishi sawasawa pande zote, hivi Tanzania tukiwa na uwakilishi mbili, hatuna *advantage* ya kupata Wabunge yaani tisatisa mara mbili? Si *advantage* kweli au ni *disadvantage*? Kwa hiyo, hata *rotation* ya Mkurugenzi au Katibu tutapata mara mbili. Sasa nilikuwa naiangalia hiyo kama hatuwezi kuiangalia na

*benefit* ambazo tunaweza kuzitumia kwa umoja wetu huu tulionao na sisi tukazifanyia kazi tukafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa ni Mheshimiwa Sanya!

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na mimi kupata nafasi jioni hii ili kuelezea machache kuhusu Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na kuendelea na ibada ya swaumu na *inshallah* Mwenyezi Mungu atutakabalie kheri zote tunazozifanya katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niwape pole wote waliofiwa katika ajali ya meli wawe na subira na wale waliokufa Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nigusie kidogo kuhusu Afrika Mashariki. Mimi nafikiri wakati umefika sasa hivi tuangalie namna gani tunaweza tukachukua soko la hizi nchi zaidi ya wenzetu wanavyochukua soko hili kwa ajili ya mauzo yao. Namna gani? Tuna gesi ya kutosha kabisa, inakisiwa kwamba tunaweza kwenda nayo hata miaka mia moja mbele na gesi hii sasa hivi inatengenezewa utaratibu wa kujengewa bomba kuletwa Dar es Salaam ili ku-*rescue environment* wakati huohuo ku-*reduce cost* ya matumizi ya majumbani

kwa kutumia umeme, kwa kutumia *cooker* na kwa kutumia mkaa ambao una athari mara mbili katika taifa letu. Lakini hebu tujiulize, iwapo sisi Tanzania na ukubwa wetu wote tuliokuwa nao na miti na mkaa wote tuliokuwa nao bado tunaji-*prepare* kuleta gesi katika miji mikuu ili isaidie kuokoa *environment*, sasa fikiria Kenya wakoje? Nchi yao ni ndogo kulikoTanzania, Uganda, Burundi na Rwanda na wao wana matatizo kama haya ya *environment*. Sasa sisi kama tutachukua mikopo kutoka *ADB* au hata *World Bank* wakati wakijua kwamba sisi tuna gesi, tunaweza tukatandika *pipelines* hata kabla ya sera kuanza tukazipeleka katika nchi jirani na wao wakafaidika na gesi hii na sisi tukapata fedha za kigeni. Hilo ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili sisi tunaangalia gesi ile kuipeleka Dar es Salaam tu lakini kuna miji mingine mikuu mingi tu, kwa nini tusijikite sasa hivi kutengeneza *cylinders* au majiko madogomadogo kwa bei nafuu tukaziuzia nchi za jirani yaani Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda na tukaweza kupata fedha za kigeni kutoka kwao na wao wako tayari kununua hicho kitu kwa sababu hawana gesi. Kwa hiyo, hii Wizara ishirikiane na Wizara ya Biashara na Viwanda, Wizara ya Nishati na Madini ili waweze kulifikisha hili suala katika nchi za jirani tufaidike na kuvuna mavuno ya gesi kwa nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kitu kimoja ambacho hatujakiangalia na sijakiona kupewa uzito lakini kina umuhimu wake nacho ni *disaster preparedness*. Sisi kama tutakubaliana na nchi hizi tunaweza tukawa na *rescue teams* kwa kila nchi ikaweza ikaisaidia nchi

nyingine badala ya kungoja misaada au *rescue teams* kutoka *South Africa.* Leo kama kungekuwa na *rescue team* ya Afrika ya Mashariki kwa ukanda wa bahari ni Kenya na Tanzania lakini kwa ukanda wa maziwa kuna Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda wanaweza wakatumia *Lake Victoria,* wakatumia *Lake Tanganyika* kwa ku-*rescue boat* zinazotembea na abiria katika maeneo yale. Sisi leo meli mbili zimeangamia katika bahari *rescue team* ya mwanzo ya Zanzibar ilitoka *South Africa,* ilikuwa iteremke labda kutoka Mombasa au kutoka Tanga au Dar es Salaam lakini mpaka watu wanakufa *the whole day* hakuna *rescue team* iliyofika. Kwa hiyo, hiki kitengo kianzishwe katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kiweze kusaidia maafa na ajali zinazotokea katika bahari na maziwa ya nchi zilizozungukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni Kilimo Kwanza. Tunapozungumzia Kilimo Kwanza haina maana kwamba tulime kwa ajili ya kushibisha matumbo yetu, hapana! Bali tuwe na *surplus* na *surplus* ili ipatikane katika nchi hii, bahati mbaya katika nchi za jirani kama Kenya na Uganda wakawa na *disaster* ya *drought*, tukawazuia na ikaonekana ni *criminal* watu wenye mahindi kwenda kuuza nchi za jirani wakati *market* iko na *surplus* ipo. Kwa nini sisi tusijikite zaidi tukawa kama ni *harbour of the agriculture* katika *zone* ya Afrika Mashariki ili *disaster* yoyote inayotokea katika nchi hizi sisi tukawa na *rescue* ya kupeleka chakula wakati huohuo tunawatengenezea mazingira bora wakulima ambao wameitikia wito wa Kilimo Kwanza? Kwa hiyo, sisi kama tutakuwa tayari kuwajengea mazingira, tukawawekea maghala ya

kisasa na tukawapa uhuru wa kuuza bidhaa zao kwa nchi jirani badala ya kungojea stakabadhi ghalani, tutakuwa tumewasaidia wakulima wetu na hilo ndilo litakaloinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni mabenki. Tazama Kenya ilivyofungua mabenki yake katika nchi hizi, kila unapokwenda unakuta *KBC* lakini sisi tuna benki gani? Tunaogopa nini kuchukua *capital flight* kupeleka katika nchi hizi? Tuyahimize haya mabenki yafungue mabenki katika hizi nchi kwa kila angalau mji mkuu wa nchi hizo iwepo Kampala, Nairobi, Kigali na hata Bunjumbura. Ndivyo ambavyo wananchi wetu wanaofanya biashara watazitumia hizi benki hata na watu wa Kenya watatumia hizi benki kwa ajili ya biashara zao baina ya nchi na nchi. Leo matokeo yake sisi tunatumia benki za Kenya lakini sisi hatuna benki Kenya, Kenya leo wamefungua benki 10 *South Sudan*, baada tu ya uhuru mwaka mmoja wana benki 10. Kenya wanachukua mahindi Tanzania wanayasaga na baada ya kuyasaga wanayatia kwenye *packet* wanauza *South Sudan* kwa sababu *South Sudan* ni walaji wazuri wa ugali. Kwa nini sisi tusianzishe viwanda vidogovidogo vya kusindika mahindi katika maeneo ambayo tunawazuia watu wasiuze mahidi yao Kenya tukachukua mahindi yale yaliyokuwa tayari yameshakuwa yameongezewa thamani tukauza Kenya, Sudan, Burundi na hata Rwanda? Kwa hiyo, kufungua mabenki na kufungua viwanda vya kusagia mahindi vitasaidia kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata maziwa ambayo tunayo, sisi tuna maziwa mengi zaidi kuliko Kenya, lakini angalia maziwa ya Kenya yanatumika namna gani? Leo Kenya unakwenda dukani unanunua mpaka *packet* ndogo ya kupaka kwenye *slice* mbili za mkate, kwa nini wakafanya hivyo? Wanafanya hivyo ili waweze kuchukua soko la mteja mpaka wa hali ya chini kabisa lakini sisi tuna maziwa hapa hatuna siagi, jibini wala hatuna maziwa yenyewe lakini Kenya wana mpango wanaita 'Nyayo' badala ya kupeleka uji kwenye shule wao wanapeleka maziwa kwa sababu yana *nutrition* za aina zote, kwa nini na sisi tusiondoe kodi kama walivyoondoa Kenya? Kwa nini tusipunguze *VAT* ili viwanda vya maziwa vikaweza kuzalisha maziwa na ku-*supply* katika shule zetu na yakapata soko tukayapeleka nchi za jirani? Lakini leo maziwa tunaagiza kutoka *South Africa*, Kenya na nchi nyingine *almost* 10% to 20% ni maji wakati sisi tuna maziwa safi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nasema kama sisi hatutaogopa kwa sababu ni waoga sana, Watanzania tuna tabia ya woga, tunaanzisha jambo halafu tunajitisha wenyewe na ukijitisha mwenyewe, hata nguo yako ukiitundika nyumbani ukutani nyumbani wakati unapowasha usiku taa ukaja mwanga wa mwezi unaweza ukafikiria ni shetani kumbe ni kanzu yako mwenyewe. Sasa na sisi ndiyo tulivyo, Wakenya wanataka nchi yetu, Wakenya wanataka ardhi yetu na Wakenya wameingia mikataba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Watanzania na Waganda, Warwanda na Waburundi, hivi kweli sisi tumwone mwekezaji ni bora kutoka India, China, Europe na kutoka Amerika kuliko kutoka Kenya

ambaye ni jirani yako na ambaye una mikataba naye na ambaye yuko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, tunaogopa nini? Waache waje Wakenya kama wanaleta *capital na capital* tutaitumia tutajenga viwanda na tutakuwa na mashamba ya kisasa siyo tukae tu, ooh, tuna ardhi kubwa watatunyang'anya, nani kakwambia wanataka kunyang'anya ardhi yako? Nani anakutisha? Hebu tujengeni mazingira ya kuaminiana kama tuna ardhi kubwa basi tuitumie ardhi kubwa kuwasaidia Wakenya na Waganda waje wa-*invest. Recently*, mimi nimemwona *investor* mmoja from Naijeria amekuja Tanzania kufungua kiwanda cha *cement,* kwa nini hatukumzuia? Kwa hiyo, sisi leo tuna *prefer* mtu atoke Naijeria kuliko mtu ambaye yuko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki? Sisi tukaribishe bwana watu kama hao waje katika Bara letu na waje katika nchi yetu na ndiyo tukaona kuna nchi ambazo zipo mbali kama Brazil, India China, Rusia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanya, ni kengele ya pili!

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa uniongezee dakika tano. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na mchangiaji wangu wa mwisho ni Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kwanza kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa katika Bunge la Afrika Mashariki kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili niseme kwamba Zanzibar kuna zao la karafuu, nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lazima tuthaminiane, tuheshimiane na tulindiane haki zetu. Kwa mfano, Kenya hawawezi kuzuia magendo ya karafuu, wanazinunua karafuu kutoka Zanzibar jambo ambalo wanaua uchumi wa nchi nyingine ambayo ni Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sasa naomba ili Jumuiya hii iwe na thamani na heshima kwa nchi wanachama basi wazuie mara moja ununuaji wa karafuu kutoka Zanzibar. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hivyo kwamba wazuie ununuaji wa karafuu kwa njia ya magendo, siyo njia halali. Kama ni njia halali basi waje wanunue. Tunataka waje wanunue karafuu kwa njia halali, lakini si kwa njia ya magendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ni kwamba nchi Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ni Tanzania imejaliwa kuwa na bahari na maziwa, nchi nyingine wanachama ambazo ni za jumuiya hii zinapitisha mizigo yao kupitia bandari zetu. Sasa ni wajibu wa nchi yetu kwanza kuziendeleza ipasavyo bandari zetu ili nchi jirani wanachama ziwezi

kupitisha mizigo yao katika bandari zetu ili nchi yetu iweze kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala la ajira katika jumuiya, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa majumuisho ya hotuba yake atueleze ni Watanzania wangapi ambao wamepata ajira kupitia jumuiya hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala zima la reli. Reli ni njia nyingine ambayo inaweza ikakuza uchumi wetu kupitia nchi wanachama wa jumuiya hii ambao watapitisha mizigo yao katika reli zetu. Kwa hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri amtake Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia masuala ya reli basi na yeye ashughulikie reli zetu zijengwe ili mizigo hii ya nchi jirani iweze kupita katika nchi yetu ili tuweze kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa nchi yetu wana haki na wajibu wa kuitangaza nchi yetu katika nyanja za kiutalii ili tuweze kuingiza mapato kupitia sekta ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile si vyema kama watatokea wanachama wengine wa jumuiya hii wakataka kutuchezea katika nchi yetu kwa masuala ya ardhi. Naomba Watanzania tuthamini ardhi yetu ili isichezewe na wanajumuiya wengine. Nina hakika kwamba Wabunge tuliowachagua wana upeo na uwezo wa kushiriki popote na kupinga chochote ambacho kitakuwa hakina maslahi kwa Watanzania. Kwa hiyo, ni wajibu wao kuhakikisha lolote ambalo

wataliona kwamba halina maslahi na nchi basi walipinge moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na ninakushukuru sana Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/2013 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sote tunavyofahamu, Wizara hii ni roho ya ustawi wa jamii yetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, hivyo majukumu yake ni mazito na yanahitaji umakini mkubwa sana katika utekelezaji. Ni kheri tuwaunge mkono na kusaidiana nao katika kuboresha na kuondoa upungufu unaojitokeza kila siku maana sidhani kuwa ni busara kukosoa tu bila kutoa suluhisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa sana katika ajira kwa Watanzania ndani ya Jumuiya. Kwa kipindi kirefu labda tangu uanzishwaji upya wa Jumuiya, wananyanyaswa sana pale inapotokea kuwa wamepata kazi ndani ya nchi nyingine wanachama haswa Kenya. Hali ya kuwa wananchi wa nchi nyingine wanapata fursa kubwa sana katika soko la ajira nchini.

Serikali iliangalie hili kwa mapana na kuchukua tahadhari stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, haki za ardhi zinakiukwa ikiwa ni pamoja na wageni kutoka nchi jirani ndani ya Jumuiya kukimbilia na kununua ardhi kwa kasi sana. Naomba Serikali iwe makini lakini pia itamkwe rasmi kuwa ardhi si sehemu ya makubaliano katika mkataba wa jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine linahusu mipaka baina ya nchi wanachama kwa maana ni mara kadhaa tumekuwa tunasikia taarifa kuwa nchi jirani zinafikia hatua hata ya kuhamisha alama za mipaka kwa makusudi ili kujiongezea nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kwa wafanyabiashara kutoka Tanzania kusumbuliwa mipakani haswa mpaka wa Lunga Lunga na Namanga hii ni pamoja na kudaiwa kulipia ushuru hata kwa mazao ya kilimo ambayo hayastahili kulipiwa. Pia Maafisa Uhamiaji wanawanyanyasa sana watumiaji wa mipaka kufikia hata kuwadai rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuingia katika shirikisho la kisiasa halifai na halina faida yoyote. Tusijiingize katika matatizo mengine ambayo hayana msingi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri asirudi nyuma katika jitihada zake za kuhakikisha ushiriki wa Tanzania katika shirikisho ni

wenye manufaa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili waelewe nini maana ya Jumuiya hii faida na hasara zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana ya kuandaa hotuba kwa kina na umakini mkubwa. Pia tunashukuru kwa taarifa za ufahamu za vitabu vilivyoambatana na hotuba, hakika huyu ni Waziri wa *standard and speed.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuanzisha vipindi kwenye redio na television vya kuelimisha umma kuhusiana na yanayofanyika kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki. Kuanzia mwaka jana Watanzania wengi tumeanza kupata uelewa mpana na kujua zaidi kuhusu shirikisho hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha mtangamano wa Afrika Mashariki, tumeona Itifaki 14 zilizokwishasainiwa na nyingi zimeridhiwa kwa nyakati tofauti, Itifaki nyingine zipo kwenye majadiliano. Naiomba Serikali ieleze Bunge kuna utaratibu gani umeandaliwa kuhakikisha Watanzania tunazifahamu Itifaki hizo na kuona yale yaliyomo ndani yake kwa maslahi ya Taifa letu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki ya Kusimamia Maliasili na Mazingira katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ya tarehe 3/04/2006 inagusa kwa kiwango kikubwa sehemu ya uchumi wetu. Bunge la Tanzania

linafahamu kwa kiasi gani Itifaki hiyo muhimu sana? Kenya wamekuwa wanatangaza vivutio vya Tanzania kwamba vipo kwao na kwa sababu ya umakini wao wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kushawishi watalii wengi kutembelea Kenya. Suala hili Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa nini imeinyamazia Kenya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Bunge ndicho chombo cha kuwakilisha wananchi wote, naishauri Serikali ilete hapa Bungeni Itifaki zote zilizoko kwenye majadiliano ili tuweze kupitia na kutoa mawazo yetu kabla ya kusainiwa na kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kujiunga na *EAC* ni kunufaika na fursa zilizopo kama Taifa lakini pia ni kujifunza kutoka kwa nchi jirani zetu mafaniko waliyoyafikia katika kuinua uchumi wao na watu wao kwa ujumla. Kwa kuwa Rwanda wamefanikiwa kupambana na rushwa na kuiondoa/kuipunguza sana, sisi Serikali imepanga mipango gani ya muda mfupi, mrefu na endelevu ya kuondoa rushwa iliyokithiri sana na inadidimiza maisha ya Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uharamia limekuwa tishio kubwa kwa usalama wa raia na mali zao. Baadhi ya majirani zetu kama Uganda, Kenya wameshaonja matatizo ya uharamia na hata sasa wanapambana nao. Ni kwa nini Tanzania haionekani kushiriki na nchi jirani kupambana na uharamia huo ili kuongeza nguvu ya pamoja?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejiandaa vipi kukabiliana na maharamia wa aina zote kutoka

kwa nchi jirani kama Wasomali wakati upo udhaifu mkubwa sana na ulinzi mipakani kwetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vitano vya Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki sijaona hata kimoja kilichotengenezewa mpango mahsusi wa Taifa kunufaika na shirikisho la *EAC* kama kilimo na usalama wa chakula, viwanda, miundombinu, utalii na nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isipokuwa makini, nchi nyingine ndizo zitanufaika na vipaumbele hivyo. Leo Kenya wananunua mazao ya kilimo na mifugo kutoka Tanzania kwa bei ndogo sana, wanakwenda ku-*pack* na kusafirisha kwenda kuuza nje na ndani kwa bei kubwa. Sisi tumekuwa ni soko la bidhaa kutoka kwenye viwanda vya Kenya, Burundi, Rwanda na Uganda. Sisi tunasubiri:-

(i) Wawekezaji wajenge na kuendeleza viwanda vyetu.

(ii) Pamoja na Tanzania kuwa na vivutio vingi, bado hatujaanza kukamata soko la watalii kutokana na sababu mbalimbali kama vile miundombinu, vyombo vya usafiri, utangazaji na kadhalika.

(iii) Tumeshindwa kusimamia bandari zetu nzuri mizigo inakwenda kushukia Mombasa, kiwanja cha ndege kina jengwa TAVETA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunao vijana wengi wamesoma, wanazurura mitaani kwenye hotel za kitalii na mashirika mbalimbali, Wakenya ndio wengi kwenye *position* za juu. Wizara na Serikali inatuambia nini kutokana na hali hii?

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza kuunga mkono bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki na kupongeza kwa ujasiri wa kutoogopa ushindani wa wenzetu wanaotuzunguka. Pamoja na hayo, kwenye soko la bidhaa, wenzetu wanafanyabiashara yao bila kikwazo na kupitisha sehemu zote kwa uhuru. Kwenye eneo la Tanzania bado kuna ukiritimba wa vizuizi barabarani na kuwakwaza wafanyabiashara pamoja na kodi ya juu kuliko wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipokuwa Namanga pamoja na Waziri wa Kenya, alikemea vituo vya kuzuia bidhaaa hata wakati mwingine wanakuja porini kuweka kizuizi, wananchi wa Longido wamenituma Waziri afanye mambo yafuatayo:-

(i) Aje Longido na Namanga ili wamueleze kero zao.
(ii) Atoe kwa kutangaza tena vizuizi vyote vitolewe.
(iii) Ajenge soko la bidhaa na la mifugo karibu na mpaka wa Namanga.
(iv) Sarafu ya Tanzania kubadilishwa kwa bei ya chini sana kwa sasa Tanzania shilingi 19 ni sawa na shilingi moja ya Kenya, hii inatunyima

kufanya biashara sawa na wenzetu. Ina maana shilingi laki moja ya Kenya ni sawa na shilingi milioni 1,900,000 ya Tanzania. Hii haiwezekani, Tanzania ndio yenye mazao na vyakula kuliko Kenya. Tanzania ndio wana mifugo mingi kuliko Kenya lakini kwa kuwa wao ndio wenye masoko tunawaleta wanunue kwa bei wanayotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni elimu. Ubora wa elimu Tanzania unazidi kuporomoka mwaka hadi mwaka huku Serikali ikiwa kimya bila kurekebisha mfumo wa elimu, naomba suala hili litazamwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri anipe majibu wananchi wa Longido wanamsubiri leo wamsikie, wanapenda awajibu kupitia majibu ya majumuisho ya bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu amlinde na kumpa maisha marefu ahsante.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Samuel Sitta kwa hotuba yake nzuri iliyowasilishwa kwa viwango vya juu kama ilivyo kawaida yake. Pamoja na bajeti finyu, maandalizi na uwasilishaji wake umeongoza katika Wizara zote *so far*. Aidha, nimpongeze Naibu Waziri Mheshimiwa Saadalla ambaye ni mchapakazi, muadilifu akiungana na Katibu Mkuu Dkt. Tax, Naibu Katibu Mkuu na watumishi weledi kama waliopo hapo Wizarani, wanatuweka

katika medani ya Afrika Mashariki, nawapongeza sana wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa tulikubaliana ili kwenda pamoja na yanayoamuliwa kwenye Bunge la Afrika Mashariki kwani kulingana na *treaty* yanayoamuliwa na *EALA* yana *supercede* ya *National Parliaments,* tulipendekeza Wabunge wa *EALA* (Watanzania) wawe *facilitated* kuhudhuria vikao vya Kamati za Bunge Dar es Salaam kulingana na Kamati wanazohusika nazo ndani ya *EALA*. Naona ni suala ambalo inabidi ku-*push* kwa pamoja, naomba muendelee kulijengea hoja nasi tutakazana kusukuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tunaanda na kuandika Katiba Mpya na yapo mambo ambayo yamepitishwa na Bunge letu la Afrika Mashariki, je, ni utaratibu gani waliojipanga nao hapo Wizarani kuhakikishia yale mambo ya msingi ambayo tumekwishaingia kwenye makubaliano hayaitaathiriwa katika Katiba Mpya?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni mikakati gani waliyonayo katika kuhakikisha kuwa Mji wa Arusha unaendana na hadhi ya Makao Makuu ya Afrika Mashariki, majengo, miundombinu, mazingira na kadhalika? Kwa nini hatuwazi kujenga Makao Makuu katika eneo kubwa, tuweke *hotel,* maduka, *airstrip* na kadhalika? Mbona hatupo *innovative* kuwaza na ku-*sketch, infrastructure* haihitaji fedha ni wazo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali ya ushindani, Bunge la *East Africa* lina Spika Mganda na

hali kadhalika Katibu na Katibu Msaidizi. Je, mmejipangaje kuhakikisha kuwa Watanzania wengi wanapata ajira *EAC* na za maana siyo uhudumu/usekretari/na ulinzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tulikuwa kwenye ziara ya kikazi Marekani na Uingereza, tulikuwa tunaulizwa kwa nini tuna–*drag* Jumuiya na kwamba kweli tuko *committed*? Tulijibu *we are not dragging or delaying we are being cautions that's all*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko pamoja.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuvunje nchi zote za Afrika Mashariki na tubaki na nchi moja ya Afrika Mashariki. Mheshimiwa Waziri na Bunge kwa ujumla wake, muungano wa watu na nchi zao ni jambo jema sana, siku zote tunapaswa kujiuliza ni sababu gani zinazotufanya tusiungane na badala ya kuungana tunakalia kuimba wimbo wa Shirikisho la Afrika Mashariki. Huo wimbo unachosha sana, *in fact* kuchelewa kuanza kwa Shirikisho letu la *EAF* ni woga miongoni mwa watu unaosababishwa na ubinafsi, ulafi wa mali na madaraka miongoni mwa watu wetu na hasa viongozi na wafanyabiashara wakubwa na wale wa kada ya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, makundi hayo ya wafanyabiashara na viongozi ndiyo hasa yenye hofu kubwa kwa kuwa wanadhani shirikisho hili likifanikiwa watapoteza maslahi yao jambo ambalo siyo kweli bali kinachotakiwa ni uadilifu katika kuendesha mambo yote. Viongozi wanakwepa kupoteza madaraka huku

wafanyabiashara wakihofu kupoteza fursa za kibiashara na ushindani kwa maslahi yao binafsi jambo ambalo siyo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, makundi hayo ya viongozi na wafanyabiashara wa nchi zetu hasa Tanzania wameugua ugonjwa HOFU-YOSIS yaani wamejitwika hali ya kuhofia ushindani kwa maslahi binafsi na wanaeneza propaganda kwa wananchi walio chini yao ili waone kuwa Watanzania hatuwezi kushindana jambo ambalo siyo kweli, tujiamini tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na hitimisho, ku-*loose sovereign state status* kwa ajili ya kuungana si jambo baya huku tukijua tutaimarisha uchumi na mshikamano miongoni mwetu. Tuache woga sasa na tuamue kuunda nchi moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki au nchi ya Afrika Mashariki. Ubinafsi, uroho wa madaraka ni dhambi mbaya sana na chanzo cha kushindikana au kukwama kwa mambo mbalimbali duniani. Tuache upofu tunaojivisha na tuungane sasa na Wakenya, Warundi, Waganda na Wanyarwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kuchangia kwa njia ya maandishi lakini pia ni vyema nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo lisilopingika kuwa ushirikiano huu utakuwa ni muhimu sana kama utakuwa na utaratibu mzuri wa kulinda uchumi wetu kwa wakati huo kutanua soko la nje kwa bidhaa zetu katika hali hiyo ni vyema nigusie mambo niliyoyagusia hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulinda uchumi wa nchi wanachama. Zanzibar kama sehemu ya Tanzania ina uchumi wake. Karafuu ni zao kuu la uchumi wa Zanzibar. Karafuu hizi husafirishwa na wahalifu na kuzipeleka Kenya jambo ambalo linadhoofisha uchumi wa Zanzibar akiwa ni mdau wa Umoja huo. Kwa maana hiyo ni lazima kuwe na nidhamu ya kiuchumi baina ya nchi hizi shirikishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhusiano wa kibiashara. Ninaelewa kuwa hili ni kati ya malengo makuu ya Umoja huu lakini ni vyema kabisa kufungua milango ya biashara na sio kuzuia bidhaa kupelekwa nchi nyingine, hii itasaidia uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimu Naibu Spika, kabla ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa neema na rehema zake kwangu. Ni wajibu wangu kusema *Alhamdulillah*!

Mheshimiwa Naibu Spika, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Kwa mantiki hiyo, tunaona haja na maana ya kuwa na ushirikiano wa Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mantiki hiyo, kila lenye faida kuna hasara zake, kabla hatujaenda mbali, tuangalie pande zote za ushirikiano au Umoja wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ulimwengu huu wa utandawazi ambao una wigo mpana pia wa ujasusi na ugaidi, hatuna budi kuwa makini sana. Ushirikiano huu au Jumuiya hii kusiwe na undani au uadui wa ndani kwa ajili ya kuangalia maslahi binafsi. Jambo hili hivi sasa lipo na ndio maana ni kama wasiwasi! Ushirikiano ni udugu lakini inakuwaje leo Kenya ndio *exporter* wa *Tanzanite* badala ya Tanzania? Madini yenye jina la nchi yetu! Je, huu ndio ushirikiano au uhujumiano? Kwa nini Serikali ya Kenya ikaruhusu *Tanzanite* iuzwe hadharani tena kwa *export trade*? Pia karafuu zao kuu la biashara la Zanzibar. Nchi zenye ushirikiano ni lazima ziwe na msimamo wa pamoja kulinda maslahi ya kila mmoja katika jumuiya badala ya kila nchi kuwa ni mhujumu namba moja wa mwenzake!

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya kazi na ajira pamoja na umiliki wa ardhi ni jambo muhimu pia kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Samuel Sitta, Naibu Waziri Mheshimiwa

Dkt. Abdulla Saadalla, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuimarisha uhusiano wa Afrika ya Mashariki pamoja na kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niendelee kuipongeza Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa ushauri wao mzuri. Nina imani Serikali itachukua maoni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasahau, napenda kutamka rasmi kuwa ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia, Mungu awape nguvu ya kutekeleza azma yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna ya kumiliki maliasili zetu, nakumbuka nchi za wenzetu za Afrika Mashariki bado zinataka maliasili ziwe za pamoja mfano ardhi na kadhalika. Naendelea kutoa rai kwa Serikali yangu kutokubali ardhi yetu yenye utajiri mwingi yakiwemo madini ya kila aina kuwa ya Afrika ya Mashariki tutakuwa tumepoteza mali nyingi ambazo ni urithi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi za Balozi zetu za nchi za Afrika Mashariki zinakabiliwa na upungufu wa watumishi, bajeti na samani, hivyo ni vema Serikali yetu iangalie namna ya kuboresha ili ziweze kuwa na hadhi pia watumishi wetu waweze kufanya kazi vema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mlima wetu wa Kilimanjaro, naomba utata wa wenzetu wa nchi ya Kenya ambao daima wanadhani mlima huu uko

Kenya sasa ufikie mwisho, mlima huu ni mali yetu Watanzania asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wetu wa Bunge la Afrika Mashariki, napenda kutoa rai kwa Serikali kuwa Wabunge niliowataja hapo juu kwa kuwa tumewachagua sisi Wabunge wa Bunge la Tanzania ni vema wawe wanarudi kutoa taarifa ya kazi zao ili nasi tujue na Watanzania wafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho narudi tena kuunga mkono hoja hii.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri na timu yake ya wataalam kwa kufanya kazi nzuri katika mazingira ya bajeti ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za mtangamano, *the four phases of integration,* nafuatilia kwa makini *stages* za *integration i.e customs union, common markert* na karibu tunaingia *single currency* au *monetary union* na baada ya miaka mingi tutafikiria hatua ya *political federation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *concern* yangu ni umuhimu wa kuwapatia wananchi elimu kuhusu mchakato huu muhimu wa hatua za *integration*. Wananchi sharti wajue maana ya *customs union* na nchi yetu inafaidikaje. Hivyohivyo kwa hatua ya *common market* au soko la pamoja, Wizara hii inatakiwa kuendesha semina kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, *monetary union,* je, tuko tayari kuingia katika muungano huu? *Should we fast-track this process?* Jumuiya ya nchi za Ulaya ambayo ina nchi 27 ni nchi 18 tu ziliridhia *monetary union* na imewachukua miaka 50 kufikia uamuzi huu. Sarafu ya nchi ni *national identity* ya nchi, kukubali kuiachia kutegemea manufaa mengi yatakayopatikana. Ni muhimu sana kufanya majadiliano ya kitaalam ya Wachumi waliobobea pamoja na Wanasheria kuhusu *pro and cons za monetary union*. Lakini pia wataalam wafanye *study* kuhusu changamoto wanazokabiliana nazo nchini za *European Union.* Kwa nini Waingereza hawajaamua kuingia kwenye *Euro zone*, wana sababu nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujifunze kutokana na *Eurocrisis* ambapo nchi kama Greece, Spain, Italy na Ireland zilijiingiza katika madeni makubwa kiasi cha kuathiri sarafu ya *Euro,* imebidi Ujerumani na Ufaransa zijitahidi kuiokoa sarafu ya *Euro* kwa kuzi-*bail out* hizo nchi za Greece na Spain. Ujerumani na Ufaransa ni nchi zenye uchumi mkubwa. Je, sisi tukiingia kwenye *monetary union* halafu tukajikuta kwenye matatizo ya sarafu itakayokuwa imechaguliwa, tutafanya nini? Hatutakuwa kwenye tatizo hilo kama Ujerumani na Ufaransa zinavyojitahdi kuiokoa *Euro?*

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya Isaka - Keza - Msongati - Burundi - Keza - Rwanda, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba reli hii ni muhimu sana kwa nchi za Tanzania, Burundi na Rwanda. Reli hii itapita Wilaya za Kahama, Biharamulo na Ngara kuelekea Rwanda na Burundi, hivyo itachochea maendeleo

katika Mikoa ya Shinyanga na Kagera. Reli hii itasomba *Nickel* kutoka Mgodi wa *Kabanga Nickel* ambao ni wa pili kwa ukubwa duniani baada ya ule wa Canada *in terms of deposits* za *nickel*. Milima yenye *Nickel* ya Kabanga – Tanzania, ni milima hiyohiyo inayokwenda Msongati, Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji katika *nickel* ya Msongati, Burundi kutaka reli kupita Uvinza. Msongati iko karibu sana na Kabanga milima hiyohiyo. Naunga mkono uamuzi wa nchi tatu za Tanzania, Burundi na Rwanda kuwa na reli hiyo ya Isaka - Keza - Msongati na Keza - Rwanda na siyo ku-*divert* reli kupita Uvinza.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kwa Tanzania kushiriki kikamilifu katika hatua za mtangamano, ni muhimu kwa Tanzania na Watanzania kujiandaa kikamilifu kushiriki katika hatua hizo za mtangamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuimarishe elimu yetu katika ngazi zote ili vijana wetu waweze kupata elimu nzuri ili waweze kushindana katika soko la ajira la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaala ya vyuo vyetu iangaliwe upya ili kuwepo na msisitizo wa kutoa *skills* mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya lugha ya kiingereza hapa kwetu Tanzania ni tatizo kubwa. Nimeshiriki katika *interviews* za *East Africa Community*

na *Africa Union*, nimeshuhudia Watanzania wengi wakikosa kazi nzuri kutokana na tatizo la kiingereza.

**MHE. DONALD K. MAX:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba awali ya yote niipongeze Wizara kwa juhudi na kwa msukumo huu wa awali katika kulinda maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Waziri na Wizara, ramani ya Dodoma imetumika na nchi ya Nigeria na Malawi wakati sisi tumekaa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utajiri, nchi tunazotaka kuungana nazo hazina asilimia 80% ya utajiri wa mali tulizonazo. Kwa kuwa hatuna uwezo wa kupata mawazo ya Watanzania wote kama tunavyoshughulikia, mimi naomba vitabu vya Wizara hii viwe vinatolewa mwezi wa sita ili Wabunge wavipitie taratibu kwani Wabunge hawawezi kuvisoma muda wa siku moja ili muda utoshe kulisaidia Taifa maana hili si suala jepesi sana.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani na uwezo na dhamira ya Mheshimiwa Waziri katika Wizara hii nyeti katika ushindani wa eneo hili la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kama nchi tujipambanue kwa kuwa na *strategic agenda.* Kenya agenda yao ni fursa ya kupumua mitaji yao na Tanzania ni eneo la kimkakati kwao. Rwanda, Burundi na Uganda agenda yao kimkakati ni eneo kutokana na ongezeko la kasi la idadi ya watu. Je, Tanzania

agenda yetu ni ipi? Huu sio ushirikiano wa Kanisa wala Msikiti, hii ni *strategic partnerships, we must have strategic agenda*.

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya kuunganisha Burundi na Tanzania *shortest distance* ni Uvinza - Msongati lakini bado naona vitabu vinaonesha kupitia Isaka. Naomba kujua mpango huu upo katika hatua gani. Lini reli ya Uvinza - Msongati itaanza?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Bunge lako Tukufu kupitia Wizara ya Afrika Mashariki liweze kutupa uwezekano wa kuruhusu Wabunge wetu wote waliopitishwa kuiwakilisha nchi katika Bunge la Afrika Mashariki, wapewe nafasi ya kuja kutueleza *(feedback)* yale yote yaliyojiri katika Bunge la Afrika Mashariki ili nasi tuwe na nafasi ya kuwahoji hususani wakati wanapitisha mikataba inayohusu maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutimiza majukumu yangu vizuri na uhai anaozidi kunijalia. Napenda kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo na usafirishaji wa mazao, ni dhahiri na wazi sisi kama Watanzania tuna fursa kubwa ya kupata soko la mauzo ya bidhaa zetu zinazotokana na kilimo katika nchi zinazotuzunguka

zilizo kuwa katika Jumuiya hii. Naongelea hilo kutokana na mfano mzuri wa mazao yanayozalishwa ndani ya Jimbo langu kama vile mhogo na mpunga. Kuna shehena kubwa sana zinasafirishwa kwenda Rwanda, Burundi na Uganda, chakula hiki kinanunuliwa kwa pesa ndogo sana toka kwa wakulima vijijini ambapo hata muda mwingine ushuru ndani ya Serikali za vijiji haulipwi. Bado zao kama mhogo likifikishwa kule likasindikwa sisi Watanzania tunarudi kununua mhogo ule kwa bei kubwa mfano biskuti zitokanazo na mhogo, wanga na kadhalika. Haya yote yanapofanyika wakati mkulima huyu hafaidiki bado tutakuwa hatuna la kujivunia katika umoja huu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya forodha na mipaka, kumekuwepo na sheria na taratibu ambazo hazitoi usawa pale mtu anaposafiri toka nchi moja kwenda nyingine au kusafirisha mzigo. Malipo yanatofautiana, usumbufu wa ukaguzi mizigo na kadhalika. Hali hii inapaswa kufanyiwa marekebisho ili tuendane na hali sawia.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hotuba ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao ya kilimo yapewe umuhimu kuuzwa katika nchi za jirani badala ya kuzuia kila wakati na kufanya wakulima wetu kuwa maskini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira, tuwe makini sana, jamii yetu bado haijatayarishwa kushindana. Ni vizuri Wizara kuongeza elimu kwa umma na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ya umeme, ni mipango ipi iliyopo ndani ya Wizara itakayoleta umeme upande wa Tanzania na Burundi kwa pamoja mipakani ili nchi zote zifaidike kwa pamoja, naomba kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraja/barabara, Jimbo la Manyovu linapakana na Burundi lakini biashara inapata kikwazo kwa sababu sehemu nyingine zina tatizo la madaraja na barabara za kuunganisha. Nini mpango wa Wizara? Maeneo hayo ni ya kijiji cha Kibande, Kilelena na Mnyama. Tunaomba maeneo hayo yafanyiwe utafiti na yajengwe kwani ni kero kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nawatakia maisha mema ya utekelezaji.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Samuel Sitta, Waziri na Mheshimiwa Dkt. Abdulla Saadalla, Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya kusimamia utekelezaji wa mikakati ya mtangamano wa Afrika Mashariki. Nampongeza pia Bibi Stergomena Tax, Katibu Mkuu na Bwana Uledi Mussa, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi na Watumishi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikutano ya kisekta na Bunge la Afrika Mashariki. Tokea niingie Bungeni sikumbuki kama kuna sheria iliyopitishwa na Bunge la Afrika Mashariki iliyowasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa. Kama ziko sheria zilizotungwa au zinazotarajiwa kutungwa, ni vizuri Bunge la Jamhuri ya Muungano likahusishwa katika kuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikutano ya kisekta, ardhi pengine haijawa agenda kwenye mikutano ya Jumuiya. Aidha, sina taarifa kama kuna Kamati ya sekta hii chini ya Jumuiya, kama ndivyo nashauri kuwa utaratibu ufanyike kushirikisha Wizara ya Ardhi kwenye Kamati inayoshughulikia masuala yanayohusiana na ardhi ili kuhakikisha kuwa masuala hayo yanapojadiliwa maslahi ya Taifa letu yanalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa Umoja wa Fedha, napongeza jitihada zinazofanywa na Wizara kuongoza njia mchakato wa uanzishwaji wa Umoja wa Fedha Afrika Mashariki. Kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana kwenye ukanda wa *EURO,* ni vizuri uanzishwaji wa umoja huo uzingatie hatua ya maendeleo ya kiuchumi wa nchi zote. Tuweke vigezo vitakavyofanya uanachama wa nchi husika kwenye Umoja wa Fedha uridhiwe baada ya kutimiza vigezo hivyo. Kigezo kimojawapo kiwe ni kiwango cha ukuaji wa uchumi, mfumuko wa uchumi pamoja na uwezo wa uchumi wa nchi husika kujitegemea *(self sustainability*).

Mheshimiwa Naibu Spika, utatu wa Jumuiya za *COMESA, EAC* na *SADAC*, naunga mkono hatua zinazochukuliwa na Wizara kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama katika kukuza ushirikiano wa kiuchumi. Tanzania kijiografia na nafasi yake *EAC* na *SADC,* ina nafasi nzuri sana na kuwa daraja la kuunganisha Jumuiya hizi na ikiwezekana ziungane kuwa moja, ni vizuri Tanzania iongoze njia katika jambo hili kwani tutanufaika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na mwelekeo wa mtangamano *(regional integration),* Wizara ya Afrika Mashariki inapaswa kuliongoza Taifa ili kupata manufaa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa malengo na mipango ya mwaka 2011/2012, Wizara itoe maelezo kuhusu hatua ilizochukua katika kuboresha mchakato wa uchaguzi wa Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwenye mchango wangu wa mwaka 2011, niliomba Wizara ishauriane na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) pamoja na kuwa uchaguzi umeshafanyika, naendelea kuishauri Wizara ya Afrika Mashariki katika mwaka wa Fedha 2012/2013 iwezeshe kuanza mchakato wa marekebisho ya Kanuni ili kuweka msingi bora wa chaguzi zijazo. Aidha, Wizara ieleze hatua iliyofikiwa katika kusainiwa kwa Miswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Bunge la Afrika Mashariki ambao

ulipitiswa na Bunge husika mwaka 2011 lakini ulikuwa haujasainiwa na baadhi ya Marais ikiwemo Rais wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, zimepitishwa sera, sheria, mipango na mikakati mbalimbali katika vyombo mbalimbali vya Jumuiya ya Afrika Mashariki na pia katika Serikali ya Muungano kuhusu Jumuiya ya Mashariki kama nyaraka hizo zilivyotajwa katika hotuba ya Waziri kwa ajili ya kutekeleza vizuri wajibu wa Bunge wa kuishauri na kusimamia Serikali. Naomba Wabunge tupewe nakala ya nyaraka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mkakati wa viwanda, naomba katika mkakati husika Wizara ya Afrika Mashariki iangalie pia viwanda vya eneo la viwanda la Ubungo (*Ubungo industrial area*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu ubia wa kiuchumi na Jumuiya ya Ulaya (*EPA*) kuhusu kutokuharakisha kusaini mikataba husika. Nomba Wizara itoe ufafanuzi kuhusu hatua za ziada zinazochukuliwa kulinda maslahi ya Taifa katika majadiliano yanayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri imetaja miradi ya nishati ambayo imependekezwa katika jumuiya. Kutokana na miradi hiyo ni muhimu kukawekwa mfumo wa Wizara ya Afrika Mashariki kushirikisha Kamati za Bunge za kisekta katika usimamizi wa Kibunge wa miradi inayohusu sekta zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania iko katika mchakato wa Katiba Mpya hivyo Wizara ya Afrika Mashariki ishiriki kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya utangamano yanayopaswa kuzingatiwa katika mchakato wa Katiba Mpya.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania walio wengi hawaelewi tofauti ya ushirikiano uliopo wa Afrika Mashariki na ule uliovunjika, elimu itolewe mara kwa mara kwa lugha rahisi kupitia vyombo vya habari na hasa redio ili wananchi wapate kuelewa kila kinachohusu Afrika Mashariki, tusione tu viongozi wetu na Marais wanatia saini wakiwa kwenye mikutano huku watu hawaelewi kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi hawafahamu sababu za kuvunjika ushirikiano wa mwanzo na pia hawaelewi sababu za kuanzishwa ushirikiano wa sasa. Wananchi wengi hawaelewi ni maeneo yapi ni ya ushirikiano, Soko la Pamoja ni nini? Wananchi wengi wanaolima nyanya Ngarenanyuki hawafahamu ni vipi nyanya zao zinaweza kufikia soko la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tutilie msisitizo katika kutumia lugha ya Kiswahili kwani wenzetu wa Kenya wanaitumia kibiashara Ulaya, Amerika na kwingineko kwa kufundisha na kutafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia uhai na uzima hadi leo nikaweza kuchangia katika Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali isiwazuie wakulima kuuza bidhaa zao, waachwe wakulima wauze bidhaa zao wanapotaka kulingana na soko. Hii itawaondoshea wakulima wetu kuondokana na umaskini uliokithiri, hali za wananchi wetu ni ngumu sana, tusiwabane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini sisi Tanzania Serikali yetu haifikirii kuvuna gesi yetu na tukauza katika nchi hizi za Afrika Mashariki? Tuangalie iwapo sisi Watanzania na ukubwa wetu twafikiria kutumia gesi katika miji yetu ili tuepushe kukata miti ovyo na kuharibu mazingira yetu hali ya kuwa sisi tuna misitu ya kutosha kuliko wenzetu hawa ambao nchi zao ni ndogo kama vile Kenya, Uganda na Burundi ambao hawana misitu ya kutosha. Kwa nini basi Serikali haifikirii kufanya biashara ya kupeleka mabomba ya gesi katika nchi hizi ili tufaidike kwa kupata fedha za kigeni na kwa kufanya hivyo tutaondokana na umaskini na wananchi wetu wengi watapata ajira.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimwa Spika, naomba tu nimuulize Mheshimiwa Waziri kuhusu suala la sanaa ya muziki na filamu katika hili Shirikisho la Afrika

Mashariki likoje? Kwani kazi za sanaa ziko kila nchi mwanachama na zinaingia na kutoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mikataba ya wasanii wa nchi wanachama inasimamiwa na nani? Pia mirahaba ya mapato kama ilivyo *COSOTA,* je, kuna mgao unaokuja?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nawatakia kheri Waziri na wote, kazi yao ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Samuel Sitta na Naibu wake kwa namna ambavyo wanatimiza majukumu yao pamoja na watendaji wengine kwa uwakilishi wetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa hatua iliyofikia kutokana na mchango wao mkubwa kwa kushiriki katika suala zima la usalama katika Jumuiya yetu pia kuongezeka kwa nchi nyingine katika Jumuiya yetu. Ila naiomba Jumuiya ijaribu kuona ni namna gani watakomesha matukio ya mara kwa mara yanayotokea baina ya Sudan Kusini na Sudan Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato ambao unaendelea Tanzania, ni vyema Wizara kupitia shirikisho hili iangalie ni namna gani wa kuwapatia wananchi wa *EA Identity* za utambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la sayansi na utafiti, ni vyema nchi zetu zikifanya tafiti za kisayansi kwa pamoja na tuweze kutoa mchango wa pamoja wa kikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara hii itueleze ni kwa namna gani miradi ambayo iliahidiwa kutafutiwa ufadhili kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki imefikia wapi? Miradi hii ni kama vile ujenzi wa kiwanja cha Ndege cha Pemba na ujenzi wa Bandari ya Zanzibar.

**MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kidogo tu kuhusu ushirikano wa kitaaluma kwa nchi za Afrika Mashariki. Kwa kuwa soko la ajira kwa nchi za Afrika ya Mashariki sasa liko wazi, ni vizuri sifa za kitaalam nazo zikafanana. Napendekeza sasa tuwe na Baraza moja la Mitihani kwa nchi za Afrika ya Mashariki, mfano *The East African Examinations Council,* kwa ajili ya mitihani ya shule za msingi, shule za sekondari - *O level na A level* na mafunzo ya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuwe na chombo kimoja cha kuchagua wanafunzi wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu, mfano *The East African Commission for Universities*. Hii ina maana kuwa *syllabus* za shule zetu za msingi, sekondari na vyuo vyote zitafanana, somo la Siasa, *Civics*, au *Political Education* linaweza kubaki kama lilivyo kwa kila nchi ili vijana wafundishwe na kuelewa itikadi (*political ideology*) ya nchi zao na si lazima somo hili likafanyiwa mitihani na Baraza la Mitihani la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, *syllabus* moja, Baraza moja la Mitihani iliwezekana wakati wa Mkoloni, nchi zote zilizokuwa chini ya Mkoloni wa Mwingireza walifanya Mitihani ya Baraza la Mitihani ya *Campridge (The Campridge Examinations Council).* Vyeti hivi vilitambulika dunia nzima, mtu angeweza kupata kazi mahali popote duniani kutegemeana na ufaulu wake. Pia angeweza kujiunga na chuo kikuu chochote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyeti vya Tanzania, Kenya, Uganda Rwanda, Burundi havitambuliki mahali popote Afrika Mashariki, isipokuwa kwenye nchi husika, ama kidogo sana na nchi zingine kwa utaratibu wa huruma wa kufananisha (*by equating*). Kama vitatolewa vyeti vya Afrika ya Mashariki, vitatambulika kwa nchi zote za Afrika ya Mashariki, mtu ataomba kazi mahali popote na kujiunga na chuo chochote Afrika Mashariki kwa sifa zinazokubalika na nchi zote za Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano wa kitaalamu pia utaleta msukumo mkubwa wa maendeleo ya kitaalamu kwa nchi zote za Afrika ya Mashariki, ili isionekane kuwa baadhi ya nchi ziko mbele kitaalamu na zingine kuwa nyuma sana kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimwa Samuel Sitta, kwa kuaminiwa na Rais kuteuliwa kuongoza Wizara hii

muhimu sana. Pia nimpongeze Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwake kushika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa mmoja wa wananchi walioshuhudia Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika 1977, ninakumbuka kwa hamu na shauku juu ya sarafu moja, juu ya mawasiliano na uchukuzi, posta na simu, bandari, reli na kadhalika. Nakumbuka jinsi kituo cha reli cha mjini Itigi kilivyokuwa kinaongoza kwa ufanisi wa shughuli za reli siyo Tanzania tu bali Afrika Mashariki nzima.

Mheshimwa Spika, Wizara hii bado haijarejesha matumaini hayo kwa wananchi wa kawaida. Naiomba Serikali kupitia Wizara hii ionyeshe kwa wananchi wa kawaida ni nini hasa maana ya ushirikiano wa wananchi wa Afrika Mashariki, vinginevyo Wizara hii itabakia kuwa ni Wizara ya viongozi tu na masuala ya itifaki tu ya viongozi kukutana X kwa X na kunywa mvinyo na kahawa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi hizi tano za ushirikiano wa Afrika Mashariki, nchi zingine ukiacha Tanzania zinaituhumu Tanzania kwa kusuasua au kuweka ngumu katika kufikia malengo halisi ya mashirikiano kufikia *political federation,* sarafu moja na kadhalika. Napenda kujua kama tuhuma hizi ni za kweli na Serikali yetu inatoa majibu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi sijashawishika juu ya hoja ya nchi zingine kumezea mate ardhi yetu. Woga huu hauna msingi kama tutaepuka kuingia mikataba itakayouza nchi yetu

mfano hai ni pale tulipoweza kuendesha Jumuiya ya Afrika Mashariki tangia Mkoloni aondoke hadi 1977, Jumuiya ilipovunjwa na viongozi wachache wenye uchu. Naamini Jumuiya kama ile inawezekana kama Tanzania itakuwa tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa heshima ya Waziri na Naibu wake kwa nia na juhudi zao katika kutekeleza majukumu yao lakini *which is the way forward now?*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dunia nzima inashuhudia mikakati na michakato mbalimbali ya nchi na makundi kujiunga ili kupata nguvu kubwa. Tanzania nasi hatujabaki nyuma kwani tumejiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki, jambo kubwa na la msingi sana ni namna sisi kama nchi tunavyojiandaa kushirikiana na wenzetu katika hatua mbalimbali, bado Watanzania walio wengi wana uoga, kuingia katika shirikisho la Afrika Mashariki hasa hatua ya mwisho ya shirikisho la kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali ifanye mpango wa kufahamu sababu na maeneo husika inayowafanya Watanzania kuogopa shirikisho na kuzifanyia kazi, ni vyema pia Serikali ione haja ya kuweka utaratibu thabiti wa kuwaandaa wananchi wake kuingia katika shirikisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni suala nyeti sana katika maisha ya wananchi na nchi kwa ujumla, hata kama tunaingia katika shirikisho ni lazima suala la rasilimali libakie mikononi mwa nchi na mwananchi, itakuwa ni fedheha kubwa sana tukiruhusu ardhi yetu kuondoka mikononi mwetu. Wananchi wa Jimbo langu wamenituma niseme kuwa ardhi ni mali yao chini ya Serikali yao na si kwa ajili ya wageni kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya kina inapaswa kufanyika juu ya hatua zote zilizofikiwa mpaka sasa za Itifaki ili kuona sisi kama nchi tuone ni kiasi gani tumefaidika. Hii itatusaidia kufahamu faida za hatua nyingine zilizobaki, hatua hizo ni ushuru wa forodha, umoja wa sarafu na kadhalika. Tusipofanya hivi tutakuwa tunaingia "kichwa kichwa" mfano mdogo tu ni je tumefaidi nini katika hatua ya ushuru wa forodha? Hii ni muhimu sana na tusiruhusu hata kidogo kupoteza kama ilivyokuwa katika shirikisho la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyochangia mwaka jana ni muhimu sheria zinazoongoza taratibu mbalimbali mfano elimu, usalama wa raia, uhamiaji na mengine, si vizuri kuacha sheria hizi bila kubadilishwa. Hadi sasa bado masuala ya uhamiaji miongoni mwa nchi hizi hazijaeleweka sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito pia kwa Serikali ijitahidi kuwahamasisha wananchi wa Tanzania kujiandaa kisaikolojia na kimkakati kuingia katika shirikisho, kaa uhamasishaji unavyofanyika katika UKIMWI, Malaria (vyandarua) na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati mwingine uandaliwe kuwahamasisha watu wakiwemo wa Jimbo langu la Kibaha Vijijini, wakae tayari ili wasije wakashtukizwa au shirikisho hasa la kisiasa lisije likawa kama *surprise* bali iwe ni jambo linaloeleweka hatua kwa hatua.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa juhudi za dhati anazozionesha kwa kutetea maslahi ya Taifa ndani ya ushirikiano huu. Pia nampongeza Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi katika kuchangia hoja hii nitachangia kwa kuuliza maswali ambayo Waziri akiyajibu yatatoa elimu kuhusu juu ya ushirikiano huu wa nchi za Afrika Mashariki. Je, Serikali inasimamiaje maslahi ya Watanzania hasa katika suala la Ardhi, Maziwa, Bahari na Miradi mbalimbali inayoendeshwa kwa pamoja katika Jumuiya hii?

Mheshimiwa Spika, hadi sasa ni juhudi zipi za makusudi zilizochukuliwa na Serikali ya Tanzania kupitia Wizara hii kuuelimisha umma wa Watanzania juu ya ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki? Je, unafikiri Watanzania wana uelewa juu ya ushirikiano huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirikisho la Nchi za Afrika Mashariki litaundwa lini? Tanzania inatoa msimamo gani wa dhati kuhusu uundwaji wa shirikisho la kisiasa la Afrika ya Mashariki?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Utalii ni nyeti sana katika nchi za Afrika ya Mashariki, je, ni kwa vipi nchi ya Tanzania kupitia Wizara hii inarahisisha kuwa watalii wengi wanaingia Tanzania na wala si Kenya?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la lugha ni kikwazo kikubwa cha ajira kwa Watanzania walio wengi, kwa nini lugha rasmi ya mawasiliano isiwe Kiswahili. Ni juhudi zipi za dhati zimechukuliwa za makusudi kukiendeleza Kiswahili? Kwa nini Taasisi ya Uchunguzi ya Kiswahili ya Afrika Mashariki isianzishwe haraka iwezekanavyo? Ni ipi lugha rasmi ya nchi za Afrika Mashariki? kwa nini? Je! ipi itakuwa ni Lugha ya Shirikisho? Kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kuna kitengo chochote cha tafiti ambacho kimeanzishwa ili kuishauri Serikali ya Tanzania juu ya Lugha ya Kiswahili, Ardhi, Rasilimali za Taifa, Biashara, Masoko ya Kijiografia ya Tanzania katika Jumuiya hii na Viwanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imejiandaa vipi kubadili mitaala ya elimu kuanzia ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na hata vyuo vikuu ili kuweza kuleta ushindani kwa nchi nyingine kama vile Kenya na Uganda?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa vipi Wizara imejiandaa kwa mkakati wa uwepo wa sarafu moja katika nchi za Afrika ya Mashariki? Je, Serikali kupitia Wizara hii imefanya juhudi gani za makusudi ili kuwalipa

haki zao wazee waliokuwa watumishi katika Taasisi na Idara mbalimbali za Jumuiya ya iliyovunjika mwaka 1977? Je! utaratibu wa sasa wa kuwapatia Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unafaa? Kwa nini? Je, hakuna njia mbadala ya kuwapata Wabunge hao badala ya utaratibu wa sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gani wa kuboresha masoko ya mipakani kama vile Sirari, Wilayani Tarime? Ni kipi cha kujivunia toka Tanzania kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Spika, kwa nini suala la *passport* lisiondolewe kabisa kwa wananchi wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mshariki?

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri kwa Waziri kwa mara nyingine namwalika Waziri afike Wilayani Tarime ili aangalie fursa zilizopo kwani Tarime ilifanywa ukanda wa Viwanda yaani Sirari-Tarime *Trade Zone* tunaweza kuliteka soko la Afrika ya Mashariki, kwa nini hataki kuja Tarime? Mara ngapi nimemwalika hataki kuja?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na wataalam wa Wizara kwa hotuba yao iliyowasilishwa vizuri na kwa kujitahidi kukabiliana na changamoto za Wizara hii ambazo si haba. Naipongeza pia Kamati na Kambi Rasmi ya Upinzani kwa maoni yao ambayo inafaa yazingatiwe na Wizara

katika majumuisho na pia kuyachukua na kuyafanyia kazi katika mipango yao. Nakubaliana na maoni yao wengi na nitachangia katika maeneo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza kwanza kwenye uhusiano usioridhisha baina ya Tanzania na Kenya, kati ya nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania ina mahusiano mazuri na Burundi, Rwanda na Uganda, ni uhusiano na Kenya tu ndio unaoonekana si mzuri. Kwa habari tulizonazo, Kenya ni mwekezaji namba mbili hapa nchini na katika hali ya kawaida tungetarajia kuwa ingetoa fursa sawa kwa Tanzania, lakini hali si hivyo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa za wafanyabiashara wa Tanzania wanaosumbuliwa huko Kenya wakati Wakenya wanaendesha biashara zao hapa Tanzania bila matatizo zaidi, kuna dalili za wazi kuwa Kenya inaendesha mkakati mkali wa ushindani kwa kuipiga vita Tanzania hasa kuhusiana na utalii wa mlima Kilimanjaro. Hivi sasa Kenya inajenga uwanja wa ndege wa Kimataifa Taveta mji ulio mpakani na karibu na mlima wa Kilimanjaro ingawa kuna historia ndefu ya Kenya kunyemelea biashara ya utalii unaotokana na mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hatua ya kujenga uwanja wa ndege Taveta wakati kama huu si ya kirafiki hasa bila kuwasiliana na Tanzania. Swali, je, Serikali imejipangaje kukabiliana na tatizo la uhusiano usioridhisha baina ya Tanzania na Kenya, uhusiano unaonekana kuinufaisha zaidi Kenya?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nitakalozungumzia ni elimu. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti uliofanywa na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya uwezo iliyolinganisha uwezo wa wanafunzi wa shule za msingi Uganda, Kenya na Tanzania. Tanzania ilikuwa ya mwisho katika hisabati na lugha (Kiswahili na Kiingereza). Swali la kujiuliza ni hili, je, matokeo hayo yalitokana na tofauti za mitaala, ufundishaji mbovu au sababu nyinginezo? Mitaala ya shule za msingi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ina uwiano wowote? Serikali ya Tanzania lazima iwe makini hasa kuhusiana na elimu ya msingi kwa sababu wanafunzi wasiopata msingi mzuri hata katika hatua nyingine za elimu wataendelea kupata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nitakalochangia ni kuhusu kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ambayo Makao Makuu yake yatakuwa Zanzibar. Ningependa kushauri kuwa kamisheni hii iandae bila kuchelewa (kama haijaandaa) mwongozo wa namna ya kutekeleza majukumu yake. Wananchi wa Afrika Mashariki wanatarajia kuwa Kamisheni hii itakuwa makini katika kueneza na kuimarisha utumizi wa Kiswahili Afrika Mashariki, Afrika na katika nchi nyingine hasa katika zama hizi za utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamisheni iandae mpango mkakati ambao ukishatekelezwa, Kiswahili kitaweza kuwa lugha ya Bunge la Afrika Mashariki na pia itumike katika mikutano ya Umoja wa Afrika. Kwa hiyo, lazima kuwe na umakini katika uteuzi wa

watumishi wa kamisheni ambao watatusaidia kutimiza ndoto ya waandishi mashuhuri wa Afrika Shaban Robert na Wole Sayink kuwa Kiswahili kitaenea hadi kiwe lugha ya Afrika Mashariki na Afrika nzima.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa mashirikiano yao na kuliendesha hili gurudumu vizuri. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ifungue ofisi ndogo kule Zanzibar yenye wafanyakazi pamoja na vitendea kazi ili watendaji watakapokuja Zanzibar wasihangaike kutafuta ofisi za kuazimwa na kufanya kazi zao. Hii italeta sana urahisi wa kuweza kujua ofisi ya uhakika iko wapi na kuweza kumaliza shida za wananchi kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itumie juhudu kadiri itakavyowezekana Balozi zetu na *(TAESA)* Tanzania *Employment Service Agency.* Ili kuongeza udalali wa wafanyakazi na pia Balozi zikubali kuwa madalali kwa kutangaza nafasi za kazi katika kila Balozi za *E.A* ili kuwasaidia sana wanaotafuta kazi kupata urahisi na kuweza kupata taarifa za uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia Wizara ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itoe elimu ya kutosha kwa Watanzania ili waielewe vema Jumuiya hii inavyofanya kazi yake na wataitumiaje katika Mashirikiano mbalimbali hasa ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara hii isaidie Tanzania kutangaza vivutio vyake kwa sababu tumekuwa tukisikia wanajumuiya wenzetu (Kenya) wakitangaza kuwa Mlima Kilimanjaro upo kwao na huku wakijua ukweli mlima upo Tanzania. Serikali ijaribu kuongea na majirani zetu ili wawe wakweli kuwa mlima upo Tanzania.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu kuhusu ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa elimu, inatakiwa itolewe hasa kwa upande wa Zanzibar kumekuwa na upotoshaji mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar kuhusu ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili ni kuiomba Serikali ya Tanzania kujenga ofisi ndogo ya Afrika Mashariki huko Zanzibar.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niruhusu nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta hotuba ya bajeti nzuri sana. Pia wawapongeze kwa kazi nzuri wanazozifanya, pamoja na hayo ninayo machache ya kuboresha hotuba ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ya Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki The *East Africa Treaty* inaeleza wazi kuwa ardhi ya nchi wanachama haipo katika mambo ya jumuiya. Hivyo, ardhi inabaki kuwa ni mali ya nchi husika. Hili ni jambo zuri lakini nina angalizo moja. Ardhi yoyote kama haijaendelezwa haina maana yoyote. Tanzania inayo ardhi ya kutosha na kwa ukubwa Tanzania ni kubwa kuliko nchi zote za Afrika Mashariki yaani ukiunganisha Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi bado Tanzania ni kubwa, lakini ukilinganisha matumizi ya ardhi, Tanzania tuko nyuma sana kwani kuanzia Ruvu, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Kagera hadi Mpakani mwa Tanzania na Uganda (Mutukula) ardhi yetu iko *idle* haina matumizi ya msingi mfano, mashamba makubwa, mashamba ya mifugo na kadhalika, kama ilivyo kwa nchi za Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipita mpaka wa Tanzania na Uganda Kikagati (Murongo), Kagera utaona ardhi yote ya Uganda imetumika vizuri kwa kugawa *blocks* za mashamba ya mifugo na kilimo mfano halisi ni mashamba ya mifugo ya Mbarara na Masaka, ni kwa nini ardhi yetu tuliyonayo ikagawiwa kwa wananchi kwa ajili ya kilimo na mifugo. Kama hatutofanya hivyo basi ni bora ardhi yetu ikawa *Commercialized* ili kuruhusu wenzetu wa Uganda, Rwanda, Kenya na Burundi waje wawekeze katika nchi yetu lakini kwa utaratibu mzuri wa kulinufaisha Taifa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki bado kabisa haujafahamika kwa Watanzania walio wengi wakiwemo hata wananchi wa mipakani mfano, ni wananchi wa Jimbo la Karagwe, Kagera, hata Ngara, Kigoma, Misenyi na Muleba na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishashauri kuwa Wizara ipeleke maofisa wa Wizara yake kwenye Halmashauri zetu, Kata zetu na hata Vijiji ili wananchi wetu waweze kushauriwa vizuri jinsi ya kutumia fursa hii ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vile vile, Serikali itangaze kwenye vyombo vya habari kama magazeti, redio*, television*, vipeperushi, mabango na kadhalika kuanzia ngazi ya Vijiji, Makanisani, Misikitini, minadani, mikutano ya hadhara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, Wabunge wote wa Bunge la Afrika Mashariki uchaguliwe na Wabunge na Nchi Wanachama na hivyo Bunge ni Jimbo lao. Mara nyingi tumeshauri Wabunge wetu hawa wapate nafasi ya kuja na kulieleza Bunge mambo yanayoendelea katika Bunge la Afrika Mashariki. Pia Wabunge wetu watupe nafasi ya kuchangia na kutoa maoni juu ya sheria, mikataba na mambo mengine muhimu yanayohusu Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki umekuwa ukilalamikiwa na wananchi wa Tanzania kuwa Watanzania hawapati nafasi za kutosha kama ilivyo kwa nchi nyingine kama Kenya na Uganda. Malalamiko haya hayana budi

kufanyiwa utafiti ili Watanzania wajue ukweli kuhusu ajira za Afrika Mashariki kwa watumishi wa kada zote kuanzia wahudumu hadi Kiongozi Mkuu. Hivyo basi, katika majumuisho Waziri atuletee takwimu sahihi za ajira kwa sasa hivi yaani (*current position).*

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara Wizara na Serikali imekuwa ikitueleza kuwa mapato ya biashara kati ya Tanzania na nchi wanachama zimekuwa sana na zinaingiza pato kwa nchi yetu. Taarifa hizi ni za kijumla mno hazijawa *supported* na takwimu sahihi. Tunaitaka Serikali ituletee takwimu hizi za nchi zote za Afrika Mashariki ili tuone kama kweli Tanzania tunafaidika au la. Kwa haraka haraka ni rahisi kusema kuwa kampuni ya AZAM ndiyo inayoongoza kupeleka bidhaa katika Soko la Afrika Mashariki lakini Kenya ina Kampuni nyingi zinazoleta bidhaa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayofanya katika kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maoni yangu katika maeneo yafuatayo:-

Kuongeza wigo wa utoaji wa elimu kwa Watanzania ili waweze kuwa na ufahamu wa kutosha na hivyo kuweza kutumia fursa zilizopo. Naiomba Serikali katika mtaala wa elimu iweke kipaumbele kuhusiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wa Kitanzania wamekuwa wakilalamika kukosa fursa za ajira katika Nchi Wanachama, lakini nchi zingine hasa Kenya na Uganda, wamekuwa wakiajiriwa sana hapa nchini kuliko vijana wetu wanavyoajiriwa katika nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha vijana wengi wa Kitanzania wanapata fursa hiyo kama ambavyo vijana wa nchi zingine wanavyopata hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na hofu kubwa kwa Watanzania juu ya Jumuiya hiyo hasa katika suala zima la wananchi wa nchi wanachama juu ya kupewa haki ya kumiliki ardhi na kuna tetesi kuwa nchi wanachama wamekuwa na uchu sana na ardhi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia vijana wengi wa Tanzania tumaini lao kubwa ni ardhi ili kujikomboa na tatizo la ajira, je, Wizara inawaambia nini Watanzania juu ya usalama wa ardhi yao kupokonywa na wageni kwa kisingizio cha Jumuiya ya Afrika Mashariki, nini usalama wa ardhi ya Watanzania?

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi, nampongeza Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa bajeti nzuri na utendaji kazi mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu, nashauri wananchi waendelee kuelimishwa juu ya maendeleo ya mchakato wa masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yaliyopo tayari, wananchi waelimishwe juu ya makubaliano yaliyo tayari kutumika, kwa mfano, masuala ya ushuru ili wananchi wasiendelee kusumbuliwa juu ya masuala ambayo tayari tumeshakubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee kama tunavyokwenda, kusonga mbele kwa makini katika kila suala lakini hasa ardhi. Msimamo wetu tuusimamie, *monetary union,* tumeona matatizo makubwa ya *eurozone,* katika ya matatizo ya *Eurozone*, Uingereza wanachekelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja naunga mkono.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii ya Afrika Mashariki katika eneo la kuhakikisha tunatumia *boarder* zetu ili kuweza kunufaika na Jumuiya hii. Nchi yetu ya Tanzania imejaliwa kuwa kati na hizo na hivyo kujikuta tumezungukwa na hizo nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio yangu kuwa tungetumia fursa hii kujiimarisha zaidi kwa kujenga *boarder* zetu kama ile ya Sirari, Namanga, Mtimwabu-Tarime, Shirati, kule Kigoma, Kagera, Tunduru na kwingineko. Cha kushangaza utakuta upande wa pili wa mpaka kwa maana nchi nyingine mfano, Kenya kwenye *boarder* ya (Sirari upande wa Tanzania

hakujaendelea na wala hamna uwekezaji wowote ule. Hii ni fedheha, mfano, utakuta bidhaa nyingi zinatoka Kenya kuja kulisha watu wa Mkoa wa Mara na Mwanza. Hii inachangia uchumi wa Kenya na kudidimiza uchumi wa Tanzania. Ni dhahiri kabisa sasa ni wakati muafaka kwa Wizara yako kuishauri Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha uwekezaji kwenye viwanda katika Mikoa ambayo ipo kandokando na nchi hizi wanachama. Hii itapunguza Tanzania kutegemea kuingiza bidhaa toka nchi jirani na badala yake kutumia bidhaa za ndani na kuwauzia hawa nchi wanachama, hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu, kuliko sasa hivi tunavyosafirisha *raw material* kwenda nchi wanachama *then* wao wana-*process* na kurudisha bidhaa kamili, hii ni hatari sana. Hivyo, naomba ujenzi wa *boarder* hizi pamoja na uwekezaji katika maeneo hayo ni muhimu sana kwani pia utatoa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa kifupi nizungumzie kuhusu wimbi kubwa na wananchi wa nchi wanachama kuingia katika nchi yetu pasipo kufuata sheria na kuingia na kuchukua ardhi ya Watanzania mfano, Wakenya waliovamia maeneo mbalimbali kule Tarime na Rorya na inaelekea wanapewa haki kuliko Watanzania, sasa sijui ni kwa sababu ya hongo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata ufafanuzi juu ya uhalali na kutokana na uhalali kuingia nchini, je, wanaruhusiwa kuingia na kufanya kazi au kuishi bila vibali?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo ni hayo tu, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu siku ya leo kwa kuniwezesha kuamka nikiwa na afya tele na kuweza kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka uliopita wakati nikitoa mchango wangu wa maandishi kwenye Wizara hii nilisema, wananchi wa Wilaya ya Micheweni au kwa ujumla wake kule Pemba Kaskazini, lakini hasa Jimbo langu la Micheweni, nilisema ni wasafiri wakubwa wanaotumia bandari ya Shimoni, Kenya na nilisema wananchi hawa wamekuwa wakipata shida sana na maofisa wa Uhamiaji katika bandari hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo pia, namwomba Waziri wa Afrika Mashariki iwapo atakuwa tayari kufuatana na mimi ili kulifuatilia tatizo hili lakini pamoja na kulimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri alinijibu atakuwa tayari kufuatana na mimi na kweli alifanya hivyo ingawaje alinipatia taarifa ya kwenda Shimoni, Kenya zilikuwa za kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo naomba nimshukuru na nimpongeze Naibu Waziri wa Afrika Mashariki kwa kulifuatilia hili na kulipatia ufumbuzi ingawaje bado yako matatizo madogo madogo yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumpongeza Naibu Waziri wa Afrika Mashariki nashauri awe na utaratibu wa kutembelea kwenye Bandari hiyo ili matatizo hayo yasiwe na nafasi ya kujirudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi nitakuwa mwizi wa fadhili iwapo sitampongeza Balozi wetu aliyeko Mombasa Kenya kwa juhudi anazozifanya kufuatilia matatizo ya wananchi wetu akishirikiana na Naibu Waziri wa Afrika Mashariki wakati alipofanya ziara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda nimpongeze tena Balozi wetu aliyeko Mombasa, Kenya hasa pale wananchi wetu wapatao- waliposhikwa kule Malindi- Kenya, kwa kufuatilia na mwisho wake wakaweza kuwa huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine wananchi wetu inawezekana wanapata shida wanapoingia kwenye bandari hii ya Shimoni, Kenya kutokana na kukosa taaluma ya kuingia katika mipaka ya nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa tatizo hili kwa wananchi wetu katika mipaka ya nchi nyingine ni wakati muafaka sasa kule Kaskazini Pemba, Wizara hii ya Afrika Mashariki kupeleka elimu kwa wananchi kama vile inavyofanya katika mipaka mingine ya nchi hii ili waweze kujua haki zao za msingi wanapoingia nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wakati wa kufanya majumuisho, nitamtaka aniambie kwa dhati ya moyo wake ni lini atafanya ziara ya kuwapatia taaluma wananchi wa Kaskazini Pemba, lakini hasa Jimboni kwangu Micheweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kazi njema.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusizishauri nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki? Nchi hizi kijiografia zimekaa vizuri, kuwa wadau muhimu kwenye Jumuiya hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kusema kuwa Tanzania bila ushirikiano wa Afrika Mashariki hatuwezi kusonga mbele kwenye masuala ya kuimarisha usafiri wa reli, barabara, anga na usafiri wa majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Watanzania tukazingatia umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii badala ya kulalamikia ushindani katika soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano wetu na Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda unatoa fursa kwa Watanzania kujiendeleza kielimu, kimaadili na kiuchumi ili kuweza kustamili ushindani uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tumekuwa na tatizo la uvivu, uvivu huzaa umaskini na umaskini huzaa wivu na wivu huzaa chuki, badala ya kuweka chuki kwa watu wenye uwezo ni vema tukajiandaa kielimu na kimaadili ili na sisi Watanzania tuweze kuuzika kwenye soko la ajira la Afrika Mashariki hata lile la Kimataifa. Vile vile ni lazima tujiamini na tujitambue. Huwezi kuelimika, kama unachukia wasomi, huwezi kutajirika kama unachukia matajiri, huwezi ukawa Taifa la Kimataifa kama unachukia raia wa nchi za nje yaani wageni. Pia huwezi kuendeleza utalii kama unachukia watalii. Vile vile huwezi kuwa na wawekezaji na kuendeleza uwekezaji kama unachukia wawekezaji. Wito wangu kwa Watanzania ni kwamba, Watanzania tuanze ushindani wenye tija badala ya kuendelea kulalamika bila suluhu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Hoja iliyopo mbele yetu ni hoja mahususi ingawa kuna uhaba wa fedha katika bajeti husika, naomba Serikali ifikirie kuiongezea fedha Wizara hii ili iweze kutimiza wajibu wake katika kutetea maslahi ya Taifa katika Jumuiya yetu ya kikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa Mjumbe wa Kamati nimehusika katika hatua zote za awali za maandalizi na matayarisho ya bajeti ya Wizara ya Afrika Mashariki, kilichotukwamisha kwanza ni ufinyu wa bajeti na kuiomba Serikali ifikie suluhu ya kuisaidia

Wizara hii kwa kulipa fedha za michango kupitia Hazina moja kwa moja ili kusaidia Wizara isipungukiwe na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigumu sana kushindana kwa haki katika medani za Kimataifa bila kuwepo wataalam na rasilimali fedha zilizotengwa maalum kwa kazi ya uendelezaji tafiti mbalimbali. Katika mazingira haya naiomba Serikali ifikie maamuzi magumu ya kutenga fedha kwa ajili hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa mtangamano wa Afrika Mashariki ni jambo la kipaumbele. Hata hivyo, upo upungufu mwingi unaowakabili wananchi walio wengi nchini Tanzania. Hivyo basi, ili tuweze kwenda na wakati na kulifanya suala la utangamano wa Afrika Mashariki, ni wajibu wa Serikali kuweka fungu maalum kwa ajili ya elimu kwa umma kuhusu utangamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni elimu pekee ndiyo itakayotoa hofu kwa Watanzania juu ya ushirikiano wa Afrika Mashariki. Wananchi wapewe elimu ya kutosha juu ya faida za ushirikiano huu wa Kikanda. Changamoto zilizopo katika ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni pamoja na uhaba wa ardhi katika maadili ya Nchi Wanachama na ndiyo maana kuna wakati yanatolewa maoni na wanachama hao wenye uhaba wa ardhi kuharakisha shirikisho la kisasa, jambo hili limekuwa likipingwa na Watanzania walio wengi kutaka shirikisho la kisiasa lisiharakishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti za viwango vya elimu katika Nchi Wanachama ni changamoto nyingine inayowakumba hasa Watanzania kuhoji kwamba itakuwaje katika soko la ajira kwani upo uwezekano wa Watanzania wengi kukosa ajira iwapo kutakuwepo uhuru wa soko la ajira miongoni mwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iipatie kipaumbele Wizara hii ili kuwezesha Wizara kuzifanya kazi zake kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono bajeti ya Wizara hii.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na afya nzuri anayonijalia kila iitwapo leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru na wewe kwa uongozi bora unaotutumikia hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii bila kuwasahau Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii kwa utendaji bora wa kazi zao, lakini kwa hotuba nzuri iliyo na mwelekeo na matumaini makubwa kwa Watanzania hasa walio Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi mojawapo kati ya nchi za Afrika Mashariki, kwa hiyo ushirikiano katika nchi hizi (*State Partiners*), ni lazima

uzingatiwe kwa kiwango cha juu katika nyanja zote za afya, elimu, biashara, *custom* na matumizi ya mipaka. Nikisema hivyo ni kwamba, huduma za afya, elimu ziwe za kiwango kinachofanana na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya ardhi yasiingiliane kabisa na sheria ya kulinda ardhi ya Tanzania itiliwe mkazo, ardhi ya Tanzania ibaki ni ya Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ingeongezwa bajeti ili kutekeleza mipango yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii iwajibike kuangalia zaidi namna nchi yetu itafaidika na ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kuwa uchumi wa nchi yetu upo nyuma ukilinganisha na nchi zingine za umoja huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuna changamoto kadhaa za ajira, Watanzania wengi hatuwezi kushindana na nchi zingine kwa kuwa nchi yetu mfumo wa elimu na lugha inayotumika haiwezi kushindana na nchi zingine. Ni vema Wizara ijipange katika hili ili kutoa ushindani ulingane na nchi zingine, au kwa kutilia mkazo lugha ya Kiingereza na au kukubaliana kwa nchi zote kuwa na lugha ya Kiswahili ili iwe lugha kuu ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine inayoweza kuwa na athari kubwa ambayo inaweza

kupelekea machafuko ni suala la ardhi ambayo ni vema Watanzania wabaki na umiliki wao na umiliki usifanywe kwa wananchi wengine wa jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa tumejifunza na kuona matatizo ya ardhi yanavyogharimu maisha ni vema yawekwe wazi na kukubaliwa kwa pamoja na wanachama wote wa Jumuiya.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Nchi za Burundi na DRC bado ziko katika vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa miongo kadhaa sasa. Kwa kutumia utaratibu wa namba kubwa (*The Law of Large Numbers*) je, DRC inaweza kuwa na amani ya kudumu na endelevu kama itajiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ilivyo Rwanda sasa? Iweje Burundi bado haijatulia na bado vikundi vinapigana na Serikali (majeshi) na kusababisha mauaji ya wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya minofu ya samaki bado inafaidisha nchi za Kenya na Uganda zaidi kuliko Tanzania ili hali Ziwa Victoria sehemu kubwa iko Tanzania (takribani 60%). Viwanda vya usindikaji vya Kenya vinatumia Sangara wanaovuliwa upande wa Tanzania. Ni muhimu tuhuishe (*harmonise*) ushuru na kodi zetu *(Tax Regime)*. Hata viwanda vyenye msamaha wa kodi, bado kodi inayolipwa Tanzania ni zaidi ya 17%, wakati Kenya kuna *Export incentives* na *bonus bila stamp duty* na ushuru mbalimbali Mialoni, Ukerewe na Mwanza pamoja na kodi ya kusafirisha nje na asilimia mbili za kodi ya maliasili, Uganda wanatoza pungufu karibu sawa na Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake wavuvi wa Tanzania wanauza samaki Kenya na Uganda, hivyo, ajira na pato kubwa kwenda Kenya na Uganda. Naomba hili lichunguzwe ili pato kubwa na ajira zibakie Tanzania. Matokeo yake viwanda vya Tanzania vingi vinashindwa kutoa ajira za kudumu kwa wafanyakazi tofauti na wafanyakazi wa Kenya wanapata mikataba ya kazi ya kudumu.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafutayo:-

Sarafu ya pamoja, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinapojiandaa kusaini makubaliano ya kuwa na sarafu moja ni muhimu kwa nchi yetu kuangalia faidi na hasara yake. Ni lazima kutambua kwamba, huwezi kuwa na safaru moja kama uchumi wako hauko *stable.* Nchi zote za Jumuiya hii ni lazima ziwe na uchumi ulio imara, usiotegemezi kwa wenzako au nchi nyingine. Je, shilingi yetu ya Tanzania iko imara (*stable*) kiasi gani? Bajeti yetu iko *stable* kiasi gani? Miradi yetu ya maendeleo inatumia fedha za ndani au za wafadhili? Jibu ni kwamba miradi mingi inategemea wafadhili. Je, ni kwa namna gani tunaweza kuwa na sarafu moja? Ni muhimu kutafakari kwa kina, tukumbuke mfano mzuri wa Norway ambayo kwa kuwa na uchumi imara sana inakataa kuwa kwenye sarafu moja ya *Euro* kwa kuogopa kushuka kwa thamani ya fedha yake na kutegemewa na nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ardhi kuingizwa kwenye shirikisho. Ardhi ni mali na Tanzania imebarikiwa kwa ardhi kubwa yenye rutuba kulinganisha na nchi zote zilizopo kwenye shirikisho. Kenya na Uganda wanashinikiza kwa bidii zote kwamba ardhi iwe ni mali ya Jumuiya kwa kuwa wao wana *land crisis,* kamwe Tanzania hili tusikubali kama ambavyo tumeanza kulikataa tangu mwanzo, ardhi ni mali ya Watanzania wa sasa pamoja na vizazi vijavyo. Tusikubali ghiliba za majirani zetu kwa *interest* zao binafsi na wala si kwa fedha ya nchi washirika. Hivyo, ni vema sisi Tanzania kama nchi tukailinda ardhi yetu tuliyojaliwa na Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu soko la pamoja, tumesaini makubalinao ya kuwa na soko la pamoja, lakini angalia wenzetu wa Kenya walivyo kuliko sisi, wao kwa kuwa na viwanda kutuzidi, sisi tumekuwa tukiwauzia malighafi wao wanatuuzia *finished goods* yaani sisi Watanzania tunazalisha tusichokitumia na tunatumia tusichokizalisha. Mfano, sisi tunauza ng'ombe Kenya, wenzetu wanasindika nyama wanatuletea huku kwa bei kubwa. Vile vile kahawa ghafla wao wanakwenda kuipakia na kuiongezea thamani wana-*blend* na kuandika *made in* Kenya, *Africafe* tunanunua kwa bei kubwa sana wakati kahawa tunalima wenyewe. Hii sasa maana yake nini? Sisi tumeuza viwanda vyote vya nguo, sasa tunauza pamba yetu Kenya kwa kunatengeneza vitenge au khanga wanatuuzia bei kubwa. Tanzania tuko *very lose* katika suala la biashara na masoko hasa kwa kutokuwa na viwanda vyetu wenyewe. Tunatakiwa tuwe makini sasa katika eneo hili la soko la pamoja isije

ikawa sisi ni wanunuzi tu wa bidhaa za wenzetu na hakuna tunachouza chenye thamani kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Soko la Pamoja la ajira, kama kuna kitu ambacho Tanzania bado hatujajiandaa vya kutosha ni kuingia kwenye soko la ajira kwa vijana wetu. Kama nchi ni lazima ijipange kutengeneza ajira kwa watu wake. Maandalizi ya kushindana kwenye soko la ajira yanaanzia kwenye upatikanaji wa elimu bora. Tujiulize, ni kwa namna gani watoto na vijana wetu wanaandaliwa kupata elimu bora? Shule nyingi za Serikali zina matatizo huku walimu hawatoshi, wanafunzi hawafundishwi kivitendo kwa kukosa maabara, mazingira ya kujifunzia na kufundishia ni duni sana. Je, kwa namna hii tutegemee nini kwa watoto wetu ambao ndio tunawategemea washindane na wenzao kwenye soko la ajira? Kama mpaka leo hii bado kuna wanafunzi wanaomaliza shule hawajui kusoma na kuandika, hawa watafanya nini kama si kuwa wafagizi kwenye ofisi za wenzao wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la ubaguzi katika kutoa mikopo ya elimu ya juu, sera ya mikopo iliyopo sasa ni kwamba, mwanafunzi atapata mkopo endapo atafanya masomo ya sayansi, ualimu wa masomo ya sayansi na jamii zake. Hebu tuwe wa kweli, hivi ni lini Tanzania tumekuwa na wahasibu, wanasheria, watawala, wanauchumi, wasanii wenye ujuzi na kadhalika wa kutosha kama tunawalazimisha wanafunzi kuchagua kusomea kozi wasizozipenda ili wapate mkopo? Tunategemea nini hapo baadaye katika ufanisi na utendaji kazi wao kwenye Jumuiya

wakishindanishwa na wenzao? Je, fani hizi ambazo hazipewi kipaumbele na Bodi ya Mikopo hazishindanishwi kwenye soko la pamoja la ajira? Tuache utani kama tunataka vijana wetu wapate ajira, ni vema sasa tuache siasa kwenye elimu na tuhakikishe kuwa kila mwenye kiu ya kuipata elimu ya juu anapata katika fani yoyote anayoitaka kwa kupewa mkopo na tuache ubaguzi wa kuwaweka wanafunzi katika makundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchukuzi ni vema Tanzania ikatilia mkazo kwenye njia za uchukuzi kama reli, bandari na barabara ili kuunganisha nchi na nchi nyingine wanachama kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa bidhaa zake, mfano, reli toka Dar es Salaam mpaka Mombasa, Dodoma – Burundi na Rwanda na kadhalika. Pia tumevusha Bandari zetu zote kwa sababu Rwanda na Burundi ni *land locked countries,* hivyo zitategemea sana Bandari zetu kusafirishia mizigo yeo na hivyo reli ni muafaka sana kwa hili suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika bajeti ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, alama muhimu za Jumuiya ya Afrika Mashariki; pamoja na bendera na wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, nataka tufahamishwe kama kuna alama nyingine za Jumuiya hiyo. Pili, kwa alama zilizopo, je, ni jitihada gani zinafanyika katika kuzitambulisha alama hizi kwa Watanzania?

Mheshimiwa Spika, elimu kuhusu Jumuiya kwa wananchi; ni ukweli usiopingika kwamba wananchi wengi zaidi ya asilimia 80 hawajui chochote kuhusu Jumuiya hii pamoja na mipango yote ambayo Wizara inayo, lakini bado mipango hiyo haitaleta tija sana. Nataka kujua ni zipi hasa jitihada za kutosha katika kutoa elimu kuhusu uwepo wa Jumuiya hii, pamoja na faida zake. Mbali ya uelewa mdogo wa Jumuiya kwa Watanzania waliowengi, lakini pia kuna uelewa mdogo kwa wanafunzi wetu hasa katika shule za msingi na sekondari. Hivyo, naiomba Wizara hii mshirikiane kwa karibu zaidi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kuhakikisha kuwa kuna mpango madhubuti kuhakikisha kwamba vijana wetu katika shule za msingi na sekondari wanafundishwa kwa kiwango kikubwa sana kuhusu Jumuiya hii, uwepo wake na faida zake. Tunaweza kuwa na mipango mizuri, lakini utekelezaji hafifu *then we are bound to fail* na wakati wote Kenya itabaki kuwa mnufaikaji mkubwa wa Jumuiya, *it is time to wake up and start working, night is over.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ndogo ya Wizara, hii ni changamoto kubwa si tu kwa Wizara hii, lakini pia kwa nchi yetu, bajeti ndogo itaifanya Wizara ishindwe kutimiza majukumu yake sawasawa. Unapokuwa kwenye Jumuiya, ni lazima kutumia fursa hasa za kiuchumi vizuri, lazima wananchi hasa wafanyabiashara wawe na elimu ya kutosha kuhusu Jumuiya na hasa soko. Hivyo, Wizara ikiwa na bajeti ndogo kama ilivyo kwa mwaka huu ambapo jumla ya bajeti ya Wizara hii ni shilingi za Kitanzania bilioni 16.6 tu, kwa vyovyote haitaweza kukabiliana na changamoto

zilizopo. Ni juu ya Wizara hii kuendelea kuomba fedha zaidi vinginevyo iwe tayari kushindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirikisho la kisiasa, hatua hii siyo ya kuikimbilia, nchi nyingi duniani ambazo zimejaribu kuingia katika ushirikiano wa namna hii zilishindwa mfano, Senegal na Gambia zilijaribu zikashindwa, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pamoja kwamba upo, lakini malalamiko ni mengi sana, wapo baadhi ya Watanzania hawaridhiki na hivi ulivyo. Jumuiya ya Afrika Magharibi *ECOWAS,* imebaki ni ya kiuchumi zaidi kuliko ya kisiasa na Jumuiya ya Ulaya *EU,* imebaki ya kiuchumi zaidi kuliko siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sana iweke nguvu zaidi kwenye ushirikiano wa kiuchumi zaidi kuliko mtangamano wa shirikisho la kisiasa. Wananchi wetu watafaidika zaidi na ushirikiano wa kiuchumi kuliko wa kisiasa, inawezekana wapo viongozi wa nchi hizi zinazounda Jumuiya ambao wana ndoto ya kuwa viongozi wa kwanza wa Jumuiya, nashauri mawazo haya kwa sasa yapuuzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii kwa majukumu yao mazito ya utumishi kwa Taifa letu na Kanda yetu ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *Treaty for the Establishment of the East African Community Article* (5), ihaririwe upya, kwani inazungumzia malengo ya Jumuiya na kuorodhesha vipengele vitatu. Lakini kihalisia kuna lengo moja tu, pia maana ya maendeleo endelevu hayajatafsiriwa vizuri kwa kiwango cha kitaaluma "*Bad drafting.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, uwiano wa wafanyakazi katika Ofisi ya Jumuiya kwa upande wa Watanzania ni mdogo. Nashauri utaratibu wa kupata wafanyakazi na Watendaji uzingatie uwiano wa nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ratiba ya Mikutano ya Wabunge wa Afrika Mashariki izingatie mzunguko wa kila nchi mwanachama kwa usawa. Arusha ni Makao Makuu ya Jumuiya na siyo Makao Makuu ya nchi yetu. Dodoma ndiyo Makao Makuu ya Tanzania na ndipo Bunge letu la Tanzania lilipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya kutangaza mali zao pia itumike kwa Viongozi wetu katika Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la saba la milenia ni uhifadhi wa mazingira endelevu. Nashauri kwamba kwa kuwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Afrika Tanzania tuna rasilimali nyingi asilia kama vile ardhi, maji, gesi, madini na kadhalika, ni vyema tukaanza kuandaa mpango mkakati endelevu wa kuuza gesi katika nchi wanachama, licha ya kukuza uchumi wetu, tutasaidia kuhifadhi mazingira. Aidha,

mpango wa Kilimo Kwanza uhamasishwe ndani ya Jumuiya, kwani ardhi tunayo, tunaweza kufanya kilimo cha pamoja kwa utaratibu tutakaokubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali kubwa na ya kuaminika duniani ni rasilimali watu. Nashauri ili kuweza kuwa na fikra zenye mitazamo inayoshabihiana, inabidi tutazame mifumo yetu ya elimu yenye kuzingatia utu wa mwanadamu ndani ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna au ni Mataifa machache sana duniani yanaweza kujikomboa kiuchumi kwa kutumia lugha za kigeni. Nashauri kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Mikutano, Makongamano, Semina, Bunge la Afrika Mashariki na kadhalika. Pia itasaidia kuimarisha umoja ndani ya Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania tunao uwezo mkubwa wa kutatua migogoro ya ndani (Kitaifa) na Kimataifa, tutumie uwezo wetu huu kama bidhaa endelevu ya kuongoza utatuzi wa migogoro ndani ya Jumuiya yetu.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ifanye bidii na mkakati wa kuwaelimisha wafanyabiashara wa Tanzania kuweza kumudu biashara huria ya Afrika Mashariki bila ya masharti.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Wizara isimamie miradi ya Tanzania inayopata baraka kupitia *EAC* ambayo inatafutiwa wafadhili ili kazi zifanyike. Kwa mfano, Bandari ya Mpiga Duri Zanzibar.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kusoma hotuba nzuri. Naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Pia naomba fedha za bajeti ziongezwe kwani ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kuna Mji Mkongwe uitwao Kilwa ambao sasa umepasishwa kuwa urithi wa dunia tangu mwaka 1981. Ni Miji mikongwe ya zamani tangu AD 900 – 1,700 Kilwa kati ya Miji mingine mikongwe mitano mbayo ilikuwa maarufu duniani na pia Africa *(old cities)* ambayo ni Lamu - Kenya, Mombasa - Kenya, Mogadishu – Kenya, Sofala - Msumbiji na Kilwa - Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hizo nyingine zinapewa pesa kwa ajili ya kuendeleza mji na Umoja wa Mataifa *UNESCO*. Je, Lindi inapewa pesa hizo? Kama hazipewi, kwa nini? Naomba jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Pamoja na kuunga mkono hoja, naomba nichangie yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mizani ya Njia panda Himo imekuwa kero, kwanza imejengwa barabarani;

pili, inasababisha foleni ya magari yanayotoka Nairobi kwenda Mombasa na Dar es salaam, kwenda Mombasa na Arusha. Kuna wakati foleni ya magari inatufikia Uchira, Himo na Uchira. naomba kujua, Jumuiya ya Afrika Mashariki ina mpango gani wa kununua mizani kubwa na ya Kisasa itakayowekwa njia panda Himo?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Namanga Himo Holili ziko taarifa kuwa kuna mpango wa kujenga barabara ya njia nne kutoka Namanga hadi Himo Holili Kenya. Ningependa kujua, barabara hii inajengwa na Serikali ya Tanzania au Jumuiya ya Afrika Mashariki? Kama ni Jumuiya ya Afrika Mashariki, barabara hiyo itajengwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya Kahe hadi Taveta inaunganisha Tanzania na Kenya. Reli hii ni muhimu hasa kwa watu wa Himo kwa sababu kama patajengwa Soko la Kimataifa Himo, wageni wengi kutoka Kenya, Somalia na Sudani ya Kusini watatumia reli hiyo kuleta mizigo yao katika Soko la Himo. Ningependa kujua kama kuna mpango wowote katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kufufua reli hiyo ili kuunganisha nchi ya Kenya na Tanzania.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa namna wanavyofanya kazi kwa maslahi na ustawi wa nchi yetu. Aidha, nakupongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutumia Vyombo vya Habari kuwaelezea Watanzania kuijua Jumuiya ya Afrika Mashariki tangu ile ya zamani na ya sasa; pia jinsi

inavyotembelea mipaka na kuona umuhimu wa kujenga masoko mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, ninayo mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bado wafanyabiashara wengi wananyanyaswa Kenya, Rwanda na Uganda hasa mipakani kwa kukosa elimu ya *Certificate of origin.* Kuna mkakati gani wa kuwaelimisha wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ajira za makundi matatu ndani ya Jumuiya ambayo ni *Executive Proressional* na *General Staff.* Kwa mujibu wa *Headquarters Agreement* nchi yetu kama mwenyeji *(host Country)* ni lazima ajira za kundi la *General Staff* wawe ni Watanzania. Lakini kwa sasa utakuta watumishi katika kundi hili wamo Wakenya, Waganda, Warundi na Wanyarwanda. Nipate maelezo, kwa nini hali hii inaendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya nchi, kuna tabia ya mtu yeyote anayepata ajira ndani ya Afrika Mashariki awe Mbunge wa Afrika Mashariki anaambiwa atangulize maslahi ya nchi mbele. Ni yapi hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samweli Sitta - Waziri wa Afrika Mashariki

na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya hasa katika kutoa elimu kwa Umma. Nimekuwa nikifuatilia katika Runinga vipindi vimepangiliwa na kuandaliwa vizuri sana na maudhui yanaeleweka vizuri kwa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasikitishwa tu na jambo moja ambalo ni kukosekana kitengo cha utafiti katika Wizara hii. Naomba Serikali kupitia Wizara husika ikubali kutoa kibali cha kuanzisha kitengo hiki, kwani bila kitengo hiki, kazi za kukuza uchumi kupitia Wizara ya Afrika Mashariki itakuwa ngumu sana, kwani masuala mengi yatatekelezwa kwa kubahatisha. Kimsingi Kitengo cha Utafiti kingewasaidia hata Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kufanya kazi na kutimiza wajibu wao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba hii nzuri sana, pia kwa utendaji kazi wa umakini na kuhakikisha Watanzania wanaelimika na Mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara hii, imefanikiwa kujenga Maktaba ya Kisasa kule Dar es Salaam na wananchi itawasaidia sana kwa kujipatia elimu pamoja na Wizara kutoa elimu ya Mtangamano wa Afrika Mashariki na fursa zilizomo kwenye mtangamano huo kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Wizara hii kwa kupitia Waziri wake inastahili sifa ya pekee jinsi Wizara hii inavyoendeshwa kwa umakini Zanzibar. Namwomba Mheshimiwa Waziri aende Zanzibar akaione Ofisi yake na mazingira ilipo Ofisi hiyo kama inastahili kuendelea kubaki hapo ilipo kwa umuhimu wake. Mimi nashauri Mheshimiwa Waziri aiondoe katika mazingira ya Ikulu na kuipeleka eneo la uhuru zaidi ili wananchi waweze kufika wakati wowote wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi waliopo kwenye Ofisi hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, upande wa Ofisi ya Zanzibar wameajiriwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Sasa naishauri Serikali kwamba iajiri wafanyakazi, tena wawemo na wataalam ambao watashirikiana na wale wafanyakazi waliopo na kwa misingi hiyo, sasa ni wakati muafaka kwa Serikali ikafanyia kazi jambo hilo kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine huwa tunasikitika kwamba ndani ya Mtangamano wa Afrika Mashariki kunakuwa na mazoezi ya kukabiliana na majanga ndani ya nchi zetu yatakapojitokeza na kwa masikitiko kabisa juu ya huu Mtangamano wa Afrika Mashariki kufanya mazoezi haya, lakini likitokea tatizo, hawa wenzetu mbona hatuwaoni? Nilidhani kama Watanzania tulipopata hili janga la kuzama kwa meli ingekuwa ni wakati muafaka kuingia kwenye *field,* kwani mazoezi tunafanya kila mwaka. Nashukuru na kuwapongeza Afrika Kusini kwa kutusaidia kwenye uokozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati muafaka sasa Serikali itafute maeneo Tanzania Bara na Zanzibar kwa kujenga Ofisi ya Wizara hii ili wawe na Ofisi zinazoendana na umuhimu wa Wizara yenyewe kwa wakati huu tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, soko la pamoja ni muda mrefu sasa kwa kutotengemaa kwa kukosa uhuru wa kuuza bidhaa za ndani kwa Jumuiya na kuwa na vikwazo. Mfano, hivi karibuni wavuvi kutokuwa na uhuru wa kuuza minofu yao nchi jirani, bali kuwapitia wawekezaji na hao wawekezaji ndio wenye viwanda katika nchi hizo. Hivyo, kuchukuliwe hatua za haraka ili kupata soko la uhakika kwa bidhaa mbalimbali zikiwemo bidhaa za kilimo na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza lugha ya Kiswahili itumike katika nchi zote ili Watanzania wanufaike badala ya kutumia lugha za Kigeni ikiwemo Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna uhuru wa kufanya kazi katika nchi ya Jumuiya endapo unataka kazi mpaka ujulikane au uwe na refa. Ajira iwe huru ili Watanzania wengi wapate ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za ujenzi wa barabara ni ndogo ukilinganisha na mahitaji. Ujenzi wa barabara umelenga mipakani zaidi, kumbe ingebidi

barabara kuu za kati zinazounganisha nchi, ni vyema zijengwe na Jumuiya. Mfano, barabara itokao Kairo kupitia Kenya kuja Tanzania kupitia Dodoma na kwenda hadi *Cape Town*, hii ilitakiwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ijenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa reli uwe wa nchi zote kwa maana ya kuunganisha nchi zote za Afrika Mashariki kwa lengo la kusafirisha mizigo kwa urahisi.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuwapongeza Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Naanza kusema kwamba Wazanzibar bado wanalalamika, kwa kuwa Zanzibar haijaingia Afrika Mashariki kama Tanzania. Hapo kabla, Zanzibar ilikuwa inangia kama nchi kamili. Kama ilivyo sasa, wanauliza, kwa nini haijaingia kama nchi? Naamini pindi mkiwapa jawabu la kuridhisha, hawataendelea kulalamika. Jambo lingine nataka kuuliza: Je, Wazanzibar mmechukua maoni yao kabla ya huu uundwaji? Kama hamjapata maoni ya Wazanzibar, hivi mmewatendea haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na nyie kuwa elimu ya kutosha itolewe kwani wananchi hawajui faida ya kuungana. Naamini wakipata elimu ya kutosha wataelewa na malalamiko yatakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ushuru wa forodha, pamoja na utayari, ushuru unakuwa sawasawa kama wa magari kwa hizi nchi za Afrika Mashariki. Lakini ni mapema mno, kwani wenzetu

uchumi wao ni mkubwa kuliko wetu. Ilikuwa tusubiri angalau uchumi utakuwa ndiyo tukawa sawa. Nataka pia kujua kwamba, tangu tuungane na hizi nchi zetu, ni changamoto zipi ambazo zimewakabili mpaka hii leo hazijapata ufumbuzi? Ni kwa nini? Hayo malengo mlojipangia yatakwenda vizuri kwa wakati uliopangwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna madai kwa Wazanzibar kuwa baada ya kuvunjika kwa Afrika Mashariki, kuna baadhi ya vitu vyao hawajapewa mpaka leo.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenye kueleweka vizuri sana, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Sitta – Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika sana kusikia kwenye hotuba kwamba Wizara imeshiriki kikamilifu kuandaa sera mbalimbali, kwa mfano, sera ya watu wenye mahitaji maalum wakiwemo wenye ulemavu, wazee, wajane, wagane na kadhalika. Ushauri wangu ni kwamba ni muhimu sera hizi zikamilike ili nchi wanachama zitunge sheria zenye uwiano katika masuala na sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kusimamia kwa umakini kwenye vikao vya majadiliano ndani ya Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, kwa mfano hatua za tahadhari Tanzania inazochukua katika

kuingia hatua ya Shirikisho la Kisasa, kwa sababu Wahenga walisema: “Haraka haraka haina baraka.” Yawezekana tukiharakisha migongano mikubwa inaweza kutokea na hatma ya Jumuiya tuliyoifufua kwa sasa ikapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatia faraja kuona kwamba Wana-Afrika Mashariki wameamua Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki kuwa Zanzibar. kwa Watanzania hiyo ni heshima kubwa sana. Kwa heshima hiyo tuliyopewa Watanzania tunapaswa kukiendeleza Kiswahili kwa kukitumia katika nyanja mbalimbali kinyume na ilivyo sasa ambapo bado tunabishana juu ya matumizi ya Kiswahili katika kufundishia masomo ngazi ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano na Wizara kuhusu umuhimu wa kuondoa vikwazo vya kiuchumi na biashara vya ukaguzi wa magari na upimaji uzito kuwa vingi, hivyo kuchelewesha muda wa abiria na mizigo barabarani. Vikwazo vya namna hii husababisha uchumi wa nchi kukua kwa kasi ndogo kutokana na upotevu wa muda na kadhalika, na kwa kuweza kushawishi vitendo vya rushwa ili kufanikisha vitendo vya upendeleo katika vituo husika. Kwa msingi huo, naipongeza Wizara kwa kuainisha Vituo vya Ukaguzi maalum katika mipaka ya nchi za Afrika Mashariki ambavyo ukaguzi utafanyika na vyombo na Taasisi zote husika katika vituo hivyo na kuwezesha magari kutembea kwa mfululizo unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchanganuo huo, naitakie Wizara na Watendaji wote utendaji wa

kiasi na viwango kwa mustakabali wa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia suala zima la Afrika Mashariki, bado Watanzania tuko nyuma kielimu, kiuchumi na kadhalika. Wenzetu Wakenya wametuzidi kielimu na kiuchumi; Zanzibar, Wazanzibar wengi wamesoma Kiswahili na Kiswahii fasaha. Ukija kwenye nafasi hizi za ajira za Afrika Mashariki kama za kufundishia Kiswahili katika Bara la Asia, Bara la Ulaya, Amerika; Walimu wa lugha hii ya Kiswahili wengi wametoka Kenya. Ni kwa nini Serikali na Wizara zinapotokea nafasi hizi za ajira za kufundisha lugha ya Kiswahili, zisitangazwe kwa Tanzania Bara na kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili Wazanzibar wengi wakanufaike na nafasi hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wazanzibar wengi wamekuwa wakilalamikia nafasi hizi za Afrika Mashariki, hawazipati kwa wakati muafaka na hawajui taratibu gani zinazotumika kupata nafasi hizo. Zanzibar hakuna Ofisi ya Wizara ya Afrika Mashariki na Ofisi kwa sasa hivi wanaoitumia ipo ndani ya Ikulu na wananchi wengi wanashindwa kupata taarifa ambazo zinahusu Wizara ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali pamoja na Wizara kutoa Semina kwa Baraza la Wawakilishi na wananchi wa Zanzibar kwa sababu wengi hawana elimu kuhusu suala hili la Afrika Mashariki, hata hawajui ajira zinatoka katika Wizara hiyo. Ni wa Wazanzibar wangapi ambao wameajiriwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoteli nyingi za kitalii za Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara ni kwa nini nafasi nyeti za ajira zinachukuliwa na Wakenya, Waugandа na Watanzania wengi wanaishia kutandika vitanda na kufyagia na hata wanapodai haki zao za msingi, wanakuwa wanafukuzwa kazi na haki zao kupotea. Ni kwa nini hoteli za Kenya na Uganda huwezi kuwakuta Watanzania ambao wameajiriwa kwenye nafasi nyeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Umoja wa Jumuiya ya Afrika Mashiriki, Watanzania wengi hawajui na hawana elimu ya kutosha kuhusu jambo hili kwa kuzingatia umuhimu wa maoni ya wadau. Ni vyema kuwashirikisha wataalam wa sekta mbalimbali katika majadiilano ya kiuchumi chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki sambamba na kuzingatia ushauri wao kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Jumuiya hiyo ya Afrika Mashariki imejipanga vipi kuelimisha wananchi hasa katika suala la uchumi, biashara, ajira na kadhalika?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi wajasiliamali Watanzania hawana elimu ya kutosha kuhusu Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki kama usindikaji, kupaki biashara zao, ni tofauti na ujasiliamali wa Kenya na Uganda. Je, Serikali na Wizara ina mikakati gani ya kutoa elimu ya ujasiriamali katika Soko la Afrika Mashariki?

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusiana na makadirio na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni, tumeshuhudia kuongezeka kwa wimbi la kuingia nchini mwetu makundi ya wakimbizi kutoka Somali na Ethiopia kwa madai ya kuelekea katika nchi za Kusini mwa Afrika. Wakati jambo hili likiingiza nchi katika mzigo wa kuwasafirisha wakimbizi hawa kurudi makwao, zipo tetesi kuwa mipango ya kuwasafirisha wakimbizi hao husukwa katika nchi jirani, na kwamba wakimbizi hao hupatiwa ulinzi na kusikindikizwa na Polisi wa nchi hiyo ili waweze kuingia Tanzania bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhujumu mwanachama mwenza, hakikubaliki hata kidogo. Lazima jambo hili lizungumzwe ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kulipatia ufumbuzi. Hivi inawezekanaje nchi mwanachama mwenza ikaona ni sawa kuwaacha wakimbizi wapite nchini mwake kiholela ili tu kukwepa mzigo wa kuwagharamia

wakimbizi hao kurudi makwao? Jambo hili linasababisha mzigo mkubwa wa gharama kwa nchi yetu katika kuwarejesha wakimbizi hao walikotoka. Lazima hatua zichukuliwe kuhakikisha kuwa pale wakimbizi hao wanapokamatwa karibu na mipaka ya nchi jirani, nchi hizo zibebe jukumu la gharama za kuwasafirisha kurudi walikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unapanua soko na fursa za kiuchumi kwa nchi wanachama, hususan katika maeneo muhimu kama uwekezaji, biashara, ajira na wigo wa ushirikiano katika nyanya za kijammii, kisiasa, ulinzi na usalama.  Hata hivyo, licha ya kuwepo kwa fursa hizi, tunashuhudia utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja ukienda kwa kasi ndogo kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo nchi wanachama kuchelewa kukamilisha zoezi la kuhuisha sheria zinazosimamia utekelezaji wa itifaki hiyo katika nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, kwa kuwa nchi wanacham zimeafikiana katika uanzishwaji wa Kamati za kitaifa za kusimamia utekelezaji wa Soko la Pamoja ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali yaliyofikiwa na nchi wanachama kabla na baada ya kukamilika kwa itifaki ya Soko la Pamoja, lazima Kamati yetu ifanye kazi kwa umakini mkubwa kwa lengo la kuondoa kasoro zilizojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati hii inapaswa kufuatilia kikamilifu utekezaji wa mikakati ya kisekta itakayosaidia Tanzania kunufaika na utekelezaji wa Soko la Pamoja, kubaini changamoto zilizojitokeza

katika utekelezaji wa Soko la Pamoja, na katika kuishauri mikakati itakayotuwezesha kuondokana na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu katika jumuiya nyingine za kanda, unaonesha kuwa, wakati wa utekelezaji wa Itifaki za Soko la Pamoja, nchi mwanachama zimejikuta zikikabiliwa na kuibuka kwa migogoro mingi, migogoro ambayo hulazimika kushughulikiwa na Mahakama za Jumuiya za kikanda. Hivyo basi, ili kukabiliana na uwezekano wa kuibuka kwa migogoro itakayohitaji kushughulikiwa na Mahakama ya Afrika Mashariki, ni vyema nchi wanachama zikaona umuhimu wa kuiimarisha Mahakama ya Afrika Mashariki. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Itifaki ya Soko la Pamoja inatoa uhuru na haki kwa nchi kutoka nchi wanachama kuweza kudai haki zao pale wanapoona haki zao zimevunjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo holela unaotumiwa na wafanyabiashara wetu kuuza bidhaa zao hususan mazao ya kilimo na mifugo katika nchi jirani hauwapatii faida wanayostahili. Hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kukosekana na miundombinu muhimu ya masoko katika sehemu za mipaka ya nchi yetu. Lazima kama Taifa, tuhakikishe tunaondokana na kasoro hii ya uuzaji holela wa bidhaa kwa kuhakikisha tunaharakisha utekelezaji wa mkakati wa ujenzi wa masoko na miundombinu muhimu kwenye mipaka na nchi jirani ili kuwawezesha wananchi kuuza bidhaa zao kwa utaratibu unaoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uuzaji holela wa bidhaa imekithiri katika mpaka wetu na nchi jirani ya Kenya kwa upande wa Horohoro. Bidhaa kama machungwa kutoka Muheza, Handeni na Korogwe; mahindi na mazao ya viungo kama karafuu, hiliki, pilipili manga, mdalasini kutoka Wilaya ya Mkinga na Muheza na halikadhalika mifugo na mbao toka sehemu mbalimbali nchini huingizwa na kuuzwa Kenya kwa bei za kutupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iharakishe ujenzi wa soko na mnada wa mifugo wa kisasa pale Horohoro, mpakani mwa Tanzania na Kenya. Aidha Serikali ihakikishe kuwa huduma ya maji inapatikana katika kituo kinachoendelea kujengwa cha utoaji huduma kwa pamoja mipakani (*one stop border post*) pale Horohoro ili kuondoa aibu kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa zao la Karafuu ambalo hulimwa vile vile katika Wilaya ya Mkinga, naiomba Wizara ione umuhimu wa kuijumuisha Wilaya ya Mkinga katika jitihada zinazoendelea ambazo zinalenga kutatua kero ya zao la Karafuu kuangukia mikonomi mwa Walanguzi toka Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Lungalunga - Tanga - Bagamoyo yenye urefu wa kilomita 400 ina umuhimu wa kipekee katika kukuza Sekta ya Utalii katika mwambao wa Pwani ya Bahari ya Hindi kutoka Mombasa, Mkinga, Tanga, Pangani, Bagamoyo na Dar es Salaam. Mbuga ya wanyama ya Saadani ambayo ipo katika ukanda huu ni kivutio cha

kipekee katika utalii kutokana na ukweli kwamba inajumuisha pia utalii wa baharini. Tukijipanga vizuri na kwa haraka, mbuga hii itasaidia sana katika uchangiaji wa pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ijizatiti katika kuhakiki kuwa inasimamia kikamilifu na kwa haraka upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii uweze kuanza ndani ya kipindi kifupi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja nikiamini kwamba Serikali itafanyia kazi changamoto nilizoziainisha na ushauri nilioutoa.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2012/2013 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Oktoba mwaka 2008, Maraisi wa Nchi wanachama wa Jumuiya zetu tatu za maendeleo, *COMESA, EAC* na *SADC* walikubaliana nchini Uganda kuanza mchakato wa uanzishwaji wa eneo huru la kibiashara, yaani *Free Trade Area (FTA)* litakalojumuisha nchi wanachama wa Jumuiya hizi. Sababu mojawapo kubwa ikiwa ni hali halisi za uanachama wa Jumuiya hizi ambapo nchi moja huwa mwanachama wa *EAC* na pia *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwapo maandalizi makubwa katika uanzishwaji wa eneo hili huru la kibiashara likishirikisha masuala ya biashara, kodi na

forodha, miundombinu, teknohama na nishati. Mwezi Juni, Marais wa Jumuiya hizi tatu waliridhia uanzishwaji wa eneo hili huru la kibiasahra katika Mkutano wao uliofanyika Afrika Kusini. Tanzania kuwa mwanachama wa *SADC* na *EAC* tayari imeingia katika makubaliano *(Memorandum of Understanding, MOU)* ya uanzishwaji wa eneo hili huru la kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakala ya makubaliano haya ambayo ninayo, inazungumzia ushirikiano katika nyanja mbalimbali kama yalivyoainishwa katika kifungu cha kwanza hadi cha tano cha makubaliano hayo. Nyanja hizo ni muhimu sana na msingi wa nchi yetu na bado mwananchi na hata sisi Wabunge hatujashirikishwa au hata kupewa elimu kuhusu makubaliano haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni kawaida kwa nchi yetu kuzinduka wakati tunapoona mambo hayaendi kama ambavyo tunataka. Hii inaweza ikatujengea jina baya la kuwa nchi ambayo siku zote ni ya kwanza katika uanzishwaji wa mashirikiano na nchi nyingine lakini inakuwa ni kikwazo katika utekelezaji. Wananchi tunaowawakilisha hawafahamu lolote kuhusu hili, sisi wenyewe wawakilishi wao hatuna uelewa wa kutosha wa jambo hili na nadhani hata wataalamu na wasomi wetu pia hawajui kinachoendelea. Baada ya muda, tunakwenda kuwauliza maoni yao kwa kitu ambacho hawakielewi kabisa au wana uelewa mdogo sana kuhusu jambo wanaloulizwa.

Kama kawaida, tunaanza kutoa visingizio kwa wenzetu kana kwamba hatukujua tulichokubaliana au hatujajiandaa vya kutosha. Mimi nafikiri ushiriki wetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni fundisho la jinsi ya kujiandaa kama Taifa ili baadaye tusionekane ni kikwazo kwa wengine. Ingekuwa vizuri wananchi wetu wakawa tayari wameelimishwa na kushirikishwa katika maamuzi yanayofanyika kuhusu jambo hili baada ya kushtukizwa wakati tayari mambo yamefika mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Afrika inahitaji umoja kukabiliana na nchi zenye nguvu kiuchumi, ila tatizo ni tunavyochukulia kiwepesi masuala ya msingi kama hili, na baadaye tunaanza kulalamika kuwa Tanzania haitaki hili au lile wakati tulikuwa na muda wa kuchambua na kutoa msimamo wetu kabla mambo hayajatuharibikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011 niliuliza swali la msingi hapa Bungeni kuhusu kuwapatia pasi za *kidiplomasia Professional Staff* Watanzania kwa kuwa ni haki yao ya msingi. Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu kuwa watalifuatilia na zaidi kinachotakiwa ni hatua hiyo ya kushughulikia suala hilo kwanza, kwani ni haki yao ya msingi. Lakini nimekuwa nafuatilia hili na *process* ilianza tu mara baada ya kuuliza swali hapa Bungeni na ilitakiwa iwe imemalizika kwa sasa, kwani Watanzania hawa wanadhalilika sana ukizingatia wafanyakazi wenzao wa nchi wanachama wanazo pasi hizo na wanapa urahisi zaidi wakati wa kuomba *VISA* kwani kazi nyingi katika Jumuiya ni mikutano mbalimbali na mingi imekuwa ikifanyika nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa nilizonazo ni kuwa, ni uzembe tu wa ndani, kwani *draft order for Governement gazette* iko tayari, ila Wanasheria ndio wazembe. Kwa hiyo, sababu ni uzembe wa Wanasheria kumaliza na kutangaza kwenye gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali inijibu, imefikia wapi kuhusu hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi najiuliza maswali yafuatayo: Je, Serikali imefanya uchambuzi wa kina na kuainisha faida na hasara za makubaliano haya kwa nchi yetu?

Je, kumefanyika upembeuzi wa madhara *(risk management)* yatokanayo na makubaliano haya kwa nchi yetu na namna ya kuyashughulikia?

Je, wafanyabiashara wetu ambao ni washiriki wa moja kwa moja wameandaliwa na kushirikishwa katika jambo hili ili kujua athari na fursa zetu kama Taifa?

Je, miradi ya pamoja imeangalia vipi Tanzania kama nchi na watu wetu kujulishwa, ni mambo yapi yatashughulikiwa au tunashirikiana na wenzetu katika nchi karibu 30 zilizomo katika makubaliano haya?

Je, wataalam na wataaluma wetu wametoa michango yao na ushauri au tunasubiri mambo yaanze ndiyo washirkishwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kuhusiana na suala hili, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anatoa majumuisho aeleze Bunge lako Tukufu, mikakati ambayo Tanzania imetumia kwanza katika kuhakikisha kuwa maslahi ya nchi yetu yamezingatiwa katika kuingia makubaliano haya. Pia ni vipi wananchi wameshirikishwa katika kutoa maoni na kuchangia mawazo yao kabla ya Serikali kuridhia kuanzishwa kwa ushirikiano huu? Maana imechukua karibu miaka mitatu kabla ya makubaliano kusainiwa, lakini ushirikishwaji wa wananchi na hata wawakilishi wao, haupo.

**MHE. MAJALIWA KASSIM MAJALIWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wa Wizara kwa hotuba yao iliyowasilishwa vizuri na kwa kujitahidi kukabiliana na changamoto za Wizara hii ambazo siyo haba. Naipongeza pia Kamati na Kambi Rasmi ya Upinzani kwa maoni yao ambayo inafaa yazingatiwe na Wizara katika majumuisho na pia kuyachukua na kuyafanyia kazi katika mipango yao. Nakubaliana na maoni yao mengi, nitachangia katika maeneo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza kwanza kwenye uhusiano usioridhisha baina ya Tanzania na Kenya.  Kati ya nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania ina mahusiano mazuri na Burundi, Rwanda na Uganda. Ni uhusiano na Kenya tu ndiyo yanaonekana siyo mazuri. Kwa habari tulizonazo, Kenya ni mwekezaji namba mbili hapa nchini, na katika hali ya kawaida tungetarajia kuwa ingetoa fursa sawa kwa Tanzania.  Lakini hali siyo hivyo kabisa. Kuna

taarifa za wafanyabiashara wa Tanzania wanaosumbulia huko Kenya wakati Wakenya wanaendesha biashara zao hapa Tanzania bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hili, kuna dalili za wazi kuwa Kenya inaendesha mkakati mkali wa ushindani kwa kuipiga vita Tanzania hasa kuhusiana na utalii wa Mlima Kilimanjarao. Hivi sasa Kenya inajenga Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Taveta, Mji ulio mpakani na karibu na Mlima Kilimanjaro ingawa kuna historia ndefu ya Kenya kunyemelea biashara ya Utalii unaotokana na Mlima Kilimanjaro, lakini hatua ya kujenga Uwanja wa Ndege Taveta wakati kama huu siyo ya Kirafiki hasa bila kuwasiliana na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali ni: Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na tatizo la uhusiano usioridhisha baina ya Tanzania na Kenya? Uhusiano unaoonekana kunufaisha zaidi Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nitakalozungumzia ni elimu. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti uliofanywa na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Uwezo, iliyolinganisha uwezo wa wanafunzi wa Shule za Msingi Uganda, Kenya na Tanzania; Tanzania ilikuwa ya mwisho katika hisabati na lugha (Kiswahili na Kiingereza). Jambo la kujiuliza ni hili: Je, matokeo hayo yalitokana na tofauti za mitaala? Ufunishaji mbovu, au sababu nyinginezo? Mitaala ya Shule za Msingi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ina uwiano wowote? Serikali ya Tanzania lazima iwe makini hasa kuhusiana na Elimu ya Msingi kwa sababu wanafunzi

wasipopata msingi mzuri, hata katika hatua nyingine za elimu wataendelea kupata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nitakalochangia ni kuhusu Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki ambayo Makao Makuu yake yatakuwa Zanzibar. Ningependa kushauri kuwa Kamisheni hii iandae bila kuchelewa (kama haijaandaa) mwongozo wa namna ya kutekeleza majukumu yake. Wananchi wa Afrika Mashariki wanatarajia kuwa Kamisheni hii itakuwa makini katika kueneza na kuimarisha utumizi wa Kiswahili Afrika Mashariki, Afrika na katika nchi nyingine hasa katika zama hizi za utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kamisheni iandae mpango mkakati ambao ukishatekelezwa, Kiswahili kitaweza kuwa lugha ya Bunge la Afrika Mashariki na pia itumike katika Mikutano ya Umoja wa Afrika. Kwa hiyo, lazima kuwe na umakini katika uteuzi wa watumishi wa Kamisheni ambao watatusaidia kutimiza ndoto ya waandishi mashuhuri wa Afrika, kwa mfano Shaaban Robert na Wole Soyinka kuwa Kiswahili kitaenea hadi kiwe lugha ya Afrika Mashariki na Afrika nzima.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki kwa jinsi anavyotetea maslahi ya nchi yetu awapo katika vikao vya nchi za Afrika Mashariki. Nampongeza na Naibu Waziri wake kwa uthibiti wake katika kuyamudu majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu unalenga moja kwa moja katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ni lugha yetu ya Taifa, lugha ya kufundishia Shule za Msingi na pia imekubalika kuwa ni lugha ya Afrika Mashariki na iweze kupenya mpaka Afrika. Lakini lugha hii kwenye matumizi yake imeleta matatizo sana kwa Watanzania. Hii ni kutokana na lugha ya Kiingereza kutumika kuwa ndiyo lugha ya kupimia uwezo wa watu kwenye usaili wanapoomba kazi. Hii imekuwa ikiwanufaisha sana Wakenya na Waganda ambao wanatumia lugha za Kiingereza kufundishia tangu Shule ya Msingi kufuatia uwepo wa Soko la Pamoja la Ajira.

Kwa nini tusitumie lugha ya Kiswahili katika usaili wa kazi ambazo hazihusiani na Mashirika ya Kimataifa ili kuwapa faida ya ushindani wa Tanzania ambao wanaanzia Sekondari kujifunza masomo yote kwa Kiingereza?

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kupongeza msimamo wa Serikali kuhusu Sera ya Ardhi, kwani itasaidia Watanzania kuanza kwanza kujua thamani halisi ya ardhi yao kabla ya wageni nao kuruhusiwa kupata ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa kifupi maeneo yafuatayo: Ushuru wa Forodha, Soko la Pamoja, Sarafu ya Pamoja na Shirikisho la Kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa na Umoja wa Forodha ni mfumo mzuri ambao kwanza Tanzania tunayo fursa kubwa. Tanzania inapaswa kuimarisha bandari zake (forodha) na pia Jumuiya ni lazima ku-*harmonized* kodi baina ya forodha zetu. Pia suala la ukiritimba bandarini uondoke na tuwe tayari kwa ushindani, maana ni soko huria. Kama nchi, tuimarishe miundombinu yetu kama barabara, reli na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika Soko la pamoja, Tanzania tunapaswa kubadilika na kwenda na ulimwengu wa ushindani. Tujipange kuuza bidhaa ambayo imeongezwa thamani *(added value)* na siyo mali ghafi *(raw material).* Hii pia itasaidia ajira kwa watu wetu, kwa mfano, kuuza unga badala ya mahindi. Tukisaga unga na kufunga tayari, tumetengeneza ajira kwa vijana wetu. Tengenezeni viwanda vya kutosha kwa bidhaa zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuhusu Umoja wa Fedha, angalia mfano wa Umoja wa Ulaya *(EURO).* Ni juu ya nchi yetu kuwa *stable* kwa uchumi wetu, tuhakikishe kabla ya kujiunga fedha yetu iwe na nguvu. Thamani ya Shilingi yetu ya Tanzania iimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu katika Jumuiya nchi yetu ihakikishe suala la ardhi ni mali yetu na sio ya Jumuiya. Angalieni wenzetu wanatamani sana ardhi yetu, wananyemelea ardhi yetu kwa udi na uvumba. Serikali iwe macho sana kwa habari ya ardhi.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napongeza dhamira ya utekelezaji wa

majukumu ya Wizara hii kwa kuwa ni kutekeleza azma ya Umoja ni Nguvu kwa Ustawi na Mendeleo ya Jamii na Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kila Serikali huzaliwa na mfumo wa Kisiasa unaozaa itikadi ya kuongoza fikra za Jamii, zimiliki aina ya malengo na dira ya shabaha za utawala bora, ustawi na maendeleo, uchumi na uwajibikaji wa uongozi wa utulivu, amani na mshikamano kati ya waongozwa na waongozaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mfumo wa *zionism* ndiyo umezaa aina ya uongozi wa nchi ya Israel, *Communism* kwa nchi mbalimbali, *Socialism* kwa baadhi ya nchi, na kwa kuwa uchambuzi wa kila nchi ya Afrika Mashariki una ubunifu wa mifumo ya kisiasa ambayo inaibuka kila siku na baadhi ya hiyo misimamo ya kisiasa haiainishwi katika kila nchi ya Afrika Mashariki. Je, nchi za Afrika Mashariki zitaweza vipi kuandaa mazingira ya vigezo vya kujenga Shirikisho la Kisiasa? Angalizo: Tanzania ina vyama zaidi ya Kenya, Uganda nao vyama vingi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, pana zoezi lipi la kidemokrasia la kuainishwa misimamo ya mitazamo ya Vyama vya Kisiasa? Hivyo, pawe na mtazamo kwa kila wananchi wa kila nchi kusema wawe na uzingativu wa siasa za nchi zao, mfumo maalum kama ilivyo Amerika na Ulaya au China. Nchi hizi zina mifumo michache ya dira za Kisiasa za kutekeleza miundombinu ya maono ya fikra mahsusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Sekretarieti na Uongozi wa Afrika ya Mashariki una umakini upi na umejizatiti vipi dhidi ya Mashirika ya Kimataifa yanayoshika hatamu za uchumi, kuwa ndiyo mazalia ya msukumo wa maamuzi ya kisiasa ya ndani ya nchi za Afrika Mashariki? Je, usalama wa uhuru wa nchi za Afrika Mashariki dhidi ya misaada ya kumeza uhuru wa uongozi na utawala wa nchi unalindwa na misingi ipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani pana *Big Power Diplomacy is Big Power responsiblity to protect big powers economy* kupitia Balozi zao, Tanzania imeathirika na mikataba mibovu ya *Big power diplomacy*. Je, Afrika ya Mashariki ipo tayari kuwa sauti ya ukombozi ya kusuta hadharani dhuluma hii? Je, Afrika ina ubunifu upi wa kuanzisha kelele dhidi ya dhuluma za Kimataifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu kwa hoja hizi. *(God bless you).*

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kwanza kuwapongeza Wabunge wapya waliochaguliwa na Bunge lako Tukufu, kwamba Wabunge waliochaguliwa ni watu makini ambao kamwe hawatakuwa wasindikizaji wa matakwa ya nchi nyingine wanachama, lakini watakuwa ni wawakilishi wa Tanzania na Watanzania ili waweze kupata tija itokanayo na umoja huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini ya Watanzania kwamba Wawakilishi wa Tanzania katika umoja huo wataleta changamoto kubwa ya

kimaendeleo na mapinduzi makubwa yatakayotawala mijadala ya Jumuiya. Lakini vile vile mijadala ambayo itakuwa inaungwa mkono na nchi wanachama wa umoja huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ya Tanzania ni mali ya Watanzania, hivyo Wawakilishi wa Tanzania ambao ni Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wasikubali kutumiwa na washirika wengine wa Jumuiya hiyo kwa misingi ya kusaidia zaidi nchi zao, badala yake maslahi makubwa ya ardhi yamsaidie Mtanzania isipokuwa kwa yale mambo ambayo tumekubaliana katika masuala ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki Watanzania wengi wanakosa ajira kuliko nchi nyingine wanachama wa Jumuiya hii. Hivyo, Wawakilishi wetu katika Jumuiya wana haki ya kuleta utetezi katika Jumuiya ili kuwe na uwiano wa ajira kwa kuzingatia maslahi ya nchi Wanachama wa Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wetu wa Afrika ya Mashariki tuliowachagua katika Bunge hili, pamoja na kutuwakilisha katika Bunge hilo, lakini wana wajibu wa kuitangaza nchi yetu Kitaifa na Kimataifa katika masuala ya kiutalii, kibiashara na kiuchumi. Kwa mfano, kuwe na haki za kuanzisha shughuli za kiuchumi, soko la ajira, soko la bidhaa, soko la mitaji na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwakuwa Tanzania ina fursa ya kutumia neema iliyojaliwa na Mungu kwa kuzungukwa na bahari na maziwa, jambo ambalo

huhitaji karibu nchi zote wanachama kutambua umuhimu wa kutumia bandari zetu, ni budi basi tuitumie nafasi hii kuitangaza ili kukuza uchumi wa nchi yetu. Lakini vile vile tuna wajibu wa kuimarisha reli zetu na nchi wanachama ili kutoa fursa ya kupitisha mizigo ya kupitia nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mmoja ana haki na wajibu wa kufuatilia haki za wananchi wake ambao wako katika nchi nyingine mwanachama wa Jumuiya hivyo. Kwa heshima ya pekee, naomba nimpongeze Balozi wa Tanzania aliyeko Kenya juu ya hatua aliyoichukua kwa vijana ambao walishikiliwa kinyume cha sheria na hatimaye kupatiwa usalama wao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Naibu Waziri una robo saa.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mie niweze kusema angalau maneno machache kuhusiana na hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuiwezesha Wizara yetu kuwasilisha hoja hii muhimu. Lakini pia sina budi vilevile kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani yake kubwa kwangu mimi kwa kuniweka

niendelee kuwa Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani hizi vilevile zimwendee Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar na Makamu wake wawili kwa kutupa ushirikiano mzuri na mkubwa sana na kutuelekeza ni namna gani ushirikiano huu na mtengamano wa Afrika Mashariki uwe unakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini shukrani nyingine vilevile nizipeleke kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa miongozo wanayotupa kiasi kwamba Wizara yetu inakwenda kwa mafanikio mpaka hivi sasa. Vilevile niwapongeze wafanyakazi wote wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na pia Watendaji wote wa Wizara nyingine za kisekta kwa sababu Wizara yetu haifanyi kazi peke yake, isipokuwa inafanya kazi na Wizara nyingine, kwa hakika tena kwa wote wa Tanzania Bara na Zanzibar, jitihada wanazozifanya ndiyo sasa wanaipa sifa Wizara yetu. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa pole na rambirambi nyingi kwa wale wote walioathirika na uzamaji wa meli. Walioathirika Mungu awape pole na awaweke mahali pema peponi kwa wale ambao hawakupatikana mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, shukrani ziende kwa familia yangu, familia ya Mzee Abdulla Saadalla Mabodi, mke wangu Dkt. Badria Abubakari, watoto, ndugu zangu wote pamoja na wananchi wote

wa Jimbo la Raha Leo kwa kunichangua. Sitawaangusha na niendelee kuwaambia kwamba umoja ni nguvu na kutengana ni udhaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingi sana zilizotolewa na Wabunge wetu, zote tunazizingatia na nitaanza kuzijibu moja baada ya nyingine. Zile ambazo itashindikana kujibu hapa basi tutawasilisha majibu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba Serikali iongeze kasi ya kushughulikia rasimu ya Sera ya Taifa ya Mtangamano. Kama ilivyoelezwa kwenye hotuba, Wizara imeishakamilisha rasimu hiyo na imeiwasilisha Serikalini na hivi sasa kuna taratibu za kukamilisha ili sera hiyo iidhinishwe na kurasimishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya ufunguaji wa ofisi Zanzibar. Kwa kweli hoja hii nilishaijibu hapo kabla kwamba Wizara yetu tayari imeshaandikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na taarifa tulizozipata mpaka hivi sasa ni kwamba kuna sehemu kama mbili hivi zimewekewa kipaumbele kwamba zitatolewa kwa ajili ya kuwa ofisi za Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tunapongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuchukua hatua haraka kama hivyo na tunasubiri ili tuanze utekelezaji wa hoja hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliguswa sana na hoja ya maandishi ya Mheshimiwa Kai ambaye anatupongeza. Kwa kweli tunazipokea pongezi hizo mimi, Mheshimiwa Waziri wangu na Wizara kwamba ni

kweli tulikwenda Shimoni tukafanya tafiti nyingi na tukakwazua vipengele vingi sana. Lakini pamoja na hili nilipenda sana tuwashajishe ndugu zetu wazawa kutoka Pemba wanaoishi kule ambao wanaitwa *stateless settlers* katika haraka hizi sasa hivi za kuandikisha wananchi katika vitambulisho vya kitaifa bora na wao kwa sababu mpaka hivi sasa ni *stateless settlers* tangu mwaka 1964/65 waende pale kwa Balozi wetu mdogo wakajiandikishe labda taratibu nyingine zitafuata baadaye, wasibakie hivihivi kuwa ni *stateless*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu kitengo cha utafiti. Hoja hii imetolewa na watu wengi sana. Kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wengi wamependekeza kuwa na kitengo cha utafiti na intelejensia. Kamati pia imeshauri jambo hilo. Wizara imepokea ushauri huu na itaendelea kushauriana na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma kuhusu umuhimu wa kuanzisha kitengo hiki. Kwa kweli ni kitengo muhimu na ninaamini kwamba kitatusaidia sana juu ya kufanya tafiti kadha wa kadha za kiintelijensia ambazo hazipatikani kwa urahisi ili na sisi tuweze kushauri na kuweka mikakati ya baadaye hasa tunapokwenda katika majadiliano na hizi nchi wanachama wengine lakini pia vilevile majadiliano katika *tripartite* ya Afrika Mashariki, *COMESA* na *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Joyce Mukya pamoja na Kamati walionesha *concern* yao kuhusiana na *tripartite* ya *COMESA*, Afrika Mashariki (*EAC*) na *SADC*. Ningependa tu kusema kwamba kabla hatujaenda kwenye majadiliano hatua zote huchukuliwa kwa umakini kwelikweli na wataalam wa

ngazi za juu ili tusije tukafanya makosa katika kuingia mikataba hii ya *COMESA, EAC* na *SADC*. Lakini lazima nikiri kwamba ni kweli itakuwa vizuri sana kama haya majadiliano vilevile yatahusisha Wabunge wa Bunge letu hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili na wao watoe maoni kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Spika na uongozi kwamba wamo katika hatua za kutaka kurasimisha namna gani masuala haya ya mtangamano wa kikanda yawe yanahusisha na Bunge. Nawapongeza kwa hilo na nina imani kwamba Wabunge wetu wa Afrika Mashariki wapo wanasikiliza hilo na wataliunga mkono.

Mheshimiwa Joyce Mukya vilevile alizungumzia kuhusu *passport* za *professionals* wanaofanya kazi Afrika Mashariki. Hili jambo limeshafika mbali sana. Hivi sasa liko katika ofisi za Mwanasheria Mkuu zinafanyiwa uhakiki wa kisheria na mapendekezo yatatoka na baadaye hili litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ambayo Mwenyekiti wa *NCCR* Mageuzi, Mheshimiwa James Mbatia alizungumza kwamba sawa katika Afrika Mashariki tunaona kuna mzunguko wa vikao vya Bunge la Afrika Mashariki katika miji mikuu ya Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi kwenye Mabunge yao wanakuja kuhutubiwa na Waheshimiwa Marais, sasa yeye anahoji kwamba mbona hajaona hili Dodoma mpaka leo? Hilo tunalichukua na kwa kweli ni jambo zuri. Tutalipeleka na mwakilishi wa *Secretary General*

hapa ambaye ni *Deputy Secretary General* amesikia hiyo. Kwa hiyo, tutalifanyia kazi na sisi tutalishikia kidedea kwelikweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja juu ya uwepo wa Kamati mpya ya Kudumu ya Bungu itakayohusiana na mambo ya kikanda ambayo Afrika Mashariki itakuwa inahusiana nayo. Kama ilivyoelezwa Bungeni na Mheshimiwa Spika, vilevile katika hotuba yetu, Wizara yetu tayari kwa kushirikiana na Bunge imeshaanza, neno mchakato tusilizungumze, tumeshaanza taratibu za kuuunda Kamati hiyo pamoja na kutoa miongozo. Naamini kwa busara za Mheshimiwa Spika, Wizara yetu na Waziri wetu haya mambo yatatekelezwa harakaharaka. Lakini pamoja na kutekelezwa harakaharaka, ni jambo la msingi ambalo litasaidia kuwepo vikao vya pamoja baina ya Wabunge wa Afrika Mashariki na Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kulikuwa na hoja ya Tanzania kusaini *EPA*. Niseme tu kwamba Tanzania tuko makini na wataalam wako makini. Hatusaini makubaliano ya *EPA* bila ya kuona kwamba na sisi tutapata faida. Siyo Tanzania tu lakini Afrika Mashariki nzima. Tusisahau tu kwamba hawahawa ambao tunajadiliana nao wanatusaidia katika mlengo mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *issue* ya mchakato wa Sarafu Moja. Mchakato huu ni vizuri tuwaelezee wananchi waelewa kwamba, hivi karibuni tu yamefanyika majadiliano makubwa juu ya kuwepo kwa *protocol* na huenda pengine itasainiwa.

Imezungumzwa hapa kupitia Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba itakuwa mwaka 2012 lakini kitakachosainiwa ambacho sasa hivi mjadala unaendelea ni *protocol* na siyo mkataba wa kuanza kutumia sarafu. Ili tuweze kuingia katika mkataba huu kuna mambo hapa yanaitwa *microfinance convergence* ambayo ni lazima tuwiane pamoja katika nchi zote hizi husika katika mfumuko wa bei, nakisi ya bajeti, akiba ya fedha za kigeni katika benki zetu, ukuaji wa uchumi na katika deni la taifa. Sasa mpaka kuwe na namba maalum ambazo zimekubalika katika hizi nchi tano ndiyo tutaanza kufikiria namna ya kuanza sera za kutumia Sarafu Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya uwanja wa ndege wa Pemba. Uwanja huu ni *proposal* ambayo ilitoka katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikafikishwa Afrika Mashariki kwa uwiano na ushirikiano pamoja na Wizara ya Fedha, *African Development Bank* wamekubaliana na Afrika Mashariki ili kutekeleza *Phase II* ambayo ni *designing* ya usanifu wa uwanja ule. *Phase* ya I, SMZ ilisema itaitekeleza kwa kushirikiana na watu wengine. Taarifa tulizozipata ni kwamba miezi miwili iliyopita baada ya kikao chetu ikafahamika kwamba ile *design* ya mwanzo ambayo ni *feasibility study,* SMZ imepata matatizo kidogo kwamba haitaweza kufanya hivyo na hivi sasa Wizara yetu imo katika mchakato wa kufikiria namna gani na mfadhili gani anaweza kufanya *feasibility study* lakini hilo jambo si la kulizungumza sasa hivi, bali vikao ndivyo vitakavyoamua namna gani tutaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na taasisi za Kiswahili, napenda kutoa tu taarifa kwamba Wahandisi kutoka Afrika Mashariki wameishafika pale Zanzibar, Ecrotanal na wameshahakiki yale majengo yana kasoro gani na yanatakiwa yafanyiwe ukarabati gani. Kwa hiyo, hii Kamisheni itakuwepo na Taasisi itakuwepo lakini kitu muhimu ni kama nilivyozungumza jana Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Spika ni kwamba uthubutu na ujasiri wa kuwatoa hawa Walimu kwenda katika hizo nchi za Afrika Mashariki ndiyo muhimu. Nimeshasema kabisa kwamba tutazungumza na *TAESA (Tanzania Employment Service Agency*) na zile *Agency* katika nchi zile nyingine ili waweze kuhabarishana siyo katika Ualimu tu lakini mpaka katika nyanja nyingine zote za kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na huu muda mdogo ambao umenipa, naomba kuendelea. Hoja nyingine ni hoja ya miradi ya maendeleo ya Wizara. Wizara yetu sisi ukiiona kwa nje utaiona kama ni Wizara ambayo inakwenda na uratibu na kuandika na kusafiri tu lakini la mwanzo ifahamike kwamba hivi sasa Wizara hii imeanzisha sera maalum na mradi maalum wa maendeleo juu ya mambo ya utafiti wa namna gani Tanzania iingie katika utafiti wa kikanda pamoja na Afrika Mashariki. Kuna mradi mwingine wa maendeleo ambao vilevile umekwishapelekwa ni kuanzisha *integration center* yaani hivi viji-*center* vya wafanyabiashara ili waweze kuwasiliana na kuna mradi mwingine ni mradi wa kuboresha Kituo cha Kitaifa cha Habari kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*

*kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaheshimu Kiti. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Abdulla Juma Saadalla, Naibu Waziri Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mchango wako mzuri sana, umesaidia kufafanua mambo mengi, tunakushukuru sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Ushikiriano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Samuel Sitta. Mheshimiwa Waziri karibu sana!

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya muda wa dakika 25 kutoa majumuisho ya michango mizuri sana tuliyoipata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi pia na kwa kauli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo ada, michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo tumeipata kwa maandishi ni Waheshimiwa Wabunge 60, ningeomba kwa kuwa muda wenyewe ni kidogo sana basi wanisamehe Waheshimiwa Wabunge majina ya Majimbo ninayo hapa, lakini nikiendelea kutaja Majimbo na kurejea Viti Maalum itachukua muda mrefu.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kauli humu ndani ni nane ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa ambaye aliongea kwa niaba ya Kamati, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mohammed Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo na hatimaye Mheshimiwa Dkt. Abdulla Juma Saadalla, Naibu Waziri wa Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Amina Clement, Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Mohamed Chomboh, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Mhandisi Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Dkt. David Mallole, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Nyambari Chache Nyangwine, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Joyce J. Mukya, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Margareth

Mkanga, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Mch. Israel Natse na Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Rose Sukum, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Mbarouk Mohamed, Mheshmiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye, Mheshimiwa Haroub Shamis, Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Rashid Ali Abdalla, Mheshimiwa Donald Max, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa David Kafulila na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hao ndiyo waliochangia kama kuna jina lolote ambalo pengine limekuja maana yake mambo yangu hapa yamefuatana kwa haraka haraka. Kwa hiyo, kama kuna jina lolote ambalo tumepitiwa, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa naye amechangia, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge 61 wamechangia kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge 8 kwa kauli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema, nashukuru sana kwa yote ambayo

tumeyapata hapa. Hakika wakati wote katika Wizara huwa ni elimu kubwa sana kupokea mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, hawa ni watu ambao ni makini, wanafahamu shughuli zao na wengi wao wana uzoefu mkubwa katika haya mambo wanayoyaongelea. Kwa hiyo, kwetu huwa ni faraja kubwa na elimu kubwa kupata maoni yao. Sasa nitajitahidi kwa muda huu mfupi sana uliobaki niweze kupitia baadhi ya hoja muhimu ambazo Waheshimiwa Wabunge wametufikishia kwa njia hizo mbili yaani maandishi na kauli.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa kwanza inahusu ushindani wa biashara. Pili, uuzaji wa mazao kuvuka mipaka ndani humu ndiyo unakuta kuna vikwazo vya biashara. Kuna masuala ya bidhaa ipi inasindikwa kwa kiasi gani ili inapouzwa itupe thamani zaidi. Kuna masuala ya viwanda na tunauziana bidhaa za aina gani. Tunasisitizwa kwamba tujitahidi, Serikali yetu izidi kuweka mazingira mazuri ili tuzidi kulitawala soko la Afrika Mashariki kwa bidhaa za aina mbalimbali. Kuna masuala ya kujipanga kuhusu maafa kwa pamoja. Kuna suala maalum la magendo ya karafuu. Uendelezaji wa bandari, ajira ndani ya Jumuiya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwanza nianze na eneo hili pana la biashara. Ndugu zangu tunakotoka ni mbali kwa sababu hata hii biashara tunayouza sasa ya dola takribani milioni 410 ni ongezeko la asilimia 400. Kabla ya hapo hatukuwa tukilitazama soko la Afrika Mashariki kwa namna ambavyo tumejipanga vizuri kama hivi sasa. Kwa hiyo, mimi ninachoweza kusema,

ukitazama uchumi wa nchi ya Tanzania ukilinganisha na hawa wenzetu ingawa hivi sasa inaonekana hatujafika mbali sana, Kenya wanatupita kwa mzunguko wa biashara takribani mara tatu na nusu lakini jamani tunakokwenda na rasilimali tulizonazo hakika sisi Tanzania ndiyo kwa siku za usoni tutakuwa ndiyo Ujerumani ya hapa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Mungu ametujalia gesi imepatikana, lakini nasema kama alivyosema Mheshimiwa Muhammad Sanya na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, tukiyachanganya haya mawili unaona kwamba badala ya sisi kuuza gesi moja kwa moja kwa wenzetu, mkakati wa Serikali ninavyoufahamu hivi sasa ni kwamba tuigeuze hii gesi iwe umeme. Sehemu moja iwe umeme, sisi ndiyo tuwe wauzaji wa umeme katika Kanda nzima ya Afrika Mashariki. Kwa sababu hata wakijitahidi namna gani wenzetu Uganda kwa kutumia Mto Nile kuna ukomo wake. Kwanza, kuna mikataba ya Kimataifa, haiwezekani kuendelea kujenga mabwawa ya kuzuia mto Nile kuendelea kupata umeme wa maji na hali ya mazingira pia mnaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi ambao tuna gesi ya kutosha badala ya kuwapelekea gesi moja kwa moja nadhani tuuze umeme na tuendeleze viwanda vya mbolea kule Mtwara, Lindi ili viwanda hivyo sasa viweze kuzalisha mbolea kwa Afrika Mashariki. Tukiweza kuuza umeme na mbolea, makadirio yaliyopo kwanza, kwa mfano, takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba umeme pekee yake unaweza kuipatia Tanzania si chini ya dola milioni 500

kwa mwaka. Hii ni zaidi hata ya mauzo yetu yote ya hivi sasa ya dola milioni 409 kwa zao hilo moja tu. Kwa hiyo, sisi tunadhani tukiwapelekea wenzetu gesi kwa wingi tunaweza tukajikuta sasa tunapeleka gesi kwa bei rahisi, wanafua umeme halafu wanatuuzia umeme, hiyo itakuwa siyo kitu kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni usumbufu wa hizi shughuli zenyewe za biashara mipakani na kadhalika. Haya mambo tunajitahidi kuzungumza na wenzetu ili kupunguza aina mbalimbali za vikwazo vilivyopo na kama nilivyoeleza katika hotuba vipo vikwazo ambavyo siyo vya forodha. Tumeunda Kamati Maalum inafanya kazi, tunakwenda tunavipunguza, tunajipima kila baada ya miezi michache kuona ni vikwazo vipi vinapungua na tuna mikutano ambayo tunaelezana yapi yafanyike katika kupunguza vikwazo hivyo. Kwa hiyo, mimi naamini kabisa biashara baina ya nchi zetu itazidi kuendelea kuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunachukua tahadhari ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba tuone usindikaji wa hizi bidhaa zetu ufikie kiwango gani ili kile tunachouza sasa kiwe na thamani zaidi, ni bora uuze sembe kuliko kuuza mahindi. Kwa hiyo, maeneo kama ya Rukwa, Iringa na Ruvuma ambako kuna mahindi kwa wingi ingekuwa jitihada yetu sasa na hii tutashirikiana na sekta zinazohusika, jitihada yetu iwe ni kuweka mitambo ya kusaga nafaka na sisi tuwe wauzaji wa nafaka siyo tu *East Africa*, lakini pia Kongo eneo la Katanga wanahitaji. Kwa mfano, Katavi na Rukwa wapo karibu sana na Katanga

waweze kuwa ndiyo eneo ambalo inatoka sembe kwa ajili ya kuwauzia majirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendawili cha hivi sasa cha sisi kuwa tunawauzia mahindi majirani halafu wao wanasaga nafaka na kuipeleka Sudani ya Kusini, hii kwa kweli haistahili kabisa. Tutaangalia hilo ili Sudani ya Kusini ipate moja kwa moja bidhaa hiyo ya sembe kutoka kwetu badala ya kuwapelekea mahindi nchi ya jirani na baadaye iyasafirishe kama bidhaa inayotoka katika nchi hiyo jirani tunayoiuzia malighafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika yale mengine yaliyosemwa kuhusu ajira za Watanzania, kwanza niseme tu ukichukua ajira ipo katika sehemu tatu. Kuna ajira Makao Makuu ya Jumuiya - Arusha na vitengo vyake. Sasa Makao Makuu ni Arusha lakini tunapata hii fursa ya kuweka Taasisi mbalimbali. Kwa mfano, Taasisi ya Kiswahili itakuwa Zanzibar na hii itakuwa ni kubwa siyo kitu kidogo kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Abdalla Saadalla. Tunashukuru sana SMZ wamekwishatupatia jengo pale ambalo tayari tathmini imefanywa na tutaanzia hapo tunalikarabati jengo hilo liwe la kisasa na itakuwa ndiyo kitovu na mahali pa utafiti wa Kiswahili kwa Duniani nzima. Kwa hiyo, tukishasema ni *East Africa* basi ndiyo kueneza kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwa mfano, Nigeria wametuma maombi ya kutaka kujifunza Kiswahili pale *University of Ibadan* ili wapate Walimu Ibadan Chuo Kikuu ili hatimaye wafundishe Kiswahili Afrika ya Magharibi. Ndiyo maana tukiitazama hii

Taasisi ya Kiswahili Zanzibar inaanzia kwenye jengo hilo, lakini kwa siku za usoni itakuwa ni Taasisi kubwa sana na niungane na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib kwamba Kiswahili jamani ni bidhaa. Tazameni Kiingereza hivi sasa ndege zote zinazoruka angani, Marubani wanalazimika uwe kabila la Taifa lolote ujue kuongea Kiingereza kwa sababu ndiyo lugha iliyotambuliwa na Shirika la Kimataifa la Safari za Anga kwamba Kiingereza ndiyo kitachotumika huwezi kusema ninapenda Kirusi, napenda Kifaransa watakuambia sawasawa lakini kwa mawasiliano unapovuka nchi mbalimbali huko angani utatumia Kiingereza na ndiyo imekuwa lugha ya biashara sasa takribani duniani nzima. Kwa sisi Afrika hapa hakuna lugha yoyote ambayo inakaribia Kiswahili. Tayari inakadiriwa watu katika Afrika kiasi cha milioni 180 wanaongea Kiswahili hivi sasa. Maana yake usitazame tu Afrika Mashariki, lakini tazama Msumbiji, tazama Malawi, tazama DRC, Zambia ni cha namna mbalimbali lakini ni Kiswahili, kupitia utafiti tutakaokuwa tunaufanya Zanzibar tutaendelea na mitaala ambayo itatupa Kiswahili safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pale Arusha kwa mfano, nitoe tu mchanganuo, watumishi wanaofanya kazi katika Makao Makuu walio wengi, tuseme mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

Watumishi kutoka Burundi ni 18, watumishi kutoka Rwanda 18, watumishi kutoka Uganda 51, watumishi kutoka Kenya 67 na Watanzania 77. Kwa hiyo, tunajitahidi, hiki ni chombo cha pamoja, lakini tunajitahidi kwa utaratibu tuliokubaliana ambao

unaitwa *quota system,* wa kugawana kwa ngazi mbalimbali, ngazi za utawala, ngazi za *operational staff* na mpaka juu wataalam tunagawana na kuna ukomo wa kila nchi. Kwa hiyo, hakuna nchi ambayo itaweza kujipendelea na kuzidi kiasi ambacho kilipangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa James Mbatia alileta rai yake inayohusu kama nimempata vizuri hapa manufaa yanayoweza kupatikana katika Itifaki kushirikiana kiulinzi. Katika Sekta ya Ulinzi, mikakati tunayo na tuna Kamati ambayo inahusiana na mambo ya ulinzi na nitoe taarifa tu kwamba mwaka huu yamefanyika mazoezi ya kijeshi sehemu mbili, moja, tumefanya Zanzibar baharini, mazoezi mengine yamefanyika Rwanda kwenye ardhi. Sasa hii ni hatua ya mwanzo tu. Tutalichukua lile wazo kwamba sasa kutokana na majanga yanayotokea tuchange nguvu pamoja badala ya kufanya tu mazoezi ya Kijeshi basi tuunde timu ambazo zitatupa nguvu ya kuweza kushughulikia maafa yoyote yanayoweza kutokea. Kwa hiyo, tuwe na nyenzo, tuwe na watumishi, tuwe na Askari ambao wanaweza kuwa ni chanzo cha kuwa *disaster preparedness unit* ya kuweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu tunakwenda vizuri, tunaomba tu kwamba ushirikiano kwa kila Serikali kwa sababu mara nyingine tunalianza jambo linakuwa na nafasi nzuri kufanikiwa likichukuliwa katika ngazi ya Afrika Mashariki nzima kwa sababu inaitwa *regional project,* halafu inatokea Serikali inachomoka inafanya jambo lake hapo katikati, sasa

inaleta mkanganyiko kwa wale ambao tunasaidiana nao na hilo ni vizuri liepukwe ili twende kwa vizuri. Nikupashana habari tu ili tuweze kusema kwa sauti moja.

Waheshimiwa Leticia Nyerere na Eustace Katagira walizungumzia sana kuhusu elimu kwa wananchi na mimi nakubali, bajeti yetu ni finyu lakini tunajitahidi kama nilivyosema katika ofisi nimegundua jambo moja zuri tu katika Wizara yangu. Huu usemi kwamba watumishi ni wavivu sijui wakoje, hapana. Kama kuna mipango mizuri ya kazi na mkapangiana majukumu, vijana hawa Wakitanzania wanaweza kufanya kazi vizuri sana, jamani tusiwakatishe tamaa vijana wetu wanapokwenda nje. Hawa Watanzania waliopo Botswana, walioko katika *Civil Aviation* katika Southern Africa wote hawa wanasifiwa kwa nidhamu, ustaarabu na uwezo mkubwa wa kufanya kazi. Asiyekubali hilo aje aone Wizarani kwangu mimi mnaona hata viwango tu vya hotuba ya bajeti hii imeandaliwa na watu wa ofisi yangu, wamestafsiri Kiingereza nadhifu, vijana wanakesha wanafanya kazi ndiyo maana unapata taarifa ya kutosha kabisa kwenye Wizara ambayo ina bajeti ndogo kuliko Wizara yoyote hapa nadhani Afrika Masharika, siyo tu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala siyo fedha tu, ni namna ya kujituma, ninazo motisha ndogondogo, natumia uzoefu, kwa mfano nimesema kila mtumishi wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki lazima awe na *Passport* ya *East Africa*, haina gharama sana lakini unamkuta Dereva wetu ana *Passport* ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, siku nyingine Katibu Mkuu akiona

mambo ni mazuri anamtuma Afisa kwa gari Dereva anapita mpaka Kigali kule na *passport* basi ameheshimika hivyo nao wanawakoga Madereva wa Wizara nyingine ambao hata kuvuka tu mpaka hawajavuka. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mambo haya ya motisha ni mambo madogo lakini yanaleta tofauti. Watu wangu wanajituma isivyo kawaida na mimi nafurahi sana kwa hilo. Nitajitihidi Mheshimiwa Dkt. Mgimwa hayupo lakini watu wa Hazina mnatusikia, tunaomba bajeti ya kutosha ili tuweze, huu mtangamano tusipokwenda vizuri itakuwa shida, vijana hawa wanajituma sana ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri itabidi niangalie kama Madereva wa Bunge wana *Passport* za Afrika Mashariki. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo limechangiwa kwa upana sana, ni hili suala la ushiriki wa Watanzania kwa ujumla katika mchakato wa majadiliano kuhusiana na kuungana katika jumuiya ya uchumi hatimaye kuwa na shirikisho la kisiasa. Suala hili linahitaji uwazi na kama ninavyofahamu hatua ya mwisho kabisa tutakayofikia katika hiyo miaka inayokuja ni kupiga kura ili kuwa na shirikisho lakini bila elimu kwa watu haiwezekani, watu wataogopa tu. Kwa hiyo, hii kazi ya kuweza kuelimisha wenzetu Watanzania wote ili waweze kuelewa kwamba ushirikiano hauepukiki kwa sababu mkishakuwa jirani ndiyo mmekuwa jirani hivyo lazima mrahisishe mambo

ili muweze kukuza uchumi kama soko moja na eneo moja la forodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengine yale yote ya ardhi, msiwe na shaka, tumekaa vizuri, tunalinda ardhi yetu. Ardhi yote haiko chini ya soko la pamoja, ardhi ni sera ambayo inahusisha kila nchi na sheria zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kweli kumetokea ujanja hivi sasa na hasa dada zetu wa Tanzania. Mtu anakuja kutoka nchi nyingine anamuoa binti wa Kitanzania, akishamuoa wanaomba ardhi, wanaanzisha kampuni, wanakuwa na kampuni moja inamiliki shamba sehemu fulani, uzoefu wetu tumeanza kuona baadhi ya hawa waoaji hawaji hasa kuoa kwa nia njema, wanachokitaka kumbe ni ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ndugu zangu mabinti wa Kitanzania muangalie sana, tusije tukaiweka nchi yetu rehani na hasa ukizingatia kwamba baadaye mtu anaanza visa, mwanamke anaachwa halafu sasa kwa kinyume kabisa yule ambaye si raia ndiyo anakuwa yuko pale. Sasa Mwanasheria Mkuu naye yupo, haya ndiyo mambo ya kuangalia, hivi hawa wanaooa harakaharaka halafu wanapata ardhi halafu wanawaacha mabinti zetu hawa kweli wamekuja kuoa ama wamekuja kuchukua ardhi tu hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya tuyaangalie. Nafikiri kinachotokea zaidi, unajua wajasiriamali katika suala la uwekezaji mara nyingi

wanakuwa ni wanaume, ndiyo wanahama mpaka huku, wajasiriamali kwa maana ya kuuza bidhaa ni wanawake lakini kuja kukaa mahali na kuhama kabisa na kujaribu kukaa Morogoro, Tanga wapi tumeona wanaume ndiyo wamejitahidi sana katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lingine ambalo tumeliona linazungumzwa sana ni uhusiano wetu na Waheshimiwa Wabunge wetu wa *EALA*. Tumeanza vizuri sana. Mheshimiwa Spika alitusaidia tukawa na semina ya pamoja na mimi niseme ndugu zetu hawa tuliowachagua safari hii ni wasikivu, tunafanya kazi kwa pamoja, Miswada tunaiyona na katika mikutano miwili ambayo mimi nimeshuhudia wameweka maslahi ya Tanzania mbele*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi kwenye hilo sina shaka lakini natoa rai kwa Mheshimiwa Spika na ofisi yake, ni vizuri tu iundwe kwa haraka Kamati ya masuala ya Afrika Mashariki, mambo yake ni mengi sana na inapokaa ndani ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, hayo ni mambo makubwa sana hayo ya nje, ulinzi usalama kushughulika na Marekani, lakini zaidi kwa sasa ni mambo kama ya nadharia tu, yanayotugusa wananchi wa kawaida ni haya ya Afrika Mashariki na ni mengi kwelikweli. Sasa namna ya kushughulika na wenzetu Wabunge wa *EALA* ni vyema Kamati ya Kudumu ya Masuala ya Afrika Mashariki ikaundwa haraka ili sasa mawasiliano yetu sasa na Wabunge wetu wa Afrika Mashariki yakawa ni ya moja kwa moja, mepesi. Taarifa mbalimbali mmekuwa mkizidai sasa zitakuwa zinapitia katika Kamati ya

Kudumu ya Masuala ya Afrika Mashariki, hapo tutakuwa tumekwenda hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli muda wa dakika 25 si rahisi kuweza kuyashughulikia mambo mazuri yaliyosemwa na Waheshimiwa Wabunge, nimalizie kwa mambo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba ni muhimu tuwahimize, sisi ndiyo Wabunge tuwahimize wafanyabiashara wetu, watumishi, wasomi wajitahidi kuzitambua fursa zilizomo ndani ya Soko la Pamoja katika Afrika Mashiriki. Kwa mfano, sasa hivi Uganda imepitisha Azimio la Bunge la kuhimiza Waganda wajifunze Kiswahili, watahitajika Watanzania kwa mamia waende wakasaidie kufundisha Kiswahili katika ngazi mbalimbali shule za msingi na shule za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa maana nyingine watu wetu watazame nje ya Tanzania, ajira isitazamwe hapahapa tu Tanzania, ni nje ya mipaka. Wapo Walimu wa Kitanzania wanafundisha Kiswahili takribani sasa wamefikia 1000 Rwanda, sasa itakuwa hivyohivyo Burundi, Uganda. Kwa hiyo, Mwalimu katika taaluma ya Kiswahili analo soko ndani ya Afrika Mashariki, lakini vilevile kwa masomo mengine ya sayansi na masomo hayo mengine yana nafasi kabisa katika…

Mheshimiwa Naibu Spika, sikumtaja Mheshimiwa John Shibuda alichangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niseme tu kwamba kwa yote haya ambayo tumeyachukua hapa hoja zaidi ya 77, tutaziweka katika Bango Kitita, tutakuelezeni kwenye kila moja hatua gani tumefikia na makusudio ya Serikali ni kufanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Wizara inashukuru sana ushirikiano ambao mnatupa na sasa baada ya maelezo hayo kwa kuwa nimekuja ili kuweza kuomba nyenzo, naomba mturuhusu ili tuendelee na kazi. Basi namalizia kwa kuwasihi sana bila usumbufu wenu ule wa kawaida, mtupatie fedha zetu maana tunaona tunachelewachelewa hapa, mtupatie fedha tuendelee kufanya kazi kuijenga Tanzania ndani ya Afrika Mashariki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA J ESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Samuel Sitta, Waziri wa Masuala ya Afrika Mashariki. Tunakushukuru sana kwa kupitia hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge na kwa kiwango kikubwa kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wameridhika. Katibu!

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 97 – Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tuko kwenye mafungu na ni fungu moja tu kwa sababu kwenye maendeleo hatujampa pesa zozote Mheshimiwa Waziri, Katibu endelea!

Kif.1001-*Administration and HR Management*... ... ... ... Shs.3,652,149,000/=

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. La kwangu ni ombi zaidi, kwa kuwa hili *block* la Afrika Mashariki kwa upande wa Magharibi linapakana na nchi ya Zambia na uzuri ni kwamba kwa Mkoa wa Rukwa, katika Kata moja ya Kisumba, tuna maporomoko ya maji maeneo matatu na ni sehemu ambayo ni muhimu sana kuendelezwa kiutalii lakini itahitajika pia kujenga daraja ambalo litaweza kuunganisha hii *East Africa* na upande wa Zambia na Mheshimiwa Waziri kwa kuwa amesema kwamba yuko tayari kushirikiana na sekta nyingine, naomba kwa kuwa ana uzoefu mkubwa pale *TIC* na ana uwezo mkubwa kwenye Serikali, atusaidie namna ya kukamilisha daraja hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hili ni ombi ambalo ndani yake limejaa ubunifu na mimi nalipokea kwa sababu ni hakika kabisa kwa sisi ambao tunaishi karibu na Mkoa wa Rukwa, kuna mambo watu hawajayatambua kule. Kwa hiyo, tutashirikiana na sekta husika ili tuhimize utalii katika eneo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Professa Kahigi, Mwalimu wa Kiswahili.

**MHE. PROF. KALIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nilikuwa nauliza kama Wizara imeshaanza kutafakari kurejesha ule utaratibu wa zamani ambapo wanafunzi kutoka Kenya walikuwa wanakuja Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanasomea pale na wanafunzi kutoka Tanzania wanakwenda kusomea Kenya na walikuwa wanadhaminiwa na Serikali zao. Siku hizi utaratibu uliopo ni ule baina ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Makerere kwamba wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanakwenda Chuo Kikuu cha Makerere na wa Makerere wanakuja Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Sasa ule uliokuwepo zamani baina ya Kenya na Tanzania haujarejeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wananchi wa Afrika Mashariki waweze kuzoeana angalau kwa kiwango hicho lazima ule utaratibu wa zamani urejeshwe siyo baina tu ya nchi ambazo zilikuwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ya zamani bali hata hizi mpya kwamba wanafunzi wa Tanzania waende Burundi wasomee kule Warundi waje Tanzania wasomee huku, Wanyarwanda

waje huku wasomee na sisi pia twende huko Rwanda tusomee huko. Kwa hiyo, sijui kama huo utaratibu wameshaanza kuutafakari katika mipango yao?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Prof. Kahigi. Huo ndiyo ulikuwa utaratibu kwa sababu tulikuwa na Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki Dar es Salaam kikiweka mkazo katika fani ya Sheria, Nairobi Uhandisi na Makerere mambo ya Udaktari. Sasa baada ya mambo kubadilika basi imekuwa tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitoe tu taarifa tunalo Baraza la Elimu Afrika Mashariki ambalo linaunganisha juhudi za kuweka mitaala yote ikae vizuri na ifanane kwa nchi zote, ili mtu akipata Shahada ya *Botany* popote iwe Rwanda, Burundi, Uganda, Tanzania basi hiyo iko sawa kabisa katika maana ya maudhui yake aliyoyapata yule mwanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatuzuii wakati huo kuanzisha taasisi ambazo zitakuwa zinachukua wanafunzi kutoka kote na hata hivi sasa ukitazama *Kampala University* pale Dar es Salaam na vyuo vingine si kwamba wapo watu wa nchi moja wanakuwa ni watu wa nchi mbalimbali. Kwa hiyo, eneo la elimu limepanuliwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwie radhi nitoe taarifa tu, kwa utaratibu ni kwamba kuanzia dakika hii kila kitu atajibu Naibu Waziri. Nafanya hivyo si kwa kulidharau Bunge lakini ni lazima tujenge uzoefu. Mara nyingine sisi

Mawaziri tunakuwa na ukiritimba kila kitu unajibu wewe, sasa hawa watajifunza lini hawa? Kwa hiyo, sasa mimi nitatulia, kama akikwama, mimi ninamwamini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba Naibu Waziri atasimama, atajibu yote yaliyosalia kwa ufasaha. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa hili ningeomba anijibu Waziri kwa sababu yeye ndiye mwenye dhamana. *Article* ya 65 ya *Treaty* inavunjwa na Waziri mwenye dhamana ni yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sera za ushirikishwaji katika kufikia malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, maoni yote, *debate* zote zinazojadiliwa katika Bunge la Afrika Mashariki, Katibu wa Bunge la Afrika Mashariki anapaswa atume rekodi ya Miswada yote katika *National Assembly* za nchi wanachama, sehemu ya (b) inazungumzia kwamba *to be laid for information. Article* ya 65 (b) inazungumzia kwamba baada ya *debate,* Katibu wa Bunge wa Nchi Wanachama azirudishe rekodi zile, baada ya *debate,* kwa Katibu wa Bunge la Afrika Mashariki ambaye na yeye ndiye atapeleka kwa *Secretary General.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mara zote anapoleta *speech* yake anaambatanisha nyuma Miswada fulani kwa mfano hapa kuna Miswada 11 na Maazimio tisa na mwaka jana hali kadhalika.

Inasemekana mpaka sasa hivi Bunge la Afrika Mashariki wameshapitisha Miswada na Maazimio 55, Wabunge hapa hatuelewi ni Miswada gani na Maazimio gani yaliyopitishwa. Inaonekana kwamba mpaka huo Muswada ambao unaleta matatizo kwa Tanzania umepitishwa lakini Bunge hatuelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini *Article* hii ya 65 inavunjwa na Waziri mhusika yupo? Ninataka ufafanuzi, ni namna gani tutafanya na kama je, ni Tanzania tu tunaovunja *Article* hii ya 65 ya *Treaty* au na nchi nyingine wanachama pia wanafanya hivyo? Ningeomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Kidogo kabla ya Waziri kujibu, naomba ufafanuzi, Mheshimiwa Mnyaa ni jukumu la Katibu Wa Bunge la Afrika Mashariki kuleta au ni jukumu la Waziri kuleta?

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu wa Bunge la Afrika Mashariki ndiyo jukumu lake kuleta, lakini Waziri hapa ana dhamana ya kufuatilia jambo hilo kwamba limeletwa.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri umedaiwa hapo.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu Mheshimiwa Mnyaa naye sijui vipi? Hili ni swali rahisi kabisa ambalo lilikuwa lijibiwe na Naibu Waziri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi, ile Ibara ya 65 inachosema ni kwamba Katibu wa Bunge la Afrika Mashariki anawasilisha kwa Makatibu wa Mabunge yote matano. Kuanzia hapo ndiyo mchakato huo unaoelezwa unatakiwa kufuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyofahamu ni kwamba hili limekuwa likifanyika bila kwenda hatua ya mbele zaidi ya kuwezesha hiyo Miswada iweze kujadiliwa na kupata baraka za Mabunge husika. Hilo mimi naona ni tatizo la kiutawala tu kwa sababu hata wenzangu Kenya, Uganda hali ni hiyohiyo. Ndiyo maana tumesema ni vizuri sasa tuwe na Kamati ya Bunge hili ya Masuala ya Afrika Mashariki, kwa sababu tukishakuwa nayo, mambo haya hayawezi yakajificha pembeni. Sasa mimi kwangu ni muhali kama Waziri niende nimwambie Spika wewe kwa nini huleti yale mambo na hivi na hivi, haiendi hivyo, kwa sababu ni kazi ya kuweza sasa kuongea na wakubwa yaani Spika wa Bunge la Afrika Mashariki na Spika wa Bunge la Tanzania kuunda huo utaratibu. Mwezi wa Nne mwaka huu ndiyo tumetengeneza sasa Waraka Maalum ambao unazingatia mambo hayo na mtayaona mabadiliko kadri tunavyokwenda hivi sasa, ahsante.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda swali langu ajibu Waziri kwa sababu ndiye anayejua maeneo nitakayouliza, kwa sababu amefika katika Jimbo langu na amefika sehemu ya Namanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Longido lipo mpakani kwa hiyo mlango wa Namanga upo katika Jimbo la Longido. Wafanyabiashara wa Tanzania

wanapata shida sana kutokana na mambo matatu makubwa, kwanza vizuizi vingi vilivyopo barabarani ambavyo mimi mpaka sasa sijui hivyo vizuizi vimewekwa kwa ajili gani. Waziri alikuja wakati mmoja akaagiza kwamba hivi vizuizi viondolewe na mpaka sasa bado vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kodi ambayo upande wetu bado kodi ni kubwa ukilinganisha na wenzetu wa Kenya. Kwa hiyo, tunapata shida sana kwa kulipa hizo kodi na kufanya biashara kuwa ngumu au kutokuwa na ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni fedha, fedha zetu ukiangalia thamani yake ni ndogo inabadilika. Laki moja ya Kenya ni milioni moja na laki tisa ya Tanzania, sasa watu wetu wanapata shida sana kufanya bishara kutokana na hiyo chenji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua tutawezaje kushindana na wenzetu? Hili Soko la Pamoja ambalo lipo Namanga, soko la bidhaa lipo Kenya, soko la mifugo lipo Kenya, masoko Tanzania ni pale Namanga Serikali itatusaidiaje?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Laizer anajua tulikuwa Longido pamoja kwa siku moja na nusu na hapo ndipo tuliwekeana sahihi masikilizano *(MoU)* na mwenzangu Waziri Silma wa Kenya. Kitu kimoja tulichojifunza ni kwamba Watanzania tunapata hasara kubwa kwa kubeba mali zetu wenyewe, kuzivusha mpaka, mathalani mifugo. Hakika watu wa

Longido na sehemu zingine za mipakani ambao wana mifugo wamekuwa wakidhulumiwa kwa sababu wanavuka na mifugo, wakifika kule wanaambiwa juu ya taratibu za kule na mara nyingine zinawashinda basi wanauza mifugo kwa haraka kuepuka kupata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeamua sasa kwenye haya maeneo ya mipakani na Namanga itakuwa ni sehemu ya kwanza, tujenge soko kubwa kabisa upande wetu. Mtu anayetaka ng'ombe aje yeye anunue pale kwa sheria zetu sisi, anayetaka mahindi na vitu vyote vya kutoka Tanzania wao waje, sisi ndiyo wenye mali. Hakuna kitu cha ovyo kama wewe mwenye mali ndiyo unajipeleka huko kwa yule kupata fedha, wanapunjwa kwa *exchange rate* na mambo mengine. Kwa hiyo, ufumbuzi mkubwa ni huu ambao tunauandaa kuanzia mwaka huu wa kuwa na soko kubwa kabisa ambalo litakuwa upande wa pili katika Wilaya ya Longido kwa ajili ya kuwauzia Kenya.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni wazi kwamba Sheria iliyoundwa na Bunge ambayo inahusiana na Viongozi wa Umma kuweza ku-*declare* mali walizonazo ililenga kusaidia na ku-*promote* masuala ya uadilifu miongoni mwetu. Nataka kujua *position au status* ya watumishi ambao wapo ndani ya *East Africa* kwa upande wa Tanzania, kwa maana ya Majaji, Wabunge na viongozi wengine iwapo huwa wana-*declare* mali zao walizonazo kama ambavyo tunafanya sisi Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wengineo au

la? Kama sivyo, nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Watendaji wote Wakuu wakiwemo Mawaziri na wale wahusika ambao wanatakiwa kisheria wawe wana-*declare* mali zao kutokana na Sheria zilizopitishwa katika Bunge hili wanafanya hivyo na mpaka hivi sasa hakuna ambaye ameitwa katika Baraza na kuonekana kwamba hakutekeleza hoja hiyo. Huo ndiyo msimamo wa Serikali na kwa yeyote atakayechaguliwa itabidi afanye hivyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza, kama Kambi ya Upinzani tunatambua Waziri wa Afrika Mashariki kachukua wazo letu la kuundwa kwa Kamati ya Bunge kwa ajili ya kushughulikia masuala yote ya Afrika Mashariki, kwa hiyo tunamshukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, kwenye suala la elimu, Waziri amezungumzia *harmonization* katika *level* ya juu ya vyuo vikuu. Sote tunajua kwamba mtoto anajengwa na msingi na katika nchi zote za Afrika Mashariki ukiondoa Uganda na Tanzania ambao mifumo yao ya elimu inafanana, nchi zingine zote zina mifumo tofauti ambayo inapelekea hata wahitimu wanapomaliza kuwa na taaluma ama kuwa na uwezo tofauti hivyo kuwa na changamoto kubwa sana katika soko la ajira. Nilitaka Naibu Waziri atueleze mbali na *harmonization* katika mitaala ya Vyuo Vikuu, kuna mikakati yoyote ya kufanya *harmonization* katika *level*

ya shule ya msingi mpaka *A-Level* ili watoto wetu waanze katika msingi mmoja na kumaliza katika msingi mmoja na vilevile kuweza kumudu ushindani wa soko la ajira katika usawa? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, napenda kumuarifu kwamba wazo la kuwepo kwa Kamati ya Afrika Mashariki ndani ya Bunge hili ni wazo ambalo nimezaliwa katika kikao cha pamoja baina ya Wabunge ambao walikwenda katika sherehe za *EALA* za miaka 10 Arusha na mimi nikiwa kama Mwenyekiti. Kwa hivyo, hii ni taarifa natoa tu na nasikitika kusema kwamba siyo wazo ambalo limetoka katika Kambi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, ni kwamba mchakato ni mkubwa na umeanza tangu kuoanisha mitaala katika vyuo vikuu, kutengeneza sekta katika vyuo vikuu na kutembeleana na kukaguana katika vyuo vikuu lakini hivi sasa tayari kumeshakuwa na mikakati maalum ambayo bado haijawa *domesticated* lakini usiwe na wasiwasi kwamba pamoja na mitaala kuwa pamoja lakini mifumo ya elimu vilevile katika kitengo cha *research* wanafanya ili waweze kuoanisha tuwe na mfumo mmoja wa elimu. Kulikuwa na wazo moja pia kwamba hata kuwe na Baraza la Mitihani la pamoja, vilevile jambo hilo limefikia katika *level* ya Afrika Mashariki na sisi tunaliunga mkono kama nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mwaka jana wakati kama huu wa hotuba ya Waziri Sitta na wakati wa mshahara wa Waziri, nilimueleza Waziri kwamba Serikali ya Rwanda ilikasirishwa sana na hatua ya Waziri wa Mambo ya Ndani kwenda Ngara na kuagiza wahamiaji haramu warudi makwao. Nilimweleza Waziri kwamba ni vizuri akae pamoja na Mawaziri wenzake wa Uganda na Rwanda wafikie muafaka, tatizo bado lipo palepale na sijapata *feedback*.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linanihusu moja kwa moja. Nitoe taarifa kwamba tarehe 28 mwezi huu, nina ziara ya Mkoa wa Kagera ya siku nne nitakuwa mpakani na kizuri zaidi pale Rusumo, Waziri wa Afrika Mashariki wa Rwanda, Madam Monique Mkaluliza atakuja pale na tutafanya mikutano pale na tutatatua mambo mbalimbali kama ambavyo tulifanya kwenye mpaka wa Namanga. Kwa hiyo, Mheshimiwa kama ukiwepo unakaribishwa sana.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kilwa Tanzania kwa maana ya Afrika Mashariki ni mojawapo ya miji ambayo imepewa urithi wa dunia ikiwemo Lamu na Mombasa nchini Kenya, Mogadishu Somalia, Sofala Msumbuji. Sasa nchi hizi huwa zinafadhiliwa na *UNESCO* tangu mwaka 1981. Kwa hiyo, mimi nilitaka kufahamu, je, Kilwa kwa maana ya Tanzania inafadhiliwa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Sekretarieti yake ina mpango kabambe na mikakati inayohusiana na mambo ya utalii na sehemu nyingi za Tanzania zipo katika mkakati huo wa utalii. Kwa hivi sasa nashindwa kumjibu tu kama Kilwa imo lakini acha tuache na kama haimo basi tutaiweka katika mikakati hiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mkiangalia muda wetu hauko upande wetu kabisa lakini angalau tumeweza kupata Wabunge wanane na Wabunge 20 hawakupata nafasi. Katibu tuendelee na utaratibu wa *guillotine* sasa.

Kif.1001-*Administration and HR Management...* Shs.3,652,149,000/=
Kif.1002 - *Finance and Accounts..* Shs.334,129,000/=
Kif.1003 - *Policy and Planning* Shs.9,698,368,000/=
Kif.1004 -*Trade, Finance and Investment*… … … Shs. 685,354,000/=
Kif.1005 - *Economic and Social Infrastructure* … Shs.655,446,000/=
Kif.1006 - *Political, Defense and Security* … … … … Shs.307,936,000/=
Kif.1007 - *Procurement Management Unit* … … … Shs.202,024,000/=
Kif.1008 - *Government Communication Unit* … ... … … … … Shs.389,664,000/=
Kif.1009 - *Government Information System* … … Shs.349,021,000/=
Kif.1010 - *Internal Audit Unit* …. Shs.164,994,000/=
Kif.1011 - *Legal Service Unit* Shs.204,582,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 97 – Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

*(Fungu hili halikupangiwa fedha ya Maendeleo)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, taarifa!

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu hivi punde limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2012/2013 na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote na Bunge zima, tunawatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na uongozi wote pamoja na Wabunge wetu wa Bunge la Afrika Mashariki. Tunawatakia kazi njema kwa mwaka ujao na tunawahakikishia kwamba tutawapa kila aina ya ushirikiano na tutajitahidi kurekebisha yale ambayo kwa upande wetu kama Bunge tunahitaji turekebishe kwa ajili ya ufanisi bora zaidi wa Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki.

Kufikia hapo, nina tangazo moja la Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* ambaye ni Mheshimiwa Iddi Azzan anatangaza kwamba kesho hakutakuwa na michezo ya kirafiki isipokuwa Jumatano 8/8/2012, siku ya Nanenane kutakuwa na michezo ya mpira wa miguu na *netball* kati ya timu ya B*unge Sports Club* na *Mwananchi Communication Limited* kutoka Dar es Salaam. Wachezaji wote wanahimizwa kufanya mazoezi ya nguvu kujiandaa na michezo hiyo. Hilo ndiyo tangazo pekee nililonalo.

Waheshimiwa Wabunge, kufikia hapo, naomba niwashukuruni sana kwa ushirikiano mlionipa kwa sababu siku ya leo ratibu ilikuwa imebana sana lakini nawashukuru kwa uelewa wenu na ushirikiano mliotupatia. Kwa jinsi hiyo, naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu, tarehe 6 Agosti, 2012, saa tatu asubuhi.

*(Saa 12. 00 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 6 Agosti, 2012, Saa Tatu Asubuhi)*